ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. ZUBEIR ALI MAULID	-	SPIKA
1. Mhe. Mgeni Hassan Juma	-	Naibu Spika/ Nafasi za Wanawake
2. Mhe. Mwanaasha Khamis Juma	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Chukwani
3. Mhe. Shehe Hamad Mattar	-	Mwenyekiti wa Baraza/ Jimbo la Mgogoni
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	-	MBM/Makamu wa Pili wa Rais /Kiongozi wa Shughuli za Serikali/ Jimbo la Mahonda
5. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi/Jimbo la Chwaka
6.Mhe. Haji Omar Kheri	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/ Jimbo la Tumbatu
7. Mhe. Haroun Ali Suleiman	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora /Jimbo la Makunduchi
8. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	-	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar/ Uteuzi wa Rais

9. Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed	-	MBM/Waziri wa Fedha na Mipango /Jimbo la Donge
10. Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	-	MBM/Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
11. Mhe. Riziki Pembe Juma	-	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali / Nafasi za Wanawake
12. Mhe. Balozi Amina Salum Ali	-	MBM/Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko Zanzibar/ Uteuzi wa Rais
13. Mhe. Balozi Ali Abeid Karume	-	MBM/Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji/ Uteuzi wa Rais
14. Mhe. Rashid Ali Juma	-	MBM/Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Jimbo la Amani
15. Mhe. Hamad Rashid Mohamed	-	MBM/Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Uteuzi wa Rais
16. Mhe. Maudline Cyrus Castico	-	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Uteuzi wa Rais
17. Mhe. Salama Aboud Talib	-	MBM/Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Nafasi za Wanawake
18. Mhe. Juma Ali Khatib	-	MBM/ Waziri Asiekuwa naWizara Maalum/Uteuzi wa Rais

19. Mhe. Said Soud Said	-	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/ Uteuzi wa Rais
20. Mhe. Khamis Juma Mwalim	-	Naibu Waziri, Wizara ya Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria na Utumishi wa Umma na Utawala Bora/ Jimbo la Pangawe
21. Mhe. Mihayo Juma N'hunga	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa pili wa Rais wa Zanzibar/ Jimbo la Mwera
22. Mhe. Shamata Shaame Khamis	-	Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ / Jimbo la Micheweni
23. Mhe. Harusi Said Suleiman	-	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Wete
24. Mhe. Mmanga Mjengo Mjawiri	-	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali /Jimbo la Mkoani
25. Mhe. Mohamed Ahmada Salum	-	Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji / Jimbo la Malindi
26. Mhe. Chum Kombo Khamis	-	Naibu Waziri wa Habari, Utalii na Michezo/Nafasi za Wanawake
27. Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	-	Naibu Waziri wa Uwezeshaji,Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto/ Nafasi za Wanawake

28. Mhe. Lulu Msham Abdalla	-	Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi/ Nafasi za Wanawake
29. Mhe. Juma Makungu Juma	-	Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira/ Jimbo la Kijini
30. Mhe. Abdalla Ali Kombo	-	Jimbo la Mwanakwerekwe
31. Mhe.Abdalla Maulid Diwani	-	Jimbo la Jang'ombe
32. Mhe. Ali Khamis Bakar	-	Jimbo la Tumbe
33. Mhe. Ali Salum Haji	-	Jimbo la Kwahani
34. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)	-	Jimbo la Kijitoupele
35. Mhe. Ame Haji Ali	-	Jimbo la Nungwi
33. Mhe. Amina Iddi Mabrouk	-	Nafasi za Wanawake
37. Mhe. Asha Abdalla Mussa	-	Jimbo la Kiwengwa
38. Mhe. Bahati Khamis Kombo	-	Jimbo la Chambani
39. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Nafasi za Wanawake
40. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Jimbo la Wawi
41. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Nafasi za Wanawake
42. Mhe. Hamza Hassan Juma	-	Jimbo la Shaurimoyo
43. Mhe. Hassan Khamis Hafidh	-	Jimbo la Welezo
44. Mhe. Hidaya Ali Makame	-	Nafasi za Wanawake
45. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu (Bhaa)	-	Jimbo la Mtoni
46. Mhe. Jaku Hashim Ayoub	-	Jimbo la Paje
47. Mhe. Khadija Omar Kibano	-	Jimbo la Mtambwe
48. Mhe. Machano Othman Said	-	Jimbo la Mfenesini
49. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi Makoti	-	Jimbo la Mtopepo
50. Mhe. Makame Said Juma	-	Jimbo la Kojani
51. Mhe. Maryam Thani Juma	-	Jimbo la Gando
52. Mhe. Masoud Abrahman Masoud	-	Jimbo la Bububu
53. Mhe. Miraji Khamis Mussa	-	Jimbo la Chumbuni
54. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Jimbo la Mtambile
55. Mhe. Mohamed Said Mohamed	-	Jimbo la Mpendae

56. Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali- Jimbo la Uzini
57. Mhe. Mtumwa Peya Yussuf - Jimbo la Bumbwini
58. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame - Nafasi za Wanawake
59. Mhe. Mussa Ali Mussa - Jimbo la Ole
60. Mhe. Mussa Foum Mussa - Jimbo la Kiwani
61. Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa - Nafasi za Wanawake
62. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis - Nafasi za Wanawake
63. Mhe. Dkt Mwinyihaji Makame Mwadini - Jimbo la Dimani
64. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy- Jimbo la Chaani
65. Mhe. Nassor Salim Ali - Jimbo la Kikwajuni
66. Mhe. Omar Seif Abeid - Jimbo la Konde
67. Mhe. Panya Ali Abdalla - Nafasi za Wanawake
68. Mhe. Rashid Makame Shamsi - Jimbo la Magomeni
69. Mhe. Saada Ramadhan Mwendwa - Nafasi za Wanawake
70. Mhe. Said Omar Said - Jimbo la Wingwi
71. Mhe. Said Hassan Said - Mwanasheria Mkuu
72. Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma - Nafasi za Wanawake
73. Mhe. Salma Mussa Bilal - Nafasi za Wanawake
74. Mhe. Shaib Said Ali - Jimbo la Chonga
75. Mhe. Simai Mohammed Said - Jimbo la Tunguu
76. Mhe. Sira Ubwa Mamboya - Uteuzi wa Rais
77. Mhe. Suleiman Makame Ali - Jimbo la Ziwani
78. Mhe. Suleiman Sarahan Said - Jimbo la Chakechake
79. Mhe. Tatu Mohamed Ussi - Nafasi za Wanawake
80. Mhe. Ussi Yahya Haji - Jimbo la Mkwajuni
81. Mhe. Viwe Khamis Abdalla - Nafasi za Wanawake
82. Mhe. Wanu Hafidh Ameir - Nafasi za Wanawake
83. Mhe. Yussuf Hassan Iddi - Jimbo la Fuoni
84. Mhe. Zaina Abdalla Salum - Nafasi za Wanawake
85. Mhe. Zulfa Mmaka Omar - Nafasi za Wanawake

Ndugu Raya Issa Msellem - Katibu wa Baraza la Wawakilishi

Kikao cha Saba – Tarehe 23 Febuari, 2017

(Kikao kilianza Saa 3:00 asubuhi)

DUA

Mhe. Mwenyekiti (Shehe Hamad Mattar) alisoma dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo: Mhe. Mwenyekiti, naomba kuweka hati mezani muhutasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa mwaka 2016/2017. Naomba kuwasilisha.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 41

Taratibu za Kuandikisha Cheti cha Kuzaliwa

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**

Kumekuwa na utaratibu wa utoaji vyeti vya kuzaliwa kwa watoto wanaozaliwa kwa kuweka sharti la mzee kwenda na cheti cha ndoa ndio mtoto apatiwe cheti.

(a) Je, utaratibu huu upo kweli.

(b) Je, kuendelea kuwa na utaratibu huu hauwanyimi watoto wengine hati ya kuwa na vyeti hivyo.

(c) Je, Serikali inaweka utaratibu gani wa kuwapatia vyeti watoto wanaozaliwa nje ya ndoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 41 lenye vipengele (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kwamba utaratibu huu upo lakini sio sharti la kupatiwa cheti cha kuzaliwa cha mtoto bali ni mahitaji tu ya mfumo mpya wa usajili wa kielektroniki ambao umeanza kutumika hivi karibuni katika Mkoa wa Mjini Magharibi, Unguja. Mfumo huu mbali ya kusajili matukio ya kijamii kama vizazi pia unakusanya takwimu mbali mbali kama za kiafya na kijamii. Mfumo huu wa ukusanyaji wa takwimu wa Serikali kwa matumizi yao mbali mbali. Suala la hali ya ndoa ya wazazi wa mtoto anayesajiliwa kwa kupata cheti cha kuzaliwa ni miongoni mwa takwimu zinazohitajiwa na Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali ambazo huzitumia katika tafiti zao mbali mbali za masuala ya kijamii.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile utaratibu huu sio sharti la kupatiwa cheti cha kuzaliwa kama nilivyoeleza awali hauwanyimi watoto wengine ambao wazee wao hawana vyeti vya ndoa au waliozaliwa nje ya ndoa haki ya kusajiliwa na kupatiwa vyeti vya kuzaliwa ni ya kila mtu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kuweka wazi suala hili.

Je, tokea kuanza usajili huo wa elektroniki mpaka dakika hii mumeshasajili vizazi vingapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kutaka kujua tokea kuanza mfumo huu ni vizazi vingapi ambavyo vimesajiliwa.

Mhe. Mwenyekiti, nataka nimwambie Mhe. Mwakilishi kuanzia kipindi cha Julai 2017 mpaka Disemba hali ya vizazi ambavyo vimesajiliwa ni ishirini na tano elfu mia tano thamanini na tano ambavyo viliandikishwa na kwa upande wa vifo pia kulikuwa na elfu moja mia nane na arubaini na saba na ndoa vile vile tumeweza kusajili mia moja na kumi na nane na talaka tano. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Suleiman Ali: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako kuuliza swali la nyongeza.

Kwanza naipongeza wizara kwa kuweka mfumo mpya wa Elektroniki mfumo mpya huu ambao upo kwa Mkoa wa Mjini/Magharibi tu.

(a) Jee, mfumo huu wa majaribio ama endelevu.

(b) Kama endelevu kwa nini usiendelee katika Mikoa mengine ili kuweka kumbukumbu zetu vizuri kwa vizazi vyetu ambavyo vinazaliwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi la nyongeza la kutaka kujua mfumo ambao wa elektroniki ambao tunaotumia kama ni majaribio ama ni endelevu.

Mhe. Mwenyekiti, dhamira ya serikali kupitia taasisi hii imekusudia kuboresha hali ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa na vyeti vyengine ili kuepusha yale mapungufu au usumbufu ambao wanapata wananchi wetu. Kwa maana hiyo, mfumo huu ni wa kuharakisha na tumeanza katika hali ya kuangalia majaribio lakini lengo na madhumuni ni kuboresha ili katika maeneo yetu yote ya Unguja na Pemba iweze kupatikana huduma hii kama ambavyo inaonekana itatusaidia zaidi.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa fursa hii na nimshukuru Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri.

Mheshimiwa katika kuboresha masuala yetu haya ambayo yanatupa takwimu katika hali ya kujijua kwamba tunaongeza, tunapungua, tunafanyaje.

Mhe. Mwenyekiti, hatua hii tunaiweka katika hatua ya usajili katika eneo moja tu la usajili.

Jee, katika hatua ambazo tunaona za kuboresha mna mpango wa kuwapatia hati hizi Masheha ili kile kitu usahihi ambacho kitakuwa kinafanyika vijijini tuwe tunakipata sio takwimu ambazo mpaka mtu atakapojisajili.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niendelee kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza la kutaka kwamba mfumo huu au huduma hii iweze kupatikana labda katika ngazi ile ya Shehia kama nimemfahamu vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, lakini nimwambie kwamba utaratibu wa usajili unaanzia katika eneo ambalo kizazi kimetokea au ile huduma inahitajika, kwa mfano kama ni Shehia ama ni kituo cha Afya ndio ambapo usajili wake unaanza taratibu zile zinakusanywa na hatimae kuweza kupelekwa katika kituo ni maalum ambacho kimewekwa kwa ajili ya kutengeneza hati hizo.

Kwa maana hiyo, kuendelea kwamba kukichukua kituo labda tupeleke katika huduma hiyo sehemu ya kwa Masheha bado utaratibu hauko hivyo na bado utaratibu wake ni ule ule kwamba tunaanzia kwa Sheha lakini tunamalizia au unasonga mbele zaidi katika hatua ya Wilaya.

Nam. 42

Ulazima wa wanandoa kupatiwa Vyeti vya Ndoa

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:**

Kwa kuwa Serikali imeweka utaratibu wa kutoa vyeti vya ndoa kwa wanandoa badala ya karatasi zisizo rasmi za ndoa. Na kwa kuwa wanandoa wengi baada ya kupewa karatasi isiyo rasmi anayosaini Sheikh anayeozesha hawatafuti tena vyeti vya ndoa mpaka litakapotokea jambo litakalomlazimu kutafuta cheti hicho.

Jee, Serikali haioni kuna haja sasa ya kuweka ulazima kwa wanandoa kuwa na vyeti vya ndoa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ – Alijibu**:**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako SMZ naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 42 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kuhusiana na usajili wa ndoa, karatasi zinazotolewa na Mashekhe mara tu baada ya kufungisha ndoa ni karatasi rasmi za Serikali ila sio vyeti vya ndoa. Karatasi ile ni tangazo (*notification)* la tukio la ndoa iliyofungwa. Karatasi hii ndio kitu cha mwanzo kinachohitajika kabla ya kutengeneza cheti cha ndoa kama ilivyo katika usajili wa kizazi ambapo mzazi hupatiwa katarasi kama hii mara tu anapojifungua, aidha hospitali au kwa Masheha kwa wale wanaojifungulia majumbani.

Mhe. Mwenyekiti, suala la usajili wa matukio yote ya kijamii yaani vizazi, vifo, ndoa na talaka kwa mujibu wa Sheria zote zinazosimamia mambo haya ni lazima na sio hiyari. Kwa bahati mbaya katika nchi yetu kumekuwa na uelewa mdogo kuhusiana na masuala haya ndio maana baadhi ya wananchi wamekuwa hawayapi kipaumbele hadi pale wanapolazimika kufanya hivyo kwa mahitaji mbali mbali kama mtoto kupelekwa Skuli, kuhitaji pasi ya kusafiria au viza kwa safari ya nje ya nchi, mikopo ya elimu ya juu na masuala ya mirathi.

Hivyo basi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ itaendelea kuchukua jitihada za kuwaelimisha wananchi wetu juu ya umuhimu wa usajili wa matukio ya kijamii na faida zake kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa majibu mazuri.

Katika majibu yako Mhe. Waziri umesema kwamba Serikali ya SMZ itaendelea ya kuchukua jitihada za kuwaelimisha wananchi juu ya umuhimu wa usajili.

Je, ni jitihada gani iliyochukuliwa ya moja kwa moja kuwaelimisha wananchi hawa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuendelea kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kutaka kujua ni jitihada gani ambazo za makusudi zinazochukuliwa na Afisi yangu juu ya kuwaelimisha wananchi wetu katika kuona kwamba umuhimu au wanapata hizo huduma za vyeti.

Mhe. Mwenyekiti, Taasisi hii juhudi ambazo inazichukua ni nyingi moja kama nilivyosema kwamba ni matayarisho mazuri ya kuona kwamba suala la elimu linapewa mkakati madhubuti na imekuwa jambo ambalo kwa kweli kwa sasa hivi ni kawaida kwenda kuelimisha katika ngazi za Masheha katika kuona kwamba wanapewa umuhimu yaani kuelekezwa umuhimu wa jambo hili ambalo linaweza likaleta faraja zaidi kwa wananchi wetu.

Lakini si hilo tu kipindi kitakachokuja cha bajeti tunakusudia vile vile kulishauri Baraza la Wawakilishi litupitishie bajeti zaidi katika kuonesha mkakati zaidi ambao unaweza ukatusaidia zaidi kufikia maeneo ambayo tumegundua kwamba ni muhimu zaidi katika kutoa taaluma juu ya masuala haya.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Nashukuru Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimsifu sana Mhe. Naibu Waziri jembe kwa majibu yake mazuri.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nataka kusema ni kwamba ulimwengu unabadilika na kwa sasa hivi kwa nchi za wenzetu kumeshakua na ndoa za mikataba ukiachia tu ndoa za kuona hizi ni ndoa za mikataba. Lakini katika maelekezo mengi

humu sijaona kama Mheshimiwa ameliweka katika ndoa za mikataba. Sasa mimi swali mimi linakuja hapa.

Sasa hivi kuna mtu anampenda mpenzi pengine anamtaka mtu kwa mbegu tu kutafuta mbegu yake kwa ajili ya kupata watoto wawili watatu na baadae kukata ndoa bila hata kugombana. Sasa ni mkataba.

Je, sasa hivi wizara yako imeshaandaa ndoa za mikataba ili watakapokuja watu wa mikataba uweze kuwa rahisi kumuelekeza kitu gani ambacho kitafanyika. Kwa sababu katika ndoa ile ya mikataba kuna na kiinua mgongo Mheshimiwa..

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa swali muhimu uliza.

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Kuna swali moja lenye (a) na (b)

(a) Je, sasa hivi wizara yako imeshaandaa ndoa za mkataba.

(b) Katika ndoa hiyo pia kuna kielelezo cha kiinua mgongo baada ya mama yule kufanya ile kazi ambayo je, uko tayari kuandaa mkataba huo hivi sasa.

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Suleiman Sarahan Said swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, kwanza mikataba ya ndoa inaruhusika na kwa jina maarufu hapa kwetu tunaita ndoa za Bomani, kazi hiyo inafanywa na Waheshimiwa Wakuu wa Mikoa.

(b) Kuna ndoa zinazokubalika kwa Dini yetu ya Kiislamu kwa baadhi ya Madhehebu. Madhehebu ya "Shafi na Sunni" hatuzikubali. Madhehebu mengine wanazikubali ndoa hizo ni "Mutwaa". Sasa kama Mheshimiwa madhehebu yake yanamruhusu basi anaweza kufanya hizo ndoa.(*Makofi*).

Lakini mambo haya yanaendeshwa kwa mujibu wa Sheria. Sheria zetu mbali mbali ndizo zinazoweka utaratibu wa kugawa mapato au mirathi, ziko Sheria za Dini ya Kiislamu na ziko Sheria za Dini nyengine na ziko *Common law* ambazo zinaruhusu utaratibu wa kugawana mali. Kwa hiyo, Mheshimiwa kuhusu suala (b) linaruhusika lakini kwa kufuata Sheria ya wahusika wenyewe. Ahsante sana.(*Makofi*).

Nam. 80

Kurekebishwa umri wa Kustaafu

Mhe. Suleiman Sarahan Said - Aliuliza**:-**

Serikali imeweka utaratibu wa sheria ambapo mfanyakazi wake akifika umri wa miaka 60 anatakiwa astaafu kwa mujibu wa sheria na akifika miaka 55 anaweza kuomba kustaafu kwa hiari na kupata haki zake zote.

a) Serikali haioni umuhimu wa kumpa nafasi mfanyakazi anayetaka kustaafu kwa hiari kumpunguzia miaka badala ya 55 ikawa miaka 50.

b) Je, serikali inazingatiaje suala la wafanyakazi wengi wa Zanzibar ambao wakifika miaka 40 huonesha dalili ya kuwa na maradhi mengi kama sukari, presha na kadhalika na wengine huomba kustaafu kwa matatizo ya afya, lakini kikomo cha kustaafu cha miaka 55 kinamfunga.

c) Je, serikali haioni kama mfanyakazi akistaafu kwa hiari anatoa nafasi kwa vijana kupata ajira.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 80 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kumjibu Mhe. Mwakilishi naomba kutoa maelezo yafuatayo:-

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na maelezo ya Mhe. Mwakilishi kwamba ni kweli Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeweka utaratibu ambao umefafanuliwa vizuri katika Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 ambapo, mfanyakazi akifika umri wa miaka 60 anatakiwa kustaafu kwa lazima na akifikia umri wa miaka 55 anaweza kuomba kustaafu kwa hiari na kupata haki zake zote.

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kutungwa kwa Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014 zilikuwepo Kanuni za Utumishi Serikalini (*GO)* za mwaka 1997 ambapo kwa mujibu wa Kanuni ya 97(a), mfanyakazi wa kiume alitakiwa

kustaafu kazi kwa lazima anapofikia umri wa miaka 60 na miaka 55 kwa watumishi wa kike na kustaafu kwa hiari kwa watumishi wa kiume wanapofikia miaka 55 na kwa watumishi wa kike wanapofikia miaka 50.

Mhe. Mwenyekiti, ili kuleta usawa baina ya watumishi wa kike na watumishi wa kiume, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar mwaka 2014 ilipitisha Kanuni za Utumishi wa Umma ambapo Kanuni ya 23(I) imefafanua kwamba, mtumishi yeyote anaweza kustaafu kazi kwa hiari atakapofikia umri wa miaka 55.

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelezo hayo sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo:-

(a) Mhe. Mwenyeiti, kutokana na maelezo niliyoyatoa kabla, serikali haijaona umuhimu wa kurejesha umri wa kustaafu kazi kwa hiari wa miaka 50 (kama ilivyokuwa kabla) badala ya miaka 55 (kama ilivyo hivi sasa). Hii inatokana na kuongezeka kwa umri wa kuishi wa watu wetu hadi kufikia zaidi ya miaka 63 (Kwa mujibu wa Sensa ya Watu na Maendeleo ya Mwaka 2012).

Mhe. Mwenyekiti, pamoja na yote hayo, Kanuni ya 25 ya Kanuni za Utumishi wa Umma inatoa ruhusa kwa Mtumishi wa Umma kuweza kuacha kazi muda wowote na kwa sababu yoyote na atasubiri kulipwa haki zake kwa mujibu wa Sheria ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ya Mwaka 2005.

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa ofisi yangu haina takwimu kuhusu uhusiano uliopo kati ya umri wa kustaafu na idadi ya watumishi wanaopata maradhi yasiokuwa na kuambukiza kama vile kisukari, presha na kadhalika, ni mapema mno kuitolea maelezo hoja hiyo.

Hata hivyo, napenda kumhakikishia Mhe. Mwakilishi kwamba serikali imeandaa utaratibu mzuri wa kumshughulikia mtumishi mweye matatizo ya kiafya. Kwa mfano, Kanuni za Utumishi wa Umma za Mwaka 2014, Kanuni ya 60 (1-5) imefafanua utaratibu wa Mtumishi wa Umma ambaye amepata maradhi kuweza kupata likizo la maradhi, huku akiwa analipwa mshahara wake kamili.

Aidha, kwa mujibu wa Kanuni 60(8) Mtumishi wa Umma hazuiliki kustaafu kazi kunakotokana na maradhi kwa sababu ya kutokufikia umri wa miaka 55, kwani kwa mujibu wa Kanuni hiyo inapotokezea Mtumishi wa Umma hawezi kuzimudu kazi zake kutokana na maradhi, Katibu Mkuu

au Mkuu wa Taasisi atapaswa kuchukua hatua za kuitaka Bodi ya Uchunguzi wa Afya za Watumishi iidhinishe mtumishi huyo kustaafishwa kwa sababu ya maradhi na kumlipa stahiki zake kwa mujibu wa taratibu zinavyoelekeza.

c) Mhe. Mwenyekiti, ninakubaliana na Mhe. Mwakilishi katika swali lake la (c) kwamba, kustaafu kazi kwa hiari kwa Watumishi wa Umma ni miongoni mwa sababu za kutoa nafasi kwa vijana kupata ajira hasa ukizingatia kuwa suala la ajira ni changamoto katika mataifa mengi duniani.

Mhe Suleiman Sarahan Said: Mhe. Mwenyekiti nashukuru, kwanza leo mimi nataka nitoe pongezi kwamba sijapata kujibiwa vizuri katika maswali kama la leo ambalo Mheshimiwa kalichanganua vizuri sana. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama ingekuwa si kwa niaba ya wananchi basi ningesema nimetosheka, lakini wacha nimuongeze swali moja lenye (a) na (b) kidogo. Sasa hivi takwimu zinatuonesha kwamba akinamama ndio wanaishi zaidi kuliko akinababa na ukipita majumbani wajane ni wengi kuliko wanaume hawako.

(a) Je, serikali haioni umuhimu wa kuwaongezea muda wanawake na kuwapunguzia wanaume.

(b) Mheshimiwa kwa utaratibu ni kwamba ni kweli kuna uwazi mzuri sana wa kuacha kazi, lakini ukiacha kazi kwa muda ambao haujafikiwa inabidi uulizwe maswali meng na ndio nikasema kwamba, kwa kipindi cha sasa hivi serikali ingewacha wazi miaka 50 kwa mtu yeyote ambaye angeacha bila ya mlolongo wowote ili hizo nafasi za vijana zikaweza kupatikana.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunaongozwa na Sheria na Sheria inayohusiana na masuala ya utumishi (Sheria ya Utumishi) imeweka bayana yale mambo ambayo yanapaswa kuyafuata katika masuala ya ajira. Kwa hivyo, nimwambie Mhe. Mwakilishi kwamba kutokana na utaratibu wa Sheria yetu ilivyo suala la kupunguza muda kwa wanaume na kuwapandishia muda wanawake wa

kustaafu hatuwezi kufanya hivyo mpaka Sheria hiyo iweze kufanyiwa marekebisho.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kuweza kunipa fursa na mimi ya kuuliza swali dogo la nyongeza.

Kwa kuwa baadhi ya wafanyakazi wa taasisi za umma wamejirejesha nyuma umri wao halisi ili wabakie kwa muda mrefu kazini. Je, serikali inalijua hilo na hatua gani imechukua.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara yetu haina taarifa ya hao wafanyakazi ambao wanaajiriwa ambao wanajirejesha muda ili waweze kupata muda mkubwa zaidi serikalini. Kwa hivyo, hilo hatuna taarifa lakini nimuombe tu Mhe. Mwakilishi kama taarifa hizo au minong'ono hiyo ipo basi tunakukaribisha ofisi kwetu tukae pamoja tuweze kushirikiana na tuweze kulitatua tatizo hilo. Ahsante.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa hii fursa. Katika mwaka wa bajeti 2016 kuelekea 2017 katika mchango wangu nilimuuliza Waziri husika juu ya suala la Wazanzibari ambao wanaomba kazi katika Utumishi Serikali na wale ambao wanashindwa kupata hiyo ajira na utaratibu gani unatumika katika kuwaunganisha wale ambao wanakosa kuingia katika ajira ili kuweza kuingia katika sekta binafsi kwa kupitia Halmashauri zetu za Wilaya pamoja na maeneo mengine.

Je, ni hatua gani za utaratibu huo umechukuliwa tangu mwaka jana kuelekea mwaka huu.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Mwakilishi arejee hilo swali lake. Kwa sababu naona kidogo kama limetoka nje ya hiki ambacho nimekizungumza.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe rudia swali lako ili Mhe. Naibu Waziri aweze kulijibu vizuri.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nitazungumza kidogo kidogo wala sitatumia Kanuni.

Mhe. Mwenyekiti, katika mwaka wa fedha 2016/17 wakati nilipokuwa nikitoa mchango wangu katika wizara husika, nilitoa ushauri kwamba kwa vijana ambao wanaomba ajira ndani ya Utumishi wa Umma, lakini wale ambao wanaokosa nikashauri kuanzisha *job centers* katika Halmashauri zetu ili tuwatafutie ajira nyengine katika upande wa sekta binafsi na tuweze kuwaorodhesha.

Mhe. Naibu Waziri kwa niaba ya wizara yake alipokea huo ushauri na akasema ataufanyia kazi ili utaratibu huo uweze kuanza na hilo wazo pia alifurahika nalo.

Sasa leo namuuliza swali kwamba tangu nilipotoa mawazo hayo mwaka jana katika wale vijana wa Kizanzibari wanaokosa kuingia katika Utumishi wa Umma ili kuanzisha taratibu hizo za *job centers* katika Halmashauri zetu, ni utaratibu gani umeanza kuweza kuwapatia ajira hawa vijana wetu ili wale wanaokosa hizo ajira ndani ya Utumishi wa Umma tuweze kuwaunganisha katika sekta binafsi. Sijui kanifahamu sasa.

Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora:
Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ushauri wake tuliuchukua na bado tunaufanyia kazi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Naibu Waziri. Mhe. Waziri kwa majibu ya nyongeza.

Mhe. Waziri wa Nchi (OR) Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma na Utawala Bora: Mhe. Mwenyekiti, namshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri aliyoyajibu, lakini pia nampongeza Mhe. Simai Mohammed Said kwa swali lake.

Mhe. Mwenyekiti, suala la ajira kwa sekta binafsi Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar haina pingamizi nalo na kuna taasisi mbali mbali ambazo zimeajiri watu kupitia taasisi hizo, lakini pia kupitia Wizara yetu ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto hii ndio Wizara ambayo ina jukumu kubwa sasa hivi kuhamasisha vijana na wananchi wake kwa ujumla ili waweze kujiajiri kwa vikundi mbali mbali na hatimaye kujiajiri.

Kwa hivyo, suala la Mhe. Simai Mohammed la kwamba serikali imejipanga vipi, serikali upande wetu sisi kama ni Wizara sisi tumeiachia Wizara inayohusika na masuala hayo kwa kushirikiana sote kwa pamoja. Lakini pia na sisi kama Wawakilishi tuna uwezo mkubwa wa kuhamasisha vijana wetu kujikusanya kwenye vikundi ili tusingojee ajira za serikali.

Nam. 8

Undelezaji wa Chuo cha Amali

Mhe. Hidaya Ali Makame - Aliuliza:-

Kwa kuzingatia umuhimu wa suala la elimu ya Mafunzo ya Amali hapa Zanzibar na duniani kote katika kuimarisha ujasiriamali kwa kupitia Vyuo vya Amali.

Je, serikali imejipanga vipi katika kutafuta wadhamini na wadau ili kuendeleza elimu hii ya mafunzo ya amali na kupata vitendea kazi kwa ajili ya wanafunzi wa mafunzo hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 8 kama ifuatavyo.

Kwanza napenda kutoa maelezo ya utangulizi kama hivi ifuatavyo:-

Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ilianzishwa chini ya Sheria Nam. 8 ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali ya Mwaka 2006 na kurekebishwa kwa Sheria Nam. 11 ya Mwaka 2007. Hii ikiwa ni kutekeleza Sera ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya Mwaka 2005. Mamlaka hii ina majukumu ya kupanga, kusimamia, kuratibu, kuendeleza na kutoa Mafunzo ya Amali nchini.

Katika kutekeleza majukumu yake, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali inamiliki na kuviendesha vituo vitatu vya kutolea mafunzo ya amali navyo ni vituo vya Mkokotoni, Vitongoji na Mwanakwerekwe. Pia, ujenzi wa vituo viwili vikubwa vya Mafunzo ya Amali huko Makunduchi na Mtambwe Daya unaendelea.

Mhe. Mwenyekiti**,** sasa naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama hivi ifuatavyo:-

Serikali kwa kushirikiana na wadau mbali mbali wa ndani na nje ya nchi inadhamini na kuendesha mafunzo ya amali na ujasiriamali, mashirikiano hayo yamesaidia katika upatikanaji wa vitendea kazi na umeleta mafanikio yafuatayo:-

i. Mamlaka ya Mafunzo ya Amali imevisajili vituo 45 vya Mafunzo ya Amali kwa Unguja na Pemba. Miongoni vikiwemo vitatu vya serikali na arobaini na mbili (42) vya watu binafsi.

ii. Kupatikana kwa msaada wa vifaa na mashine za kisasa za karakana, pamoja na vitendea kazi kwa ajili ya wanafunzi vyenye thamani ya Dola za Kimarekani laki tano (USD. 500,000.00) kutoka Serikali ya Jamhuri ya Kiislamu ya Iran. Vifaa hivyo vimefungwa katika Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Mkokotoni, Unguja.

iii. Ujenzi wa vituo viwili vipya katika maeneo ya Makunduchi kwa Unguja na Daya kwa Pemba unaendelea kwa mashirikiano na Benki ya Maendeleo ya Afrika (*ADB)*. Vituo hivyo vitakapokamilika vitawekwa mashine na vitendea kazi vya kisasa katika fani za useremala, ufugaji wa kuku, ng'ombe na mbuzi, uvuvi, ufundi elektroniki, ufundi wa vyombo vya moto na kilimo. Ujenzi wa vituo hivi vinatarajiwa kumalizika mwishoni mwa mwaka 2017. Pia serikali kwa kushirikiana na Serikali ya India inakusudia kukiimarisha Kituo cha Mafunzo ya Amali cha Vitongoji katika fani ya kutengeneza na kuhifadhi chakula cha kusindika *(agro processing and packaging)* na katika utunzaji hoteli (*hospitality)*. Serikali ya India itatoa vifaa na wataalamu.

Pia, Mamlaka ya Mafunzo ya Amali hivi karibuni imeifanyia mapitio Sera ya Elimu na Mafunzo ya Amali ya 2005 na imeandaa rasimu ya Sera mpya ya Elimu ya Ufundi na Mafunzo ya Amali. Katika rasimu ya sera hiyo mpya, mkazo mkubwa umewekwa katika kujenga mashirikiano na taasisi binafsi na mashirika ya kujitegemea na matayarisho ya mitaala mipya na kupatikana kwa vifaa vya kufundishia na mazoezi ya vitendo.

Mhe. Mwenyekiti**,** pamoja na mafanikio hayo, serikali itaendelea kushirikiana na Washirika na Maendeleo katika kuimarisha Mafunzo ya Kazi za Amali ili vijana wetu wengi zaidi waweze kupaata ujuzi na maarifa yatakayowawezesha kujitegemea na kupunguza idadi ya vijana wanaotafuta kazi. Ahsante.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Mwenyekiti ahsante. Kwanza nimpongeze Mhe. Naibu Waziri kwa majibu yake mazuri na yenye umakini ndani yake lakini pia niipongeze Wizara kwa kazi kubwa inayoifanya juu ya suala la kuwapatia vijana wetu elimu. Pia napenda nimuulize swali moja lenye (a) na (b) la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Waziri katika mizunguko yetu mingi tuliyoifanya katika Vyuo vya Amali tumeona kwamba Chuo cha Amali ambacho kiko juu zaidi ni cha Mkokotoni, lakini kuna changamoto kubwa sana juu ya Chuo cha Amali cha Kengeja.

(a) Je, Wizara imejipanga vipi katika kukisaidia Chuo hichi hususan kwenye suala hili la vifaa (vitendea kazi).
(b) Je, ni masomo gani ambayo yamepewa kipaumbele zaidi kwenye haya mafunzo ya amali ambayo vijana hawa wanaweza wakayasoma kwa vizuri zaidi na wakaweza kupata ajira kwa wepesi na kwa haraka.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake lenye sehemu (a) na (b).

(a) Kwanza niseme kwamba Kengeja si kituo cha Mafunzo ya Amali ile tunaita ni Sekondari ya Ufundi. Lakini hata hivyo tunaelewa kwamba ina changamoto nyingi na Wizara kwa kushirikiana na wafadhili na wahisani itahakikisha kwamba zile changamoto zilizopo katika Skuli ya Ufundi Kengeja zinapatiwa ufumbuzi kama tulivyoipatia ufumbuzi Skuli ya Ufundi Mikunguni.

(b) Tumezitaja fani ambazo zinasomeshwa katika vituo hivyi, umetajwa usaramala, fundi bomba, masuala ya hoteli, umeme na kadhalika. Kwa hivyo, kuna fani zaidi ya nane ambazo tunadhani kwamba zitasaidia vijana kuweza kujiajiri, fani hizo zinatolewa sasa na nyengine mpya zitatolewa baada ya vituo hivi viwili kukamilika. Ahsante.

Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kwa kunipatia nafasi hii. Kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijalia leo hii nikaweza kusimama tena katika Baraza hili Tukufu. Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza.

Tangu vifunguliwe Vyuo hivi vya Amali naamini wanafunzi wengi tayari wamemaliza masomo yao, naomba kumuuliza wanafunzi wangapi tayari wamewapa mikopo baada ya kumaliza mafunzo hayo ya amali.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa suala lake linadai takwimu naomba suala hili tumjibu kwa maandishi hapo baadae. (*Makofi*)

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuuliza swali dogo la nyongeza. Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, vijana wengi wamejitokeza kupata mafunzo ya amali lakini baadhi yao hukosa vyeti vya mafunzo yale ambayo wanasoma. Kwa mfano kama mafunzo ya sanaa Jumba la Sanaa liliopo pale Mwanakwerekwe.

Jee, Wizara yako ina mpango gani wa kushirikiana na Wizara ya Habari kuwapatia vyeti wanafunzi wale wanaosoma masuala la sanaa na ku- *design* ili kutambulika masomo yao.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kwamba sisi Wizara ya Elimu tumeanzisha Mamlaka ya Vyuo vya Amali na Mamlaka hizo ina kazi moja wapo ni kusajili Vituo vya Amali kama Chuo ulichokitaja kitakuwa hakijasajiliwa itakuwa ni vigumu kupatiwa vyeti. Lakini kama kitasajiliwa na kufuata masharti ya usajili ya Vyuo vya Mamlaka ya Amali basi vitaweza kutoa vyeti na vikapatikana vyeti. Lakini mpaka visajiliwe rasmi. Kwa hivyo, ningeshauri kwamba Chuo hicho kama hakijasajiliwa basi kisajiliwe ili kuweza kutoa mafunzo yake ya halali na kutoa vyeti ambavyo vitatambulika.

UTARATIBU

Mhe. Suleiman Makame Ali: Mhe. Mwenyekiti, Kanuni ya 37 "Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo anatakiwa kulijibu swali hilo kwa ukamilifu na usahihi na kwa ufupi".

Nimemuuliza Mhe. Naibu Waziri, Wizara yake ina mpango gani wa kushirikiana na Wizara ya Habari kwa sababu wale vijana pale wanasoma masuala ya sanaa ku-*design* vitu mbali mbali.

Je, Wizara yake ina mpango gani wa kushirikiana kwa sababu nina imani kwamba itakuwa hawajasajiliwa Wizara wa Elimu lakini Wizara ya Habari wako wana kila kitu wale. Je, Wizara yake ina mpango gani wa kushirikiana nao kuwapatia vyeti. Hilo sijapata jibu lake.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Naibu Waziri njoo uweke sawa swali hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kujibu kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema kwamba katika masuala ya taaluma na Sheria lazima wananchi na sisi Wawakilishi Sheria tumezipitisha wenyewe tuweze kuzifuata. Wizara ya Elimu imeanzisha mamlaka kwa sheria ya kutoa leseni na ruhusa ya kuanzisha vituo vya amali. Kwa hivyo, ushirikiano uliopo ni kwamba Wizara ya Elimu haiwezi kushirikiana na Wizara ya Habari baada yake ni kwamba walioanzisha Chuo hicho waombe ruhusa, waombe leseni katika Mamlaka ya Vyuo vya Amali ili uendeshaji wa Vyuo vyao upate uhalali. Hilo ndilo jibu sahihi kabisa.

Nam. 95

Makampuni ya Wageni katika Biashara ya Utalii

Mhe. Omar Seif Abeid - Aliuliza**:-**

Kwa kuwa kumekuwa na Makampuni ya *"Tours Operator*" ambayo wamiliki wake ni wageni hayapo chini ya Jumuiya ya watembeza wageni *ZATO* na ambayo yanaingiza na kupokea wageni wengi. Na kwa kuwa Makampuni hayo yanasadikiwa kuwa huwatumia wenyeji kama kivuli cha kufanya biashara zao.

a) Je, Serikali kwa kushirikiana na *ZATO* wana mpango na mkakati gani wa kuyatambua Makampuni hayo.

b) Je, ni Makampuni mangapi kama hayo ambayo yamebainika kufanya hivyo na ni hatua zipi zilizochukuliwa baada ya kubainika kufanya udanganyifu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako napenda kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 95 lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, hivi sasa Kamisheni ya Utalii inaendelea na uhakiki wa miradi yote ya utalii ili kujua pamoja na mambo mengine wamiliki halisi wa miradi hiyo. Katika kufanya kazi hii Kamisheni ya Utalii hushirikiana na wadau tofauti ikiwemo Jumuiya ya Makampuni ya kutembeza Watalii (*ZATO)*, Jumuiya ya Wawekezaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar (*ZATI)*, Jumuiya ya Wawekezaji wa Utalii Pemba (*PATI)*, Jumuiya ya waongozaji Watii (*ZATOGA)* na raia wema wenye kupenda maendeleo katika nchi yetu. Tunayo matumaini makubwa kwamba tutaweza kuwabaini wale wote waliofanya udanganyifu wakati wa uanzishwa wa miradi yao na kuwachukulia hatua za kinidhamu na kisheria.

b) Mhe. Mwenyekiti, ipo baadhi ya miradi ambayo taarifa za uanzishwaji wake hazikuwa sahihi. Kamisheni ya Utalii imeshachukua hatua mbali mbali kwa miradi hiyo kwa mujibu wa makosa husika ikiwemo kuwataka wageni kuuza hisa zao kwa wazawa na kufuta vibali vya kazi na ukaazi kwa wahusika.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri ya kuonesha mwelekeo lakini nina swali la nyongeza lenye kifungu (a) na (b), kwa ruhusa yako naomba nimuulize.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Mhe. Naibu Waziri amekiri kuwepo kwa mapungufu hayo na ili kuhakikisha kwamba makosa kama hayo hayajirejei tena.

(a) Je, tayari hatua hizo za kuwafutilia vibali hao watu waliobainika kuwa Makampuni yamefanya makosa hayo zimeshatekelezwa.

(b) Kwa kuwa ni muda mrefu sasa na kutukosesha mapato. Jee, Wizara haioni kwamba iko haja ya kuwataka watu hao pamoja na adhabu hiyo ya kufutiwa vibali vya kazi na ukaazi, iko haja ya kulipa fedha ambazo wamezifanyiwa udanganyifu kwa muda wote huo. Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye kipengele (a) na (b) kama ifuatavyo.

(a) Mhe. Mwenyekiti, katika operesheni yetu tunayoifanya kwa wale ambao wamebainika na makosa haya tayari watu hawa wameshaanza

kuchukuliwa hatua zikiwemo kama nilivyojibu katika swali mama ikiwemo kuwaamuru kwamba hisa hizi waziuze kwa wazawa.

(b) Wizara inaona.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwanza nimshukuru sana Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mwanana na naomba kumuuliza swali moja tu dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kamisheni ya Utalii ina Bodi inayosaidia uratibu wa shughuli mbali mbali za utalii ambapo Bodi hii inaingiza hao wadau wenyewe waliozungumzwa hapa na kuibua vitu vingi sana.

Sasa ni lini Bodi hii katika mwaka wa Fedha 2016/2017 ilikutana na kusaidia kuratibu shughuli hizi za kiutalii ambazo changamoto zake Mhe. Mwenyekiti, pale kazizungumzia. Ninakushukuru sana Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu swali lake Mhe. Miraji Khamis Mussa kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nakiri kwamba katika Kamisheni ya Utalii ipo Bodi ambayo inashughulikia mambo haya ikiwashirikisha hizi Jumuiya ambazo tumetaja hapa za watembezaji wa wageni.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Mwakilishi kwamba Bodi hii kwa mwaka huu wa fedha bado haijaanza kufanya kazi kwa sababu uteuzi wake haujakamilika rasmi. Kwa hivyo, itaanza kazi rasmi pale uteuzi wake utakapokamilika na kuendelea kuwapa ushauri na kushirikiana na Jumuiya hizi ambazo zinasafirisha na kutembeleza wageni.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Ali Khamis Bakar: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii kuweza kuuliza swali la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naipongeza Wizara ya Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo kwa kazi kubwa ambayo wanaifanya kwa kututolea taarifa mbali

mbali ambazo tunazipata katika Zanzibar hii. Pia nampongeza Mhe. Naibu Waziri kwa majibu mazuri ambayo anatupatia.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumuuliza swali moja la nyongeza kama ifuatavyo.

Ni hatua gani ambazo mtazichukua ikiwa mtagundua watu ambao wamefanya udanganyifu.

Mhe. Naibu Waziri wa Habari, Utalii, Utamaduni na Michezo: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu swali lake la nyongeza Mhe. Ali Khamis Bakar kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, hatua ambazo tutazichukua pindi watu ambao watabainika kufanya udanganyifu kwanza ni kuwazuia leseni na wasiendeshe biashara hii na pia wafuate taratibu ambazo Sheria ya Utalii imetaka zifuatwe kwa mujibu wa Sheria yetu ya Utalii.

Ahsante Mhe. Mwenyekiti. (*Makofi*)

Nam. 53

Madeni ya Serikali kutoka Taasisi Binafsi

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza**:-**

Pamoja na kazi nzuri inayofanywa na Wizara ya Fedha katika harakati zake za kukusanya mapato na kuratibu shughuli zote za fedha za ndani na nje ya nchi bado taasisi mbali mbali za Serikali zinadai madeni makubwa katika taasisi binafasi.

a) Je, Serikali imechukua hatua gani kwa Kampuni ya *Zantel* na *Zanzibar Food* ya Malik Faraji kwa madeni yanayodaiwa hadi sasa.

b) Je, ni jumla ya kiasi gani cha fedha Kampuni hizo zinadaiwa na Serikali.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu**:-**

Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake namba 53 lenye kifungu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

a) Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi kuwa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya uongozi wa Dkt. Ali Mohamed Shein, kupitia Wizara ya Fedha na Mipango na taasisi zake za Mamlaka ya Mapato *TRA* na Bodi ya Mapato *ZRB*, imeongeza jitihada za ukusanyajaji wa mapato ya ndani ili kuimarisha uwezo wa Serikali kutoa huduma bora kwa wananchi. Ni kweli pia kuwa miongoni mwa jitihada hizo ni kufanya ukaguzi *tax audit* kwa walipakodi ili kujiridhisha kuwa wametimiza kikamilifu matakwa ya Sheria za Kodi. Chini ya utaratibu huo, aghlabu *TRA* na *ZRB* hugundua kodi ambayo haikulipwa na hivyo kutoa madai kwa mlipakodi husika. Hadi mwisho wa mwezi Januari 2017, *ZRB* inawadai walipakodi saba jumla ya TZS 3.45 bilioni na wengine kumi jumla ya Dola za Kimarekani 161,878.82.

Mhe. Mwenyekiti, katika kukomboa kodi hizo, kwa kawaida Serikali kupitia *ZRB* huchukua hatua za kudai kodi hiyo kwa mlipa kodi husika na kunapojitokeza ugumu wa kulipwa, huchukua hatua zaidi za kukomboa zikiwemo za kufunga biashara ya mlipa kodi hadi deni hilo lilipwe au kumtaka mtu mwengine mwenye fedha za mlipa kodi kulipa deni hilo moja kwa moja *ZRB* au pia hutumia njia ya kukamata mali au hesabu za Benki za mlipa kodi husika na kudai kodi hiyo kupitia Mahkama.

b) Mhe. Mwenyekiti, ni kweli pia kuwa Kampuni za *Zanzibar Telecom Ltd* (*Zantel)* na Kampuni ya Malik Faraji ni walipa kodi waliosajiliwa na *TRA* na *ZRB* na kuwa Kampuni ya *Zantel* ni miongoni mwa Kampuni zinazofanyiwa ukaguzi. Hata hivyo, kama tunavyofahamu, utoaji wa taarifa za mlipa kodi unaweza kuathiri sana mwenendo wake wa biashara, uwezo wake wa ushindani na kwa mlipa kodi aliyesajiliwa katika soko la hisa, linaweza pia kuathiri thamani ya hisa zake. Hivyo ni utaratibu wa kawaida kwa nchi nyingi kukataza taarifa za mlipa kodi mmoja mmoja kutolewa kwa mtu mengine au kutolewa hadharani.

Mhe. Mwenyekiti, kwa Zanzibar, Kifungu cha 13 cha Sheria ya Bodi ya Mapato Namba 7 ya 1996 na kifungu cha 49 cha Sheria ya Usimamizi na Utaratibu wa Kodi kwa maana ya *Tax Administration Procedure Act* Sheria Namba 7 ya mwaka 2009, vinakataza mtu yeyote kutoa hadharani taarifa ya mlipa kodi mmoja mmoja. Kwa sababu hizi za kisheria, naomba nisijibu hadharani masuala ya Kodi ya Kampuni ya *Zantel* na Kampuni *ya* Malik Faraji au kampuni nyengine yoyote.(*Makofi*).

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja mazuri kabisa ya Mhe. Waziri wa Fedha nimpongeze kwa kunijibu swali hilo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli katika majibu yake amesema kwamba serikali inadai jumla Bilioni TZS 3.45 na inadai Dola 161,878.82 ni pesa nyingi sana kwa nchi hii.

a) Je, Wizara yako ina mpango gani kabambe wa kuona kwamba fedha hizo zinapatikana basi angalau nusu au robo.

b) Umesema kwamba kujibu hadharani ni makosa kwa kitaratibu na kwa mujibu wa sheria uliyozitaja hapo. Je, utakuwa uko tayari kunijibu masuala hayo kwa faragha.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba swali (b) alirudie.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe rudia swali la (b).

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana. Katika majibu yake Mhe. Mwenyekiti, amesema ni kinyume cha utaratibu, hupaswi kutaja madeni ya kodi hadharani. Jee, utakuwa tayari kunijibu masuala hayo kwa maandishi au faragha mimi na wewe.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la nyongeza la Mhe. Abdalla Maulid Diwani lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Jitihad kubwa inafanywa kupitia chombo chetu cha *ZRB* kuwafuatilia hawa wote wanaodaiwa na sisi tunaamini kwamba fedha hizo zitapatikana kwa ukamilifu wake. Na kama nilivyosema katika jibu la swali mama ni kwamba zipo njia tofauti zinazotumika. Zitatumika njia ya kwanza za kuwasiliana nao, ikishindikana kama wana fedha kwa watu wengine kuzitafutia utaratibu fedha hizo zikalipwa moja kwa moja *ZRB*, lakini iwapo itashindikana basi kufunga biashara zao, lakini hata ikishindwa hiyo basi kwenda mahakamani. Kwa maana hiyo njia hizo zinafanywa zitafuatwa. Kwa hivyo, ningeomba tu wahusika wote wanaodaiwa kutumia njia za busara ili kuhakikisha kwamba madeni yao wanayasawazisha bila ya kuchelewa zaidi.

b) Lakini hili la pili nilijibu kwa mujibu wa Sheria inakatazwa kabisa kutoa taarifa kwa mtu mwengine, lakini vile vile kuzitoa taarifa hizo hadharani hii ni kwa mujibu wa Sheria ambazo sheria hizi tumezitunga ndani ya Baraza hili. *(Makofi)*

Mhe. Simai Mohammed Said: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kuniona na mimi. Ningependa nimuulize Mhe. Waziri swali moja tu la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa Kampuni ya *Zantel* huko nyuma umiliki wake ulikuwa pamoja na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, pamoja na *Etisalat* na baada ya *Etisalat* kuamua kuuza hisa zao, wakati huo hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zilikuwa asilimia 18, baada ya kununuliwa na *Millicom* au wenyewe ndio hao wenye *Tigo* pia, hisa za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar zimepungua kwenda 15.

a) Je, ni sababu gani za msingi zilizosababisha hisa zetu kupungua wakati tuna Wajumbe wawili wa Bodi katika Kampuni hii yetu ya simu ya *Zantel*.

b) Katika mwaka wa fedha 2013 Waziri wa Fedha hapa alikiri juu ya mkataba wa Kampuni ya *Zantel* pamoja na serikali hasa katika suala la kutumia *Fiber Optic* ambayo imetandikwa katika visiwa vyetu vya Unguja na Pemba. Katika mkataba huo hadi leo ni kiasi gani cha fedha ambacho serikali imeweza kufaidika juu ya mkataba huo, ambapo serikali imewekeza asilimia mia juu ya mia katika hiyo *Fiber optic*. Ahsante.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Simai Mohammed Said swali lake la nyongeza lenye vifungu (a) na (b) kama ifuatavyo.

a) Mhe. Mwenyekiti, kuhusu hisa za serikali ni kweli kama alivyosema Kampuni hii mwanzo ilikuwa ikimilikiwa na Kampuni ya *Etisalat* na SMZ, na SMZ ilikuwa na hisa ya asilimia 18. Lakini mara baada ya kampuni hii, *Etisalat* kuuza hisa zake wenye Kampuni ya *Millicom* kulihitajika kuongeza mitaji kwenye Kampuni hii ya *Zantel* na kutokana na kwamba SMZ haikuweza kuongeza fedha zake kwenye Kampuni ya *Etisalat* bila shaka yoyote hisa za SMZ zilipungua. Kwa hivyo, *dilution* ilitokana pale palipotokezea kuongezeka kwa mtaji katika Kampuni ya *Etisalat* na SMZ haikuongeza mtaji huo. Kutokana na sababu hizo hisa hizo zilipungua kutoka asilimia 18 kuja asilimia 15 na hizo ndio sababu za msingi zilizotokezea kutokea *dilution* za hisa za SMZ.

b) Lakini suala jengine ni kweli kuna mkataba baina ya SMZ na Kampuni hii ya *Zantel* katika matumizi ya mkonga *fiber optic* na niseme

kwamba kutokana na matatizo yaliyotokezea ambayo tumeshayazungumza muda mrefu sana katika Baraza hili, la kwamba Kampuni ilipokuwa ikimilikiwa na Kampuni ya *Etisalat* na SMZ haikuweza kufanya vizuri. Kulikuwa na *conditions* nyingi ikiwemo moja kuwekeza katika kuunga huu mkonga wetu uliopita baharini na kumalizia na Pemba hiyo kazi haikufanyika. Kwa maana hiyo Kampuni hiyo haikuweza kuuza ile *space* ya ziada iliyotakiwa kuuzwa na kampuni hii kwa makampuni binafsi. Kutokana na sababu hiyo hakuna faida yoyote iliyopatikana, iliyowezesha kupata mapato ya serikali katika kipindi hiki.

Mhe. Mwenyekiti, lakini naomba tu kumjibu Mhe. Simai Mohamed kwamba hivi sasa chini ya umiliki wa *Millicom* na SMZ, kampuni hii imeanza kufanya faida na kutokana na faida hiyo tumeona tuna mwanga wa kwamba sasa serikali inaweza kufaidika kutokana na hisa zake, na kutokana na kwamba kampuni hii tayari inafanya faida.

Vile vile kuna kamati maalum iliyoundwa na serikali na kamati hii inafanyakazi ya kupitia mkataba baina ya Kampuni ya *Zantel* na SMZ, na itatoa mapendekezo yake ili kuelewa au kuweza kupata uhakika wa kwamba maslahi ya SMZ na maslahi ya Zanzibar yanalindwa kwa kupitia mkataba wa *Zantel* na SMZ.

UTARATIBU

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, nasimama kwa kutumia Kanuni ya 37,

Kanuni ya 37

"Waziri au Mjumbe yeyote anayeulizwa swali ambalo ana madaraka nalo atakuwa na wajibu wa kujibu swali hilo kwa ukamilifu, kwa usahihi na kwa ufupi isipokuwa kwamba swali aliloulizwa Waziri mmoja linaweza kujibiwa na Waziri mwengine au na Mwanasheria Mkuu".

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nikiri majibu aliyotoa Mhe. Waziri ni mazuri, lakini bado napata utata, kwa sababu wakati nazungumzia suala la hisa...

Mhe. Mwenyekiti: Sasa Mhe. Mjumbe, Kanuni inasema kama amejibu kwa usahihi na wewe umethibitisha. Sasa usitengeneze swali jengine. Kama umeridhika kwamba amejibu vizuri.

Mhe. Simai Mohammed Said: Mhe. Mwenyekiti, naomba unifahamu, naomba nimalize basi.

Mhe. Mwenyekiti: Umesema kwamba amejibu vizuri na ndio Kanuni inavyosema.

Mhe. Simai Mohammed Said: Nataka niweke kitu sawa. Sijakusikia.

Mhe. Mwenyekiti: Kwa hivyo, tuendelee. Wewe kaa tu Mhe. Waziri ameshajibu. Umeridhika kwamba amejibu vizuri ndio jawabu uliotoa. Kwa hivyo, kaa chini Mhe. Mjumbe. Swali linaendelea. Mhe. Wanu swali la nyongeza.

Mhe. Wanu Hafidh Ameir: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kumuuliza Mhe. Waziri swali moja la nyongeza. Kwanza nimsifu Mhe. Waziri kwa majibu yake mazuri ya ufasaha na yenye kufahamika kabisa. Lakini ningeomba nimuulize swali moja la nyongeza.

Kwa kuwa wakati anamjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani alijibu kwamba Sheria zinakataza kutoa taarifa hadharani, lakini kwa mujibu wa Sheria zetu Mwakilishi ana haki ya kupata taarifa yoyote ambayo anaitaka *as long as* taarifa ile haitumii vibaya, lakini anaitumia kwa maslahi ya umma kwa ujumla.

Jee, Mhe. Waziri wa Fedha kukataa kumuwekea wazi *information* ambayo Mhe. Abdalla Maulid Diwani ameiomba, jee haoni kama anakwenda kinyume na fursa, yaani na *privileges* ambazo Wawakilishi wanatakiwa kuwanazo, mbali na Sheria ambazo ame-*note* kwamba mtu yeyote, Mwakilishi sio mtu yeyote.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Mwenyekiti, naomba kujibu swali la Mhe. Wanu Hafidh Ameir kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nilieleza kwamba Sheria zetu, Sheria iliyoanzisha Bodi ya Mapato inakataza kabisa kutoa taarifa za mlipa kodi kwa mtu mwengine ama hadharani. Hilo moja.

Lakini vile vile Sheria yetu ya *TAPA* nayo inakataza hivyo hivyo na Sheria nyingi duniani, nchi nyingi duniani zimeweka utaratibu huo na yapo mambo ambayo nimeyasema kama tutatoa taarifa hizo, hizi kampuni zina washindani wao, zisije zikatumika taarifa hizi vibaya. Ningewaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi kwenye hili tusijiingize tukaja tukawa tunatumika katika kufanya

biashara au ushindani wa kibiashara na makampuni hayo tutakuwa tunakwenda kinyume na Sheria.(*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, lakini kwa kupitia suala hili lililoulizwa ningemuomba tena Mhe. Abdalla Maulid Diwani, kukubaliana na sisi kwamba suala hili tunalifanyia kazi, hizi kampuni zote mbili tunazungumza nazo. Kwa hivyo, katika mazungumzo hayo ni vyema wakatustahamilia, wasiombe taarifa hizo mpaka pale tutakapokamilisha mazungumzo na walipa kodi hao. *(Makofi)*

Nam. 96

Makampuni ya Nje Kulipa Kodi Katika Sekta ya Utalii

Mheshimiwa Omar Seif Abeid - Aliuliza:-

Kwa kuwa sekta ya utalii inagusa sehemu nyingi zenye kuingiza mapato na kwamba kuna watu wengi wanajishughulisha na kubeba na kuwatembeleza wageni katika sehemu mbali mbali, ambapo watu hao hupata pesa nyingi kuliko mamalishe ambao wao hulipa kodi ili kuchangia pato la taifa la ndani ya nchi. Kwa kuwa Makampuni yaliyoko nje yanayojishughulisha na kuwaleta wageni hapa Zanzibar malipo yake hufanywa huko huko nje jambo ambalo linatukosesha mapato.

a) Je, Serikali imechukuwa hatua gani kuhakikisha kwamba kila mtu au taasisi inayojishughulisha na biashara za kuingiza au kutembeza wageni wanalipa kodi ipasavyo ili kuchangia pato la Taifa.

b) Je, Serikali kwa kushirikiana na *ZATI* wana mpango gani wa kufahamu ni Makampuni Mangapi ya watu wanaoingiza na kutembeza watalii.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango - Alijibu:-

Mhe. Mwenyekiti, kabla ya kujibu swali nambari 96 lenye vifungu (a) na (b) la Mhe. Mjumbe, naomba kutoa maelezo ya jumla kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, ni kweli kuwa utaratibu wa huduma za utalii unahusisha wadau wengi, wakiwemo Watembeza Wageni *(Tour Operators)* na mawakala wa safari wa nje ya nchi, Mashirika ya ndege, watembeza wageni wa hapa nchini, mahoteli na watoa huduma wengine wa ndani ya nchi. Ni kweli pia kuwa watoa huduma walioko nje nchi hulipwa fedha zao huko huko wanakotoa

huduma hizo kwa watalii wanaokuja nchini. Mhe. Mwenyekiti, serikali inasimamia kodi zinazohusiana na huduma zinazotolewa nchini kutoka kwa walipa kodi waliosajiliwa nchini.

Baada ya maelezo hayo ya jumla, sasa naomba kujibu swali la Mhe. Mwakilishi kama ifuatavyo:-

a) Hatua zinazochukuliwa na serikali katika kuhakikisha kila mtu au taasisi iliyopo nchini na kutoa huduma za utalii analipa kodi ni pamoja na :-

   i. Kutakiwa kukata leseni kutoka Kamisheni ya Utallii;
   ii. Kuwasajili kwa ajili ya kulipa kodi anayostahiki (*VAT* au Kodi za Kutembeza Wageni kutegemeana na mauzo yake;
   iii. Kutakiwa kuwasilisha "Return" kila mwezi kwa mauzo aliyofanya na kulipia kodi anayostahiki;
   iv. Kufanyiwa makadirio ya kodi ya Mapato na kutakiwa kulipa kila unapofika muda (robo mwaka);
   v. Kuchukua hatua za ukaguzi na usimamizi wa sheria (*law enforcement*) kadri inavyohitajika zikiwemo kutakiwa kupata Hati ya Kodi *(Tax Clearance*) kila mwaka kabla ya kupata leseni mpya;
   vi. Kufanya mazoezi maalum kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi kubaini watu au Taasisi zisizokwepa kulipa kodi zinazostahiki.

b) Mhe. Mwenyekiti, serikali kupitia Kamisheni ya Utalii na Bodi ya Mapato inafahamu idadi ya Kampuni zinazoingiza na kutembeza watalii hapa nchini.

   Kwa mujibu wa taarifa za Kamisheni ya Utalii makampuni ya wanaotembeza watalii, yale yaliyokuwa *registered* nchini ni 239. Aidha, zipo gari ambazo zinazochukua watalii *private hired* zipatazo 600.

Nam. 59

Ukosefu wa Soko la Kuuzia Samaki Ziwani

Mhe. Suleiman Makame Ali - Aliuliza:-
Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi hii, kabla ya kujibiwa swali hili ningeomba wizara inahohusika, kwa sababu nililipeleka wizara ya Mhe. Haji Omar Kheir na nikaenda kufanya marekebisho. Sasa ningeomba kwa vile Mhe. Waziri yupo anijibu kwa faida ya wananchi. Nililipeleka kwenye Wizara ya Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, lakini lilipelekwa wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwa hivyo, kwa vile Waziri yupo ningeomba nikapata majibu.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe hebu elezea tena vyema swali lako.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Swali langu hili nililipeleka kwenye Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ na nikaenda kufanya marekebisho, lakini cha kushangaza limerudi tena kwenye ile Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Sasa kwa vile serikali ipo, hususan Mhe. Waziri mwenyewe yupo ningeomba kupata majibu kwa faida ya wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Mjumbe lakini sasa kwa utaratibu swali mapema ili Waziri ajiandae. Kama Waziri husika uliyemtaja atakuwa yuko tayari basi tutamuomba ajibu, kama hayuko tayari kwa swali hili itakuwa hawezi kujibiwa. Mhe. Waziri uko tayari swali kulijibu.

Mhe. Waziri wa NChi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa utaratibu ni kwamba swali linapelekwa kwa wizara husika, Baraza la Wawakilishi kama alikwenda Mhe. Mjumbe kupeleka marekebisho basi Baraza ndio liliwajibika kuniletea mimi au kuleta kwenye Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa. Sasa kwa kuwa lilikwishafika Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, wacha lijibiwe wizara hiyo, kama kuna masuala yanayohusu Tawala za Mikoa basi Waziri wa Ofisi ya Rais yupo nitaelezea lakini kwanza lijibiwe na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante Mhe. Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi - Alijibu:-

Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako napenda kumjibu Mhe. Mjumbe swali lake nambari 59 kama ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kuna masoko ya aina mbali mbali yanayojengwa kwa nia njema na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa ajili ya kuwahudumia wananchi wake kutoka taasisi mbali mbali. Aidha wizara yangu inahusika kwa ujenzi wa masoko maalum ya kuuzia samaki kupitia mfuko wa serikali pamoja na wahisani mbali mbali, pale ambapo wananchi wanapohitaji. Masoko hayo ambayo ndio tunayoyajenga ndio tunaweza kuyafanyia ukarabati, kwa kupitia Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi lakini pale bajeti inaporuhusu.

Mhe. Mwenyekiti, soko la Ziwani analolizungumzia Mhe. Mwakilishi analolizungumzia Mhe. Mwakilishi linasimamiwa na Halmashauri ya Wilaya ya Chake Chake, hivyo ninamshauri Mhe. Mjumbe awasiliane na Mamlaka husika ya Halmashauri hiyo kwa kupata ufumbuzi wake, na akubali kutoa mashirikiano ya hali na mali kwa Halmashauri hiyo, ili wananchi wetu wapate huduma hiyo na serikali kuweza kupata mapato yake kama inavyostahiki. Ahsante.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba kuuliza swali dogo la nyongeza.

Wananchi wale kwa siku nyingi wanateseka kwa kufuatia huduma ile Chake Chake na maeneo mengine. Je, ni lini soko lile watajengewa ili kupatikana mapato ya serikali yanayotokana na eneo lile pale na wananchi kuondokana na usumbufu.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi kwamba kama nilivyojibu kwenye jibu langu mama kwamba pale bajeti itakaporuhusu basi tutafanya ukarabati. Lakini vile vile uwasiliane na Halmashauri husika ili uweze kupata maelekezo zaidi kama tulivyosema. Wizara ya Kilimo inajenga masoko maalum.

Mhe. Ali Suleima Ali: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, Wizara ya Kilimo, Mifugo na Uvuvi kazi yake kubwa kuhakikisha kwamba wananchi wanakwenda kuvua na kupata samaki kwa ajili ya manufaa ya wananchi, lakini katika suala lililoulizwa hapa baada ya wavuvi hao kurudi huwa wanapata adha kubwa sana ya kuuza samaki wao sehemu ambapo panaridhisha wanachukua hatua kwenda Chake Chake mbali na hapo wanapotoka inakuwa usumbufu.

Je, kwa kuwa Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuti ni muhusika wa uvuvi, Tawala za Mikoa kupitia Halmashauri ni taasisi ambayo inahusika na masoko, yeye kama Wizara ya Kilimo ina mpango gani wa kushauriana na Halmashauri ili wahakikishe kwamba soko hilo linapatikana kuondoa usumbufu huo.

Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake kama ifuatavyo.

Tutakaa na Wizara husika ili kuweza kutatua tatizo hili kwa kusaidiana Wizara hizi mbili. *(Makofi)*

Mhe. Panya Ali Abdalla: Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mzuri ya Mhe. Waziri naomba kuuliza swali moja dogo la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kuwa soko hili limekodishwa kwa mtu na analiendesha ina maana fedha anapata anapeleka Halmashauri. Jee, Halmashauri kwa kuwa inapata fedha za huyo mkodishwaji kwa nini wasifanye juhudi ya kulitengeneza soko hili au wana mpango gani wa kulitengeneza soko hili kwa kuwa bado linaendelea na huduma.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum ya SMZ: Mhe. Mwenyekiti, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama hivi ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, soko linalozungumziwa ni soko la Ziwani na kama limekodishwa ni usahihi kwamba mapato yake yatakuwa yanakwenda Halmshauri. Hivyo niseme kwamba katika mipango yake ya Halmashauri ya kuliendesha soko hili itategemea mkataba namna ulivyoandikwa. Mkataba uliopo ni kwamba Halmashauri itapokea kodi na matengenezo ya soko hili yatafanywa na mkodishwaji. Kwa hivyo tutaangalia kama Halmashauri ama Mkodishwaji amevunja vipengele vya mkataba, Halmashauri itafanya maamuzi mengineyo

Kama mkodishwaji atakuwa amefanya yeye makosa ya kuvunja mkataba basi vile vile Halmashauri itakaa kupitia Wanasheria wa Serikali ili kuona tunavunja huo mkataba na Halmashauri iweze kuchukua nafasi yake ya kulitengeneza soko hilo, ili wananchi waweze kupata huduma kama ilivyokusudiwa.

Nam. 25

Ufadhili wa Benki ya Damu

Mhe. Abdalla Maulid Diwani - Aliuliza:

Benki ya Damu ilikuwa inafadhiliwa kwa 100% ambapo kwa sasa taasisi ya *CDC* (Marekani) wameshaondoa ufadhili wao na hivyo kitengo hicho hakiwezi kujiendesha kwani kina mahitaji mengi ikiwemo ununuzi wa vipimo, vifaa, mafuta, posho za wafanyakazi na kadhalika.

(a) Je, Wizara ina mpango gani wa kutafuta Mfadhili mwengine ambae anaweza kusaidia Benki hiyo.

(b) Je, Wizara ina mpango gani wa kuongeza wafanyakazi ili kupunguza uhaba na ugumu wa kazi kutokana na kusimamishwa kwa ufadhili waliokuwa wakilipa mishahara wafanyakazi waliohamishwa.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:

Mhe. Menyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mwakilishi swali lake Nam. 25 lenye kifungu (a) na (b) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa napenda nichukue nafasi hii kwa niaba ya Wizara yangu nitoe shukurani za dhati kwa Mheshimiwa Abdalla Diwani Muwakilishi wa Jimbo la Jang'ombe pamoja na Mhe. Mkuu wa Mkoa wa Mjini/Magharibi Mhe. Ayoub Mohammed Mahamoud Jecha na kikundi cha GA pamoja na Dkt. Juma Abdalla Mabodi, kwa kuhamasisha siku ya uchangiaji damu na kuleta hamasa na mafanikio makubwa katika matemebezi ya uchangiaji wa damu uliofanyika hapo katika Mnara wa Mapinduzi uliopo Mwembekisonge.

Mhe. Mwenyekiti, tunawashukuru sana kwa dhati Waheshimiwa hawa na tunawaomba Waheshimiwa wote Wawakilishi kufanya kampeni kama hii katika majimbo yenu na kwa upande wetu Wizara ya Afya tunaahidi kuwapa mashirikiano ya kutosha.(*Makofi*).

a) Mhe. Mwenyekiti, Banki kuu ya Damu haikuwa inafadhiliwa asilimia mia moja na *CDC* kwani wafanyakazi wote wa Kitengo hicho mpaka sasa ni wafanyakazi wa SMZ na wanalipwa mishahara na SMZ, lakini pia jengo pamoja na baadhi ya vifaa ni vya SMZ, *CDC* ilikuwa inatoa *top up allowance*, yaani posho ya nyongeza ya mishahara kwa wafanyakazi hao.

Mhe. Mwenyekiti, ili kufanikisha shunguli za utendaji za Mpango wa Damu Salama, Wizara ya Afya imeomba katika bajeti ya shilingi 150,000,000/- kwa ajili ya uendeshaji wa shughuli hizo. Aidha Wizara inaendelea na mchakato wa kutafuta wahisani wengine ili waweze kusaidia eneo hilo hilo. Hivi karibuni taasisi ya *Global Fund* imekubali tena kushirikiana nasi.

Mhe. Menyekiti, kwa sasa Wizara inaendelea na ajira zake kwa kada za madaktari na kada nyengine za juu za afya, kwa mfano Wafamisia, Madaktari n.k. Hivyo nafasi kwa kada hizo ziko wazi. Aidha pindipo Wizara ikiona ipo haja ya kuongezewa wafanyakazi katika kitengo hicho basi itafanya hivyo kwa kupitia Kamati ya kupanga wafanyakazi *(Deployment Committee)* ya Wizara ya Afya.

Mhe. Abdalla Diwani Maulid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipatia nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Pamoja na pongezi nilizopewa katika kadhia nzima ya uchangiaji wa damu napenda kuliambia Baraza lako tukufu kwamba nafahamu nilivyochangia mpaka tukafikia pale, na hivi karibuni inasaidikiwa karibuni wagonjwa sita walifariki dunia kwa ukosefu wa damu, ilitokana na vifaa ambavyo vilikuwa vinadhaminiwa na *CDC*.

a) Je. Wizara yako imepata hasara ya namna gani baada ya udhamini huu kuondoka.
b) Wizara yako imepata faida gani baada ya mradi huu wa *CDC* kuondoka.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Abdalla Maulid Diwani swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, Waswahili wanasema, "Paukwapo paukwa". Kwa hivyo kwa kuondoka kwao moja kwa moja hasara itakuwepo lakini na faida kubwa pia ipo, kwa sababu wafanyakazi ambao wanalipwa mishahara na SMZ waliopo katika kitengo hicho wanaendelea na kazi na kwa kweli hakuna siku ambayo wamesimama kutokufanya kazi ya ukusanyaji na utafutaji wa damu

salama katika maeneo mbali mbali, wafanyakazi katika kitengo hicho wanafanya kazi pale Ofisini kwa kuchukua damu za wale ambao wanakuja.

Lakini pia huwa wanatoka asubuhi kwenda katika maeneo mbali mbali kuhamasisha na kupata michango ya damu za wananchi na kuleta katika kitengo hichi kwa manufaa ya kuwasaidia wananchi wetu ambao wagonjwa na watakuwa wanahitaji damu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza.

Mhe. Mwenyekiti, ukweli usiofichika kwamba Zanzibar kumeanza kujitokeza upungufu wa damu na hii kutokana na kukosekana kwa basi lililokuwa likitumika...

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa naomba ukae kidogo. Waheshimiwa Wajumbe muda wa maswali umemalizika, kwa hivyo ninaongeza dakika kumi na tano kwa mujibu wa kifungu cha Kanuni cha 39(3) tunaendelea.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, swali langu Zanzibar ukweli usiofichika kumeanza kujitokeza upungufu wa damu kwa kiwango kikubwa na kama tunavyojua damu ni uhai wa mwanadamu na hii inatokana na kukosekana kwa basi lililokuwa likitumika kukusanyia damu kwa kipindi kisichopungua mwaka basi lile haliendi limeharibika halifanyi kazi.

Jee, lini na taarifa hizi za kukosekana kwa basi ziko wizarani kwenu, lini Wizara yako itanunua basi jengine kwa madhumuni ya kukusanya damu ili watu wetu tunapokuwa tunaumwa tuwe tuna uhakika wa kupata damu hapa nchini kwetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mhe. Mwenyekiti, uhaba wa damu hausababishwi tu na uharibifu wa basi lile, isipokuwa pia unasababishwa na uhamasishaji mdogo ambao hata nyinyi Waheshimiwa Wawakilishi tuliwaomba muhamasishe wananchi wenu katika kuchangia damu katika sehemu ambazo wapo wapo, Sasa basi lile Wizara yangu sasa hivi imo katika mpango mkubwa wa kulifanyia matengenezo pindipo tutafanikiwa kupata hizi pesa, lakini pia tulifanya mazungumzo na wenzetu wafadhili wa China ili kuona ile hali kwamba watasaidia

kulitengeneza au vipi tuna tamaa kubwa kwamba huenda wakatupatia basi jipya.

Kwa hivyo tunawaomba Waheshimiwa Wawakilishi na nyinyi pia mashirikiano yenu ya kutosha ili kufanikisha kuwahamasisha wananchi kuchangia damu, kwa sababu basi peke yake halitosaidia kama wananchi hawatopata hamasa ya kutosha ya kuweza kujitokeza kikamilifu katika kuchangia damu.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja tu la nyongeza.

Kwa kuwa Mhe. Waziri alijibu kuwa Serikali inachangia au inatoa fedha pamoja na wafadhili katika kitengo hichi muhimu katika kuokoa maisha ya watu, kwa mwaka wa fedha 2016/17 tulipitisha bajeti kwa Taasisi hii ni kiasi gani cha fedha kimepatikana hadi sasa ili sisi Wawakilishi tupime kile kiwango cha ufanisi katika uendeshaji wa taasisi hii.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, naomba nimjibu Mhe. Miraji Khamis Mussa swali lake la nyongeza kama ifuatavyo.

Mheshimiwa kiasi halisi cha fedha ambazo zimepatikana kwa kushughulikia jambo hili nakuomba radhi nitakujibu kwa maandishi kwa sababu inabidi nikupe *exactly amount of money* na hapa sikuweza kuikariri, kwa hivyo kwa hili naomba nikujibu kwa maandishi.

Nam. 17

Uharibifu wa Bomba la Maji Uliosababishwa na Ujenzi wa Barabara

Mhe. Masoud Abrahman Masoud - Aliuliza

Ujenzi wa barabara za ndani katika Shehia ya Bumbwisudi eneo la Popo kwenda Mambosasa umesababisha uharibifu wa bomba la maji na kuwasababishia wananchi usumbufu kwa kukosa maji safi na salama.

Jee, ZAWA wanazo taarifa za uharibifu wa bomba hilo na kama wanazo wana mpango gani wa matengenezo ya bomba hilo ili huduma ya maji safi na salama iweze kurejea kwa wananchi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira - Alijibu

Mhe. Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake nambari 17 kama ifuatavyo:-

Lakini kabla ya kujibu swali lake, naomba nianze kwa kumshukuru kwa dhati kabisa Mhe. Mwakilishi kwa kutupatia taarifa, kupitia swali lake alilouliza ya kuvurugwa kwa mabomba ya maji kutokana na ujenzi wa miundombinu ya barabara katika jimbo lake. Aidha namuomba sana Mhe. Mwakilishi ikiwa yeye mwenyewe binafsi au wananchi wake wanapokuwa na taarifa kama hizo wasiache kuwasiliana na taasisi husika ambayo ni Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa kila inapowezekana.

Mhe. Mwenyekiti, sasa naomba niendelee kumjibu swali kama ifuatavyo.

Taarifa za uharibifu wa bomba hizo zimepokelewa na Mamlaka ya Maji tayari imekwenda kulikagua eneo husika na kubaini uharibifu wa miundombinu hiyo, kwa kuwa uharibifu huo umetokana na ujenzi wa barabara iliyosimamiwa na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi chini ya mradi wa *MIVAP*. Mamlaka tayari imewaandikia barua Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa kutafuta namna na jinsi ya kulitatua tatizo hilo.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, pamoja na maelezo ambayo kayatoa Mhe. Waziri majibu ambayo hayakuridhisha kwa sababu suala hili lina zaidi ya mwaka mmoja tokea kuvurugwa mipira hii.

a) Je, ZAWA haina ma-*inspectors* ambao wanakagua miundombinu wakati wanapojenga barabara.

b) Hii kazi ya kurudisha miundombinu ya maji baada ya ujenzi wa barabara ni jukumu la nani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake la nyongeza lenye (a) na (b).

a) Ni kwamba Mamlaka inao wakaguzi lakini inawezekana ikawa hawajafika katika sehemu husika kwa wakati muafaka, na kama nilivyokuwa nimejibu katika swali mama ni vyema tukapata taarifa ikiwa wewe mwenyewe au mwananchi wa eneo husika kwa sababu ya kusaidiana.

b) Kwa vile hii njia au barabara ilikuwa inafanywa na mradi na baada ya kutupatia taarifa hizi tumewasiliana na Wizara ya Kilimo kama nilivyokuwa nimejibu kusudi waweze kuirejesha hii hali, tayari tumekubaliana na karibu in shaa Allah itafanyika hii kazi.

Mhe. Machano Othman Said: Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba kuuliza swali moja la nyongeza lenye vifungu (a) na (b).

Wananchi wa Popo ni wananchi wa Shehia ya Bumbwisudi ambayo iko katika Jimbo la Mfenesini na sio Bububu, na kwa utaratibu wa kawaida mradi wowote unapofanyika mtenda mradi lazima kwanza kabla ya kuondoa miundombinu awasiliane na ZAWA kama anaondoa mabomba ya maji na kama umeme awasiliane na Shirika la Umeme.

a) Je, inaonesha mradi huu umefanyika bila ya kushirikishwa ZAWA na kama ni hivyo kwa nini hawakufanya makisio mwanzo.

b) Wananchi wa Popo, Bumbwisudi yenyewe pamoja na Bumbwisudi kwa Goa wanalo tatizo la maji baadhi ya siku na hawa wanapata maji kutoka kisima cha Ndagaa, lakini kwa muda mrefu wapiga maji au mafundi wa maji wa Kisima cha Ndagaa wanakataa kuleta maji Bumbwisudi kwa Goa na Bumbwisudi yenyewe kwa madai kwamba kisima cha Ndagaa ni kwa ajili ya wananchi wa Wilaya ya Kati.

   Je, huu ndio msimamo wa Serikali kwamba kisima kikiwa Wilaya nyengine wilaya nyengine wasipate. Na kama sio je, Wizara yako iko tayari kumchukulia hatua mpiga maji wa Ndagaa ili kuleta amani na kuwapatia huduma za maji wananchi wa Bumbwisudi.

Mhe. Naibu Waziri wa Ardhi, Maji, Nishati na Mazingira: Mhe. Mwenyekiti, ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Machano Othman Said swali lake lenye vipengee (a) na (b) kama ifuatavyo. Lakini Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze kujibu swali la (b) kwanza.

b) Inawezekana kukawa kuna taarifa nyengine au sababu nyengine zaidi ya hiyo ambayo umeiainisha. Lakini nikwambie kwamba Wizara yangu ipo tayari kushirikiana na wewe kubaini tatizo na kasoro aidha kwa watendaji au katika eneo husika la ukosefu wa maji katika eneo ambalo umelitaja.

a) Ni kwamba kikawaida iwe hivyo panapofanywa mradi basi wenye miundombinu husika aidha *ZAWA* au *ZECO* wanahitajika kuwepo

kusudi kushauri au kubaini kwa haraka ile kasoro ambayo itatokezea. Lakini ikitokezea bahati mbaya imefanyika kazi bila ya taasisi husika kuwepo ni wajibu wetu kurejesha huduma ile na siyo kulaumu.

Nam. 38

Uwekaji Matuta Barabarani

Mhe. Omar Seif Abeid (Kny: Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini) – Aliuliza:

Barabara ya kuingilia Skuli ya Regeza Mwendo kuna matuta (*bumps*) 3, Skuli ya Bububu matuta 3, Skuli ya Mwera kuna matuta (*bumps*) 6, Skuli ya Dunga kuna matuta (*bumps*) 4, Skuli ya Uzini kuna matuta (*bumps*) 8. Matuta hayo yanasaidia sana kupunguza mwendo wa kasi wa Madereva na kuwapa fursa wanafunzi kuvuka barabara kwa usalama zaidi.

Aidha, kutoka Kituo cha Polisi Mazizini mpaka Chukwani Jeshini kuna matuta (*bumps*) 8 barabarani ambayo hayana alama za kuwatanabahisha madereva.

(a) Kwanini Wizara haisimamii uwekaji wa matuta (*bumps*) kama hayo katika Skuli ya Fuoni, Kisauni, Maungani, Kombeni, Bwefum, Kiembesamaki Msingi na Sekondari na Skuli ya Mitondooni ili kuwasaidia Wanafunzi wa Skuli hizo.

(b) Wanafunzi wangapi wamegongwa na gari wakivuka barabara kuingia na kutoka skuli ya Kiembe Samaki kwa mwaka 2014/2015.

(c) Sheria gani ya nchi inatoa ruhusa kuweka matuta kwa baadhi ya skuli na nyengine kutowekwa matuta hayo.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji - Alijibu:

Mhe. Mwenyekiti, naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nambari 38 lenye kifungu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na Mhe. Mwakilishi juu ya utafiti alioufanya kuwa maeneo yetu yaliyowekwa matuta kwa kiasi fulani yamesaidia

kupunguza ajali. Hata hivyo, kuweka matuta katika barabara kuu si utaratibu mzuri na haupo Kisheria.

Mhe. Mwenyekiti, matuta hulazimika kuwekwa kutokana na matukio yaliyokwisha kutokea na ambayo hujirudia mara kwa mara na husababisha vifo au ulemavu kwa binadamu. Matokeo hayo hujitokeza kutokana na sababu mbali mbali zikiwemo mapungufu ya alama za usalama barabarani, ukosefu wa elimu kwa watumiaji barabara pamoja na usimamizi wa sheria za barabarani.

(a) Mhe. Mwenyekiti, Wizara yangu haijapanga kuweka matuta katika maeneo ya Skuli ya Fuoni, Kisauni, Maungani, Kombeni Bwejuu, Kiembesamaki Msingi na Sekondari na Skuli ya Mtondooni. Badala yake itaimarisha uwekaji wa alama husika pamoja na kushirikiana na Jeshi la Polisi kwa kutoa elimu ya matumizi mazuri ya barabara pamoja na usimamizi wa Sheria zinazohusika

(b) Mhe. Mwenyekiti, kwa mwaka 2014/15 ajali 23 zilitokea na kusababisha vifo vya watu watatu.

(c) Mhe. Mwenyekiti, hakuna sheria yoyote inayotoa ruhusa ya kuweka matuta kwa baadhi ya Skuli na kutoweka matuta hayo kwa Skuli nyengine.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri naomba kumuuliza swali dogo la nyongeza kama hivi ifuatavyo,

Kwa kuwa Mhe. Wazari amekiri kwamba zipo skuli zimewekewa matuta kama vile alizozitaja katika jibu lake na kwa sababu matokeo hayo ya kujirejearejea yameshajitokeza mara mara kadhaa katika Skuli ya Kiembesamaki Msingi. Kwa sababu Skuli ya Kiembesamaki ina *highway* ambayo madereva wake hupita kwa mwendo wa kasi jambo ambalo tumeshashuhudia ajali kadhaa za wanafunzi wa skuli hiyo zikitokea.

Je, serikali haioni kwamba iko sababu ya kujenga matuta katika Skuli ya Msingi ya Kiembesamaki (b) penye skuli tatu kwa pamoja pale kama ambavyo ajali zinaonyesha kujitokeza mara kwa mara pamoja na kuwa na Polisi wanaosimama pale barabarani.

Mhe. Naibu Waziri wa Ujenzi, Mawasiliano na Usafirishaji: Mhe. Mwenyekiti, ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Omar Seif Abeid swali lake kama ifuatavyo.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema mwanzo kwamba sisi huwa tunapenda sana barabara kuu zetu hizi tusiziwekee matuta, bali tunaendelea kusisitiza kwamba wananchi wafuate sheria za usalama barabarani na waendeshaji wa vyombo vile vile wafuate sheria za usalama barabarani.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kama nilivyosema Jeshi la Polisi hivi sasa limekuwa likiweka askari wake pale wakati watoto wanakwenda skuli na wakati wa kutoka. Mimi nasisitiza kwa vyombo vya usalama barabarani kuendelea kuhakikisha kwamba sehemu zile wanaendelea kuzifanyia uangalizi na Polisi wanakuwepo wakati wowote ili wale wote ambao watakwenda kinyume na sheria zetu za barabarani wachukuliwa hatua. Lakini *highway* kuweka matuta si jambo ambalo tunalipendelea sana Wizarani.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana kakae muda wa Maswali na Majibu tuliokubaliana umekwisha. Waheshimiwa Wajumbe naomba niwatangazie matangazo yafuatayo:

Waheshimiwa Wajumbe tunaarifiwa kwamba Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt Ali Muhamed Shein anatarajiwa kuzungumza na Wajumbe wote wa Baraza la Wawakilishi katika ukumbi wetu wa juu siku ya Jumapili tarehe 26/2/2017 mnamo saa 4:00 asubuhi. Shime Wajumbe wote tuhudhurie katika mkutano huo na tunatakiwa tuwe tumeshakaa katika nafasi zetu ifikapo saa 3:30 barabara asubuhi.(*Makofi*).

Tangazo jengine linalofuata kutoka kwa Kamati inayohusika. Taarifa ya Kikao cha Kamati ya Maadili. Wajumbe wote wa Kamati ya Maadili na Kinga za Wajumbe wanaombwa kukutana katika chumba cha Kamati Nam. 3 baada ya kuahirisha Kikao chetu cha asubuhi ya leo.

Pia kuna tangazo jengine kuhusu Kamati ya Mwenyekiti wa Kamati ya Mifugo, Utalii na Uwezeshaji anawatangazia Wajumbe wote wa Kamati hiyo mkutano wa chumba namba 10 baada ya maswali na majibu.

Vile vile Mwenyekiti wa Kamati ya Sheria, Utawala Bora, Idara Maalum kutakuwa na Kikao mara baada ya kumalizika kipindi cha maswali na majibu saa 4:30 katika ukumbi wa Kamati juu. Hayo ni matangazo na kwa sasa naomba niwatangazie wageni waliofika katika ukumbi wetu wa leo.

Katika ukumbi wetu tumepata wageni wafuatao, wageni wetu ni kutoka Wizara ya Uwezeshaji Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto kutoka kwa Mhe. Moudline Cyrus Castico wageni wenyewe ni kama wafuatao:

1. Ndg. Sharifa Muhammed
2. Ndg. Mohammed Yussuf
3. Ndg. Maryam Salum
4. Ndg. Aunak Nassor
5. Ndg. Ali Mohammed Suleiman
6. Ndg. Mohammed Ali Omar
7. Ndg. Mohammed Kinana
8. Ndg. Yussuf Ali Mjombo
9. Ndg. Hamad Khamis Jecha

Waheshimiwa Wajumbe hawa ni miongini mwa Wafanyakazi wa Wizara hiyo ambao wanafika kazini mapema sana. Kwa hivyo Mheshimiwa ameona awatambue na awalete hapa iwe ni kichocheo kwa wengine na wao wafanye hivyo.(*Makofi*).

Ahsanteni.

HOJA ZA RIPOTI ZA KAMATI

Muhtasari wa Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2016/2017

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako naomba niusome muhtasari wa ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi kwa Mwaka 2016/2017.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu aliyetujaalia afya na uzima na tukaweza kukutana tena hapa katika Baraza hili kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu tuliyokabidhiwa na wananchi.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati naomba ukae kidogo kwa muda nataka nimpishe Mhe. Naibu Spika anataka kuja kunipokea subiri.

(Hapa Mhe. Naibu Spika, alikalia kiti)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, endelea.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo):

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa hatuna budi kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehma mwenye kurehemu aliyetujaalia afya na uzima na tukaweza kukutana tena hapa katika Baraza hili kwa ajili ya kutekeleza majukumu yetu tuliyokabidhiwa na wananchi. Vile vile, sina budi kukushukuru wewe binafsi kwa kunipatia fursa hii kuwasilisha mbele ya Baraza hili kwa niaba ya Kamati yetu Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo, tunaomba kwa ruhusa yako Muhtasari huu usomwe sambamba na Ripoti yetu na ziingizwe kwenye *Hansard*.

Mhe. Naibu Spika, kwa dhati kabisa, tunatoa shukrani zetu kwa mashirikiano makubwa tuliyoyapata wakati wa kutekeleza majukumu yetu ya Kamati kwa uongozi wa Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi na Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na pamoja na Taasisi zote zilizo chini ya Wizara hizo ambao ndio wahusika wakuu waliofanikisha hadi Kamati yetu inawasilisha ripoti hii mbele ya Baraza lako.

Mhe. Naibu Spika, aidha, napenda kutoa shukrani zangu za dhati kwa wadau na wananchi wote wa Unguja na Pemba ambao walishiriki kikamilifu pale Kamati ilipotaka kukutana nao kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya Kamati, jambo hili liliipa faraja kubwa sana Kamati kuona ni kwa kiasi gani wananchi wapo karibu na chombo chao cha Baraza la Wawakilishi na kuthamini juhudi zinazofanywa na Wajumbe wa Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, vile vile naomba nitoe shukrani kwa Wajumbe wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo pamoja na Makatibu wetu ambao ndio waliofanikisha ufanisi na umahiri wa wajumbe katika kutekeleza majukumu yao. Naomba kwa ruhusa yako niwatambue kwa majina Wajumbe na Makatibu hao kama hivi ifuatavyo:

1. Mhe. Yussuf Hassan Iddi	-	Mwenyekiti
2. Mhe. Hamida Abdalla Issa	-	Makamu Mwenyekiti
3. Mhe. Ali Salum Haji	-	Mjumbe
4. Mhe. Bihindi Hamad Khamis	-	Mjumbe
5. Mhe. Ussi Yahya Haji	-	Mjumbe
6. Mhe. Moh'd Mgaza Jecha	-	Mjumbe

7. Mhe. Hamad Abdalla Rashid	-	Mjumbe
8. Ndg. Salum Khamis Rashid	-	Katibu
9. Ndg. Asma Ali Kassim	-	Katibu

Wizara ya Fedha na Mipango

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli kwamba Wizara hii ndio roho ya nchi yetu kwani imepewa jukubwa kubwa sana la kusimamia ukusanyaji wa mapato ya nchi na usimamizi wa matumizi ya fedha za wananchi. Kamati yetu imeridhishwa na juhudi za ukusanyaji wa mapato zinazofanywa na Wizara pamoja na Taasisi zake ikiwemo Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) na Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*) jambo ambalo limepelekea kuongezeka kwa mapato ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka ulioisha. Kuongezeka kwa mapato haya kumetokana na juhudi na mikakati ya Wizara katika kuhakikisha makadirio ya mapato yaliyokusudiwa kukusanywa yamefikiwa na Serikali. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hata hivyo pamoja na mikakati hiyo iliyowekwa Kamati yetu inaamini kuwa bado tatizo la kuvuja kwa mapato na vile vile bado yapo maeneo ya ukusanyaji wa mapato hayajafikiwa. Kwa hivyo Kamati yetu inaitaka Wizara kuongeza juhudi ya kuweka mikakati madhubuti ili kuhakikisha mapato ya nchi hayavuji na kila anayestahiki kulipa kodi basi alipe bila ya kuwa na muhali wowote.

Mhe. Naibu Spika, kuna kauli ambazo huzungumzwa na baadhi ya watu kuwa, mapato yote yanayokusanywa na *TRA*-Zanzibar hupelekwa Tanzania Bara, Lakini naomba kuchukua nafasi hii kuwaambia wananchi kuwa, mapato yanayokusanywa na *TRA*-Zanzibar yanaingia katika Mfuko Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na yanatumika Zanzibar, wanaokaa wakisambaza fikra potofu kama hizo kwa wananchi hawaelewi ukweli wa mambo na tunaomba wananchi wa Zanzibar waondoe fikra hizo na waone kuwa Muungano wetu haupo kwa kukandamiza Zanzibar bali ni kwa kuinua uchumi wa Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, katika suala la usimamizi wa fedha za umma kwa ujumla bado kuna tatizo, hii inatokana na ukweli kwamba Sheria ya Manunuzi na Kanuni zake hazifuatwi ipasavyo, na sote tunafahamu kuwa asilimia 70 ya matumizi ya fedha yanakwenda kwenye manunuzi. Ukiukwaji huu wa Sheria ya Manunuzi hupelekea upotevu mkubwa wa fedha za umma, kwani Kamati imebaini kuwa zipo baadhi ya Taasisi ambazo hufanya manunuzi hewa lakini vile vile kutokana na uhaba wa maafisa wanunuzi zipo baadhi ya Taasisi

ambazo wahasibu au washika fedha ndio wanakuwa maafisa wanunuzi. Tunaomba sana wakati itakapoanza kutumika Sheria mpya ya Manunuzi iliyopitishwa na Baraza hili iwe ndio suluhisho la matumizi ya fedha yasiyotumia utaratibu wa Sheria.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu ilifanya ziara katika mashamba ya Mipira kisiwani Pemba, katika ziara hiyo Kamati ilikutana na viongozi na wafanyakazi wanaoyashughulikia mashamba hayo ambao wameunda kikundi kinachojulikana kwa jina la *JIWEZESHE GROUP*. Kabla ya mashamba hayo kutumiwa na kikundi hiki, Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Mipango iliingia mkataba na Kampuni ya *AGROTEX* ambapo Kampuni ilitakiwa kulipa USD 100,000/- (Dola laki moja) kwa kila mwaka. Hatma ya Kampuni hii ilishindwa kulipa fedha hizo kwa Serikali kwa kipindi cha miaka minne (4) na vile vile iIishindwa kulipa mishahara kwa wafanyakazi. Hadi Kamati yetu inawasilisha ripoti mbele ya Baraza hili, Kampuni hii bado inadaiwa na Serikali USD 400,000/- (Dola laki nne) kama ni kodi ya mashamba hayo.

Wafanyakazi ambao walikuwa wanayashaghulikia mashamba haya, waliamua kujikusanya pamoja na kuunda kikundi ambacho kinajulikana kama *JIWEZESHE GROUP* kwa ajili ya kuendeleza shughuli za uvunaji wa mipira. Idhini ya matumizi ya mashamba hayo yalitolewa na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini – Pemba kupitia barua ya tarehe 10 Februari, 2016 yenye Ref: NO. MKP/K.6/3/1/VOL.VII/115 ambayo inaonekana kwenye kitabu chetu cha ripoti.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu haikuridhishwa na uidhinishaji wa matumizi ya mashamba hayo uliofanywa na Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Kwani wakati uamuzi huu unafanywa mkataba kati ya Serikali na *AGROTEX* bado haujavunjwa.

Vile vile, Kamati yetu imesikitishwa sana kuona kuwa azma ya kuanzishwa kwa mashamba haya ambayo ilikuwa ni kuinua pato la Taifa na uchumi wa nchi haijafikiwa, kwani mapato mengi ya Serikali yaliyokusudiwa kuingia katika Mfuko wa Serikali hayakuingia kama ilivyotegemewa.

Mhe. Naibu Spik, maoni na maagizo ya Kamati juu ya kadhia hii yanaonekana katika ripoti ya Kamati, lakini Kamati inasisitiza kuwa Wizara ihakikishe Kampuni ya *Agrotex* inalipa deni ambalo linadaiwa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inampongeza sana Mhasibu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kipindi kifupi alichokaa katika nafasi hii

mabadiliko yamenza kuonekana katika ukusanyaji wa mapato na matumizi ya fedha. Kamati imeridhishwa na utaratibu ulioanza kwa baadhi ya Taasisi ya kukusanya fedha kwa kupitia benki na sio kulipa *cash*, jambo hili ni moja kati ya mambo yaliyopelekea kuongezeka kwa mapato, hata hivyo Kamati yetu inamtaka Mhasibu Mkuu wa Serikali utaratibu huu wakulipia benki utumike kwa Taasisi zote za Umma ili kuziba mianya ya kuvuja mapato.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala la uwekezaji ni moja katika sekta inayosimamiwa na Wizara hii kupitia Mamlaka ya Uwekezaji na Vitega Uchumi Zanzibar (*ZIPA*), juhudi zinazofanywa na *ZIPA* zinaonekana kwani ipo miradi mingi inayoendelea ambayo imetokana na kuwepo kwa Mamlaka hii. Hata hivyo, yapo malalamiko makubwa sana juu ya utendaji wa Mamlaka hii ambapo malalamiko haya yanaleta picha mbaya katika sekta ya uwekezaji nchini. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha na Mipango kukaa pamoja na *ZIPA* kuona chanzo cha malalamiko haya yaliyopo yanasababishwa na nini, kama ni utendaji kazi wa Mamlaka au ni Uendeshaji wa Afisi ya Mamlaka. Vile vile Kamati inaitaka *ZIPA* itekeleze majukumu yake kwa uwazi kabisa ili kuepusha malalamiko na kuweza kuwavutia wawekezaji nchini.

Mhe. Naibu Spika, Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ambao upo chini ya Wizara ya Fedha una jukumu kubwa la kulipa viinua mgongo na pencheni kwa wastaafu. Hata hivyo kutokana kuimarisha kwa Mfuko huu miradi mbali mbali ya maendeleo imeanza kufanywa ili kuimarisha maendeleo ya Mfuko kwa maslahi ya wanachama wake. Kamati inaitaka *ZSSF* kuhakikisha inasimamia vizuri miradi yake ili lengo lile lililokusudiwa la kuimarisha Mfuko linafikiwa kwa maslahi ya taifa na wanachama wake. Vile vile, suala la ukataji wa Bima katika miradi hii ni la msingi sana ili kuifanya miradi hii iwe salama zaidi na kutumika kwa muda mrefu, lakini bado ipo miradi ya *ZSSF* mpaka muda huu ambayo haijakatiwa Bima. Kamati inaitaka Wizara ya Fedha kusimamia suala hili la ukataji wa Bima kwa miradi ya *ZSSF* kwa Shirika Bima la Zanzibar.

WIZARA YA BIASHARA, VIWANDA NA MASOKO

Mhe. Naibu Spika, Wizara hii ni moja ya Wizara ambazo imekusanya sekta muhimu sana katika kuimarisha uchumi wa nchi. Ni ukweli usiopingika kuwa nchi nyingi zilizoendelea zimeendelea kutokana na kuimarika kwa sekta ya viwanda na biashara, kwani ni sekta huinua uchumi wa nchi kwa kasi kubwa sana. Kuimarika kwa sekta hizi kunatokana na kuwepo Sheria na Sera ambazo zitaweka mazingira mazuri na rafiki ya kuwavutia wawekezaji katika kuanzisha viwanda ambavyo baadae hupelekea kuimarika kwa biashara.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa azma ya Serikali katika awamu hii ni kuimarisha sekta ya viwanda nchini ipo haja kubwa sana kwa kuzingatia Sheria na Sera zetu zinazohusu masuala ya uwekezaji wa viwanda nchini, lakini vile vile kuwe na mipango madhubuti ambayo itapelekea kuimarika kwa sekta hii. Hata hivyo kuwa na mipango ni suala moja na kusimamia utekelezaji wa mipango hiyo ni suala la jengine. Kwa hivyo mambo haya mawili yanatakiwa yaende sambamba ili kuona kuwa mipango tunayojipangia inatekelezwa. Kamati yetu pamoja na Wajumbe wa Baraza hili tunaamini kuwa jambo litakalowezesha kufanikiwa katika kuimarisha sekta hizi ni ni kuwepo kwa mashirikiano ya dhati baina ya Serikali na wawekezaji.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, moja ya chombo muhimu ambacho kinaweza kupelekea mazingira bora ya uwekezaji na biashara ni Baraza la Kusimamia Utoaji wa Leseni ambalo limeundwa kwa mujibu wa Sheria Namba 13 ya 2013 ambapo jukumu kubwa la Baraza hili ni kusimamia Taasisi zote zilizopewa mamlaka ya utoaji wa leseni kwa lengo la kuweka mazingira bora ya utoaji wa leseni. Kamati yetu inampongeza Waziri wa Biashara na Viwanda kwa kuliunda Baraza hili hivi karibuni. Baraza hili kutokana na upya wake linakabiliwa na changamoto kama zinavyoonekana katika ripoti yetu ya Kamati.

Hata hivyo, Sheria iliyounda Baraza hili limetoa uwezo kwa Baraza kutaka taarifa zinazohusuana na masuala ya leseni kwa Taasisi yoyote inayohusika na utoaji wa leseni, lakini bado kuna baadhi ya Taasisi ambazo zimetakiwa kuwasilisha taarifa hizo hadi hivi sasa hazijawasilisha. Chombo hiki kipo kisheria na kinatekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria, tunaomba sana Taasisi yoyote ambayo ilitakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza hili basi kamati inawaomba wawasilishe taarifa hizo. Narejea tena kusema kwamba taasisi yoyote ambayo ilitakiwa kuwasilisha taarifa zake mbele ya Baraza hili basi kamati inawaomba wawasilishe taarifa hizo.

Mhe. Naibu Spika, zao la Karafuu ni zao ambalo linaingizia mapato katika nchi na kuchangia pato la taifa, usimamizi wa zao hili ni suala moja muhimu sana hasa ikizingatiwa kuwa Zanzibar tunalitegemea sana zao hili katika kuimarisha uchumi wetu. Ni wazi kuwa asilimia 90 ya zao hili linatoka kisiwani Pemba, ipo haja kubwa sana ya kuweka mazingira mazuri kwa wakulima wa zao hili ili washajihike katika kuliimarisha zao la karafuu. Tunafahamu kuwa Serikali ina dhamira ya dhati katika kuhakikisha inaimarisha zao hili, hii inatokana na kuwepo kwa Sheria maalumu ambayo inasimamia masuala ya karafuu.

Mhe. Naibu Spika, Serikali imekuwa ikichukua jitihada mbali mbali katika kuhakikisha inazuia magendo ya karafuu jambo ambalo limekuwa ni tatizo

kubwa sana hasa katika kisiwa cha Pemba, lakini bado tatizo hili limeonekana kuwepo kwa baadhi ya watu kuendelea na biashara hii ya magendo ya karafuu jambo ambalo linaweza kupelekea athari kubwa sana kwa karafuu yetu ya Zanzibar katika masoko ya nje. Kamati inaiomba sana Serikali kuzidisha juhudi katika kuhakikisha kuwa inadhibiti moja kwa moja magendo ya karafuu na kama sheria ya karafuu ina mapungufu basi tunaiomba wizara ilete marekebisho ya sheria hiyo ili tuipe meno na nguvu zaidi kwa ajili ya kuilinda na kuihifadhi karafuu yetu.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu ilifanya ziara katika nyakati tofauti kisiwani Pemba na kutembelea baadhi ya vituo vya kuuzia karafuu, ni jambo la kusikitisha sana kuona kuwa asilimia kubwa ya karafuu zinazalishwa Pemba lakini hadi hii leo vituo vya kuuzia karafuu vinatumia vifaa vya zamani katika kusafishia karafuu. Kamati yetu inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Biashara kuhakikisha kuwa inapeleka mashine za kisasa za kusafisha karafuu kisiwani Pemba ili kupungunguza gharama za karafuu kuanza kusafishwa Pemba na baadae zikifika Unguja zisafishwe tena.

Mhe. Naibu Spika, Taasisi ya Viwango Zanzibar (*ZBS)* ni moja ya Taasisi ambayo inasimamiwa na Wizara ya Biashara na jukumu lake kubwa ni kuhakikisha kuwa bidhaa zote zinazoingia nchini zinakuwa na ubora kwa ajili ya matumizi ya mwanadamu. Taasisi hii kwa Zanzibar bado ni changa lakini hata hivyo tayari imeshaanza kutekeleza majukumu yake. Uchanga wa Taasisi hii unatokana na ufinyu wa bajeti na unapelekea kushindwa kutekeleza majukumu yake ipasavyo. Hata hivyo, Kamati imeridhishwa sana na jitihada ya Serikali kutaka kuipatia *ZBS* vifaa mbali mbali vya maabara pamoja kujenga maabara za kisasa.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu inaendelea kusisitiza kuwa utendaji kazi wa taasisi hii unategemea wataalamu, maabara za kisasa na vifaa vya maabara, tunaomba sana ili kumlinda mtumiaji kuweza kutumia bidhaa zenye ubora Serikali iharakishe inaimarisha taasisi hii hatua kwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yetu ilipata kutembelea Afisi za Shirika la Ubora la Tanzania (*TBS*) na kuona hatua kubwa ambazo zimefikiwa za kimaendeleo kwa Shirika hili ikiwemo pamoja na kuwepo kwa maabara zenye mashine za kisasa kwa ajili ya kupima ubora wa bidhaa mbali mbali. Vile vile imeanzisha Afisi zake katika baadhi ya Mikoa ya Tanzania ambayo inapitisha bidhaa kwa wingi. Maendeleo haya hayakufikiwa isipokuwa ni kwa kupatiwa bajeti za kutosha pamoja na kuwa na wataalamu ambao hutumia taaluma zao kwa ajili ya

maendeleo ya Shirika. Si vibaya kuiga wenzetu wa *TBS* ili na sisi tupate maendeleo makubwa katika taasisi yetu ya *ZBS*.

WIZARA YA KILIMO, MALIASILI, MIFUGO NA UVUVI

Mhe. Naibu Spika, ni dhahiri kuwa Wizara hii ndio uti wa mgongo wa nchi yetu, uhai wa wananchi upo katika Wizara hii. Wizara hii imejumuisha sekta nne muhimu sana katika maisha ya mwanadamu ambazo ni sekta ya kilimo, sekta ya maliasili, sekta ya mifugo na sekta ya uvuvi. Katika kila siku ya maisha yetu sekta hizi tunazifanyia kazi na wadau wakuu wa sekta hizi ni wakulima, wafugaji na wavuvi na wanaonufaika na sekta hizi ni wananchi wote kwa sababu kila siku sote tunakula kupitia bidhaa za kilimo, tunajenga na kupika kupitia maliasili, tunawekeza kupitia bidhaa za mifugo na mazao ya baharini. Mifano hii ni kuthibitisha kuwa Wizara hii ndio uhai wa wananchi na hakuna anayeweza kubeza umuhimu wa kuwepo kwa Wizara hii.

Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wa Baraza hili pamoja na wananchi wanapaswa kufahamu kuwa jukumu la kuimarisha sekta hizi sio la Serikali wala sio la Waziri bali ni jukumu letu sote. Ili haya yafanikiwe tuwape mashirikiano mazuri viongozi wanaohusika na Wizara hii, Wajumbe wa Baraza hili na wadau wa sekta pamoja na wananchi wote. Kamati imeridhishwa na jitihada za Serikali kupitia Wizara ya Kilimo na kuhakikisha kuwa sekta kuu nne zinaimarika, na ni wazi kuwa kuimarika kwa sekta hizi ni kuimarisha uchumi wa nchi na kuinua kipato cha mwananchi wa kawaida.

Mhe. Naibu Spika, suala la kuwepo kwa wataalamu wa kutosha ni jambo lisiloweza kuepukika katika nchi yoyote ambayo inajipanga kupiga hatua ya maendeleo, na moja ya Wizara ambayo inatakiwa kuwa na wataalamu wa kutosha basi ni Wizara hii ya Kilimo. Hii inatoa huduma moja kwa moja kwa wananchi kupitia sekta zake. Hata hivyo, Kamati yetu imebaini kuwepo kwa tatizo la wataalamu wa kutosha katika Wizara hii jambo linapelekea malalamiko makubwa kwa wadau wa sekta hizi. Pamoja na jitihada zinazochukuliwa na Wizara katika kuhakikisha kuwa inasomesha watumishi wake lakini pia bado kuna tatizo la kuweka vipa umbele vya kuwasomesha watumishi ili kupunguza uhaba wa wataalamu.

Katika suala hili, Kamati yetu inaitaka Wizara sasa ianze kuweka mpango maalumu wa kuwa na vipa umbele kulingana na mahitaji ya wataalamu katika Wizara wakati wanapotoa nafasi za kuwasomesha watumishi wao. Lakini vile vile suala hili liende sambamba na kuweka masharti maalumu kwa mtumishi yeyote atakayesomeshwa na Wizara kuendelea kubaki katika Wizara kwani

imeonekana kuwa lipo tatizo kwa baadhi ya wataalamu wakishakusomeshwa na Wizara kuacha kazi au kuchukua likizo bila ya malipo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kwa ufupi sana kwa umuhimu wake niizungumzie Sekta ya Uvuvi, sekta hii ni moja ya sekta ambayo Serikali inaitegemea kupata mapato yatokanayo na sekta hii. Lakini bado sekta ya uvuvi Zanzibar kulingana na raslimali ya bahari tuliyonayo haiendani na ukubwa wa raslimali yetu. Kwa mfano; katika bajeti ya mwaka wa fedha 2016/2017 Makadirio ya bajeti katika sekta ya uvuvi ni Tshs. 1,000,949,000/- katika pato la Taifa.

Kulingana na ukubwa wa raslimali ya bahari tuliyonayo na mchango wa Sekta ya uvuvi katika pato laTaifa bado ni mdogo sana. Hivyo, Kamati yetu inaipongeza Serikali kupitia Wizara hii kwa ajili ya jitihada kubwa inazozifanya katika kuimarisha sekta hii ya uvuvi nchini kwa lengo la kuinua kipato cha wananchi na pato la Taifa.

Tunaomba sana jitihada za Serikali zizidishwe katika kuhakikisha kuwa raslimali tuliyonayo ya bahari inatumika ipasavyo kwa lengo la kuimarisha uchumi wa nchi yetu. Tunaamini kuwa Zanzibar inaweza kujiendesha kwa kutumia bahari tu kwani ipo mifano ya nchi nyingi za visiwa zilizoendelea kwa kutumia bahari tu. Kwa mfano, baadhi ya Wajumbe wetu wa Kamati walibahatika kutembea katika visiwa vya Maldives ambavyo ni visiwa vilivyoendelea sana na uchumi wake unategemea bahari na utalii. Kwa kuwa na sisi raslimali hii tunayo hatuna sababu na sisi kwa nini tusiweze. Hivyo basi kamati inaishauri Serikali Kuu kuyafanyia kazi mapendekezo yaliyowasilishwa kuhusiana na safari ya Maldives hatua kwa hatua.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikumbushie kwa Serikali kufanya uharaka wa kuileta Sheria ya Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu iliyopitishwa na Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania mbele ya Baraza hili ili kukidhi masharti ya kifungu cha 132 cha Katiba ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, suala la kutumia baadhi ya maliasili katika nchi limeruhusiwa kufuatana na taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria, Kanuni au Miongozo iliyotolewa na Wizara. Hivi karibinu Wizara ya Kilimo imekuwa ikitoa matangazo mbali mbali juu matumizi ya maliasili ya mchanga jambo ambalo limepelekea kuelewaka vibaya kwa baadhi ya wananchi na kuzidi kujenga hofu juu ya kuendelea kutumia maliasili hiyo. Kutokana na uelewa huo mdogo wa wananchi, Kamati yetu inaitaka Serikali kupitia Wizara ya Kilimo kuwasilisha taarifa maalumu kuhusiana na hali halisi ya uchimbaji

wa mchanga Zanzibar ili Wajumbe wa Baraza hili na wananchi wote wapate kuelewa faida na athari zilizopo na muelekeo wa Serikali kwa baadae.

HITIMISHO

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa shukrani za dhati kwa Wajumbe wote wote wa Baraza hili kwa utulivu wao katika kipindi chote ambacho nilikuwa nikiwasilisha Muhtasari huu wa Ripoti ya Kamati. Nawaomba sana waijadili kwa kina ripoti hii na hatimae kuikubali.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja, ahsante sana *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Waheshimiwa Wajumbe mjadala unaanza, kwa hivyo mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Suleiman Sarahan Said na baadae atafuata Mhe. Mohammedraza na baadae ajitayarishe Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

Mhe. Suleiman Sarahan Said: Ninashukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii na mimi kutoa maoni yangu kidogo kwa ajili ya kuboresha Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo ili tuweze kufanikisha zaidi.

Awali ya yote kwanza napenda kumpongeza sana Dkt. Ali Mohamed Shein kwa ridhaa yake kuongeza mshahara kwa asilimia katika Wizara ya Fedha na pia kuwa anatoa ruzuku ya shilingi elfu ishirini kwa kila mtu ambaye amefikia umri wa miaka 70, tunamuomba Mwenyezi Mungu akimjalia atapunguza miaka kidogo angalau baada ya miaka 60 pia wapate na wengine. Hilo ni ombi tu Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye mada yenyewe. Katika ripoti yetu hii kuna mambo mengi sana ambayo kwa kweli hii ripoti imejitosheleza lakini lazima tukubaliane tu kwamba haja bado ipo hasa Wizara yetu hii ya Fedha nayo ndio Wizara mama ambayo kila mmoja anakuwa ndio kilio chetu. Bila ya fedha hatuwezi kufanya kitu chochote maana yake hii ndio kila kitu.

Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi nakuja kwanza kwenye suala ambalo kwa kweli ni uvujaji wa pesa maana yake hizi uvujaji wa hizi pesa ambazo katika kamati humu imeelezwa katika maelekezo mengi. Mheshimiwa tuna mambo mengi ambayo yanaharibu pesa zetu za umma. Mheshimiwa nianza kwa suala la

kusema kwamba bado Zanzibar ardhi ni mali serikali utashangaa mpaka leo wizara na nyumba za viongozi wetu bado tunakodi, mheshimwa hapa tunapoteza pesa nying.

Mheshimiwa ningeshauri sana serikali yetu ikajitahidi kwa kila inavyowezekana kuondokana na tatizo hili ili fedha hizi ziingie katika mifuko mengine ambaya ni mahitajio ya jamii kuliko fedha hizi kwa njia moja au nyengine badala ya kodi zile mimi ninaamini kuna *percentage* za watu zinakuwemo. Mheshimiwa ningeshauri sana serikali ikajitahidi kuliondoa hili ili kupunguza miaya hii ya ofisi.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nazungumzia tena katika Wizara ya Fedha. Mheshimiwa serikali yetu hapa ilipiga marufuku gari ikifika saa nane za mchana, gari za serikali isitembee wote ni uhujumu uchumi gari zinatumika vibaya, gari hizo hizo zinachoka haraka. Suala lile limepotea gari zinatumika kiholela, mafuta yanatumika kiholela, matokeo yake bado serikali ile ile inakuwa ndiyo muhimili wa kufanya masuala haya.

Ningemuomba Waziri masuala kama haya yote ni upunguzaji wa matumizi mabaya. Kwa hivyo ningemshauri kwamba gari za serikali ikiwa hazina umuhimu basi zisitembee baada ya kazi ili tuweze kupunguza maelekezo mazuri. Lakini pia Mheshimiwa ningemshauri kwamba uchakavu wa magari, magari yote mabovu ambayo tayari kwa kweli kama ni Mkaguzi Mkuu ameshayakagua kwamba magari haya yamechoka au yana ubovu, mheshimiwa magari yasiwachwe mpaka yakawa hayana thamani, iwe mapema yaondoshwe katika kupata nafasi na pia zipatikane fedha kwa kununulia magari mengine kuliko kuacha yakachakaa na mwisho wake tukaliuza gari shilingi elfu 40,000 au 30,000 imekuwa kama muwa, mheshimiwa ningeomba kupunguza miaya hiyo ili tuweze kuendana na hali yetu.

Mhe. Naibu Spika, nakuja kwenye suala la manunuz. Nimeangalia katika ripoti asilimia 100 ya pesa zetu za serikali asilimia 70 zinafanya manunuzi na bado sheria yetu hii ya manunuzi bado inatukandamiza. Ningekushauri mheshimiwa jitihadi zako zitafanywa ili manunuzi yakaenda vizuri ili fedha hizi zikaweza kuokoka. Kwa hivyo, mheshimiwa ningeomba sana suala hilo ili angalau basi tuweze kupunguza punguza ili fedha ambazo zinapotea ziweze kunapatikana.

Mhe. Naibu Spika, ningeongeza suala la fedha. Fedha mheshimiwa tunaihitaji na mwenye kulipa kodi akipata masumbufu kidogo anapata kukwepa kodi. Kwa hivyo ningeshauri tuboreshe vituo vyetu vya kulipa kodi, lakini mheshimiwa naweza kuchukulia kwamba kama jengo letu la *ZRB,* unakwenda

pale unamaliza mambo yako kama unatumia benki ya *PBZ*, unafanya mambo yako na *ZRB* unamaliza pale pale, lakini kuna mabenki mengine yako mjini, *ZRB* iko hapa. Sasa ningeshauri kituo kimoja kikarudi mjini pale ili kupunguza ulipaji huu ambao naweza kusema kwamba usumbufu unakuwa mkubwa kwa ulipaji kodi. Sasa inakuwa mtu mpaka ahangaike mchana kutwa kwa kulipa kodi moja inakuwa hapa kumpunguzia mazingira yake, kwa hivyo ningeshauri tu Mheshimiwa ili tuweze kwenda na hali hiyo.

Mhe. nimeona katika ripoti yetu tumeisifu sana benki ya *People's Bank* ambayo inafungua matawi yake mengi. Ningeitahadharisha kidogo Mhe. Naibu Spika, *speed* isiwe kubwa ingawa tunataka mapato tunataka na faida. Tushayafungu mabenki katika kipindi cha nyuma na baadae tukaja kuyafunga yote. Sasa ningeishauri tunapoweka mguu tusiondoke tena. Kwa hivyo tufungue mabenki lakini kwa uhakika, kwa hivyo hili nilikuwa nalishauri tu, kwa hivyo mheshimiwa haya ni ushauri wangu napeleka kwamba uweze kuangalia wapi tutaboresha.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nimeona katika wizara tumewapeleka wachumi lakini katika baadhi ya sehemu kuna wachumi. Mheshimiwa hawa wachumi wasiende wakawa kule kama tunamwita huyu maana yake Mwangalizi wa Ofisi. Mheshimiwa kama tumemjua mtu huyu ni mchumi tumempeleka wizara ende akatuchumie, mheshimiwa ningetaka uchukue ripoti ya kila mwaka amekuchumia nini katika wizara ile, siyo tunapeleka mchumi kama Mwangalizi wa Ofisi, kama umeamua kuwapeleka wachumi na kazi ni uchumi aweze kujitahidi kuweza kufikia malengo yaliyokusudiwa. Mheshimiwa hiyo nilikuwa naendeleza maelekezo.

Mhe. Naibu Spika, katika mambo ambayo ni muhimu na wizara yako pia ndiyo inayohusika kuna watu muhimu sana lazima tuwatizame kwa jicho la huruma sana. Wwatu wengi kuanzia juzi, jana wameshapiga makelele sana lakini mheshimiwa madereva wa magari ya serikali, mheshimiwa wapiga taipu, mheshimiwa watunza nyaraka ni watu ambao watu wetu ambao mishahara yao tunaikadiria ndio mshahara ambayo ya chini. Lakini ni watu muhimu sana na ndio wanaofanya watu wale tuweze kupiga hatua hapa tulipo kwa mambo mengi. Mheshimiwa ningeshauri tu kwamba watu wa kama wale kuwe na eneo maalum tu la kutizama tusiangalie tu wafanyakazi wa serikali halafu analipwa, wale watu wana kazi za ziada ambazo wanazifanya.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli nimeangalia humu nimeona hujuma za uchumi nyingi tu zimo lakini moja nilichukulie shamba la mipira yaliopo Pemba na hapa Unguja, mwekezaji huyu mheshimiwa anadaiwa karibu Dola laki nne.

Mambo kama haya Mheshimiwa kwa kweli yanaturudisha nyuma, Dola laki nne si pesa ndogo tunashindwa na mashine tu za hapo hospitali wakati mamilioni ya pesa yakiwa kwa utaratibu ambao tunafanya mikataba. Mheshimiwa mimi ningeshauri sana mwekezaji atakapokuja malipo yake anze mwanzo ndio afanye shughuli, leo afanye shughuli halafu alipe huyo si mwekezaji, baadae ndio wanatutoroka, baadae wanatufukisha katika mazingira mabaya ambayo hatma yake ni kufikishana katika vyombo vya sheria lakini sisi ndio tunaokula hasara kwa sababu ndio ameshachukua pesa ameshafanya alichofanya halafu anaondoka.

Mhe. Naibu Spika, katika jumla ya mambo ambayo nimeona *ZRB* humu wanapata mapato yao sana na mengine hasa ni vyanzo vinavyotoka uwanja wa ndege. Mheshimiwa wewe ukiwa ndio Waziri wetu wa Fedha kila hali lazima kila jambo likuguse. Mheshimiwa tuna uwanja wetu wa ndege ule mpya, wewe unaona kwamba uwanja mdogo huu, kodi inayopata kutanuka inapata hii. Lakini tungepata uwanja wa ndege ule mpya basi tungeweza kukusanya kodi vizuri zaidi. Ningekushauri sana mheshimiwa ukatumia jitihada zako tukaumaliza uwanja wa ndege ili tukapata mapato mengi zaidi.

Mheshimiwa kwa kweli hilo ningeshauri sana, lakini jengine mheshimiwa wewe ukiwa ndio kiongozi wetu wa fedha sifikirii kama kuna sehemu inayokufunga kwamba usizungumze na mabenki au usizungumze na watu ambao wana taaluma ya fedha ukawasaidia wananchi wanaowenza kujijengea mahoteli, wanaoweza kupata mikopo ya kirahisi ili kodi hizi nazo mambo yale yanapofanikiwa, basi tutazidi kupokea kodi ambazo zitatusaidia. Kwa hivyo, mheshimiwa ningetaka ufanye kazi ya ziada kuzungumza na mabenki na kuweka miundo mbinu mizuri ya kukopesha ili wananchi wetu waweze kufanya vitu vingi zaidi ambavyo vitatusaidia katika mazingira yetu.

Lakini mheshimiwa pia nimeona katika mifuko ya barabara. Mheshimiwa mifuko ya barabara nimeona kuna mgongano ingawa si mgongano lakini nilitaka utizame kwa kina pamoja na mambo yote. Mheshimiwa Mfuko wa Barabara una maeneo mawili, una eneo la barabara kuu na kuna na maeneo ya barabara za ndani ambazo zinakamatwa na Tawala za Mikoa. Mheshimiwa hichi kitu hapa ni kizito kidogo, mtendaji wa barabara mheshimiwa ni Mawasiliano na Usafirishaji lakini Tawala za Mikoa ndio maeneo yake. Sasa mheshimiwa kwa kweli mungelitazama sana hili ili kulitazama kuwa na urahisi kwa sababu barabara za ndani au barabara za mijini ukimuuliza mtu wa Mawasiliano na Usafirishaji akwambia mimi hazinihusu lakini ukimuuliza mtu wa Tawala za Mikoa subiri nipate pesa. Sasa mheshimiwa hapa tungelitazama hili kwa maendeleo ya watu ili ukaliweka vizuri watu hawa wawili wasivutane

na kila mmoja naamini anaweza akafanya ushabiki wake masuala yasiende vizuri.

Lakini nimeona pia mheshimiwa ningetaka kukushauri pia kuna mfuko wa *ZSSF*. Mheshimiwa nimeona humu kwamba hauna Bima. Mheshimiwa *ZSSF* ni kwa kweli imefanya mambo makubwa sana na imetumia pesa nyingi sana katika kuekeza katika maeneo mengi ya hapa Zanzibar, vimetajwa viwanja vya watoto, vimetajwa mambo mengi tu lakini Bima haina. Mheshimiwa ningeishauri chombo hichi ukakifanyia kila jitihada ikakata Bima, mambo wanayofanya ni makubwa uliyaona tu hivi karibuni mvua zilinyesha tu basi tuliona pale Kijangwani mapembeya hayaonekani.

Mheshimiwa tutakuja kula hasara kubwa sana kubwa sana, tushafika mbali tutarudi nyuma, nyuma mpaka tuanguke bondeni. Mheshimiwa ningeshangaa sana kwamba tulichelewa tumechelewa kukata Bima, kwa hivyo nishauri tu kwamba haraka hizi shughuli zifanyike ili kuokoa hiyo hali.

Mheshimiwa habari za viwanda, bado Zanzibar viwanda havijakuwa tunavyo ambavyo hivi vingetusaidia ajira, vingetusaidia kila kitu. Mimi naamini kwamba Waziri wetu wa Viwanda anajitahidi kwa kila hali lakini inawezekana bila ya kupata nguvu ya fedha inakuwa kazi kidogo inamuiya vigumu. Kwa hivyo kuna sekta hapa lazima mheshimiwa tuiangalie vya kutosha.

Lakini mheshimiwa tunakuja kwenye suala la kilimo. Mheshimiwa kilimo ndio uti wa mgongo hilo tukubali lakini naweza kusema kwamba Mhe. Waziri wa Kilimo ana nia safi na kwa kweli amejitahidi kuboresha watu katika maelekezo tofauti ambayo watu wale wameweza kujitanua katika mambo ya kilimo kama mananasi, matikiti sasa hivi yanaletwa kwa magari na mambo mengine mengi sana, maziwa ya ng'ombe na kila kitu lakini bado tunamuhitaji kumuongeza nguvu nyingi sana.(*Makofi*).

Huyu Mheshimiwa kama juzi alivyosema yeye hajakataa kwamba tatizo lake kuna Mjumbe mmoja alimwambia kwamba akifika miaka mitatu kama hajamaliza kilimo hapa, bora astaafu, hiyo si kweli mheshimiwa, si kwamba ana nia hiyo. Mheshimiwa huyu namtetea kazi aliyokwisha ifanya ni kubwa sana na kwa kweli kichokuwa kimebakisha labda ni mchele. Sasa tumuongeze nguvu mpunga uwe mwingi ili ahadi yake ifikie, matunda mengine yote kwa ukweli sasa hivi Zanzibar yanajitosheleza sana kweli kweli. Kwa hivyo mimi najitahidi kumpa sifa kwa kazi ambayo ameifanya.

Mhe. nataka tuangalie kitu ambacho kwa ukweli kina ubora wake sasa suala la kilimo ametaja mwenyekiti pale kwamba ni suala zito linahitaji wataalamu, linahitaji na mambo mengi na Mheshimiwa Waziri ni mzoefu. Mheshimiwa ukae naye kitako muzungumze umsaidie nguvu lakini pia tutakapokuwa tumemaliza, maana yake jitihada na maneno yote yaliopo kwetu sisi hapa ni wali ndio unaotuhangaisha mheshimiwa...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Suleiman umebakisha dakika mbili

Mhe. **Suleiman Sarahan Said**: Nashukuru. Mheshimiwa chakula chetu sisi Wanzanzibari ni wali, tutapiga makelele lakini wali ndio muhimu na mimi namuambia Mhe. Waziri fanya mambo yako yote umeshakuwa tayari sasa mchele tunautaka jitahidi tupate mabonde tuweze kulima na matreka ili mchele upatikane. Kwa hivyo, mheshimiwa hilo lilikuwa ni jambo ambalo ni la busara zaidi.

Lakini Mheshimiwa jambo la mwisho ambalo dogo tu ambalo nalizungumzia ni kwamba wizara yetu tujitahidi sana katika kuondokana na mambo haya ya rushwa na mambo madogo madogo. Mheshimiwa *machine* za kukusanyia pesa zitawale tutaondokana na suala hili na kuoneshana vidole na kila maeneo itakuwa kompyuta inafanya ndio inafanya kazi wewe kazi yako ni kulipa.

Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii na naiombea dua kamati yetu Mwenyezi Mungu aijalie baraka, naiunga mkono *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Suleiman Sarahan Said, sasa hivi namkaribisha Mhe. Mohamedraza Hassanali baada Mhe. Raza, Mhe. Nadir hayupo, kwa maana hiyo ajitayarishe Mhe. Rashid Makame Shamsi.

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Naibu Spika wa Baraza la Wawakilishi kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Uzini kupitia Chama cha Mapinduzi kwa kuweza kunipa nafasi hii na kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa pumzi na sote aliweza kutupa pumzi kufika hapa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika nichukue nafasi hii kuipongeza kamati hii iliyokuwa imetoa ripoti yake ikiongozwa na wizara tatu hizi Wizara ya Fedha, Wizara ya Biashara na Wizara ya Kilimo. Kwanza kabisa Mhe. Naibu Spika napenda kuwapongeza Mawaziri wote watatu wanaziongoza hizi wizara pamoja na wasaidizi wao wote.(*Makofi*).

Tukianza na Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda Mhe. Bi. Amina Salum Ali, tukianza vile vile kumpongeza Mhe. Waziri wa Kilimo na wasaidizi wake mzee wangu Mhe. Hamad Rashid lakini vile vile nikimalizia kumpongeza Waziri wa Fedha kaka yangu Dkt. Khalid pamoja na wasaidizi wake *(Makofi)*
Mhe. Niabu Spika, nazipongeza hizi wizara na mimi naamini Rais kafanya kazi kubwa hizi wizara hajazikosea kuzipa Mawaziri pamoja na watendaji wake wote. Kwa hivyo, naamini uwezo wao na usikivu wao hawa Mawaziri pamoja na wasaidizi wao wana uwezo, wana hekma, wana busara, wana usikivu kwa sababu kwa bahati nzuri katika hawa mmoja amenilea. Mhe. Naibu Spika, ambaye lazima niseme kweli na nimshukuru Mhe. Waziri wa Biashara Bi. Amina Salum Ali ni mzazi wangu na ameweza kunilea huu ndio ukweli. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika suala la uchumi wetu wa Zanzibar. Mheshimiwa sisi Wawakilishi wote tumekusanyika hapa tumekuja kwa niaba ya wananchi lakini Wawakilishi wote tuliokuwemo humu ndani tuko kutekeleza ilani ya Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, katika hili sote tunatakiwa kwanza tukubali kwamba suala la kodi ni muhimu kwa kila Mzanzibari, kila mfanyabiashara na kila mwananchi anapaswa kujiuliza Zanzibar kaifanyia nini na kalipa nini kwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar. Hili ni jambo muhimu sana Mhe. Naibu Spika.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, fedha zitakazokuwa zinakusanywa katika nchi yetu hii mapato ndio sis Wawakilishi tutafanikiwa pamoja na Waziri wa Fedha akiongozwa na Rais wetu Makamu wa Pili wa Rais kutekeleza yale mambo ambayo yapo ndani ya ilani ya uchuguzi wa Chama cha Mapinduzi. Kwa hivyo sote tuje kwamba suala la kodi, suala la fedha, suala la kukusanya mapato ni letu siye sote Wazanzibari na wananchi na viongozi, si suala la serikali. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, mimi nitoe tu rai katika ukusanyi wetu wa mapato ili tuweze kuweza kukusanya zaidi.

Mhe. Naibu Spika, hili suala la *TCRA* najua mimi kama mfanyabiashara na kwa bahati nimekuwa Mwakilishi kwamba suala la *TCRA*, hizi simu zote *Vodacom*, *Zantel*, *TTCL*, *TIGO* tunapaswa kujua kupitia *TCRA* ni *minutes* ngapi Zanzibar wakazi wake wanatumia na zile kodi ambazo zinasimamiwa na *TRA* na *ZRB*.

Mhe. Naibu Spika, katika mazingira lazima tuwe na ubunifu na kufanya *statistics* kuona kwamba zile *minutes* zinazotumika Zanzibar visiwa vya Unguja na Pemba, kwa hizi simu zote. Je, zinatosheleza tumefanya *statistics* kwamba mapato yetu ya kupitia *TRA* Zanzibar, kupitia *ZRB* Zanzibar jee, makusanyo haya na matumizi yale yanakidhi mahitaji ya wale ambao

wanaochukua kodi zetu tunazolipa ili *TRA* Zanzibar, *ZRB* Zanzibar ikaweza kuwa na gawio au ikawa na makusanyo ya uhakika. Sasa Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo muhimu lazima twende katika ulimwengu wa sasa, lazima tubadilike. Kwa hivyo, lazima tuwe stamakini kuona kwamba hizi simu zetu zote kwa upande wa Zanzibar. Sasa *TCRA* ndio inayoweza kutupa ili wafuatiliaji hawa wa *TRA* na *ZRB* wakaweza kufanya utaratibu mzima wa makusanyo kama yale.

Mhe. Naibu Spika, *challenges* ziko nyingi najua serikali yetu na uchumi wake unachopata ndio unachotumia na mambo mengine tunatakiwa tugharamie ili tupate vitendea kazi. Lakini vitu ambavyo mimi naamini Wizara ya Fedha kupitia *TRA*, *ZRB* Mhe. Naibu Spika, nasema kwamba kazi wanayoifanya Zanzibar ni kubwa sana na inafaa Wazanzibari wote kuiunga mkono serikali nzima kupitia Wizara ya Fedha kwa ubunifu, uwezo, usikivu wa viongozi wetu na watendaji wetu wote waliokuwepo *ZRB*, *TRA* na sehemu zote pamoja na wizara nyengine. Kwa hivyo, Mheshimiwa haya makubwa ni mashirikiano. Kwa hivyo mashirikiano ya Wizara hizi zinaweza kutupa nafasi nzuri. Mhe. Naibu Spika, hili ningeomba Wizara ya Fedha inayohusika ikafanya utaratibu wa kuona haya makusanyo yetu ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, la pili vile vile suala letu la bandari. Mhe. Naibu Spika, bandari yetu *Alhamdulillah* tunamshukuru Mwenyezi Mungu mizigo inaingia. Hofu yangu ni kwamba kama tutafika pahala kama huko nyuma makontena yakizidi Mwenyezi Mungu akituletea neema lazima Mheshimiwa tuwe na ufumbuzi wa kuziweka kontena tukiacha pale sehemu ya Bwawani. Mhe. Naibu Spika, Bwawani tuna muda wa kukabidhi makontena pale, lakini naomba serikali kupitia Wizara ya Fedha na kuhakikisha kwamba uzuri kwamba kila meli inayokuja juu ya kuwa watendaji wetu ni wazuri, lakini kila meli inayokuja tuhakikishe tunatoa *service*, tunaziteremsha kontena na kama kuna uwezekano tunawapa motisha *staffs* wanazipakia kontena ili kila wakati bandari yetu tuwe na *turnover* nzuri.

Mhe. Naibu Spika, *turnover* nzuri, mapato mengi inategemea juu ya upokeaji wa kontena. Kontena tukija tukijaza pale halafu na meli zita-*divert* na ku-*divert* kwake Mhe. Naibu Spika matarajio ya mapato yale ya mwezi tuliyokuwa tunategemea Mwenyezi Mungu akitujaalia tunasema safari hii *ZRB* watatukusanyia bilioni 20, bandari upande wa *TRA* tutapata bilioni 15.

Mhe. Naibu Spika, kama hatujajiwekea mikakati juu ya yote haya tunayofanya ya *figures* na tukafika pahala pamoja tukapakosea utakuta na mapato yote haya yanakuja chini. Kwa hivyo, uzuri Mhe. Naibu Spika, unajua mimi kwa

ushamba wangu nimepepeleza wakati nilipokuwa mdogo, ng'ombe yule kila ukimpa majani mazuri tutakuwa tunapata maziwa mazuri na maziwa yatakuwa mengi. Lakini ng'ombe yule yule ukianza kumkamua, kumkamua mwisho utamkamua damu, ukimkamua damu ina maana tunaumia sote. Kwa hivyo, vizuri kama tuna ng'ombe ambaye Mwenyezi Mungu ametupa Shifaa kwa Zanzibar iwe tunampa majani mazuri kila wakati, majani ambayo mabichi yasiwe makavu. Maana yake Mheshimiwa hata sisi hatutakiwi kukaa kwenye matawi makavu tunatakiwa kukaa kwenye matawi mabichi kama ya CCM ndio maana tumekuwemo sote humu ndani.(*Makofi*).

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, langu mimi kubwa ni suala la uchumi ambalo hili ndio linalotupa Mawizara yote haya kufanya kazi. Sasa Wizara inayohusika lazima kuwe kuna mashirikiano, Wizara ya Miundombinu, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, wizara hizi ziwe kila wakati zina *coordinate* kuona pahala gani pana mapungufu ili mahitaji yetu sisi Wawakilishi tunaokuja hapa tukazungumza masuala ya wananchi, mapato vile vile yawe yameingia. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, hilo ilikuwa moja ambalo nataka litizamwe na hasa huko tunakokwenda kwa sababu kuna *competition*, kuna bandari lakini nina imani kama tutaweza kuwa na *space* za kutosha, kila wakati meli Mhe. Naibu Spika kutokana na Zanzibar itakuwa mapato yetu hayateremki labda yanaweza kupungua kwa *season*. Lakini kwa Zanzibar mimi nataka niwaambie Wazanzibari na Wawakilishi wenzangu kwamba Zanzibar ni sehemu pekee katika Afrika Mashariki na Kati na nimshukuru Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi hakuna kodi iliyopanda. (*Makofi*).

Kwa hivyo nitoe wito kwa wafanyabiashara akiwemo na Raza tusitoe sababu kodi imepanda kwa sababu faida iliyokuwa unapata *twenty percent*, imepungua *five percent* unasema kwamba aah! kodi imepanda. Lazima tubadilikeni wakati mwengine anaingia papa, papa akiingia lazima anatikisa. Kwa hivyo kuna uzuri wa jambo tuwe tunaridhika lakini tusitoe sababu kwamba Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar hakuna mfanyabiashara sote, naapa kwa jina la Mwenyezi Mungu anayekula hasara na kwa kweli bei tunayoipata hapa hakuna katika Afrika Mashariki na Kati.

Mhe. Naibu Spika, leo nenda *port* pale utalipa gari milioni 3,000,000 lakini tatizo linakuja hapa, sasa wewe kama unalipa milioni 3,000,000 umeambiwa Zanzibar utoe hizo halafu unataka kupeleka Bara, Bara kule utalipa milioni 10,000,000. Lakini Zanzibar bado kutokana na umaskini hatuna viwanda Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imewapa ahuweni Wazanzibari kuanzia chakula, nguo na kila kitu.

Lakini sasa unapotaka kupeleka Bara unasema aah! unasema mimi nimelipia Zanzibar, gari Dola elfu, mimi kule Bara nikatoe Dola elfu haiwezekani hivyo. Mhe. Naibu Spika, mimi juzi nilikuwa na gari yangu nimelipa milioni 2,500,000 gari ya *Noah* nilipotaka kupeleka Bara nimekwenda *TRA* nikawaambia bwana hii gari yangu nataka kupeleka Tanzania Bara, akaniambia Raza sikiliza ulipe nyengine milioni 3,000,000 ili pesa ziingie serikalini halafu ndio upeleke Dar es Salaam, *Is that the problem*. Kwa hivyo tusichukue vitu tukachanganya kwamba unalipa ushuru unasema unapewa ushuru mara mbili, hapana kwa sababu na sisi kule, wao wakinunua na sisi huku *ZRB* upo utaratibu unatumika isiwe mkuki kwa nguruwe kwa binadamu mchungu.

Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, Zanzibar tuna fursa zote lakini unapotaka kupeleka Dar es Salaam kama mafuta umelipa galoni Dola thumni, kule wenzetu Bara utakuja kulipa kwa mujibu wa *rate* ile ya *TRA*. Lakini Zanzibar sisi kwa sababu hatuna viwanda Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inaongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein, mwenye huruma, hekma tumeekewa viwango ambavyo vya kawaida. Hapa tokea kaingia Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi chakula hakuna kodi si sukari, si mchele kwa maslahi ya Wazanzibari kwa sababu nchi yetu bado hali yetu ngumu hatuna viwanda, hatuna dhahabu, hatuna korosho, hatuna kahawa, hatuna gesi. Kwa hivyo tumepewa upendeleo maalum na wenzetu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wameikubali hiyo. Sasa ninachotaka kutoa ufafanuzi kwamba Zanzibar hakuna kitu kilichopanda. Kwa hivyo, naomba tuwe na mwamko wa kulipa, tuwe na mwamko wa kusadiana. Mhe. Naibu Spika, mimi nikaona kwamba niende katika suala zima la upokeaji wa makontena na utaratibu mzima, hakuna mtu aliyekamilika.

Lakini vile vile nije vile vile suala hili la *ZRB*. Mhe. Naibu Spika, *ZRB* nawapongeza na taasisi zote pamoja na mabenki ya *PBZ* na *TRA* sehemu zote hizi. Lakini Mhe. Naibu Spika, tatizo napata moja nataka nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha. Leo unakwenda ku-*renew road license*, una-*renew* gari unaandikiwa karatasi ya kawaida kama shilingi 20,000, shilingi 50,000 au unataka kutoa kontena unaandikiwa shilingi 400,000 kwa mkono, papaa!

Mhe. Naibu Spika, unakwenda *ZRB* ku-*renew road license*, *road license* yake ni Shs.3,000/=. *ZRB of course* wao wanakwenda na *systematic* wanataka kujua kwamba fedha hizi zinaingia kwenye utaratibu mzuri. Lakini ndio duniani kama simu na nini ambalo ni jambo lakini Mhe. Naibu Spika, unachukua fomu unakwenda benki pale kuna fomu zaidi ya nne unapigiwa muhuri, unakwenda *ZRB*, *ZRB* wana fomu, hiyo ya shilingi 3000 tu, halafu fomu zaidi ya 12 Mhe. Naibu Spika, hakuna anayeweza kumudu hivyo. Yaani ile gharama ya fomu

tayari Shs.3,000/=. Sasa mimi niiombe tu Wizara ya Fedha halafu kwenda kwenye *PBZ* ni sehemu ya biashara pale mnakusanya watu foleni. Kwa sababu mimi nilipokuja kuambiwa hili nikasema aah! hapana unajua wakati mwengine watu wanavuta tumbaku, wanakunywa kahawa, mimi nikaona na mimi niende mwenyewe pale nikashuhudie.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nilikwenda nikayakuta lakini…

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mohamedraza umebakiza dakika tatu.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Naam, duu! mheshimiwa nipo kwenye...

Mhe. Naibu Spika: Umebakiza dakika tatu.

Mhe. Mohammedraza Hassanaali Mohamedali: Kwa hivyo, niiombe basi Wizara ya Fedha kwa kushirikiana kuondosha ule urasimu watafute njia ili kuepukana na zile gharama za karatasi zinazotumika nyingi.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho niiombe Wizara ya Fedha kupitia serikali wakati wa bajeti mara nyingi na huu ushahidi upo tunapopitisha bajeti kuna wizara inakuwa haijatekeleza ahadi. Mimi ninayo kwenye *hansard* ipo Waziri wa Fedha aliyetangulia Mhe. Omar Yussuf Mzee, ni Waziri wa Fedha tena wa CCM, alisimama mara mbili miaka miwili iliyopita, akasema hivi kwenye *hansard*, "Raza Mwakilishi wa Jimbo la Uzini pitisha hiyo bajeti ya Wizara ya Miundombinu katika wiki moja kwa sababu Wizara ya Miundombinu haina bajeti, pitisha bajeti ya Wizara ya Miundombinu wiki ijayo nitawatilia pesa tukakumalizie barabara zako za Uzini, hiyo ya Pagali, Dongongwe, Miwani".

Matokeo yake Mheshimiwa huu ni mwaka wa tatu kwamba Waziri wa Fedha ameahidi kwa niaba ya serikali pitisha Raza kwa sababu ukipiga kelele bajeti ukiizuia hapapiti jambo. Kwa hivyo tunakuomba pamoja na Mawaziri wenzake Mhe. Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi wote pale basi tupitishie hii Waziri wa Fedha ameshasimama. Kwa hivyo, ninaomba tu Mheshimiwa kwa heshima zote zile ahadi zilizokuwa zimetolewa na serikali Waziri wa Fedha akisimama, Makamu wa Pili wa Rais akisimama kuzitolea naomba Mwenyezi Mungu akitujaalia tukija huku tuje angalau ziwe zimeshatekelezwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ya muda niunge mkono Wizara ya Kilimo, niunge mkono Wizara ya Biashara mimi naona njia kubwa sasa hivi ni kuhakikisha tunakuwa wabunifu wa kutafuta mapato kuliko kwenda kutoa lawama kwa sababu uwezo tunao na mimi najiamini tufike Zanzibar kama tulivyokwenda sasa hivi serikali yetu tunajitosheleza katika kukusanya mapato yetu.

Mhe. Naibu Spika, nawaambia Wazanzibari bora tule sembe tujiamulie mambo yetu wenyewe Zanzibar hii na Mapinduzi yetu matukufu na mfano huu upo tayari. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, napongeza na kuzipongeza wizara zote, naziunga mkono wizara zote kwa asilimia zaidi ya mia moja na sekunde mbili.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Mohammedraza. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Rashid Makame Shamsi akimaliza ajitayarishe Mhe. Shehe Hamad Mattar na baadae atafuata Mhe. Panya Ali Abdalla.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuichangia Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo iliyowasilishwa hivi punde.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa uwasilishaji mzuri, na nimpongeze sana Mwenyekiti Mhe. Yussuf Mwakilishi makini wa Jimbo Fuoni kwa umakini wake katika kuiwasilisha ripoti hii.

Vile vile niwapongeze tena kwamba ripoti hii ambayo umetuletea kwa kweli ni ripoti ambayo imejaa mambo mengi ambayo ni muhimu katika kuendeleza shughuli mbali mbali zinazohusiana na fedha, biashara na kilimo. Mapendekezo yao na changamoto walizozitoa ni halisi na laitani kwamba Wajumbe tungekuwa hatuna fursa basi ilikuwa ripoti hii inatosha kabisa kuweza kuzisaidia wizara hizi tatu. Lakini kwa sababu Wajumbe tuna fursa na sisi ya kuweza kuchangia na mimi nichukue nafasi hii kuweza kuchangia machache katika kuendeleza mustakabal mzima wa maendeleo ya shughuli za fedha, biashara na kilimo katika nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi nielekee katika suala zima la uwekezaji. Katika suala la uwekezaji kutokana na ripoti hii imetajwa uwekezaji wa Hoteli ya Bwawani. Mhe. Naibu Spika, nafikiri wakati umefika wa sekta hii ya uwekezaji kuwa na umakini mkubwa sana. Kuna manung'uniko na malalamiko mengi sana katika

mikataba ambayo serikali inaingia na wawekezaji. Inaonekana kwamba tuna wawekezaji ambao ni wababaifu, wawekezaji ambao hawana uwezo wa kuwekeza katika nchi yetu. Hii inapelekea nchi yetu kuingia hasara katika mikataba mbali mbali ya uwekezaji.

Mhe. Naibu Spika, inashangaza sana kuweza kusikia pengine hoteli kama ile ya Bwawani au maeneo mengine yamepewa mwekezaji kwa miaka 99. Kwa kweli mimi naishangaa serikali inabidi hivi sasa lazima tuweze kuangalia mikataba ya wawekezaji, huwezi kuwekeza maeneo ambayo serikali hii inayategemea kiuchumi kwa miaka mingi kama hiyo, tutakuwa tunawaweka wapi vizazi vinavyokuja. Mimi nafikiri Mwanasheria Mkuu wa Serikali yupo suala hili la idadi ya miaka katika kuwekeza katika maeneo mbali mbali ya nchi yetu lazima itazamwe upya, alau tuwekeze katika kiwango cha miaka 30, 35 na sio miaka 99, tunajitia katika umaskini na kuweza kuwatajirisha wachache.

Mhe. Naibu Spika, nielekee sasa katika suala zima la uimarishaji wa viwanda. Serikali ya Jamhuri ya Muungano ya Tanzania sasa imekaza buti katika suala zima la kuwekeza katika viwanda. Nafikiri umefika wakati na sisi Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kuweza kulitazama suala hili la kutilia mkazo uwekezaji katika viwanda. Uwekezaji katika viwanda utaweza kupunguza sana tatizo la ajira kwa vijana wetu. Tukubali kwamba Serikali hii ya Mapinduzi katika miaka ya sabini iliwekeza sana katika suala la viwanda, na laitani kama mwenendo ule ungeendelea basi hivi sasa tusingekuwa tukizungumzia suala la ajira katika visiwa vyetu. Lakini kutokana na ubadhirifu na wizi katika viwanda vile imepelekea viwanda vingi kuweza kufa, hivi sasa kazi ni kubwa ya kuweza kuona kwamba tunafufua upya viwanda vyetu.

Lakini niiombe sana wizara unayohusika na viwanda tusiangalie tu viwanda vikubwa tuweze kuangalia viwanda vya wajasiriamali wadogo wadogo. Hivi viwanda kama tutaviangalia vizuri na kama tutapata uwezo wawekezaji hawa wa viwanda vidogo vidogo tuna nafasi sana ya kuweza kuona kwamba tatizo la ajira katika nchi hii linapungua. Kama kuna mwekezaji hata katika kiwanda cha kuchonga kama anawezeshwa vizuri, huyu ana uwezo wa kuajiri vijana 10 au 15 na mwengine mwenye kiwanda kidogo cha ushoni akiwezeshwa maana yake anaweza kuajiri vijana 10 au 15, lakini macho yetu sana yako katika viwanda vikubwa. Kama tuta-*base* katika viwanda vikubwa peke yake basi hatuwezi kwenda. Uchumi huu unaoendeshwa na wale ambao wawekezaji wadogo wadogo ndio wanaoendesha uchumi wa nchi, hata tukienda katika nchi za wenzetu viwanda vinaanzia chumba kimoja tu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa Pakistan kipindi fulani, hizi nguo tunazozifaa ambazo zinashonwa katika sehemu hizo unakuta ni chumba tu kidogo wanashona na ku-*pack* na watu wawili au watatu. Leo macho yetu sana yako kwa wafanyabiashara wakubwa katika kuwekeza baada ya kuwawezesha wale ambao wanawekeza katika viwanda vidogo vidogo. Kwa hivyo, nisisitize sana Wizara hii inayoshughulikia na viwanda kuweza kuona maeneo haya ya kuweza kuwasaidia wale ambao wanataka kuwekeza katika viwanda vidogo ili kuona tunakuza mitaji yao na hatimae kuweza kuleta manufaa kwa nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nielekee sasa katika suala zima la usimamizi wa fedha za umma. Ripoti hii imeeleza vizuri sana, ukweli ni kwamba tuna upotevu mkubwa wa fedha na hapa nimuombe sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango ndugu yangu atakapokuja, juhudi zilionekana katika kuona kwamba tunaziba mianya ya fedha. Hivi karibuni kulitokea upotevu wa fedha na kuna wafanyakazi ambao walisimamishwa kazi kutokana na kupisha uchunguzi. Nina imani kwamba hatua zimechukuliwa zikiwemo za kuunda tume na nina imani kwamba tume hiyo imemaliza kazi, ningemuomba sana Waziri wa Fedha atupe taarifa juu ya hatua zilizofikiwa kuhusiana na sakata hilo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli upotevu wa fedha huu unachangiwa na mambo mengi, unapopita katika taasisi zetu mbali mbali tuna wataalamu wazuri wenye elimu kubwa katika mambo ya fedha, lakini unakuta mapungufu mbali mbali. Unakuta vielelezo vya matumizi wakati mwengine havijazwi vizuri au havipo, lakini vile vile unakuta baadhi ya taasisi hata zile Bodi za manunuzi hazipo au hazifanyi kazi kwa mujibu wa utaratibu wa sheria. Vile vile kuna matumizi mabaya ya fedha.

Mhe. Naibu Spika, kubwa zaidi katika suala zima la uuzaji wa mali chakavu, unaikuta gari imenunuliwa miaka mitatu halafu unasikia gari hiyo inauzwa na mnunuzi ni yule yule ambaye alipitisha katika ununuzi. Sasa hii hali inashangaza sana. Tunatembelea baadhi ya wizara au taasisi kutoka Zanzibar kwenda Dar es Salaam unamkuta mtu anatumia fedha za kigeni inakuwaje, hivi vitu vipo. Ningemuomba sana Waziri wa Fedha na Mipango kuweza kuzipitia sheria vizuri lakini vile vile usimamizi mzuri wa watendaji wetu ambao hawana uaminifu.

Mhe. Naibu Spika, nielekee sasa katika suala la bahari kuu. Kwa kweli Zanzibar ina utajiri mkubwa sana kama utatumika vizuri. Suala la bahari kuu bado hatujalitumia vizuri. Lakini vile vile tukiangalia hii mamlaka ya uvuvi wa bahari kuu Zanzibar inapata asilimia ndogo sana kutoka Muungano juu ya

uvuvi wa bahari kuu, lakini Zanzibar yenyewe ina nafasi kubwa sana ya kuweza kuitumia bahari kuu.

Kwanza wenzetu wamependekeza humu, zile meli za uvuvi kuweza kufikia katika bandari yetu lazima Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kama ilivyopendekezwa ikae na wizara inayohusika ili kuona kwamba meli za uvuvi zina uwezo wa kuekeza katika bandari zetu. Kuna faida kama tatu ambazo zinaweza zikapatikana.

Kwanza vijana wetu tu wanaweza kuunganishwa katika meli hizi na wakaweza kupata ajira, lakini vile vile kujiongezea ujuzi katika uvuvi wa Bahari Kuu. Kama tutakuwa na vijana ambao watakuwa wamepata ujuzi kupitia meli hizi ambazo zinavua katika Bahari Kuu hatimaye serikali inaweza ikawekeza wenyewe katika Bahari Kuu kwa kuweza kununua meli ya uvuvi. Mimi nashangaa sana kwamba nchi hii haina uwezo au haijaamua kuwa na meli ya uvuvi wakati visiwa hivi vimezungukwa na bahari. Watu wanatoka nchi za nje kuleta meli zao na kuvua katika bahari zetu wakati sisi wenyewe tunashindwa kununua meli ya uvuvi na suala la elimu ya uvuvi hapa ilikuwepo katika Chuo cha Uvuvi pale Lumumba, ilianzisha *course* za uvuvi sijui zimefikia wapi.

Lengo la Rais yule Mhe. Aboud Jumbe Mwinyi ni kuweza kuona kwamba vijana wanakuwa wanapata elimu ya uvuvi na hatimaye kuweza kuitumia bahari kuu, lakini leo ni mwaka wa ngapi nchi hii ambayo imezungukwa na bahari haina hata boti ya uvuvi. Hii ni aibu.

Mhe. Naibu Spika, faida nyengine ambayo inaweza kupatikana iwapo meli hizi zitaegesha ni kwamba kuna samaki ambao huwa wanavuliwa kinyume na taratibu za mikataba, samaki wale kiilivyo wanatakiwa wauzwe katika nchi husika na hii itaweza kurahisisha kupata samaki kwa bei rahisi na wananchi wetu wanaweza kufaidika. Leo Tanzania Bara wanaitumia fursa hii ya kuweza kuzitumia meli za uvuvi kuziegesha katika bandari na hatimaye kuweza kuteremsha samaki wale na kuuzwa kwa wananchi. Kwa hiyo, fursa hii Zanzibar tunaikosa. Sasa niwaombe sana wizara zinazohusika na hili basi kuweza kuona kwamba tunatumia fursa za meli hizi za uvuvi katika kuona kwamba...

Mhe. Naibu Spik: Mhe. Rashid Makame Shamsi umebakiza dakika mbili.

Mhe. Rashid Makame Shamsi: Ahsante sana. Mhe. Naiba Spika, nimalizie na suala zima la hatimiliki za maeneo hususan maeneo ya kilimo. Maeneo ya kilimo kama vile ya misitu, ya kilimo chenyewe na mifugo.

Ripoti hii imeonesha kwamba mpaka leo kuna maeneo mengi yanayomilikiwa na wizara hii ambayo hayana hatimiliki. Maeneo haya tokea mwaka 1964 hayana hatimiliki, hii ni aibu kwa serikali. Hii inasababisha maeneo haya kuvamiwa na mengi yameshavamiwa, yanavamiwa na watu binafsi lakini hata viongozi wanavamia maeneo haya. Sasa sijui kizazi kijacho tutakifikisha wapi iwapo maeneo yetu haya ya kilimo, misitu hayana hatimiliki kiasi cha kwamba yanavamiwa kiholela na hatimaye tunabakiwa na maeneo kidogo.

Kuna eneo la Shamba la Makurunge, Bagamoyo. Shamba lile lilikuwa ni eneo ambalo lilikuwa linatumika kwa mifugo lakini hivi sasa limeweza kuvamiwa mpaka limebaki karibu ya robo ya eneo ambalo lilikuwa ni la asili. Kwa hivyo, hii kwa kweli ni hali ambayo ni mbaya na niiombe sana wizara inayohusika na kilimo kuweza kuona maeneo yake yote yanaipatia hatimiliki ili kuweza kuona kwamba hayawez kuvamiwa na wajanja.

Baada ya kusema hayo Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipa nafasi hii na niziombe wizara zinazohusika kuweza kujitahidi. Tunazipongeza zinafanya kazi lakini zijitahidi katika kuona kwamba changamoto hizi zinapungua siku hadi siku ili kuona kwamba nchi yetu inapata maendeleo.

Baada ya hayo niunge mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja ahsante sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Shehe Hamad Mattar baadae atafuata Mhe. Panya Ali Abdalla na kama muda utatosha, ninadhani utatosha atafuata Mhe. Nadir Abdul-latif.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Mhe. Naibu Spika, ahsante nami nitoe shukurani kwa kunipa nafasi hii lakini pia nitoe shukurani kwa Mwenyezi Mungu kunijaalia afya njema.

Mhe. Naibu Spika, na mimi niungane na wenzangu katika kuipongeza ripoti hii ya kamati kwa jinsi walivyochambua kwa kwenda ndani sana kuonesha mambo mbali mbali waliyogundua na kutolea mapendekezo. Mhe. Naibu Spika, na mimi ni mmoja wapo kusema kwamba ripoti hii kama ingekuwa sio lazima basi tungeliiachia tu ikafanyiwa kazi kwa wizara zinazohusika, lakini kwa kuwa japo kidogo na sisi tuweze kutohowa mambo kidogo kidogo ambayo yameachwa.

Mhe. Naibu Spika, kwanza niipongeze Wizara ya Fedha na Mipango, naipongeza katika kutekeleza mambo yake ambayo yamepangiwa wakishirikiana na Waziri husika, Waziri mahiri pamoja na watendaji wake. Lakini vile vile Wizara ya Fedha naipongeza hasa pale walipoanza katika utekelezaji wa ujenzi wa ofisi za kudumu kwa kisiwan Pemba. Mara nyingi sana hapa tulikuwa tunapiga kelele kwamba serikali inapoteza pesa nyingi sana kwa kukodi majengo kwa ajili ya ofisi zetu za serikali, lakini hatimaye kilio hicho kwa kuwa Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein ni sikivu na inasikia kilio cha wananchi na sisi ndio tunaowakilisha wananchi, sisi ndio midomo ya wananchi. Kwa hivyo, imeliona hili sasa wameanza kujenga ujenzi huo kule kisiwani Pemba katika eneo la Gombani, eneo ambalo litabeba Ofisi ya Rais Katiba na Sheria na Utumishi wa Umma pamoja na Wizara ya Uwezeshaji, Wazee, Vijana, Wanawake na Watoto. Nawapongeza sana.(*Makofi*).

Vile vile pamoja na pongezi hizo nina masikitiko yangu kwa Idara ya Mhasibu wa Mkuu wa Serikali. Idara hii ndio inayohusiana na kuona maslahi ya wahasibu walioko Zanzibar wanapata maslahi yao ipasavyo. Katika kikao kilichopita niliwahi kutoa kero ambayo inawafika Wasaidizi Wahasibu Wakuu walioko Pemba kulingana na kunyimwa stahili zao kama wenzao ambao wanapata hapa Unguja.

Mhe. Naibu Spika, Wahasibu wale walioko katika wizara zilizoko pamoja na mashirika yaliyoko sawa sawa na hapa Unguja wamekuwa na kero hii kwa muda mrefu, watu ambao na wao wanajituma, wamejituma kwa kutafuta elimu, elimu zao walizonazo huku ni sawa sawa na hizo walizonazo hapa Unguja. Lakini wasaidizi wahasibu hawa hadi leo haijachukuliwa hatua ya kuwalipa mishahara kama wanavyostahiki wenzao hapa Unguja. Ni kilio kikubwa sana na inapoteza nguvu ya kufanya kazi kumuona mtu ambaye pengine wamesoma chuo kimoja, wana cheti sawa lakini maslahi wanapishana na majukumu ni mamoja.

Mhe. Naibu Spika, hawa hawawezi kufanya uhasibu waliopo hapa Unguja kama hawajapata mashirikiano na wahasibu walioko Pemba. Kwa kweli ni jambo la kusikitisha sana Mhe. Naibu Spika, watu hawa mpaka leo pamoja na Waziri kupiga kelele lakini watendaji wake wamekuwa ni wagumu. Mimi nataka kujua ni kitu gani kinachozuwia mpaka leo suala hili halijamalizika. Naomba sana atapokuja Waziri katika kutoa ufafanuzi au kamati ilivyoona au kama hawakuliona mimi nalitoa katika kamati yao walisimamie na suala hili.

Mhe. Naibu Spika, katika kuchangia kwangu niende kwenye ukurasa wa 7. Ukurasa huu unazungumzia masuala ya mashamba ya mipira. Mhe. Naibu Spika, utakuta mara nyingi sana nazungumzia masuala ya mashamba ya mipira usione ajabu, huko ndiko nilikoanzia kufanya kazi, tokea naanza kulipwa shilingi kumi hadi leo nalipwa kama ninavyojaaliwa kulipwa. Kwa hivyo, nayajua sana mashamba haya naona ugumu wake na dhamira yake ilivyoletwa serikali mashamba haya ili yaweze kuisaidia mapato serikali, lakini leo naona bado huu unakuwa ni mtaji wa watu wachache ambao wanajinufaisha na serikali bado inabakia hili ni shamba la bibi. Nasema bado mipira inakuwa ni shamba la bibi kila mmoja anavuna halafu anaondoka, wamekuja Wasomali, wamekuja *AGROTEX*, wamekuja wengine lakini bado mapato halisi hasa ya serikali sijaona kwamba yapo yanayotosheleza.

Mhe. Naibu Spika, hivi sasa mashamba haya tulisema kwamba amekatishwa mkataba *AGROTEX*, lakini nakumbuka Mhe. Waziri katika jibu lake nilipomuuliza mashamba haya akasema yameshakatishwa mkataba, lakini pia vile vile nikashangaa kuona kwamba mashamba haya nasikia wamepewa watu wengine, sioni uchoyo napenda kwa sababu ni sehemu ya ajira, lakini taratibu zimefuatwa? Leo kama mkataba wa *AGROTEX* haujakatwa au haujavunjwa, leo wanapewaje hawa kikundi cha *Tujiwezeshe Group*. Jee, jamani inawezekana ndoa juu ya ndoa? Kwa sababu kama mkataba Waziri wa Fedha alisema kwamba tumo njiani katika kuvunja mkataba kupitia mwanasheria haujavunjwa, leo tunasikia kwamba tayari wamepewa watu wengine. Jee, hawa waliopewa wamejazishwa mkataba gani. Hili na jambo la kushangaza hapo tutakuwa tunafanya mambo ambayo hayana mwelekeo.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia vile vile mashamba haya ripoti hapa inaeleza kwamba *AGROTEX* anadaiwa Dola laki nne kwa serikali. Sio hilo tu, wafanyakazi wa mashamba yale wanadhalilika kwa kujituma saa kumi na moja tayari wanakuwa ndani ya pori hata zana hawana wanajitegemea na leo mpaka kampuni inafungwa ina madeni ya mishahara. Naomba serikali kwamba kadri wanavyosimamia deni hili la *AGROTEX* kulipwa wahakikishe kwamba na wao wafanyakazi hawa waliokuwa mashamba ya mipira wanalipwa mishahara yao kuwa hii ni haki yao.

Mhe. Naibu Spika, sasa sijui katika ziara yao pia vile vile kamati katika kutembelea mashamba haya namuuliza Mhe. Mwenyekiti jee, waliona lile suala ambalo nililiona na kulitolea ripoti hapa kwamba mashamba ya mipira yanalimwa mazao ya kudumu na watu binafsi. Hata Waziri wa Fedha na Mipango alipanga kwamba atakapokuja Pemba atakwenda kukagua yeye anasema hakuna, lakini mimi nilimwambia wamo na mashamba yamo ambayo

yanalimwa mikarafuu na akifika atakwenda kuikuta. Lakini kwa shughuli zilizomkabili Waziri wa Fedha naamini kwamba labda ziara ile ataendelea kuja lakini sijui kamati hii jee, hili ililigundua. Kama hawajaligundua basi hili jambo lipo wala si la ubishi wala ufisadi. Kwa hivyo, na wao waliangalie jee, mashamba haya yatakuwa na wamiliki wangapi, serikali imeyalipa imeyapima mashamba haya kuona kwamba iweze kuyadhibiti, lakini leo wanatokea watu wanasema bado ni mashamba yao. Kwa hivyo, serikali naiomba hapoa iangalie ni kitu gani itafanya kuhakikisha kwamba haya mashamba hayamilikiwi na watu wawili.

Mhe. Naibu Spika, niendelee kuchangia katika ripoti hii ya Kamati ya Fedh katika ukurasa wa 11. Nimeona katika jadweli hapa hali nzima ya ukusanyaji wa mapato. Kwanza naona mwelekeo ni mzuri kwa kipindi cha Julai hadi Disemba kuona kwamba makadirio yalikuwa 133 bilioni lakini hadi kufikia Disemba 2016 tumepata bilioni 104. Hii hali ni nzur na mwelekeo ni mzuri. Naamini kwamba usimamiaji huu ukiendelea haitakuwa na sababu serikali kutekeleza yale ambayo imejipangia katika bajeti iliyopita. Kwa hivyo, nawapongeza sana katika hili.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, hapa katika jadweli hii kuna kitu kinaonesha kodi ya miundombinu. Naomba sana katika ripoti hii mwenyekiti atakapokuja anieleweshe pengine kodi hii ya miundombinu waliyoiweka hapa ni ipi, kwa mimi tu ninavyoifahamu kuna miundombinu ya barabara lakini hata kwenye bili za umeme sasa zimeanza kuingizwa miundombinu. Sasa niipongeze Wizara ya Fedha kupitia Mfuko wa Barabara kutumia ile miundombinu wakaweza kujenga barabara za vijijini ambazo hivi karibuni tumezipitia ziko katika hali nzuri zimepunguza tatizo la barabara za vijijini.

Sasa lakini kama kuna hii miundombinu ambayo sijaona utekelezaji wake ya umeme, kama imo kwenye ripoti hii basi naomba sana serikali nayo ijiandae kwa kufanya kama vile inavyofanya barabara. Miundombinu ya umeme itumike kwa kuwafikishia wananchi vijijini. Sasa hivi wananchi wengi wanahitaji umeme lakini una vikwazo vikubwa, kama serikali haijaweka mradi maalum umeme tutakuwa sisi huku tunadaiwa na shirika lakini umeme upo unazunguka katika *wire* bila kutumia, kwa hivyo ni hasara. Ni vyema kwamba miundombinu inayokatwa katika bili za umeme basi miundombinu hii nayo itumike katika kuwafikishia wananchi walio wengi katika vijiji vyetu mbali mbali vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kuchangia upande wa kilimo. Kila siku tunasema kilimo ni uti wa mgongo. Mhe. Naibu Spika, kilimo kweli Zanzibar

kama tutapania tuna uwezo wa kujitosheleza kwa chakula bila ya kuagizishia kupitia chakula kikuu wali lakini hata matunda na mazao mengine mbali mbali. Ardhi yetu bado inakubali tena ardhi yetu Mwenyezi Mungu kaipa sifa ya matunda yote yanayozaliwa na mazao yanakuwa na ubora wa kipekee. Kwa hivyo, na mimi naunga mkono sana katika hili la kilimo kwamba ikiwa serikali tutalipa nguvu na kufanya kilimo hicho kiwe ni bora bila ya kubahatisha kwa kweli tunaweza tukaona kwamba tumewasaidia wananchi wetu, tumeisaidia serikali yetu kutumia fedha zetu za kigeni ziliomo ndani kwa ajili ya kwenda kuagizia vitu kutoka nje, kitu ambacho kinawezekana kujiepusha na hilo.

Naomba sana serikali iendelee kusimamia masuala haya ya kilimo, kwanza kwa kufanya tafiti mbali mbali, kwanza hii ardhi yetu wenzetu nchi za jirani hawawezi kulima mpaka kwanza wafanye utafiti wa udongo, udongo huu unahitaji nini, una kasoro gani, tulime kilimo gani, sisi tunabahatisha tu hapa. Naomba hii Idara ya Utafiti ya Kilimo ifanye kazi ipasavyo na tafiti hizo baadae zitolewe kwa wananchi ili waweze kufaidika nazo, tukifanya hivyo basi naona hatua kubwa tutapata na kilio cha kwamba tunakula mapembe wali ambao sio mtamu basi tutaondokana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Spika, suala la biashara. Biashara nayo ni sehemu moja ambayo itaweza kutusaidia katika nchi yetu hii ya Zanzibar, jambo hili ambalo ni tukufu sana hata Mtume wetu Muhammad *(S.A.W)* basi alitumia biashara ikawa ni ukombozi katika maisha yao. Kwa hivyo na sisi kufanya njia kama hii ni vyema sana lakini biashara hii ambayo tunayo hapa bado ina vikwazo mbali mbali. Tunataka kufanya kufanya viwanda kupitia biashara hiyo, lakini bado tunapiga kelele viwanda viwanda. Naomba sana serikali hapa suala la viwanda vikubwa na vidogo...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Shehe Hamad Mattar: Vichukuliwe umuhimu wake. Lakini pia vile vile Mhe. Naibu Spika, namalizia ahsante sana kwa kunikumbushia. Kwa upande wa bahari, tuitumie bahari. Nchi za wenzetu visiwa kama hivi wanajitosheleza kwa kupitia bahari. Hii raslimali jamani tusiipoteze tuitunze na tuienzi na tuona kwamba itatusaidia katika kizazi chetu cha sasa na cha baadae.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango wangu huo naunga mkono hoja ya Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa asilimia mia juu ya mia. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Shehe Hamad Mattar. Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Panya Ali Abdalla anafuata Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf, kama muda ukitosha atachangia Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nichukue fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia uhai na uzima tukaweza kufika hapa. Pia nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii nikaweza kuchangia machache katika wizara hii.

Awali ya yote napenda nichukue fursa hii kuwapongeza sana Waheshimiwa Mawaziri wetu, Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kwa utendaji wao wa kazi mzuri na Mwenyezi Mungu Inshaallah awazidishie waendelee vizuri.

Mhe. Naibu Spika, mimi nataka nianze na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango kwa kutoa angalizo kwamba serikali iwe makini katika mauzo na manunuzi. Mhe. Naibu Spika, fedha nyingi za serikali zinapotea katika eneo hili la manunuzi na mauzo. Mhe. Naibu Spika, manunuzi serikali iangalie huwa fedha inatumika nyingi, lakini vitu vinavyonunuliwa ni *fake*. Utakuta matumizi yake ni ya muda mchache tu vitu vimeshaharibika na fedha ya serikali imetumika nyingi. Lakini katika mauzo utakuta vitu vya serikali vinauzwa kwa bei ndogo ukilinganisha na ile bei ambayo imenunuliwa, kwa sababu ya kuwa hapauzwi ila watu wanarithishana. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, nimuombe sana Mhe. Waziri aliangalie sana jambo hili.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia suala la madeni. Mhe. Naibu Spika, nimuombe na ninakuwa na matumaini makubwa kwa Waziri wa Fedha na Mipango alivyokuwa yuko mahiri sana, niombe madeni ya wadaiwa ambao wanachukua mikopo pengine katika mabenki na katika serikali. Mhe. Waziri kuwa makini kwa hili na usione muhali, lazima fedha za serikali zinazodaiwa ziweze kulipwa ili ziweze kukidhi katika mahitaji mengine. Mhe. Waziri kuwa makini juu ya hilo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo nataka nizungumzie kuhusu maghala ya serikali. Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nilitaka kujua kuna maghala ambapo katika taarifa hii tumeambiwa kuna maghala yamekodishwa. Nilitaka kujua maghala hayo yaliyokodishwa mkataba wake umekodishwa kwa muda wa miaka mingapi.

Pia nikitoka kwenye suala hili la maghala, niende katika masoko. Mhe. Naibu Spika, masoko ni jambo muhimu sana hasa ukiangalia tuna wajasiriamali wetu ambapo wamefuata wito wa serikali kujitokeza katika shughuli mbali mbali za kujijengea uchumi wao. Kwa hivyo ni lazima tuwe na masoko ya uhakika ambayo yataweza kuwafanya wajasiriamali wetu hawa kuwa na mwamko mkubwa wa uzalishaji mali, lakini pia na kuwa na ari kubwa ya kufanyakazi.

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko ili aweze kulidhibiti soko la ndani kwa ajili ya wafanyabiashara wetu. Soko hili la ndani vipi ataweza kulidhibiti Mhe. Waziri, kwanza lazima tuwe na mitaji ya kutosha kwa wajasiriamali wetu ili mitaji hiyo sasa iendane na wataalamu ambao wataweza kutoa taaluma nzuri kwa wajasiriamali, ili waweze kutumia vizuri fedha zao katika uzalishaji. Hapo Waziri aandae sasa masoko kwa ajili ya wajasiriamali wetu ili waweze kuzalisha mali kwa wingi, lakini pia kuweza kupata soko la ndani na la nje. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kwa sasa wajasiriamali wanajituma mali wanazo za kuzalisha lakini wanapata usumbufu wa masoko, tuna wajasiriamali ambao wanalima kilimo cha mwani na ukiangalia huko katika soko la kimataifa inasemekana soko lipo zuri, lakini wao bado wanaendelea kuumia wajasiriamali wetu hawa na kuwavunja moyo kwamba wao bado wanauza bidhaa hiyo kwa bei ya chini kabisa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri hili suala ni la kuona imani kwa wananchi wetu, kuweza kuwapatia masoko ya uhakika. Lakini pia na wanaoanika madagaa, hawa wanafanyakazi na wao kwa bidii kubwa sana. Kwa hivyo, ni lazima tuweze kuona suala la kuwatafutia soko, waanikaji wa dagaa ambapo dagaa hili hili linanunuliwa, wenzetu wanakwenda kuliuza kwa bei kubwa. Sisi watu wetu wanaumia saa zote wako katika jua kuanika madagaa lakini dagaa lao linakuja kununuliwa kwa bei ndogo ambayo inafanya kuwachosha na kuwavunja nguvu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, nimuombe Mhe. Waziri kuangalia soko hili la wajasiriamali wetu ili waweze kuondokana na lile suala zima la umaskini.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende katika Benki yetu ya Zanzibar (*PBZ)*. Kwanza kabisa nitoe pongezi za dhati kabisa katika benki hii, kwa kweli wanachapa kazi vizuri na utendaji wao kwa sasa umekuwa mzuri, nawapongeza kwanza kwa kuongeza matawi wanajitahidi kwa kuongeza matawi, lakini pongezi zaidi kuweza kuweka *ATM* kuisogeza katika Baraza letu hili la Wawakilishi. Ni jambo ambalo sisi Waheshimiwa hapa litatupa urahisi wa kuweza kutumia bila ya kupata usumbufu. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, niombe benki hii kuweza kuongeza soko katika Afrika Mashariki ili tuweze kupiga hatua kubwa zaidi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pia kuna tatizo la sheria ambayo inakosesha wao kufanya kazi zao vizuri, ambapo imeainishwa hapa na ripoti. Kwa hivyo, naomba sheria hii ya *Transfer of Property Decree* iweze kufanyiwa marekebisho ili benki yetu hii iweze kufanyakazi zake vizuri.

Mhe. Naibu Spika, pia katika benki kuna malalamiko ya wanaokopa wakawa hawalipi. Mhe. Naibu Spika, niiombe serikali ichukue juhudi za makusudi ili kuweza kuwadhibiti watu hawa ambao wanakopa wakawa halipi na hii inaweza ikaishusha hadhi benki yetu kwa kupungukiwa na mitaji ikaweza kufanyakazi vizuri. Maana hiki ni chombo cha kijamii, tunaweza tukawakosesha wenzetu haki na wao ya kwenda kukopa pale na wao wana haki kama walivyo na haki wengine ambao wamepata mikopo. Kwa hivyo, Mhe. Naibu Spika, ni suala la kuangalia anayekopa ni lazima alipe na serikali iangalie ni utaratibu gani kama kakopa halipi, basi afilisiwe hata kitu chake kiuzwe lakini fedha ziweze kurudi na wengine wafaidike.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda katika Mamlaka ya Uwekezaji. Nichukue fursa hii kumpongeza kwa dhati kabisa mwekezaji wetu Ndugu Said Bakharesa kwa kuweza kuimarisha nchi yetu kwa majengo mbali mbali ikiwemo bandari zetu kwa kutuwekea bandari vizuri, na pia Kiwanda cha Maziwa na vyenginevyo ambavyo vinasaidia kutoa ajira kwa vijana wetu.

Mhe. Naibu Spika, mimi niiombe serikali imshauri kwa sababu hapa ripoti imetuonesha yeye ana nia ya kujenga nyumba hizi za ghorofa moja, sita na nyumba za chini. Mimi niseme labda tu serikali imshauri kujenga zile nyumba za ghorofa pekee ni suala la msingi, kwa sababu kwa sasa tuna ufinyu wa ardhi. Sasa tukichukua sehemu kubwa tukajenga pengine nyumba za chini itakuwa ndio bado yale yale, kwa sababu tuangalie tu mfano ambao ametuonesha Muasisi wetu Hayati Abeid Aman Karume kwa kujenga zile nyumba za Michenzani, eneo dogo lakini limeweza kubeba watu wengi na sera ile ingekuwa tumeiendeleza, basi tungekuwa kwa sasa bado ardhi ya kuitumia tunayo. Mhe. Naibu Spika, pia mimi napendekeza sera ambazo ziko nzuri zinaweza kuleta faida kubwa kwa taifa letu basi ni vizuri zikaendelezwa, hata ukija utawala mwengine basi kuifuata sera ile sio vibaya.

Mhe. Naibu Spika, niende katika mashamba haya serikali ya mifugo. Mimi nasikitishwa sana na usimamizi wa mashamba ya mifugo. Kwanza kuna shamba ambalo mimi mwenyewe nalikumbuka Shamba la Pangeni, utoto wetu ndiko ambako tukiokota embe huko, ni shamba lilikuwa zuri, lilikuwa na mifugo mizuri. Lakini kuambiwa leo shamba hili linavamiwa, limekosa hati

miliki tangu miaka hiyo ninayofahamu mimi mpaka leo kwamba shamba hili halina hatimiliki ni kitu ambacho bado kinanisikitisha.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, shamba hili la mifugo halafu linavamiwa pengine kwa kukosekana senyenge. Ni kweli kulikuwa kuna senyenge, lakini shamba la mifugo pia tunashindwa hata kubuni mbinu ukipanda tu ile miti ambayo tunayolishia mifugo mijenga uwa ambayo ukiipanda tu ukilizungusha lile shamba, basi shamba hilo litakuwa liko katika hifadhi na mtu hatoweza kuiba, kwa sababu ile miti ina fursa ya kujenga uzio mzuri tu na uzio huo pia utakuwa ni malisho ya wanyama. Mhe. Naibu Spika, kweli tushindwe kwa hili, halafu shamba livamiwe lichukuliwe. Halafu kinachonisikitisha zaidi kuambiwa katika ripoti hii kuwa, katika mifugo inayofugwa pale kuna mifugo ya serikali, lakini kuna mifugo ya watu binafsi humo humo ndani ya shamba la serikali. Mhe. Naibu Spika, hili ni jambo ambalo mimi halinipi matumaini, naona kuna hadaa fulani inatendeka. Kwa sababu kama mifugo inafutwa humo humo yako wewe mtu binafsi na ya serikali imo humo humo, mimi nitapata uhakika gani na pia hapa niambiwe kwenye mifugo hiyo ya serikali kuna ng'ombe wangapi katika shamba hilo la Pangeni lakini pia kuna mbuzi wangapi ambao wanalihusu hilo shamba la serikali.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, pia tuna tatizo la uhaba wa madaktari wa mifugo. Kweli hili ni tatizo wanyama wanakufa ovyo kwa kukosa huduma hii kwa haraka. Unaweza kumtafuta daktari yuko mbali kabisa na kwamba yuko peke yake katika Wilaya. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, kuongeza madaktari wa mifugo ni jambo muhimu sana, lakini pia taaluma kwa wana mifugo wenyewe. Mhe. Naibu Spika, tukitoa taaluma ya kutosha kwa wafugaji wetu basi naamini yale matatizo madogo madogo wanaweza kuya-*solve* wenyewe madogo madogo bila ya kumuona huyo daktari. Kwa hivyo mimi naomba kuwapatia taaluma watu wetu hawa wanaofuga.

Mhe. Naibu Spika, mwisho niungane na wenzangu kuipongeza sana ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, lakini pia kumpongeza kwa dhati kabisa Mwenyekiti wake ambaye aliweza kuisoma ripoti hii kwa ufafanuzi mkubwa, na uelewe mkubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naomba na mimi niunge mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Bi. Panya Ali Abdalla. Sasa ni zamu ya Mhe. Nadir Abdul-latif na baada ya hapo atafuata Mhe. Asha Abdalla Mussa.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Ahsante sana Mhe. Spika, Bismilahi Rahman Rahim.

Mhe. Naibu Spika, mimi nitamaliza dakika 50 kwa sababu wizara tatu dakika 15 ni ndogo sana. Lakini nitakwenda ninavyofahamu hivyo ninavyofahamu mimi mwenyewe hivyo kuchangia.

Mhe. Naibu Spika: Jipange vizuri uende vizuri dakika 15 tumekubaliana kwenye Kanuni uzitumie hizo hizo dakika 15. Nina wachangiaji 25, kwa hivyo na wenzio wanataka nafasi.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Sawa mimi mpaka dakika ya hamsini nitakuwa nimeshamaliza hotuba yangu.

Mhe. Naibu Spika, mimi kwanza ningeenda mbio mbio kwenye Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi, halafu Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko halafu nitamalizia na Wizara ya Fedha na Mipango.

Mhe. Naibu Spika, ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi zile meli ambazo zipo *offshore* za nchi za nje, wale ambao ni *foreigners* wanachukua vibali kwetu wavua *deep-sea*, ningeomba sana Mhe. Waziri wale watu bora ungewaondosha, kwa sababu hawaleti maslahi yoyote ndani ya nchi yetu, wanavua samaki wengi sana wanafaidika wao kuliko tunavyofaidika sisi. Kwa sababu ingekuwa ndani ya zile meli mmewaweka watu wa *ZRB* au wa *TRA* kila samaki anayevuliwa anachukuliwa asilimia, basi hapo ningesema waweke. Lakini kwa vile ambavyo wanalipa tu leseni dola 5,000 au 10 kwa mwaka, lakini wanavua matani ya samaki halafu wanaondoka zao bila ya kuleta ripoti au kujua kiwango gani wamekivua.

Kwa kweli tunakula hasara kubwa, kwa sababu samaki nchi za nje ni ghali sana. Samaki aina wa Tunda mdogo tu anaweza kufika shilingi laki tatu, lakini cha kushangaza kodi wanayolipa ya leseni ni ndogo, na ukiangalia hakuna wazalendo ni wafanyabiashara, kwa sababu kumiliki meli ya kuvua ni fedha nyingi sana, na ndio maana wafanyabiashara wa *local* hawawezi kumiliki meli za kuvua za *deep sea*. Kwa hivyo, ningeomba sana Mhe. Waziri kwa hisani yako hawa watu bora kwa fedha wanazolipa bora tuzisamehe, kuliko wanavyomaliza samaki wetu na wananchi wetu kukosa samaki na kuweza kututia hasara ya kodi katika nchi yetu.

Vile vile niende kwa ufupi na usahihi kwenye wizara yako Mhe. Waziri napendekeza sana kwenye suala la kushirikiana na Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango na wewe mwenyewe Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kufungua angalau Kiwanda cha Boti ndani ya nchi. Kiwanda hiki kisiwe hata kikubwa kiwe *medium standard*, cha *size* ya kati ambacho kitaweza kuzalisha boti za uvuvi za *size* ya chini, pamoja na *size* ya kati kati ili wananchi wakaweza kununua boti kwa fedha ndogo na mpya. Leo wananunua maboti *used* maboti ambayo hayana kiwango, hayana kiwango na fedha nyingi, kwa sababu tu hawajui *price market* ya nje iko vipi. Lakini mimi ningeomba sana mngeshirikiana wizara hizi tatu pamoja na kuangalia vipi mnaweza kufanya mkafungua kiwanda cha maboti kikazalisha ndani ya nchi na mkapata kuuza *East Africa*, kwa sababu ni nchi ambayo ina bahari na wavuvi wengi watanunua kutoka Zanzibar kwa bei nzuri.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, tumeona katika suala la ulimaji, wakulima kwa kweli wanapata tabu kwenye masuala ya matrekta. Utakuta kwenye Wilaya nzima kuna trekta mbili ambazo ni hasa sehemu zenye wakulima wanaolima wanapata tabu katika kusubiri kulimiwa sehemu zao na juu ya hivyo wanalipishwa. Kwa hivyo, ningeomba sana wizara yako ingefanya mikakati yote kuleta matrekta ya kutosha katika kila Wilaya basi angalau yasipungue, kama kuna majimbo matano basi matrekta yawe 10 mawili mawili au moja moja, lakini kila sehemu iwe na trekta lake, kuliko sasa hivi wanapata tabu. Utakuta mtu mwenye fedha analishia anapata kupelekewa yeye mwanzo, kwa sababu watu wengine hawana kitu wanawekwa mwisho, na ni vitu ambavyo ni muhimu katika mambo ya kulima.

Vile vile Mhe. Naibu Waziri alipoulizwa maswali juzi, kuhusu suala la mbegu mnazopeleka. Kuna mbegu ambazo mmeshazipeleka mpaka kwa wananchi kwa ajili ya kulima, basi mnakuta zina-*fail*. Suala hili kwa kweli sio zuri. Kwa hivyo, ningeomba sana wakati mnanunua au kabla hamjafanya *process* yoyote za kuwapelekea wananchi, basi bora kwanza zifanyeni vipimo, zijaribuni ili mtakapozitoa kwa wananchi zisiwe zime-*fail* kwa sababu wananchi mwisho watakuja kuona hii wizara vipi, hii serikali vipi inatupa dawa *fake* kwa nini hawajazichunguza mwanzo. Mimi ningeomba sana vitu kabla ya kupewa wananchi, ndio kama haya masuala ya vyakula, kabla hatujaona vyakula hivi havifai basi visiingie kwenye jamii mpaka vichunguzwe kwa hali ya juu. Mhe. Naibu Spika, kwenye Wizara ya Uvuvi nimeshaondoka zamani, ninakwenda kwenye Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko kwenye suala la *Zanzibar Bureau of Standard (ZBS),* ningeshauri sana Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko awe makini na watendaji wake, vifaa vinavyoingizwa Zanzibar havina viwango vingi, na zaidi vitu *used* kutoka *European Countries* ambavyo wanaleta kama mafriji, madude ya kupikia makuka, mavitu ya *electronic* yote mabovu. Vitu vyengine wananunua bodi mbali na mashine mbali wanakuja kuziungia Zanzibar. Kwa hivyo, ningemuomba sana hii Mhe. Waziri *ZBS* hii ifanye kazi vizuri hata kama wataruhusiwa watu walete *used* basi ziwe *used* ambazo ni *second condition* ni nzuri.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, minong'ono imezidi, tumsikilize Mhe. Mjumbe.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba *ZBS* ifanye kazi vizuri ma-*used* hayakatazwi kutokana na hali yetu, lakini walete zenye sura sio *used* ambazo kama wanawaletea wanyama wakati huku kuna binadamu, *used* zinazoletwa hazifai Zanzibar. Namuomba sana Mhe. Waziri akashirikiana na watendaji wake vifaa vitakavyoingia Zanzibar viwe *quality* nzuri hata kama *used* hata kama nguo za mtumba basi ziwe nzuri, lakini tunaletewa vitu ambavyo havina kiwango, wananchi wanauziwa vitu ghali halafu hizo *used* zenyewe zina bei kuliko vitu vipya saa nyengine kwa sababu tu jina kubwa UK, Amerika kumbe madude mabovu yameshatupwa.

Jengine ningemuomba sana Mhe. Waziri wa Biashara katika sehemu ambayo wanatumia pale Maisara kufanya maonyesho basi ile sehemu wangeiomba wakaijenga wakaitia zege, wakajenga *hall* kama *Diamond Jubilee* Dar es Salaam ikawa *special* kwa ajili ya watu ambao wajasiriamali wale wadogo wadogo kufanya maonyesho yao ya kudumu, kuliko tu kwamba leo tunataka tufanye kitu tunakwenda kufunga maturubali tunaondoka yanafunguliwa, hivyo tutakuwa hatufiki, tufanye kitu kama tunataka kuendesha nchi yetu kwenye masuala ya *show* masuala ya uchumi basi tuweke kitu cha kudumu kiwepo ndani ya nchi inajulikana hapa siku inayofanyika *show* ya bidhaa fulani kitu kipo tayari hakuna haja ya kwenda kufunga turubali wala kufunga kitu chochote.

Lakini vile vile Mhe. Waziuri wa Biashara kushirikiana na Waziri wa Uvuvi masuala mengi yapo ndani ya Zanzibar ya uchumi, masuala ya wakulima ukiangalia *fruits* tunazo nyingi, embe, ndimu, ndizi, mananasi ni kitu cha kukaa pamoja wakaanza kuanzisha viwanda vidogo vidogo vya *juice* za mananasi kama alivyoanzisha Bakharesa, Serikali kwa nini ishindwe, wakae wenyewe

waingize *Management* au wajenge wakae na mtu *private sector* au *business man* ambaye anataka kushirikiana nao waingie *joint venture*, wafanye biashara. Lakini leo viwanda hapa hatuna vya *juice*. Nampongeza muwekezaji Bakharesa kwa upande fulani kwa masuala ya maziwa na vitu vyengine lakini viwanda vyake viko Tanzania Bara sisi tunataka Zanzibar, *medium size industries* au *factories* viwepo hapa zifanye kazi na zile *capital* zake sio kubwa.

Sasa mimi ningependekeza sana hizi Wizara ziwe zinakaa kuangalia hii mifumo ambayo wataweza kuanzisha viwanda vidogo vidogo kutokana na *fruits* zetu na vitu vyetu. Pia ukiangalia wanao uwezo wa ku-*export* wakatafuta viwanda vya *packing* vizuri, wakatia matunda yetu yale machungwa wakayafanyia-*packing* vizuri wakayapeleka nje kama wanavyopeleka nchi nyengine.

Lakini vile vile Mhe. Naibu Spika, ningeomba na bidhaa feki waziangalie tena kuna vitu feki vingi sana Zanzibar hata nguo, kiatu watu wanaandika kiatu cha *NIKE* kumbe sio *NIKE Original* ni *NIKE fake*, mtu anauziwa kiatu cha *NIKE* laki mbili anaambiwa *original*, kumbe kile kiatu shilingi elfu 15 hakifiki. Vitu vinavyouzwa mjini vyote hakuna *NIKE Original* pale, wala hakuna *perfume original* ni maduka machache wanaomiliki vitu *original*. Sasa ningeomba sana wafanye utaratibu wa kupita sio vitu watu wapandishe bei wanavyotaka, leo wanamwambia mtu nakuuzia hii *GUCHI* kwa sababu anajua Kampuni ya *GUCHI* ni kubwa sana na mtu aliyekuwa hajui anaamini, kumbe vile vitu ni *copy*, tena *third copy* wala sio *second grade* na hivi ndio watu wanavyodhulumiwa Zanzibar.(*Makofi*)

Mimi nakwenda kwenye Wizara ya Fedha na Wizara ya Fedha hii ndio nilikiuwa naisubiri. Mhe. Naibu Spika, ninachotaka kumwambia Mhe. Waziri wa Fedha kwamba tunamuhitaji bado awe Waziri wa Fedha ambaye hana madudu na hatokuja kuingia kwenye madudu, kwa sababu Wizara hii ya Fedha ndio kila kitu katika nchi yetu na ndio moyo wa nchi na ndio uchumi wa nchi, yeye ndio anayetegemewa, bila ya yeye humu ndani wala tusingekuja tungekuwa tunakaa nyumbani, Wizara ya Fedha ndio kila kitu.

Lakini ninachotaka kusema Mhe. Naibu Spika, nchi yetu ina viongozi wazuri Mhe. Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi ni Rais ambaye hana mambo ya rushwa, anachukia rushwa, anachukia masuala ya magendo, anachukia masuala ya ubadhirifu wa fedha, anapenda wananchi wake. Lakini ukiangalia watendaji sizungumzi Waziri, watendaji wengine wanafanya ionekane Serikali nzima haina maana kwa watu watano au sita ndani ya Wizara, wanakifanya Chama cha Mapinduzi kilaaniwe nje kwamba

kina wizi kumbe wao ndio wizi watu watano au sita. Mhe. Naibu Spika, tuna viongozi wazuri tuna viongozi ambao tunawajua hawa wazuri na hawa ni mapapa ambao magendo wameweka mbele tunawajua. Lakini tunachotaka kusema isifike hatua kwamba watu wachache katika watendaji wa Wizara wanaingiza mpaka viongozi wa juu wanasemwa, Serikali inasemwa, Chama kinasemwa kwa sababu ya wao.(*Makofi*).

Lakini nitakwenda kwenye mifano midogo kwenye ripoti hii ya Kamati ya Fedha wenyewe wenye Kamati wamezungumzia suala la mchanga, wameona mchanga kwamba umetumika kwenye barabara ya Fuoni shilingi milioni 250 mchanga tu kwenye kuingizwa mchanga, ni suala ambalo kwa kweli hizi fedha ni za wananchi sio fedha za mtu mmoja, ifike hatua tuwaonee huruma fedha za wavuja jasho, tuonee huruma pesa za wananchi, Serikali inakopa, Serikali inakopeshwa, Serikali inafanya kila njia iweze kujiendesha iweze kuendesha wananchi na kuwasaidia, lakini leo watu wanaitia Serikali hasara, matokeo yake inadaiwa fedha sijui mpaka sisi wengine tutazeeka tutakuwa hatumalizi kulipa madeni.

Lakini niende kwenye suala la miradi Mhe. Naibu Spika, vitu vyovyote Waziri wa Fedha awe makini sana. Kuna meli zilikuwa zikiingia kipindi cha nyuma, meli nzima mtu tajiri analeta ya saruji, unga, mchele baada ya kuwa-*declare* ile meli inabeba tani 300, basi inaandikwa tani 140 kwa kuwa tu wakwepe ushuru. Wizara yenyewe na inaweza kuwa Waziri wa Fedha hajui lakini watendaji wa kule chini wanajua na hichi ndio kukwepa kwao fedha nyingi sana wanakwepa hasa watu wenye uwezo kwenye masuala kama haya, mtu analeta kontena ndani ina thamani ya milioni 500 ana-*declare* milioni 36. Mhe. Waziri uwe makini sana nyuma kumeshafanyika meli wana-*declare* tani mia tatu wana-*declare* mia na thalathini wewe hujui, na mzigo watu wanaingiza ndani ya nchi matokeo yake wanashusha bei wanaumiza wafanyabiashara wadogo kumbe wao wameshaiba kodi.(*Makofi*).

Lakini ninachotaka kusema chengine masuala ya barabara. Mhe. Naibu Spika, masuala ya barabara hizi *tender* lazima hizi pesa lazima tuzionee huruma, hawa wanaojenga barabara hawafai wanadanganya, barabara tani kumi na tano uzito inayobeba mpaka tani ishirini wanajenga kwa zaidi ya bilioni moja. Nimefanya *survey* zaidi ya kampuni tatu nchi za nje wanasema wanao uwezo wa kujenga tani sitini ya uwezo barabara kwa dola haitozidi laki nne, wakati wao wanajenga tani 15 ambazo hazina kiwango ikimaliza leo tu baada ya mwezi mmoja imejaa mashimo, imejaa matuta matuta.

Lakini hii inachangiwa kwa sababu kuna watu inaonekana wanampendelea mtu fulani na huyu *MECCO* kwa nini kampuni zote abebe yeye, unakuta Zanzibar asilimia 90 anajenga *MECCO* anawazidi wenzake kwa sababu ndani ya kule kwenye masuala yale watu wana mtu wao ameshahonga fedha anapewa *tender* ile, kuna watu wengi wanaomba wana kiwango kuliko *MECCO* na wana vifaa hawapewi *tender*. Barabara za Unguja na Pemba anazijenga yeye kila siku kwa kuingiza tu mambo yake kwa uenyeji anapewa *tender* hazina kiwango, fedha inayolipishwa kwenye barabara Mhe. Waziri utatakiwa utafute na wewe ndio mtoaji wa fedha unatakiwa uangalie fedha unazozitoa kuwapa Waziri wa Mawasiliano ni nyingi, barabara changa la macho tunadanganywa.(*Makofi*)

Barabara huko ulaya mimi nimezungumza na wahandisi kuwauliza kwa kufanya *research* tu Uturuki tu wananambia sisi tunajenga kilomita moja yenye upana wa mita 14 yenye tani sitini kwa milioni mia nane ya Zanzibar. Leo Zanzibar tunajenga sisi kiwango kibovu bilioni 1 na milioni 300, hizi ndio faida zinazoliwa za wananchi. Lakini hapa sasa ndio hayo ninayozungumza hii Serikali inaonekana kwamba haifanyi kitu kwa sababu ya watu hawa, hawezi kiongozi wa juu akamsimamia wa chini yule mwenye madaraka Mhe. Waziri upige *search* kama ulivyowasimamisha watu mwanzo watu uliowakamata, najua utapigwa majungu, watakusema lakini endelea na kazi yako kama ulivyoweza kuzuia mwanzo endelea kufuta. Sisi tunaona na tutaku-s*upport* kama mtu kweli hujamuonea kafanya manyago, wewe msimamishe kazi tu.(*Makofi*)

Jengine Mhe. Naibu Spika, suala la *Airport* ya Zanzibar imesomewa Al-badri au vipi, mbona haimalizi. *Airport* ya Zanzibar fedha zilizotumika nyingi, *airport* ni ghali dunia nzima na ndogo hii hatuoni aibu sisi. *Airport* ya Tanzania kubwa mara mbili nafikiri na nusu kuliko ya Zanzibar lakini bei takriban sawa sawa. Suala la *Airport* mimi nimelifanyia *survey* vile vile, nimechukua nikaongea na watu *Engineers* nimewatumia kila kitu, wanasema Wazungu *European Standard* haitozidi dola milioni tisini kuijenga *Airport* ile wakati sasa hivi dola milioni 218 na haijamaliza inakwenda suala la *Airport* ya Zanzibar. Na cha ajabu zaidi kwamba *Airport* kama ile hawapewi ma-*contractors* wadogo wadogo, wanapewa *contractor* waliobobeya inakuwaje *Airport* inafeli, *Airport* hata ku-*park* ndege haitoweza pale ilipo haijafungwa hata ile jeti bado, ikifungwa jeti ya watu kwenda kwenye *departure* haitoweza ku-*park* ndege kubwa pale.(*Makofi*)

Haya ni maajabu na haya ni maajabu ambayo yanasababishwa na watu wachache na hili ndilo suala ambalo lilifanya Serikali iingie kwenye deni kubwa kwenye suala la *Airport*, *Airport* haimalizi tutabakia kwenda kuomba

misaada, kuomba Mabenki waje wamalize lakini tuna deni watu washakula, watu washaharibu na hawajafanywa kitu. Hili Mhe. Naibu Spika, *CAG* alitaka kwenda kufanya uchunguzi akaomba milioni 30 utafiti tumefanya, akaambiwa na Wizara ya Fedha sasa sijui hii iliyopita akaambiwa huku kuna milioni tano tu, hivi nani mwenye mahisabu yake akaumize kichwa kuchunguza *Airport* ile mahisabu yote kwa milioni tano, wanamkwamisha mtu kwenye mahesabu na huyo *CAG* nai itafika wakati tutamchunguza, itafika hatua watu wanamfelisha kwenye uchunguzi kwa sababu tu hawajataka kutoa fedha ikachunguzwe. (*Makofi*)

Naomba sana Mhe. Rais na Mhe. Makamu wa Rais upo…….

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika zako mbili malizia.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Nimesema mwanzo Wizara tatu dakika 15 hakuna kitu ndio maana tunasema… *(Makofi).*

Suala la *Airport* nazungumza tena Serikali imeingizwa kwenye hasara mbaya sana. *Airport* ya Zanzibar hasara kubwa sana na tumefeli hivi kweli *Engineer* wa kujenga *Airport* akafelishe *Airport* ndogo kama hii, inamaanisha kuna watu waliingizwa mwanzo wanaowataka wenyewe kichwa mchungwa hawajui kitu wameharibu. Hilo mimi nimeshalisema na nitaomba sana nitalifuatilia zaidi.(*Makofi*)

Jengine suala la *PBZ* na *TRA* mimi nawashukuru viongoi wao wa juu ni watu wazuri sioni kama wana masuala ambayo ya kwenda kinyume nyume, lakini watendaji na haya mambo yanasababishwa kuna sehemu kuna madeni miaka kumi watu hawajesha kulipishwa lakini lilichangia na rushwa, itakuwaje kwamba Serikali inakusanya kodi kila siku *ZRB* au *TRA* mtu afike miaka kumi anakuja kudaiwa leo anaambiwa una deni la toka mwaka 2000 hujalipa wewe mpaka 2017 haiingii akilini, kuna watu walikuwa wanakula rushwa viongozi wao hawajui na watu wale ambao wamesababishiwa madeni wenye biashara wakati sio yao. Unakuta mtu toka mwaka 2010 kashakodisha sehemu yake mara nne kwa watu tofauti, kwa nini wasikamatwe wao akakamatwe mtu mmiliki, hivi vitu vipo watendaji nawaamini Makamishna waliopo ni watendaji wazuri wako safi mpaka sasa hivi, lakini watendaji wao kwa kweli wamefanya mambo sio mazuri. (*Makofi*)

Ningeomba sana masuala haya yasirudie mtu kama inakusanywa kodi isizidi miezi sita akionekana huyu mfanya biashara hajalipa miezi sita jengo lifungeni,

msingojee miaka kumi mkaja mkambaka mtu mwengine. Lakini Mheshimiwa....

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Nadir muda wako umekwisha.

Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf: Mimi nashukuru lakini ndio ukweli haujamaliza, mimi nashukuru sana na hii naiunga mkono. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi na tupo pamoja ahsante sana. Na hii ripoti nai--*support* kidogo tu. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Asha una dakika kumi na zinakutosha, sawa.

Mhe. Asha Abdalla Mussa: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kunipa nafasi hii ili kuzungumza machache na kuchangia katika ripoti.

Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi niungane na Wajumbe wenzangu kwa kuwapongeza Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo kwa kazi nzuri ambayo wameifanya na kutoa maagizo katika Wizara ambazo wanazisimamia, naamini wazi kwamba maagizo haya yakitekelezwa basi mambo yatakuwa mazuri.

Mhe. Naibu Spika, nianze kuchangia mambo haya yafuatayo. Kwanza nitaenda moja kwa moja kwenye sekta ya kilimo. Mimi nitazungumzia suala zima la zao la mwani. Wananchi wa ukanda wa pwani ambao wanalima zao hili la mwani wamevunjika moyo na kusababisha uzalishaji wa mwani kuwa mdogo kwa sababu ya bei ya mwani. Tunaiomba Serikali kwamba ione umuhimu wa kuwapa kipaumbele wakulima hawa wa mwani kama walivyopewa kipaumbele wakulima wa karafuu.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye shamba la mifugo la Pangeni. Mhe. Bi. Panya Ali Abdalla nimpongeze sana yeye kwa kulizungumzia suala zima la mazingira ya shamba hili la Pangeni, mazingira ya shamba hili kweli si mazuri lakini pia kuna matatizo ya maji na pia kuna matatizo makubwa ya njia. Hata hivi sasa ukiamua kutembelea katika shamba lile basi wakati wa mvua huwezi kufika katika eneo husika. Inasikitisha kwamba mwaka 2007 Mhe. Rais Mstaafu Mhe. Amani Abeid Amani Karume aliahidi kuitengeneza njia ile ambayo inatoka Pangeni mpaka Kichwele mpaka sasa njia ile haijafanyiwa kazi. Naomba sana Serikali ifanye jitihada ya kuhakikisha kwamba inaifanyia matengenezo njia ile.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala zima la madeni ya shamba la mipira. Kwenye ripoti hii kamati ilitembelea mashamba yaliyopo Pemba, lakini nataka

kukuhakikishia kwamba Mhe. Naibu Spika, mashamba haya Unguja yapo na hususan shamba lililopo Kitope Kichwele, inasikitisha hadi leo wafanyakazi ambao walikuwa wanafanyakazi katika shamba hili hawajalipwa pesa zao na wameweza kufungua kesi mahakamani, lakini cha kusikitisha waliomfungulia kesi hiyo Mahakamani hayupo hapa nchi. Kwa hivyo mpaka sasa kuna baadhi ya wafanyakazi ambao ni walinzi wanaolilinda shamba lile lakini tokea miaka hiyo ambayo mwekezaji amekimbia mpaka sasa hawajalipwa pesa zao lakini bado wana moyo wa kulilinda shamba lile.

Mhe. Naibu Spika, shamba hili liko katika hali ya hatari zaidi kwa sababu wananchi wamelivamia kwa kukata miti iliyomo ndani ya shamba hilo, lakini pia wenye mifugo wanapeleka mifugo yao na kuharibu mazingira. Naomba sana Wizara ya Fedha ichukue juhudi ya kuwaajiri watu hawa ambao wapo wanajitolea tokea kipindi hicho mpaka sasa ili waweze kulihudumia shamba hili kwa ajili ya kuweka mazingira yaliyo sahihi.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie na Bodi ya Mapato Zanzibar yaani *ZRB*. Kamati imesema kumekuwepo na baadhi ya wafanya biashara ambao hushirikiana na watumishi wa umma wasiokuwa waadilifu kuwepo kwa kukwepa kulipa kodi. Suala hili lipo kuna baadhi ya wafanyakazi wa umma wanashirikiana na wafanya biashara hawa wanakwepa kulipa kodi Serikalini badala yake wanachukua wao mapato haya na kujinufaisha wao kuliko kuinufaisha Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mhe. Naibu Spika, kumekuwa na nyumba nyingi ambazo zinalaza wageni lakini hawajasajiliwa lakini *ZRB* wanakwenda kukusanya mapato hatujui mapato haya yanakwenda wapi. Ningependa sana kumuomba Mhe. Waziri wa Fedha kupitia hii Bodi ya Mapato ya Zanzibar (*ZRB*) kuhakikisha kwamba haya mapato wanayoyakusanya kupitia wafanya biashara ambao wanalaza wageni kinyume na utaratibu, basi tuone kwamba nyumba hizi zinasajiliwa rasmi na kuhakikisha kwamba mapato yote yanaingia Serikalini.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda niseme niishie hapa naunga mkono ripoti hii, lakini pia niseme kwamba Mhe. Waziri wa Fedha pamoja na Wizara nyingine zilizohusika wakifuata maagizo haya na kuyatekeleza natumai Serikali yetu itakuwa imefanya jambo kubwa sana.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana naunga mkono *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Nakushukuru sana Mhe. Asha Abdalla Mussa. Waheshimiwa Wajumbe bado nina wachangiaji 15 na tunatarajia ripoti hii kufanya majumuisho leo jioni. Kwa hivyo tukifika jioni tukija hapa tutatengua

Kanuni ile ya Muda ili angalau kila mtu hata dakika kumi kumi aweze kuchangia, sote tuweze kuchangia. Na kwa wale ambao wanahisi kwamba anaweza kupeleka maoni yake kwa maandishi basi ningeomba sana wafanye hivyo.

Lakini tukifika jioni kama nilivyosema mwanzo tutafanya tutatengua kifungu cha Kanuni ya Muda wa dakika 15, tufanye dakika 10 ili ili kila mmoja wetu aweze kupata nafasi ya kuchangia.

Baada ya kusema hayo Waheshimiwa wajumbe naahirisha kikao hichi hadi Saa 11.00 jioni nawashukuruni sana.

(Saa 6.56 Mchana Baraza liliahirishwa hadi Saa 11.00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano Yanaendelea)

Mhe. Naibu Spika: Mchangiaji wetu wa mwanzo atakuwa ni Mhe. Maryam Thani baadae atafuata Mhe. Omar Seif Abeid ambaye simuoni hapa na baadae anaweza kufuata Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mhe. Maryam karibu.

Basi aje Mhe. Miraji Khamis Mussa.

Mhe: Miraji Khamis Mussa: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia jioni hii ya leo ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo. Kwanza nimpongeze sana Mwenyekiti pamoja na Kamati yake kwa ripoti yake nzuri, imezingatia mambo mengi sana na wameishauri vizuri Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba niungane na Kamati katika ukurasa wa mwanzo wa kitabu hichi kunako eneo la mfululizo wa maagizo yale ya kamati iliyopita ya Baraza la Wawakilishi na wao wameyaona na wameyafanyia kazi na wameweka muendelezo wake. Eneo lenyewe ni asilimia 29 ya ajira kwa mgawanyo ule wa asilimia 29 na 79 kama ambavyo wameandika katika kitabu hichi mgawanyo wa ajira kupitia *TRA*.

Mhe. Naibu Spika, eneo hili lina masikitiko makubwa sana na kwa muda mrefu na ni sehemu niseme tu ya changamoto katika serikali zetu hizi mbili. Tumetoa wenyewe wenyewe asilimia hizi za mgawanyiko huo wa nafasi lakini utekelezaji wake umekuwa mgumu. Kwa hivo hadi sasa wakati tunapitia ripoti

hii kuna asilimia ndogo sana ya nafasi za Wazanzibari kuingia katika chombo hiki kikubwa kwa mgawanyiko ulikuwepo hivi sasa. Hata ukifuatilia utakuta hata ile asilimia 2 ya ajira kwa wale wanaoajiria Wazanzibari pia haifikiwi. Kutokana na mapendekezo haya ya kamati wao waliyakuta kamati zilizopita, hapa wameweka ni sehemu ya muendelezo wa hili. Basi tuiombe serikali katika yale mambo ambayo watakuja kutupa majibu ya moja kwa moja hasa pale mwezi wa Septemba, basi hili nalo liwe ni sehemu ya kuwa limeshatatuliwa na utaratibu unaendelea kwa mujibu wa mgao ule ambao tumejiwekea wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, naomba nende katika ukurasa wa 5 kunako utekelezaji wa bajeti, lipo eneo ambalo linaigusa Wizara ya Fedha hasa Kitengo kile cha Uhakiki Mali. Juzi tu tumepitisha Sheria ya Fedha, Sheria ya Manunuzi. Sheria mbili zile zitatusaidia sana kusogeza utaratibu mzima wa manunuzi lakini huko tunakotoka yapo mapungufu mengi yalitokana na sheria iliyokuwepo, lakini pia yalitokana na wasimamizi wa ile sheria yenyewe au wale ambao wanapaswa kufuata sheria ili twende katika ustaarabu mzuri wa matumizi ya fedha za umma na uhaulishaji wa mali za serikali.

Mhe. Naibu Spika, lipo tatizo katika eneo hili, kwanza katika mfumo wa uwekaji kumbukumbu za mali za serikali pana tatizo kubwa sana katika eneo hili. Ukitembelea Wizara za Serikali kila Wizara ukimwambia akupe *asset register* uone zile mali za serikali zinahifadhiwa vipi, labda *depreciation* yake inakuwaje. Hakuna mfumo wa pamoja lakini hakuna hata hivyo vitabu vyenyewe baadhi ya taasisi za serikali. Kwa hivyo lipo tatizo kubwa katika eneo hili.

Mhe. Naibu Spika, wakati fulani sisi tuna kamati ambayo ilitembelea karibu Wizara na Taasisi zote. Tulikwenda Mkoa wa Kusini Unguja, tukaulizia *asset register* halipo, lakini tukaulizia mali ziliopo katika mkoa ule, wakazisema. Lakini mali ambazo katika kuendeleza kuwahoji kuna mali za magofu yale ambayo yalikuwa yamo ndani ya Mkoa wa Kusini, kuna nyumba ambazo zilikuwa zipo ndani ya Mkoa wa Kusini, basi nyumba zile tunawauliza wanasema sisi tuliletewa tu agizo na agizo lenyewe lilikuja kwa mdomo kuwa mali hizi ziende katika taasisi nyengine, kitu ambacho sio utaratibu wa serikali.

Mhe. Naibu Spika, uwepo wa *asset register*s hizi hata ile mali itakapokuwa inahamishwa kutoka taasisi moja kwenda nyengine basi pale inapotoka pawe na utaratibu mzuri lakini na kule inakokwenda pia kuwe na utaratibu mzuri. Pia tulitembelea Wizara ya Kilimo kukawa pia kuna agizo la kamati nyengine kama kamati hii ya Baraza. Kuna gari pale ilikuwa inatumika katika Wizara ya Kilimo, kuna mtendaji mmoja kaondoka na gari ile mpaka kwenda kunako

Tume ya Ukimwi, kipindi hicho Tume ile iko katika Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais. Lakini sasa mtendaji yule karudi huko huko Wizara ya Kilimo, hiyo gari amerudi nayo, gari kaiwacha kule. Lakini kile kipande cha *asset register* ya Wizara ya Kilimo inaonekana pale.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukisogea katika wizara ile ambayo alikwenda nayo ile gari na baadae haikurudi, tunajua ni gari ya serikali lakini kwa nini inapotoka kwenda katika taasisi nyengine hawa walitakiwa watoe lakini na taasisi nyengine ipokee, sasa ndio utaratibu mzuri. Kwa hivyo hakuna utaratibu mzuri katika eneo hili la uwepo wa *asset register* mali za serikali zikawa zinasimamiwa vizuri lakini eneo moja ambalo nilikuwa nataka kulizungumzia ni hili la mfumo ule ambao ungetolewa pamoja katika kusimamia mali na lile punguzo la thamani na zile mali zenyewe kama ambavyo nilisema mwanzo ile *depreciation* yake, wawe wanawekewa utaratibu kwa hivyo utaratibu sasa haupo. Sasa tunamuomba Mhe. Waziri wa Fedha katika eneo hili alisimamie vizuri tumepisha sheria nzuri ambayo naamini tukiisimamia vizuri itatufikisha pahala pazuri ili kuepuka mali hizi za serikali kupotea bila ya sababu yoyote.

Mhe. Naibu Spika, nije katika eneo hili la Wizara ya Fedha la madeni ya mashamba ya mipira, tumeona kamati wameripoti vizuri kuna deni la dola laki 4, tukifuatilia utaratibu mzima ambao tuliipata hii Kampuni tunakuta tuliingia naye mkataba, mwaka wa mwanzo hakulipa dola laki moja kwa sababu mkataba unaonesha malipo yake ni dola laki moja, mwaka wa pili umepita ni zimekuwa dola laki mbili, mwaka wa tatu dola laki tatu, mwaka wa nne dola laki nne. Hapa serikali ndiyo inakuja kutoa ripoti kwamba hii kampuni imeshindwa. Mhe. Naibu Spika, miaka minne hakuna utaratibu wa kulipa na hajalipa hata mwaka mmoja, tumekaa mpaka ndani ya miaka minne, ni kitu gani kilichotufikisha huku, mkataba ulikuwa unasemaje, hata tukae miaka minne kampuni haijalipa tunakuja kushtuka kipindi cha miaka hii minne ndio tunakuja kumuona.

Mhe. Naibu Spika, lakini pana tatizo ndio maana nikasema kwamba utaratibu huu tutakapokuwa tunao mzuri katika kuweka mali za taasisi basi tuone katika maeneo hayo tunakwenda vizuri. Hapa kuna agizo la Mkuu wa Mkoa limetoka ndani yake. Mkuu wa Mkoa huyu katoa barua ya kukipa kikundi badala ya hii kampuni, mkataba haujavunjwa, Mkuu wa Mkoa anatoa barua. Sasa mali hii ukiifuatilia ni mali ya nani ya Serikali Kuu kupitia Wizara ya Fedha au Mkuuwa Mkoa wa Kaskazini Pemba. Sasa baadae katoa hapa barua na *reference* ipo, sasa tunaona muingiliano wa majukumu. Sasa tuone pale ambapo tutakuwa tuna usimamizi mzuri na kila mtu anajua mali yake, ndio maana tukasema tuwe na utaratibu mzuri wa kulinda mali zetu kupitia *asset*

register ambayo kila moja atajua hii mali yangu hii si mali yangu. Sasa hapa Mkuu Mkoa ameingia katika utawala wa mamlaka nyengine. Sasa Mhe. Naibu Spika, tuombe sana utaratibu huo tuwe tunakwenda nao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, lakini ukurasa unaofuata mahala ya serikali tunaona pia katika eneo hili kuna mahala saba yameuzwa na unapouza mali ya serikali, upo utaratibu umewekwa wazi, sijui yameuzwa mwaka gani lakini naamini ukifuatilia utaratibu wa kuuzwa maghala haya haukwenda vizuri. Mhe. Naibu Spika, tunamuomba Mhe. Waziri atwambie tu takriban haya maghala saba yameuzwa kwa utaratibu gani, kulikuwa kuna tenda au kuna ule utaratibu wa matangazo ya kuuza mali za serikali, tujue ule utaratibu kwa ujumla, walipitia katika eneo gani mpaka maghala saba haya yameuzwa lakini kwa nini serikali inauza mali zake. Leo tunaweza tukauza magari kwa sababu yameshakuwa machakavu, lakini kuuza maghala kwa maana kwamba unauza na eneo pia. Sasa sijui utaratibu gani uliotumika hapa.

Mhe. Naibu Spika, sasa nimuombe Mhe. Waziri wa Fedha basi kidogo aje atupe utarabu ambao wenzetu waliotumia. Lakini nisisitize katika haya yaliyobakia basi iwe ni sehemu ya *assets* za serikali, tusiendelee kuyauza haya kwa sababu iko siku tutakuja kuuza kila kitu basi hata tutakapokuja kutaka kuhifadhi au kuhuisha maeneo yetu kiserikali tutashindwa. Kwa hivyo nimuombe Waziri wa Fedha katika eneo hili.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu eneo la Bodi ya Mapato, mimi naomba nilichangie eneo hili kwa mara zote tunajua kwamba Bodi ya Mapato ni Wakala wa Serikali na anafanya kazi kubwa sana. Mimi niwapongeze viongozi wa Wizara lakini niwapongeze na viongozi wa Bodi ya Mapato. Katika tathmini ukipeleka ile ya uwajibikaji katika makusanyo yake, ripoti zake za makusanyo kwa ule uwakala wa serikali nzima kwa sababu hapa ndipo tunapopitia au tunapoponea. Hatujapata ripoti za tathmini ambazo zinatuonesha kwa kiwango hichi walichokusanya basi wamefanikiwa kwa kiasi kizuri sana. Lakini wadaiwa wapo wangapi, leo tuliambiwa pale kuonekana tunapewa yale madeni ya jumla tunayodaiwa lakini mengine ambayo yalikopwa lakini kuna watu tunawadai sisi kupitia taasisi hizi.

Mhe. Naibi Spika, sasa kile kipimo cha uhalisia cha kupima taasisi hii kwa kazi wanayoifanya haipatikani, kupatikana kwake maana yake wende hawa wakafanyiwe ukaguzi yakinifu kwa mapato yao tu yale wanayoyakusanya, *sources* zetu zote ziwekwe wazi. Kiwango gani kinachotakiwa tukipate lakini mwisho wa mwaka tuone haya tumefanikiwa na haya hayakufanikiwa na yapo katika uratibu gani ambao tunaweza tukaufahamu.

Sasa Mhe. Waziri wa Fedha tuone tuna Mwenyekiti wa Kamati katika eneo moja ambalo la kupima uwezo wa Wakala katika ufanisi wake wa kazi ni lazima tufike pahala kunako eneo la ukusanyaji wa mapato haya kama ni wakala wa Serikali nalo likaguliwe mapato tu, kwa msururu mzima wa zile *sources* ambazo zinaingiza mapato ya Serikali Kuu, basi tuone sio tunafika pahala tunakuja kupiga makofi kwa hesabu ya jumla tumekusanya bilioni 6 mwaka jana zilikuja bilioni 2, lakini bilioni 6 kwenye *sources* zipi na tulikuwa tufanikiwe vipi. Sasa lazima kunako eneo hili kila baada ya muda tuweke utaratibu wa kuonyesha.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Miraji Khamis Mussa: Aah! ndio tunatumia dakika kumi kumi, maana yake hatujatengua muda.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimalizie katika eneo la mfuko wa Barabara. Eneo hili lipo tatizo la utumiaji wa fedha zile za mfuko pale ambapo tunawatafuta wakandarasi wetu, ile *value for money* haipatikani. Sitaki nizungumze sana kwa sababu Kamati ya Fedha hii na Kamati ya *PAC* kuna mambo yanaingiliana unaweza ukasema huku na kule ukaja kuanza kuyasemea kabisa. Lakini niseme kwa ujumla naomba nilizumze hili kunako utaratibu mzima wa kuwapata wakandarasi hapa hatuko vizuri. Wapo watendaji ambao hawaitakii mema serikali hii wana-*deal* zaidi na *interest* zao, wanatutafutia makampuni ambayo uwezo wake hata wakijenga hizo barabara ukenda ukazikagua hufiki katika madhumuni halisi ile *value for money* haipo. Kwa hivyo nikuombe sana Mhe. Waziri katika eneo hili na mwenyekiti wa Kamati jitahidini sana kutafuta watu waadilifu, makampuni ambayo yana uwezo yapo, ushindani utapatikana katika mfumo ule ule wa *tender* lakini kazi ifanyike vizuri. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, na mimi naomba nianze kuzitumie zile dakika 10 kama ambavyo ulitushauri mapema. Liko eneo moja la *ZSTC* nitamuandikia Mhe. Waziri kwa maandishi. Nakushukuru sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe kama mtakumbuka mchana kabla ya kuondoka hapa nimesema kwamba itatubidi kwanza kutokana na ratiba yetu inabidi leo tumalize ripoti ya Kamati hii.

Lakini nikasema kwamba tutakubaliana hapa tutumie dakika 10 badala ya dakika 15 kwa sababu wachangiaji bado ni wengi. Sasa nilikuwa namuomba

Waziri katika Ofisi ya Rais atutengulie kifungu cha kutumia dakika 15 badala yake tutumie dakika kumi. Mhe. Waziri karibu.

KUWEKA KANDO KANUNI YA 58(6)

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Rais na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi: Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa maelezo yako uliyoyatoa ya awali yanaashiria juu ya umuhimu wa kumaliza kazi ambazo tumejipangia kwa mujibu wa mtiririko wa kazi yaani *order paper* ya leo na kwa kuzingatia wachangiaji wengi wana dhamira ya kutaka kuchangia.

Naomba Mhe. Naibu Spika, tuweke Kanuni kando chini ya Kanuni ya 58 (6) inayohusiana na muda ili tuweze kupata nafasi ya kuchangia wachangiaji wengi kwa madhumuni ya kupunguza muda kutoka dakika 10 kwa kuongeza wigo wa wachangiaji wengi.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Naomba kuwauliza wale wanaokubaliana kwa kuchangia kwa dakika 10 wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda. Tunaendelea Waheshimiwa.

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Mchangiaji wetu anayefuata ni Mhe. Abdalla Maulid Diwani baadae atakuja Mhe. Bahati Khamis ajitayarishe.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa fursa hii nikachangia ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia mchana huu kukutana.

Mhe. Naibu Spika, nikenda moja kwa moja katika hoja yangu kwanza niipongeze Kamati kwa kazi nzuri waliyoifanya kwa kuleta ripoti mwanana kabisa ambayo haina shaka ndani yake. Leo hii tunaipitia au tunaichangia ili ipate nguvu serikali kuyafanyia kazi yale yote tunayoyachangia. Isiwe haya tunayoyachangia humu ikawa kama tunapiga kelele tu tunaimba tarabu halafu

tunaondoka, itakuwa hututendei haki. Tunazungumza mambo ya msingi kabisa na yenye mustakbali wa maendeleo ya nchi yetu basi naomba sana Mawaziri haya masuala muyachukue na mtakapokuja katika mwezi wa Septemba yawe yameshapatiwa majibu yake.

Mhe. Naibu Spika, niende katika hoja katika ukurasa wa 3 ambapo tunazungumzia Taasisi za Muungano tunakuta *TRA* pale. Kwanza nipongeze *TRA* Zanzibar chini ya uongozi wa Kamishna Mcha wanafanya kazi vizuri sana. Katika taasisi ninayoitambua mimi ya Muungano au taasisi inayofanya kazi Zanzibar basi *TRA* wale jamaa wanastahiki pongezi sana tena, wanafanya kazi vizuri sana, hawamuonei mtu, wanasimamia sheria zao ipasavyo hatimaye wanafika malengo ya kukusanya na nchi yetu inaenda mbele zaidi. Lakini katika hayo napata wasi wasi kwamba kuna mambo ambayo ni haki yetu kama Zanzibar tunanyimwa kutokana na hii *TRA*. Hapa katika ripoti ya Kamati Mhe. Naibu Spika, naomba ninukuu kidogo ili nione mwanga wapi umekalia.

Ripoti ya Kamati inasema Kamati yetu iliendelea kusisitiza kuharakishwa kwa marekebisho ya muundo huo wa uongozi wa Mamlaka ya Mapato *TRA* iliyopo hivi sasa, kwani imekuwa ni kero ya muda mrefu na Kamati zilizopita zimekuwa zikilizungumzia suala hili mara kwa mara, tunaomba sana utekelezaji wa agizo hili kwa hatua iliyofikia ifanywe haraka ili kuondoa kero hii ya muda mrefu. Vile vile Wizara isimamie *I mean that* ni Wizara ya Fedha si Wizara nyengine yoyote.

Mhe. Naibu Spika, vile vile Wizara isimamie utekelezajiwa wa makubaliano ya ajira ya asilimia 21 katika kitabu hicho wamekosea lakini kwa asilimia 21 kwa Wazanzibari na 79 kwa Bara, Zanzibar hatupati kulikoni. Ripoti ya Kamati Mhe. Waziri imekuelekeza, itakapokuja Septemba tujue nini tunafanyiwa, imefika wakati sasa hivi lazima tulilie haki zetu, sio hapa tu hata kwa upande wa *BOT* ni hayo hayo. Mhe. Naibu Spika, wanaonekana zaidi wale kule akina Mushi na wengineo, samahani sijamtaja mtu jina ni kabisa hilo, akina Mushi wana nguvu zaidi katika vyombo vile kuliko sisi huku kina Hamad wanatuonea. Kwa hivyo haki yetu tupewe katika hicho, ifike wakati lazima haya yanayoandikwa au yanayoelekezwa na Baraza la Wawakilishi yasimamiwe ili ipatikane haki katika vyombo hivyo vya muungano. Hicho tu cha kuchekesha zaidi ndani ya *TRA* hata muundo wao nimekuja na *diary* ya kwao hii *TRA* uthibitisho tosha.

Mhe. Naibu Spika, humu ukiangalia wana *address* au wana mawasiliano na Mameneja wote wa Mikoa, Zanzibar hatumo na Zanzibar nayo ina meneja wake hata jina nimtaje Ali Bakari yupo pale humu hayumo. Lakini cha

kushangaza zaidi hata huyu Kamishna wetu sisi hapa tuna *Deputy Commissioner* wa *TRA* ambayo imekusanya *custom* na *income tax*. Lakini katika utendaji wao wa kazi *deputy* yule Kamishna wa *TRA* anawajibika kwa Kamishna wa *customs* ni tatizo. Huu muundo ilikuwa hata iwe vipi lazima wakati panapo *Commissioner General* wana Makamishna wake wawili wale, basi Kamishna mmoja yuko Zanzibar kwa sababu ni *Deputy Commissioner Tanzania Revenue Authority.*

Mhe. Naibu Spika, lakini vyereje Kamishna yule anawajibika kwa Kamishna wa *Custom Excise Duty* ni makosa ni ya muda mrefu haya, mwenye macho haambiwi tizama na sisi pengine kwa hofu yetu au tunaogopa, tumeungana hizi nchi Tanzania Bara na Visiwani nchi mbili sawa sawa hakuna tofauti ya udogo, ikiwa udogo wa watu au tuseme ukubwa wa eneo namna gani. Lakini tumekwenda katika Muungano zimeenda nchi mbili. Kwa hivyo inapokwenda fursa zitumike vile vile tulivyokubaliana. Suala la ajira asilimia yetu 21 tuipate, hata thamani ya *Deputy Commissioner* wetu wa *TRA* apatikane. Kwa hivyo Mhe. Waziri ninajua ripoti itakuja na siku zote mnazungumza katika kero zenu hizo ijapokuwa hizo kero hamziweki wazi mnazibana bana hatufahamu kwa sababu gani. Laiti kama mngekuwa mnazizunguza hizi kero halafu mnaziweka wazi ingetusaidia hata sisi wengine wakaidi tukenda kupambana nayo hili.

Mhe. Naibu Spika, niende katika suala langu jengine nizungumzie juu ya suala la *ZRB*, nayo niipongeze *ZRB* inafanya kazi vizuri sana, inakusanya mapato vizuri sana lakini baadhi ya tu maofisa wa *ZRB* sio waaminifu na hawaitakii mema Zanzibar. Hapa juzi niliuliza swali lakini Mhe. Waziri akalizonga zonga kidogo pengine hakulifahamu au vipi nilizungumza suala zima la kupatana katika ulipishaji wa kodi, nilikuwa na maana hii ambayo naomba kuelezea. Mhe. Naibu Spika, unapokwenda Ofisa wako katika hoteli zetu umekuta wageni 40 basi ili ufaidike wewe unamwachia mwenye hoteli yule wageni 20 tuwaandike kwenye kitabu cha mapato ya *ZRB* hawa 20 tukubaliane mimi na wewe. Wewe chukua kumi na mimi nichukue kumi tuendelee mbele ndio kodi ambayo niliyokusudia mimi kwamba wanapatana ambao si utaratibu. Wageni wote wanatakiwa waandikwe kwenye vitabu vile ili kodi yake ikusanywe iendelee mbele kupeleka katika Serikali yetu. Ndio maana nikasema kwamba hata baadhi ya maofisa *ZRB* si waaminifu kwa sababu hilo suala linafanyika sana. Mimi niko kwenye *field* ya hoteli nakumbana nayo.

Mhe. Naibu Spika, si hilo tu hata kutozwa kodi kwa vishindo, nilizungumza katika Baraza lililopita la bajeti mpaka leo bado muundo ule unakwenda tu, kwa nini unakwenda kukusanya kodi na masilaha. Kuna wageni unaingia vyumbani kwa sababu gani hatuna njia nyengine ambayo iliyokuwa nzuri.

Mgeni kaja Zanzibar kutembea *paradise Island,* leo hii usiku kalala chumbani mgeni anagongewa mlango anakuta maofisa wana *SMG,* hee*!* sio vita vile watu wamekuja kustarehe huku. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, watendaji hawa basi hii tabia waondokane nayo ili twende katika kukusanya kodi kwa njia nzuri na watu wazidi kuipa sifa nchi yetu. Kwa sababu nchi yetu inasifika sana nje lakini tunaiharibu katika mifumo hii tu kama ukusanyaji kodi na mengineyo.

Mhe. Naibu Spika, niende mbele nizungumzie juu ya ukurasa wa 14 wa *People Bank of Zanzibar*, nayo niipongeze wanafanya kazi vizuri kila pahali sasa hivi wanatufungulia *ATM* wanafungua matawi, lakini pale katika Benki ya Zanzibar Tawi la Malindi bado kuna changamoto. Mhe. Naibu Spika, usiombe mwisho wa mwezi huu ukenda pale kuna vidirisha pale vitano lakini utakuta wafanyakazi wawili foleni yake mpaka nje aibu. Kwa sababu siku zote mnaajiri watu wako wapi watu wa kukaa katika *tellers* zile wakafanya kazi. Leo utakuta *tellers* ziko mbili tu msongamano wa watu chungu nzima pale tunapotezeana muda angalau benki unakweda pale dakika zako kumi au tano umalize kazi, ukenda benki unatumia zaidi ya saa moja masaa mawili hasara hiyo, itatupeleka kubaya, pamoja na kufanya kazi vizuri sina mashaka kwa hilo najua wanafanya kazi vizuri wanaboresha kila kitu lakini changamoto ya zile *tellers* zao katika sehemu ya kutoa na kuweka fedha kidogo ningeomba basi wabadilike.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, na Mhe. Waziri unalifahamu lishaulizwa sana suala hilo lakini bado hawataka kubadilika. Nitaomba sana lazima wabadilike tunakwenda na wakati sasa hivi tuondokane na kwenda kukaa benki masaa mawili saa moja mnatupotezea muda. Mhe. Naibu Spika, wabadilike waweke *tellers* wengi katika madirisha yale watu waingie pale watu waingie pale dakika tano sita bila foleni wafanye kazi.

Mhe. Naibu Spika, nikenda mbele nakwenda katika Mfuko wa Barabara. Mimi leo kupongeza tu na kusema madogo tu niupongeze vile vile unafanya kazi vizuri sana Mfuko wa Barabara. Lakini kufanya kazi wakati wote Mfuko wa Barabara nao tuuangalieni tena, shilingi mia moja kwa lita kwenye Mfuko wa Barabara bado tunaionea na mahitaji ya barabara sasa hivi iko kwao wao wanajenga barabara zetu vizuri sana lakini mapato yamekuwa kidogo.

Ninafikiri Mhe. Naibu Spika, hili ningeomba tu uje na hoja rasmi ya kuweza angalau basi kutoka shilingi mia angalau tuwape japo hamsini au mia mbili, wakusanye nyingi ili waweze kutoa zile pesa na kuweza kutujengea barabara zetu na Zanzibar yetu hii ikang'ara kwa sababu kumekuwa na changamoto sana ya makusanyo madogo. Inapokuwa makusanyo madogo huwezi ukatoa pesa

zile kwa wakati au miradi ya ujenzi wa barabara yakaenda kwa wakati. Ni kusuasua ikawa tunasubiri tu mpaka yapatikane mwezi huu, tukate huku yaongezeke lakini utakapoongeza hii shilingi mia nyengine au shilingi 50 basi inaweza ikatupa nguvu ikawa kidogo tuna pesa za kujidaia tukaweza kufanyia kazi vizuri.

Mhe. Naibu Spika, vile vile niende katika mradi wa nyumba *ZIPA*, ninashukuru sana dhana nzima ya Mhe. Rais wa Zanzibar Dkt. Ali Mohamed Shein katika kuweka wawekezaji kweli Zanzibar baada ya miaka 5 hii kumalizika itakuwa imepiga hatua na imeng'ara kwa kweli, tunampongeza sana kwa moyo wa ujasiri kuweza ku-*propose* mpaka sasa hivi kwa wajenzi mbali mbali wa majumba ya maendeleo katika nchi hii. Lakini uhalisia wa nyumba hizi zinazojengwa sasa hivi...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Abdalla Maulid Diwani: Ahsante sana ninaendelea. Katika nyumba hizi basi angalau naziwepo na zile nyumba za wafanyakazi angalau wale wa kima cha chini waweze kuzinunua. Majumba yanayojengwa kule ya dola laki mbili na nusu, laki tatu na nusu hawa wenzetu sisi watakuwa na uwezo kweli. Huu mradi umejenga zaidi kwa wageni watu wenye pesa kuliko sisi wenyewe. Kwa hivyo ningeomba tu Serikali ikae nao hawa watu angalau waweze kuwapangia kwamba ije miradi ambayo hata wafanyakazi wenye kima cha chini mishahara yao waweze kununua nyumba zile, ukitizama sasa hivi hata huo mchanga wenyewe ushauzuiliwa pengine viwanja wanataka kunyan'ganywa ili watu pesa zile wende wakanunue zile nyumba kwa bei rahisi waweze kuendelea na maisha yao.

Mhe. Naibu Spika, niende ya mwisho kabisa kwa sababu muda umekuwa mdogo nazungumzia Wizara ya Fedha na Mipango ikiwa chini ya daktari. Wizara ya Fedha katika bajeti iliyopita tulisema maneno haya kwamba kuna baadhi ya wafanyakazi si waaminifu lakini Mheshimiwa ka-*react* haraka iwezekanavyo kachukua hatua na akaunda Kamati au Tume Teule ya Kuchunguza, yale mambo yameshakwisha ninafikiri hata ile Kamati imeshavunjwa. Nini kinachoendelea muda huu ile Kamati ilikuwa karibuni miezi 6 sasa hivi miezi 8 kuna watu wengine wako nje maskini ya Mungu, wengine hawahusiani hata na hizo pesa wametiwa kwa sababu ya ushoga wa mtu na mtu ikaonekana kama kaingizwa, basi iwekwe wazi kama kesi inapelekwa Mahkamani wapelekwe Mahkamani wakishapelekwa Mahkamani waambiwe kinachoendelea ili wajitambue, muda ushakuwa mwingi, uchunguzi ushapita.

Mhe. Naibu Spika, nitaomba sana kwa Mhe. Waziri katika hili uliangalie najua umeweka taratibu zako na utafute njia nyengine kwamba wasiokuwa na hatia warudishwe, wenye makosa washtakiwe wasiofaa wafukuzwe, wafungwe yote inawezekana. Lakini wale ambao hawana hatia tunawaumiza. Ninaomba sana Mheshimiwa.

Mimi nilikuwa niseme hayo tu kwa muda huu ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hiyo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Abdalla Maulid Diwani. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Masoud Abrahman Masound baada ya hapo atafuata Mhe. Bahati Khamis.

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii jioni hii. Mhe. Spika, mimi nianze moja kwa moja na Wizara ya Biashara.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi wafanyabiashara wengi katika maeneo mbali mbali ya Zanzibar biashara zimekuwa ngumu kidogo. Lakini Mhe. Spika, hali ya leseni za biashara zimekuwa kubwa, nimuombe Mhe. Waziri mfanyabiashara wa mama ntilie kwa siku moja anapewa risiti anachangia shilingi elfu moja. Kwa mwezi ukipiga itakuwa ni shilingi 30,000/= ukipiga kwa mwaka anachangia pesa nyingi sana karibu laki tatu na.

Lakini la kushangaa Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu ilitembea hospitali ambayo tunasema ni kubwa kwa Zanzibar ambayo ni *Global* inatozwa leseni ya shilingi laki mbili kwa mwaka, ni suala la kusikitisha na linatoa machozi. Mama ntilie anatozwa shilingi 360,000/= lakini *Global* anatozwa shilingi laki mbili kwa mwaka mmoja. Kwa hivyo niomba Wizara hii ya Biashara ifanye kazi yake vizuri na ihakikishe Waziri wa Fedha ile kwenye kodi basi ile kodi itolewe kodi ambayo ina uhakika. Mwenye biashara ya shilingi milioni tatu anafanya kwenye eneo la Bububu anakatishwa leseni ya shilingi laki moja lakini mwenye biashara ya mabilioni ya shilingi anatozwa shilingi laki mbili inasikitisha na inauma sana. Kwa hivyo niiombe Serikali kwenye hili ihakikishe angalau inachunguza hii hali ya leseni za biashara. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye Mhe. Waziri wa Kilimo. Kwanza nimpongeze sana Mhe. Waziri wa Kilimo kwa ahadi yake ambayo kaiweka muda wa miezi kumi atajitahidi sana, sasa hivi miezi kumi tumeshatimiza kuwa tutakuwa uagizishiaji wa chakula utapungua na niseme tu

anajitahidi sana na Mwenyezi Mungu ampe nguvu za kutusaidia zaidi ili ahakikishe hili linafanikiwa.

Mimi niende moja kwa moja kwenye suala la kilimo cha kutegemea mvua. Kilimo cha mpunga mara hii matrekta yameanza mapema sana nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na watendaji wake, lakini niseme bado matrekta ni kidogo sana kwa Zanzibar. Matrekta Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi mara nyingi inapofikia msimu wa kilimo huwa unasikia kuwa Serikali wameagizishia matrekta. Lakini baada ya miaka mawili matrekta yale yote huyaoni, hatuna uhakika yamekwenda wapi. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri atakapokuja hapa labda atwambie mwenzangu mmoja alisema kila majimbo matano wapate matrekta mawili. Lakini mimi ninachoomba haya matrekta mengi ambayo yameagizishiwa kuanzia mwaka 2010 alipokuwa kakamata utawala Dkt. Ali Mohamed Shein basi atwambie matrekta yote yaliyoagizishiwa, mangapi mazima yanafanya kazi na mangapi hayafanyi kazi na mangapi yaliyokuwa yameondoka yameuzwa au yamefanywa shughuli nyengine atuthibitishie hilo.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri kwenye hili kuna suala zima la pembejeo. Nimpongeze Mhe. Waziri mpunga wa mbegu tumeupata lakini kwa bahati mbaya mbegu zilizoletwa mara hii sio mbegu bora ni mbegu ambazo ndani ya *packet* ambayo ina mpunga wa mbegu humo mna mpunga wa *super DC,* mna mpunga wa saro, mna *super bikeni* ndani ya kipaketi kimoja. Kwa hivyo lile lengo la wakulima kupewa mbegu bora halipo. Kwa hivyo nimuombe Mhe. Waziri labda akija hapa atuthibitishie kwa sababu wakati mwengine suala hili la mbegu linakuwa tunachanganywa na neno mbegu. Kwa sababu Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi aliambiwa kuna mbegu nzuri sana tukaletewa Nerika, lakini mbegu ile haifai hata kula.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo na hizi tumuombe sana Mhe. Waziri atakapokuja hapa atuambie, lakini pia kuna suala la mbolea, mbolea wakulima sasa hivi wameamka wakulima wengi wanalima, suala la mbolea inakuwa kidogo sana. *Packet* ya kilo 25 mnaambiwa wakulima wanne mgawane kwenye kipaketi hicho kimoja. Pengine mkulima ana ekari mbili anatakiwa achukue kilo kumi na mbili na nusu kwa kweli haitoshelezi. Kwa hivyo naomba Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri atakapokuja hapa atwambie. Lakini pia nimpongeze Mhe.Waziri katika zile ekari 50 jimbo langu limefaidika ambalo litapata pembejeo za aina zote kwenye ekari hizo 50.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye mpunga wa umwagiliaji maji, juzi nilimuuliza Mhe. Naibu Waziri wako hapa Serikali ina mpango wa kuweka

miundombinu ya umwagiliaji maji, suala langu nilipomuuliza aliponijibu sikumuelewa vizuri. Nia ya Serikali sasa hivi kuhakikisha tuna eneo dogo lakini tunazalisha mpunga mwingi. Lakini sasa hivi kinachojitokeza kwa wakulima wenyewe wanatakiwa wajenge misingi, wenzetu wa *TASAF* wanakuwa wanatusaidia, ninashukuru na Serikali inakuwa inatusaidia suala la umeme, lakini bado wakulima ni mzigo mkubwa kumwambia ajenge msingi wa matofali na kazi hii bado wanapewa wakulima. Kwa hivyo niiombe Serikali ukija hapa utwambie basi ile misingi angalau utaweza kutusaidia kwa kujenga kwa matofali lakini pia uniahidi kutupatia mbegu bora ambayo wakulima wetu haitowapa tabu katika kuhakikisha wanazalisha mpunga mzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, Kizimbani Mhe. Waziri unakujua ni mwenyeji sana miaka miwili au mitatu iliyopita tuliwenda kuweka jiwe la msingi kwenye kiwanda ambacho tunategemea kitasindika mazao. Lakini kiwanda kile tunaona Mhe. Waziri mpaka leo hatujui mwisho wake utakuwa nini na matunda Zanzibar sasa hivi kama unavyoona, sasa hivi ukitembea barabarani vikeri vyote vina embe dodo na embe shomari, zinaharibika bure. Kwa kweli kama tungekuwa na viwanda wananchi wetu wangekuwa wamepata angalau pahali pa kupeleka matunda yao. Kwa hivyo niombe kile kiwanda ambacho kimetengenezwa kule Kizimbani uweze kutupatia maelekezo yake.

Lakini pia wenzangu walichangia kuwa suala la kuanzisha viwanda vidogo vidogo, kwa hivyo na mimi niliunge mkono na ikiwezekana Mhe. Waziri basi uje utwambie kama bajeti ijayo labda kwenye vikundi fulani vya ushirika vitaweza kupatiwa fedha kwa ajili ya kujenga hivyo viwanda vidogo vidogo.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo lilizungumziwa na wenzangu ni suala la *ZIPA*. Mheshimiwa tulikwenda semina kwenye hoteli ya Ngarawa, lakini kwa bahati nzuri semina ile iliandaliwa kwa makusudi na wawekezaji. Tulipokwenda pale wenzetu watu wa *ZIPA* waliambiwa maneno makali sana na kuna baadhi ya watu waliokuwa hawana woga waliwataja watu kuhusu kukosa vibali kwa muda mrefu lakini bahati mbaya sana bila ya kujielewa watu wa *ZIPA* siku ya pili walipewa vibali, kwa hofu ile ambayo ilijitokeza kwenye kikao kile. Mhe. Naibu Spika, niombe kwa Mhe. Waziri suala la urasimu kwa uwekezaji linatusababisha wawekezaji wengine kuondoka Zanzibar kwenda kuwekeza nchi jengine, kwa hiyo niomba nalo pia lipunguzwe.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala jengine lililojitokeza Mhe. Waziri ni suala la upotevu wa pesa Wizara ya Fedha wenzangu wamelisema na mimi naomba niliseme tupewe maelekezo au tume ile ambayo iliteuliwa ilifikia hatua gani?

Mwisho Mhe. Naibu Spika, niunge mkono Mawaziri wote watatu lakini naomba Mhe. Waziri wa Fedha aongeze juhudi zaidi, kulikuwa na kikao kimoja ambacho tuliwahi kukaa pahali fulani na leo kwenye *paper* yake imejionesha kuwa mapato ya serikali yamekua kwa asilimia kubwa. Kwa hivyo namuomba Waziri wa Fedha aongezwe juhudi yeye na watendaji wake ili lile lengo la serikali lipate kufikia. *(Makofi)*

Lakini pia nimuombe Mhe. Waziri wa Kilimo naye aongeze juhudi hasa kwenye maeneo ya umwagiliaji maji kwa sababu maeneo yako lakini mabonde tu hayafanyi kazi vizuri, namini yakitengenezewa miundo mbinu mizuri tutaweza kuzalisha mpunga na ile ahadi yake aliyoiweka basi itaweza kutekeleka.

Lakini pia na Mhe. Waziri wa Biashara na yeye nimuombe hapa ndio kwenye roho yetu mapembe yako bei juu...

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika moja ya kumalizia

Mhe. Masoud Abrahman Masoud: Sukari iko juu sana, nimuombe Mhe. Waziri wa Biashara na yeye afanye kazi ya kufuatilia huko vyakula vinako nunuliwa nchi mbali mbali ili wananchi wapunguziwe bei tuweze kuondoa ukali wa maisha.

Mwisho naunga mkono ripoti ya Kamati kwa Mawaziri wote watatu kwa asilimia mia kwa mia.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Bahati Khamis Kombo baadae ni atafuata Mhe. Omar Seif Abeid.

Mhe. Bahati Khamis Kombo: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii jioni hii nikaweza kuchangia machache.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nimpongeze Mhe. Waziri kwa kazi zake nzuri anazozifanya na pia niwapongeze wote walioshiriki katika kamati hii kwa kazi zao nzuri walizozifanya na kutuletea ripoti hii. Sasa Mhe. Naibu Spika, naenda moja kwa moja katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF).*

Mhe. Naibu Spika, kamati katika kutembelea kwake imeona kwamba kutokuwepo na elimu ya kujiunga na mfuko bado ni mdogo kwa wananchi hasa sekta isiyokuwa rasmi. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli wananchi bado hawajakuwa na uwelewa huo lakini serikali itabidi ifanye kazi kubwa ya

kuwapa taaluma wananchi ili waweze kujiunga na mfuko huo. Mhe. Naibu Spika, wananchi wanahitaji elimu mijini na vijijini ili kuimarisha zaidi wajiunge na mfuko huo kwa maisha ya baadae.

Mhe. Naibu Spika, kamati ilibaini kuweko kwa mwitikio mdogo katika Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Pemba. Mhe. Naibu Spika, tunajua kwamba sote Unguja na Pemba tunategemea sana zao la karafuu na wananchi wa Pemba hasa ndio zao la kubwa wanalotegemea. Sasa tuangalie kwamba muda huu uliopita mwaka jana wa siku kuu ilikuwa karafuu ni kidogo lakini jee, mwaka huu tulioelekea mbele karafuu tunaamini ziko na kwa wingi tuangalie kipato gani ambacho tutapata kwa mtiririko unaofuata.

Mhe. Naibu Spika, sasa niende katika ukurasa wa 24 Ofisi Kuu Pemba. Kamati iliona kuwa kuna uhaba wa wataalamu katika fani mbali mbali lakini Mhe. Naibu Spika, tujue kwamba wananchi au wafanyakazi wako tayari kusoma lakini kikwazo chao kikubwa ni fedha, na kwa kweli kukosekana kwa wataalamu wa uhasibu au ununuzi na ukaguzi ni tatizo katika ofisi zetu. Kwa hivyo naiomba serikali iwatafute wafanyakazi katika ofisi hizi ambao wana muelekeo mzuri wa kupewa mafunzo na ya kakamata ndani ya kichwa chao ili waweze kusomeshwa.

Mhe. Naibu Spika, niende moja kwa moja katika ukurasa wa 28 Kiwanda cha Makonyo Pemba, kina uchakavu wa mashine na pia *spares* hakuna. Mhe. Naibu Spika, kwa kweli kiwanda hiki kinategemewa na wananchi wengi hususan wajasiriamali, wajasiriamali pale wanakwenda kununua manukato mbali mbali, kuna baadhi ya wajasiriamali wengine wanakwenda kununua manukato ya sabuni kwa kutengeneza sabuni aina mbali mbali lakini kuna wajasiriamali wengine huenda pale kwa kununua mafuta na kuuza nje ili kupata risiki zao. Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri mashine hizi ambazo zimeshakuwa chakavu basi zifanyiwe ukarabati ili kiwanda kisije kikapotea kama vilipotea viwanda vyengine.

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu kuna wafanyakazi ambao wasiokuwa waaminifu wanaweza kuzitoa mashine zetu pale na kuzipoteza na siku mbili, tatu tukaona kwamba kimeshafunguliwa kiwanda chengine cha makonyo lakini kilichotumika ni mashine yetu pale bila sisi wenyewe kujijua. Mhe. Waziri namuomba sana alitilie mkazo hili ili kiwanda chetu kiweze kuimarika.

Mhe. Naibu Spika, nikimalizia kwa kweli nitarudi nyuma kidogo lakini kuna wafanyakazi wa *TRA* kutoka Bara wanawadhalilisha madereva wetu wa Pemba na hili limenitokea hata mimi mwenyewe nikiwemo ndani ya gari pamoja

dereva wangu, amekuja mfanyakazi kutoka *TRA* kataka kitambulisha cha gari kigamba cha gari kile, nikamwambia kigamba cha gari hapa hakipo lakini kopi zake zote zimo na hakuna tatizo lolote. Mhe. Naibu Spika alituambia kwamba gari tuipeleke kituoni Polisi, nikamuuliza yende kituoni kwa tatizo gani na kopi yake bado imo humu ndani ya gari. Sasa hapa namuomba Mhe. Waziri atakapofanya majumuisho atuelekeze mpaka kile kikadi cha gari tukitoa *photocopy* nacho kibakie katika gari au tuache tu ile *photocopy* tu katika gari.

Mhe. Spika kwa hayo machache naunga mkono hotuba hii naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Sasa ni zamu ya Mhe. Omar Seif baadae atafuata Mhe. Dk. Makame Ussi.

Mhe. Omar Seif Abeid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika na mimi kunipa nafasi ya kuchangia ripoti hii ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ya Baraza la Wawakilishi.

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi naungana na wenzangu kwa kuwapongeza kamati kwa kazi nzuri iliyofanya na kwa uwelewa na kwa umahiri mkubwa wameweza kuwasilisha ripoti hii iliyo sheheni mambo mengi mazuri. Mhe. Naibu Spika, mimi kwa kuanza naanza na mashamba ya mipira. Suala la mashamba ya mipira hapa kamati iliainisha deni la dola laki nne ambalo linadaiwa hii kampuni ya iliyokuwa ikishughulikia na mambo ya mpira.

Mhe. Naibu Spika, bila ya kuona vibaya maana ni jambo kusikitisha kwamba kama alivyozungumza wenzangu kampuni hii imeondoka na deni letu la dola laki nne fedha nyingi sana wakati siye tuna shida ya pesa za kusukumia maendeleo kwenye majimbo yetu, hatuna maji, hatuna mambo mengine chochote kama alivyosema Mwenyekiti Miraji pale mwaka wa kwanza, mwaka wa pili dola laki nne, mwaka wa tatu, mwaka wa nne na bado mtu huyu anatizamwa na mpaka kifikia hatua ya kuondoka na dola laki nne. Kwa hivyo mimi kwa upande huu nilikuwa naomba kwamba pamoja na mambo mengine lakini serikali itoe tamko la kumtaka mdaiwa alipe dola laki nne za watu tunazomdai mali ya wananchi wa Zanzibar, jasho la watu wa Zanzibar lirejeshwe hata kama na yeye ni Mzanzibari lakini si lake peke yake ni pesa za umma zirejeshwe ili serikali iweze kufanya mambo mengine.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu nikiwa bado niko hapo hapo kwenye mamba ya mpira mimi nafikiria uamuzi wa Mkuu wa Mkoa wa kutoa barua hii kwa ajili

ya wananchi waliojikusanya pamoja lilikuwa na mantiki moja ambayo na mimi nakubaliana nayo kwa kipindi kilichopita. Tumeshuhudia kwamba baada ya uchaguzi mashamba ya mikarafuu yamekatwa mikarafuu mengi imekatwa ikateketezwa, sasa mimi naunga naye mkoni kwamba ingelikuwa hakuna hiki kikundi hichi cha wananchi waliopewa hayo mashamba ya mipira yangeweza kuhujumiwa na serikali ikapata hasara kubwa zaidi.

Kwa hivyo mimi naunga mkono juhudi hii lakini pia kuwepo na utaratibu maalum hivi sasa wa kuyarejesha tena mashamba haya kwenye umiliki kwa sababu ingawa bado yako kwenye umiliki, lakini inasemekana kwamba kuna baadhi ya mashamba yenye mipira waliokuwa na mashamba yao kama pale kama shamba la Rakki, Pogwa, Bahrain Finya, kuna baadhi ya watu wanapanda mikarafuu na wakidai kwamba mashamba hayo bado ni mali yao. Ushahidi upo na wakitaka Waziri kuyaona basi itakwenda kuona kwamba kuna watu bado sasa hivi wanadai madai kama hayo. Kwa hivyo, kuwaachia wale wananchi wakawemo mule ni kama ni ulinzi wa lile shamba za mipira.

Mhe. Naibu Spika nikirudi hapo katika *page* 8 kuna kitu cha kuzungumzia kuhusu maghala ya serikali yanaonekana kwamba kuna mengine yameuzwa na saba yameuzwa na majengo manane ya kampuni yameuzwa. Mheshimiwa na mimi nakubaliana na maoni na kamati kwamba sasa hivi imefika wakati wa serikali kudhibiti mali hasa haya maghala kuendelea kuyatoa kwa sababu sisi kuna matatizo mengi yanayohusiana na mambo ya maghala. Mhe. Naibu Spika, leo tulikuwa tunapiga kelele Tume ya Uchaguzi haina hata ghala lakini kumbe baadhi ya maghala yameuzwa yangekuwepo yangetumika, kuna vifaa vya maafa, wakati wa maafa hakuna ghala la kuhifadhia mambo kama hayo. Hivyo na mimi natoa wito kwamba sasa hivi hasa maghala ya serikali iwe ni marufuku kwa namna yoyote kuliuza wala kulikodisha nafikiria ni wakati muafaka wa kufanya hivyo.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia kwenye Wizara ya Fedha bado niko na mambo ya viinua mgongo. Mheshimiwa wafanyakazi wetu wengi wanakuwa ni maskini pamoja na juhudi nzuri kubwa sana na nampongeza Rais Dkt. Ali Mohamed Shein kwa juhudi anayochukua kupitia Wizara ya Fedha kuhakikisha kwamba wastaafu wanapatiwa haki zao haraka, hili ni jambo la kufurahisha. Kwa hivyo nachukua nafasi hii kuwapongeza Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi na Waziri wa Fedha kwa bidii kubwa wanayoifanya ya kulipa viinua mgongo kwa wastaafu kadri inavyowezekana, ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia nakwenda katika ukurasa wa 11 *ZRB.* Mheshimiwa *ZRB* nimeona katika ukurasa wa 11 kwenye makusanyo yao wamesema kuna baadhi

ya mambo wamepindukia viwango, utekelezaji wao mengine yako kwa asilimia mia moja na ishirini na sita. Naendelea kusema jambo hili mimi linanitia wasi wasi, kwa nini tuandike asilimia mia moja na ishirini na sita. Hii inaonesha kwamba wakati wanapofanya tathmini hawana takwimu halisi katika vianzio vyao wanavyokusanyia kodi. Lau kama kungekuwa na takwimu sahihi isingefikia kiwango cha kusema wamefika asilimia mia moja na ishirini na sita kwa sababu wangejua wao sisi pahala fulani tunakusanya shilingi kumi, pengine shilingi ishirini, pengine mia tano wakifika hesabu yao ya *hundred percent* ndio ingelikuwa ile *hundred percent* kwa takwimu ingelikuwa na takwimu.

Kwa hiyo, mimi napendekeza na nawaomba sana na nawasifu kwa utekeleza mzuri lakini ni vizuri vigezo vya takwimu wakawa navyo kabla ya kutoa hesabu zao, si vizuri kusema mwamba umefikia lengo la asilimia mia moja ishirini na sita, kwanini ufikie asilimia mia moja ishirini na sita. Hii inaweza kutoa mwanya kwa watu ambao si waaminifu wakaweza kufanya udanganyifu. Mhe. Naibu Spika, ni vyema wakafanya takwimu wakajua vianzio vyao halisi vyote ni kiasi gani watakusanya ili halisia yao ndiyo iwe *hundred percent*.

Mhe. Naibu Spika: Umebakiza dakika mbili.

Mhe. Omar Seif Abeid: Mhe. Naibu Spika, narudi katika Shirika la *ZSTC*. Mheshimiwa niongeze kidogo naipongeza sana Shirika hili kwa ajili ya kuwa na mpango wa kuwawezesha wakulima kupanda mikarafuu. Mheshimiwa tuna lengo la kukuza kilimo cha karafuu lakini kama nilivyosema lakini kama nilivyosema muda wote sisi kwamba sisi wajibu wetu ni kuwawezesha wakulima wakapanda mikarafuu ili kufikia lengo. Kwa hivyo ni imani yangu kwamba Wizara ilitazame hili na iweze kulifanyika haraka iwezekanavyo.

Mhe. Naibu Spiia, naenda kwenye Wizara ya Kilimo hasa kwa upande wa mazao ya baharini kwa samaki. Mheshimiwa mengine nitayachangia kwa maandishi kwa ajili ya ku-*save* muda nisiweze kuwazuia na wenzangu, lakini kumezungumzwa kama kuna tatizo la kupatikana vifaranga vya samaki.

Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana kama tumeshajipanga na hili tufanye utaratibu wa kuzalisha vifaranga vingi vya samaki na kamba kadri inavyowezekana pia kuweka muda maalum wa uvunaji wa mazao haya. Naomba Waziri atakapokuja aniambie ni muda gani wamejipangia kwa ajili ya uvunaji wa haya mazao ya baharini hasa majongoo na vitu vyengine.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi naunga kwa asilimia mia moja.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa anayefuata ni Mhe. Dk. Makame Ussi baadae anayefuata Mhe. Tatu Mohammed Ussi.

Mhe. Dk. Makame Ussi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi na mimi niwe mmoja kati ya wanaochangia mada hii leo.

Kwanza nipende sana kuwapongeza waandishi wa ripoti hii kwa kazi nzuri waliofanya, lakini pia sijasahau pia kuwapongeza wale wote wanaohusika katika wizara zao ambao ndio waliotoa taarifa sahihi zikawezesha kutengeneza kitabu kizuri kama hiki.

Kwanza kwa kuanza nianze na mchango wangu nianze na Wizara ya Fedha. Kamati imeripoti kwamba mapato yaliyopatikana kwa kipindi cha Julai/Disemba ni Bilioni 249.47 ambayo hii ni sawa sawa na asilimia 30 ya mapato yaliyokadiriwa kwa wakati huo. Tukiangalia hii ni chini ya *fifty percent* yaani ni chini ya asilimia 50 ya mapato. Sasa *trend* hii tukiiangalia kwa ufupi tunaweza kusema kwamba kama itakwenda kama hivi labda makusanyo hayatazidi asilimia sitini.

Mhe. Naibu Spika, lakini hiyo pia haitoshi kuna matumizi ambayo pia amesema kwamba zimetumika shilingi bilioni 247.97 ambayo uwiano wake unakuja katika *parallelogram*, maana yake uko karibu sawa na ukiangalia tofauti iliyobakia ni bilioni 1.5, bilioni 1.5 ni nyingi sana kwa makusanyoya akiba unayobakisha lakini ni kidogo sana kwa serikali. Sasa mimi ningependekeza sana Wizara ya Fedha wakasimamia sana ukusanyaji wa mapato kwa kuongeza wigo wa mapato yenyewe na kusimamia uvujaji wa mapato hayo yasivuje.

Halafu tukienda katika *program* kuu ya usimamizi wa uwekezaji wa mali za umma. Mchangiaji mmoja hapa mwenzangu alisema kwamba kuna matatizo makubwa sana kwenye kuweka kumbukumbu za mali za serikali. Ni kweli ukienda mawizarani huko kuna baadhi ya sehemu kumbukumbu namna zinavyoweka haziridhishi, kuna baadhi ya mali hazimo, kuna baadhi ya mali zimeondoshwa zimepelekwa kwengine hazionekani. Kwa hivyo mwenzangu akapendekeza kuwe na *asset register* ambalo lina mfumo mmoja kwa wizara zote na Wizara ya Fedha nadhani wao wangetoa *format* ya kuweka *asset register* za aina fulani, ili bidhaa zote au mali zote za serikali ziwe zinasajiliwa kwa uangalifu na kwa umakini. Na hata *depreciation* yake namna

inavyofanywa wanafanya *linear depreciation* ambayo kwa kweli baada ya miaka minne au mitano au sita unaweza ukakuta thamani ya bidhaa au mali ya serikali ni ziro, wakati ambapo bado chombo kile au kama gari kama nini bado kiko katika hali nzuri. Matokeo yake ikitokezea kuuzwa kinauzwa kwa bei ndogo. Sasa naomba pia Wizara ya Fedha wapendekeze namna ya kufanya *depreciation* ambayo itawezesha kufanya *re-evaluation* kwa kila baada ya kipindi.

Mhe. Naibu Spika, halafu tena ambacho pia nimeona ni tatizo ni mambo ya tenda, kwa kweli *tendering system* yetu si nzuri. Kuna baadhi ya manunuzi yanafanywa bila ya kufuata utaratibu wa tenda ule unaotakiwa na serikali, na kwa hili pia naomba Wizara ya Fedha waweke *format* nzuri ya *tendering system* ili kila mmoja afuate utaratibu huo.

Mhe. Naibu Spika, nikienda tena kwenye ujenzi wa ofisi hizi za serikali hasa ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Fedha Pemba. Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Fedha Pemba ni moja katika miradi mingi sana ya wizara hii juu ya ofisi za serikali, naipongeza sana Wizara ya Fedha kwa kazi hii. Lakini pia nashauri kwamba uangalifu ufanyike ili isije ikatokezea kama ile Ofisi iliyojengwa kule haijamaliza imeshaaza kupasuka, na ripoti yake ile hatuwezi kuiingilia sana kwa sababu iko Mahakamani lakini kwa kweli pale kidogo wasimamizi walikosea.

Mhe. Naibu Spika, nikija tena kwenye *ZSSF*. Miradi ya uwekezaji kwenye *ZSSF* ni moja kati ya maeneo yanayoweza kuimarisha maendeleo ya mfuko huu. Ipo miradi iliyokamilika kama hii ya Kariakoo na kule Tibirizi Pemba, iko mengine ambayo imo katika hatua za kumalizika au hatua za kuendelezwa, lakini zipo changamoto ambazo zinaikabili hii *ZSSF*. Sasa naishauri sana *ZSSF* pamoja na kazi nzuri wanazozifanya nadhani ipo haja kwa mfuko huu kusimamia vizuri zaidi miradi yake, ipo haja pia kufanya utafiti wa kina juu ya miradi inayokusudiwa, kwa sababu tumepata tatizo kule Pemba Tibirinzi tunaambiwa watu kwenda kule kwenye kiwanja chenyewe hawapendi sana, hivyo ni hasara kubwa sana. Kiwanja kimejengwa kwa thamani kubwa lakini watu kukitumia kile kiwanja hawakitumii ipasavyo. Kwa hivyo, ni hasara kwa kweli.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia tunapendekeza kwa *ZSSF* uandaliwe utaratibu maalum wa kuwapatia mikopo ya kujenga wafanyakazi, kwa maana kwa kweli maisha ya wafanyakazi hayaridhishi wanakaa kwenye nyumba ambazo kwa kweli hazistahiki kwa mfanyakazi wa serikali kukaa kwenye nyumba hizo, kwa sababu uwezo wao ni mdogo wa kujenga nyumba. Kwa hivyo, wakisaidiwa

mkopo angalau wataweza kujenga kibanda ambacho kinaweza kikatizamika na wakaishi vizuri hususan baada ya kustaafu.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda haraka haraka, nakwenda kwenye Mfuko wa Barabara. Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa kazi za mfuko huu ni matengenezo ya barabara kwa kushirikiana na wizara husika, na wizara husika hapa ni Wizara ya Mawasiliano. Naipongeza sana kwa juhudi zake inazofanya kuziendeleza barabara zetu, lakini pia kuna matatizo ambayo yametajwa ambayo nayo pia nayaunga mkono pamoja na changamoto zilizomo. Na nashauri kwamba mfuko ufanye utafiti wa kina kwa barabara zote sio hizo kubwa tu, hata barabara za ndani kwa sababu zile ni muhimu, zile ndio zinatoa kama ni bidhaa, zinatoa watu kuwaleta hapo barabara kuu na kwenda safari zao nyengine. Kwa hivyo, nawashauri sana waziangalie na barabara za ndani, barabara za ndani ni mbaya sana hususan kwenye majimbo huko.

Mhe. Naibu Spika, sasa niingie kwenye Wizara ya Biashara kwa haraka haraka nasema. Moja katika majukumu makubwa ya wizara hii ni kudhibiti upatikanaji, usambazaji na ubora wa bidhaa. Sasa kuna mambo mengi, kuna mambo ya bidhaa imeshazungumzwa kwamba bidhaa zinazokuja nyengine zimesha-*expire*, nyengine zishakuwa hazifai kwa binadamu. Kwa hivyo, nashauri wizara hii wajitahidi sana kufuata Sheria za Biashara kikamilifu ili kuepukana na hii kuleta bidhaa ambazo hazina viwango. Waweke wataalamu wa kutosha katika sehemu zote zinazohusika, viwango…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa una dakika mbili za kumalizia.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Dakika mbili ooh! Ahsante.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwenye Wizara ya Kilimo hapo tena hapo kwenye Wizara ya Biashara naiachia nakwenda kwenye Wizara ya Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kilimo ni tegemeo la dunia nzima kwa chakula, hakuna kiwanda kinachozalisha chakula. Kwa mfano, mpunga hakuna kiwanda kinachozalisha mpunga ni kilimo ndicho kinachozalisha mpunga, mpunga ule tena unapolekwa kiwandani kutengenezwa tu. Sasa ni muhimu sana kilimo tukakipa kipaumbele.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, katika nchi yetu hapa kwetu uzalishaji wa kilimo kwa kweli ni mdogo, watu duniani mpunga wanazalisha si chini ya tani 18 kwenda mbele kwa hekta, hapa kwetu ni chini ya tani 5 kwa hekta, ni ndogo sana. Kwa hivyo tunapaswa kujitahidi. Kilimo ni utafiti lazima tufanye utafiti tuweze kuendeleza

kilimo, bila ya utafiti hakuna kilimo tutapanda mazao yale yale siku zote na tutakuwa hatuna tunachokipata. Jasho jingi mkulima litamtoka lakini mapato yake ni madogo. Kwa hivyo, mimi nawashauri sana Wizara ya Kilimo kuhimiza utaratibu wa kupanda, kupalilia na kuvuna kwa wakati ili kuhakikisha mazao yanapatikana.

Mhe. Naibu Spika, jambo la pili watumie mbegu zilizo bora, najua haya yanajulikana sana lakini nasisitiza tu kutumia mbegu zilizo bora ambazo kama zile wanazotumia wenzetu, si vibaya tukazichukua tukazileta hapa tukazifanyia utafiti tukaweza kuzitumia kama wanavyozitumia wao na sisi tukazalisha kama wao au zaidi.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi: Umekwisha looh! Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii, nasema mimi naunga mkono hoja hii kwa asilimia mia. Ahsante sana. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Tatu Mohammed Ussi baadae atachangia Mhe. Hamad Abdalla Rashid Gerei

Mhe. Tatu Mohammed Ussi: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kuweza kunipa nafasi hii. Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kunijaalia kunipa uzima na afya nikaweza kusimama jioni hii kuchangia Ripoti ya Kamati ya Fedha, Kilimo na Biashara.

Mhe. Naibu Spika, mchango wangu moja kwa moja utakwenda kwenye ukurasa wa 22, uwekezaji katika Hoteli ya Bwawani. Mhe. Naibu Spika, hapa tunaona Hoteli ya Bwawani imepata mwekezaji, sasa nilikuwa nashauri serikali na kule Pemba ziko hoteli ambazo kwa kweli hali yake haziridhishi. Kwa hivyo, nilikuwa naiomba serikali hoteli hizi nazo ziangaliwe ili wakipatikana wawekezaji nao wapewe, kwa sababu kuna Hoteli ya Mkoani, hoteli ile kwa hivi sasa imekuwa ni ghala la wavuta bangi, walevi na mambo yote ya uasharati yanafanywa mle. Kwa hivyo, nilikuwa naishauri serikali ile hoteli itengenezwe nayo ikipata mwekezaji apewe au hata kupewa wafanyabiashara kwa ajili ya kuekea vitu vyao. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, hoteli ile imekuwa ni kero kubwa kwa wananchi wa Mkoani.

Mhe. Naibu Spika, lakini pia mchango wangu mwengine niuelekeze katika Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF)*. Moja ninalotaka kulizungumza ambalo Mhe. Bahati ameshalizungumza kuhusu elimu ya kujiunga na Mfuko kuwa ni ndogo kwa wananchi iliyo katika sekta isiyo rasmi. Mimi nisisitize tu Mhe. Naibu Spika, niwaombe wahusika wa Mfuko huu kuendelea kuwashajihisha watu hao katika sekta isiyo rasmi ili kujiunga na Mfuko huu, kwa sababu waliwahi kuifanya kazi hii kipindi cha nyuma na watu waliitikia wito na wakaweza kujiunga.

Mhe. Naibu Spika, jengine hapo hapo kuna muitikio wa wananchi wa Pemba katika kutumia Kiwanja cha Kufurahishia Watoto Pemba. Mhe. Naibu Spika, mimi nakubaliana na changamoto waliyoiona kamati ni kweli na hii inatokana na mazingira ya hali ya kile kisiwa chenyewe cha Pemba. Mhe. Naibu Spika, uwanja wa Kariakoo uliopo hapa Unguja unaingiza watu wengi kwa sababu Mkoa wa Mjini/Magharibi una watu wengi, wanaingia kwa wingi mpaka siku za Jumamosi na Jumapili tunawaona. Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa upande wa Pemba kiwanja kile kinaingiza watu siku za siku kuu, kwa nini basi ikawa hivyo? Mhe. Naibu Spika, mazingira ya Pemba tunayajua imejigawa katika Wilaya 4, mtu anaona tabu kutoka Mkoani akatoa shilingi 3000 akafuata kiwanja Chake-Chake kutokana na hali ya umaskini. Vile vile mtu wa Micheweni naye pia ni shida hususan kutokana na hali ya usafiri wa kwetu, tusifichane kwetu ikifika saa kumi jioni gari kutoka Chake-Chake kuja Mkoani ni tatizo na gari iliyopo Mkoani kuja Chake-Chake ni tatizo, sasa suala hili ndilo linachangia.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini pia ukubwa wa nauli nalo linachangia kwa sababu hapa Unguja utatoka Bububu, utatoka wapi mpaka ukija kiwanjani ni shilingi 300 unaingia kwenye uwanja. Sasa kutokana na hali hiyo Mhe. Naibu Spika, naiomba Wizara iweze kutujengea angalau viwanja vidogo vidogo kwenye Wilaya zile za mbali kama ya Mkoani na Micheweni kwa ajili ya kuwahifadhi watoto wetu. Kwa sababu wazee tunataka watoto waende kiwanjani lakini hali inakuwa hairuhusu na watoto wetu wanapata tabu, na hili nililizungumza hata nilipochangia katika bajeti iliyopita, kwa hivyo na leo naliomba tena hili liangaliwe sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa nije kwenye viwanda, naomba viwanda vifufuliwe ili vijana wetu waweze kupata ajira. Mhe. Naibu Spika, tunalia na suala la ajira lakini tukipata hivi viwanda basi vijana wetu tutapunguza lile tatizo la ajira.

Halafu Mhe. Naibu Spika, niende katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko nimuombe tu Mhe. Waziri azidi kututafutia masoko, pamoja na

jitihada zake anazofanya, lakini azidi kututafutia masoko kwa sababu masoko kamati wameona kuwa ni tatizo. Kwa hivyo kuna wajasiriamali wetu walio wengi biashara zao zinadhorota kutokana na ukosefu wa masoko.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Kwanza nimpongeze Mhe. Waziri wa Kilimo kwa jitihada yake kubwa anayoifanya katika kuimarisha kilimo. Lakini Mhe. Waziri nimuombe tu kuwahimiza wale mabwana na mabibi shamba wasikae ofisini tu wapite kwenye mabonde kuwahimiza na kuwaangalia wakulima wana matatizo gani, wawaelekeze namna wa utumiaji wa mbolea, namna ya utumiaji wa kupanda mipunga.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo naunga mkono ripoti hii asilimia mia moja. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Tatu. Mchangiaji anayefuatia ni Mhe. Hamad Abdalla Rashid Gerei baadae atachangia Mhe. Hidaya Ali Makame.

Mhe. Hamad Abdalla Rashid: Ahsante Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii kutoa maoni ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo ambayo kwanza niwapongeze wajumbe wote wa Kamati pamoja na Mwenyekiti kwa mashirikiano yao makubwa tuliyokuwa nayo wakati wote au kipindi chote ambacho tulikuwa tunafanya kazi hii.

Mhe. Naibu Spika, sina budi kuwapongeza Mhe. Waziri wa Fedha, Mhe. Waziri wa Kilimo na Mhe. Waziri wa Biashara kwa mashirikiano yao makubwa ambayo wametuonesha wakati wote tunafanya kazi zetu kwa uangalifu mkubwa. Mhe. Naibu Spika, kwa sababu na mimi ni Mjumbe wa Kamati hii sitokuwa na mengi ya kuchangia bali nijazie nyama kidogo tu na nianze pale kwenye shamba la mipira ambapo wenzetu wengi wamepasemea.

Mhe. Naibu Spika, kamati imeona vizuri matatizo yaliyopo pale lakini na mimi napenda kujazia nyama tu kidogo ambayo inaonesha dhahiri kwamba hapa palitokea muingiliano wa madaraka, kwa sababu shamba linamilikiwa na Wizara ya Fedha lakini aliyetoa barua ni Mkuu wa Mkoa. Mhe. Naibu Spika, hii haikupaswa ilikuwa ni Waziri wa Fedha mwenyewe ndio mwenye mamlaka na haki ya kutoa barua kwa wale ambao wamekabidhiwa hili shamba.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo niende Shirika la Taifa la Biashara. Kama nilivyosema wenzetu Mawaziri na watendaji wao wote walitupa mashirikiano mazuri na mpaka tukaweza kugundua kitu ambacho kidogo humu ni muandiko

tu labda umekosewa au kimesahaulika. Katika kufuatilia tulipata taarifa kutoka kwa Mhe. Waziri wa Kilimo na kamati imeona kabisa kwamba *spices* zinazouzwa nje zina soko kubwa lakini bado fursa hii hatujaitumia vilivyo. Lakini tulipata taarifa kwamba *spices* zetu za Zanzibar zilipata athari kidogo ya dawa ya mbu hii ambayo tunapiga hapa Zanzibar kwa nia ya kutokomeza ugonjwa wa malaria.

Mhe. Naibu Spika, *spices* zetu ziliingia vimelea vya dawa hizi na vimesababisha kuteremsha soko. Kamati tuliona ni vyema basi Mhe. Waziri wa Kilimo na Mhe. Waziri wa Biashara wakishirikiana na Mhe. Waziri wa Afya wakae pamoja ili wanusuru sasa zao letu la karafuu nalo lisije likafikwa na kadhia hii, kama tunavyojua karafuu sasa hivi ndio zao kuu la taifa. Sasa narudia tu kusisitiza kwamba ni vyema Mawaziri hawa watatu wakae pamoja kujadili namna gani tutazikinga karafuu zetu nazo zisije zikafikwa na kadhia hii ili kuokoa zao letu hili la karafuu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo kama nilivyosema sina mchango mkubwa narudia tena kuwapongeza Mawaziri wetu na watendaji wao wote na kamati nzima kwa ujumla, akiwemo mwenyekiti wetu msikivu, mwelekevu, mpole ambaye katufikisha hapa kuweza kutengeneza programu hii pamoja na watendaji wetu wa Baraza.

Mhe. Naibu Spika, ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ninakushukuru sana Mhe. Hamad Abdalla Rashid Gerei. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hidaya Ali Makame na ajitayarishe Mhe. Mussa Ali Mussa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Naibu Spika, ahsante kwa kunipatia na mimi fursa na nafasi nzuri ya kuweza kuchangia Ripoti ya Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza nichukue fursa hii kuipongeza kamati hii kwa kazi kubwa waliyonayo na waliyoifanya kwa kupitia maeneo haya yote na kuweza kuona mambo mbali mbali, pia kuweza kukutana na changamoto mbali mbali ambazo wameweza kukabiliana nazo na kuweza kuzitatua baadhi yao. Niwapongeze na niwaambie kwamba wazidishe juhudi kwa sababu kamati yao ndio muhimili wa taifa, kwa sababu tunaambiwa kwamba kilimo ndio uti wa mgongo wa mwanadamu. Kwa hivyo wajitahidi sana na waendelee kujitahidi.

Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kuanza kuchangia ripoti hii moja kwa moja nianze kwenye Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi; kwenye wizara hii nitakwenda kwenye sekta ya uvuvi.

Mhe. Naibu Spika, kwenye sekta ya uvuvi Wajumbe wa Kamati wameweka changamoto nyingi ambazo wameweza kukutana nazo kwenye sekta hii, lakini katika changamoto hizo ambazo wamekutana nazo moja wapo ni ya uvuvi haramu. Uvuvi haramu bado upo na uvuvi huu bado unaendelea. Kwa kusema hivyo kwamba kuna ushahidi tosha wa uvuvi huu kuwa unaendelea. Pia katika hizo changamoto ambazo waliziona wakasema kwamba kuna uhaba wa vyombo vya kufanyia doria huko baharini.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mimi niseme kwamba uvuvi haramu unasababishwa na wavuvi wenyewe na wavuvi ndio wanaofanya hili jambo kwa kutegemea labda wao watapata fedha nyingi zaidi. Lakini hii ni kwamba ni kujiharibia kwa sababu tumeona athari nyingi ambazo zimetokea baharini mpaka muda huu kutokana na huu uvuvi haramu. Tunafahamu kwamba kulikuwa kuna mambo mengi ambayo yalikuwa yanaonekana baharini wakiwemo samaki na matumbawe ya aina mbali mbali na sasa hivi yametoweka, lakini hata hao samaki wakubwa na wadogo pia sasa hivi wametoweka kutokana na huu uvuvi haramu.

Vie vile kuna baadhi ya hizi aina za *sea food* mambo ya kome, chaza na wengineo pia sasa hivi tunakuta kwamba hawapo wanatoweka kwa wingi kutokana na uvuvi huu. Kwanza ni kuuwa matumbawe, lakini pia kupiga mabomu kwenye hizi bahari na kuchafua kila kitu kilichokuwemo humo na kupelekea ubovu uliokuwemo ndani ya bahari zetu sasa hivi. Kwa kweli bahari sasa ni mbaya hazina kitu na zinasikitisha. Kwa sababu kipindi cha nyuma nakumbuka mimi nikiwa ki-Hidaya kiduchu nakwenda pwani sijafika hata mwambani lakini narudi na polo la pweza, chaza, kome, tagwe, wote hao, lakini sasa hivi Mhe. Naibu Spika, nikwambie ule ukweli kwamba utafika kukaribia Pemba wewe kwa miguu, hujakutana na hata lile kombe la dodoki mule njiani angalau ukaweza kutia kipoloni mwako au mkobani mwako. Kwa kweli hii hali inasikitisha.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwenye uvuvi huu wa samaki tunakuta kwamba hali inasikitisha kwa sababu viumbe baharini vinatoweka kwa kasi kubwa. Kwa hivyo, nimuombe Waziri husika tuzidi kujitahidi juu ya suala hili kupiga vita huu uvuvi haramu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kuhusu hili suala la vyombo vya doria basi Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi akishirikiana pamoja na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango hili suala tulisimamie, hivi vyombo viweze kupatikana. Kwa sababu huu uvuvi haufanywi na wavuvi wetu tu waliokuwepo hapa, lakini kuna na meli tofauti, vyombo tofauti vinavyotoka nje ya nchi yetu kuja kufanya huu uvuvi wa haramu na wakafanya mambo haya kinyume na sheria zetu zilizokuwepo hapa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende pia kwenye sekta hiyo hiyo ya kilimo katika suala la mifugo. Kwenye suala la mifugo huku nako sasa hivi tunakwendea kubaya kwa sababu tumeona sasa hivi hii sekta nayo inaendelea kufa, itakuwepo kwa watu ambao wanajiweza ambao wana hali zao wanamiliki hivi vitu, lakini kwa wale wenzangu na mimi maskini, wakulima na wakwezi, hili suala la mifugo linaendelea kwisha. Kwa sababu tunaona kwamba kuna haya mashamba ambayo yalikuwa yanamilikiwa mpaka muda huu na serikali lakini mashamba haya yalikuwa yamewekwa *special* kwa ajili ya mifugo, mashamba haya yanatoweka kiufupi maana ile hadhi yake imeshapotea.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kuna mashamba ambayo tayari Wajumbe wenzangu wameshayataja lakini kuna shamba ambalo mimi nalifahamu la asili shamba yake ni shamba la *Paidoc***.** Shamba hili lilikuwa ni la mifugo na mpaka muda huu lipo, lakini hivi sasa ninavyosema Mhe. Naibu Spika, ukipita pale wewe utaona jangwa nuru tu ya uwanda huoni ng'ombe, huoni membe, huoni kongoo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwenye barabara ya Dole kwenda Maili Sita ulikuwa ukipita kwenye njia ile kama si mtalii basi utaona fahari, kama ni mtalii basi utaona fahari. Kwa sababu ile njia ilikuwa imefurika na mifugo ya kila aina wakiwemo ng'ombe wakubwa wa maziwa, ng'ombe wa nyama, mbuzi na kuku. Lakini kwa kweli hali ya kusikitisha sasa hivi katika mashamba yale yalioko Kizimbani *Paidoc* na *ZAPOCO* hatufahamu kuna kitu gani ambacho kinaendelea juu ya mashamba haya lakini kwa kweli hadhi yake imepotea na haipo. Mhe. Naibu Spika, *Paidoc* palikuwa panafugwa ng'ombe na maziwa yalikuwa yananywewa Zanzibar nzima hii, ng'ombe mmoja aliyekuwa akichinjwa pale Dole nzima, Kizimbani na Kianga yake basi watakula na watajisikia, lakini sasa hivi ng'ombe hao hawapo wala mbuzi hawapo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, pia palikuwa na sehemu pale ya kufuga kuku ambayo ni *ZAPOCO*. Hii sehemu ilileta manufaa makubwa sana kwa wananchi wote kwa sababu ajira zilipatikana na vilaji vilipatikana, nyama zenye ubora na hadhi ya hali ya juu kwa kuku hawa lakini pia na mayai. Hii sehemu sasa hivi haifanyi

kazi hatujui sababu nini, tukiwa kama ni wananchi lakini pia ile hadhi yake inapotea kwa sababu sasa hivi pamebakia mwitu tu, utaona watu wawili watatu ambao wapo lakini hujui wanajishughulisha na kazi gani mule ndani, hujui ile sehemu pale sasa hivi ipo kinamna gani. Mhe. Naibu Spika, tungemuomba Waziri atujuilishe juu ya hii sehemu jee, sasa hivi iko kinamna gani na inafanya kazi gani. Kama haina kazi yoyote inayofanya basi tungeiomba sana Wizara sehemu ile irejeshwe hadhi yake, kama hakuna mkandarasi basi atafutwe wa aina yoyote lakini suala la kuku pale liweze kuendelea tumechoka na Peduu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiwa na dakika mbili.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Mhe. Naibu Spika ahsante. Sasa niende kwenye suala la mwisho Sekta ya Masoko. Kwenye sekta hii nako tunakwenda chini kiufupi kwa sababu nitalizungumzia suala la mafuta ya nazi Zanzibar. Zanzibar ni sehemu ya mafuta ya nazi, viwanda vilikuwepo zikiwemo chanja za asili ambazo zilikuwa zinasindika hizi mbaya zinazotoa mafuta ya nazi sasa hivi zimetoweka, mafuta ya nazi hayaonekani bali unaoonekana ni uchakachuaji. Kwa sababu hakuna mafuta ya nazi ni maji yaliyochanganishwa na mafuta ya "*ok"* tukauziwa huko tukaambiwa mafuta ya nazi. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mafuta ya nazi yametoweka kabisa Zanzibar wakati tunafahamu kwamba mafuta ya nazi asili yake ni Zanzibar. Kwa nini? tunamuomba Mhe. Waziri atueleze na atufafanulie na atupe njia ya kufanya juu ya suala hili ili haya mafuta ya nazi yarudi Zanzibar kama mwanzo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nije pia kwenye suala la *spices*. Mhe. Naibu Spika, Kizimbani ndio muhimili mkubwa wa *spices* tunafahamu sote, pilipili manga, uzile, hiliki, tangawizi, kila *spices* tunayoifahamu Kizimbani inapatikana. Mhe. Waziri tunamuomba sana suala la kiwanda cha *spices*, tunajitahidi wakulima soko hatuna juu ya mazao haya, tunakaa na pilipili manga majumbani mpaka zinafanya mkovu, mteja atakupitia wewe aje akwambie kilo shilingi 2,000 hutompa wakati nje unasikia shilingi 27,000. Kwa hivyo, tunamuomba sana Mhe. Waziri nalo atupe njia.

Mhe. Naibu Spika: Malizia Mheshimiwa.

Mhe. Hidaya Ali Makame: Ahsante Mhe. Naibu Spika, namaliza kwa kusema kwamba naiunga mkono ripoti hii ya Kamati kwa asilimia 99, hizo nyengine zilizobakia nitaendeleza baada ya majibu ya Waheshimiwa Mawaziri. Ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Mussa Ali Mussa na baadae atachangia Mhe. Ali Suleiman Ali.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana na mimi nakushukuru kwa kunipa nafasi hii Mheshimiwa ambaye ni mzee wako ukaniona na mimi nichangie ripoti hii ya kamati. Mimi nitakwenda kwenye jimbo langu la Ole.

Jimbo langu la Ole kuna kituo cha kilimo kinaitwa Dodeani. Hiki ndio kituo kikuu cha kilimo ukitoa kile cha Matangatuani, hiki kilikuwa ni nambari mbili, ndicho kituo ambacho kilikuwa kinatoa mazao yote tunayoyajua kama vile miembe, minazi, migomba yote ilikuwa ikipatikana hapa. Kituo hiki kina eneo kubwa sana la kilimo cha mpunga lakini cha kushangaza kituo hiki leo kimebakia jina, ingawa kina maghala makubwa ya kisasa ya serikali lakini maghala yale yapo tu kungojea mbegu itakayoagiziwa kutoka Bara kuja kuwekwa pale pamoja na madawa watu kuja kuuza, lakini mashamba yote ya kituo hicho wamepewa wananchi wanalima binafsi. Wenyewe watu wa kilimo wako pale wafanyakazi wanangojea tarehe 15 au 25, jioni wanaondoka wanakwenda zao.

Mhe. Naibu Spika, sasa hivi kituo kile kimedhalilika hatupati tena chochote kutoka kwenye kituo kile, kituo ambacho kilikuwa na miti mikubwa mi-*cypruss* wakaja wajanja wakaiuza wakauziwa matajiri wakenda wakachonga majahazi. Sasa miti ile haikupandwa tena haipo tena na ile iliyokuwepo pesa nina uhakika kabisa hazikuingia serikalini. Kituo ambacho kilikuwa kinasifika kwa kuzalisha michungwa, midimu, milimau, Zanzibar yote kila mtu anayetoka Unguja akija Pemba anafikia kituo kile kuchukua miche kuja kupanda Unguja. Miembe yote unayoisikia wewe akina mwarugo ilikuwa inatoka katika kituo kile cha Dodeani, mbegu zote za mpunga hizo uchuki, hakuyawiki, bwana harusi, sijui mbegu gani zote zilikuwa zinatoka Dodeani.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, leo nasikitika sana, wazee wetu walisema "Pavumapo palilie si kazi kula mirika". Leo Dodeani imefikia imedhalilika, haina faida yoyote inayotoa kutoka kwenye Serikali hii ya Mapinduzi ya Zanzibar. Pamoja na majengo mazuri ya kisasa leo kuna mashimo Dodeani yalichimbwa kuhifadhiwa matangi ya petroli na matangi yale yakazikwa yakawekwa pale udongo mwingi ukawekwa juu, leo matangi yale yako chini yanaoza na maskini kamati imepigwa changa la macho imekwenda pale hawakutaka kukitembelea au hawakuelezwa kama kuna kituo cha Dodeani, hawakwenda kuyaona madhambi yale, madhambi yaliyojificha kama yaliyojificha ya

Uwanja wa Ndege. Uwanja wa Ndege wa Zanzibar hakuna madhambi kuna maporomoko ya madhambi pesa nyingi zimepotea.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, katika jimbo hili la Ole pana kituo cha maogesho ya ng'ombe, lipo hodhi la ng'ombe Mchangani, kituo hiki nacho kina majengo ya kisasa mazuri, lakini la kushangaza lile shimo lililokuwa likiogeshewa ng'ombe sasa hivi wacha maji hata tope hamna linadidimia. Serikali pale ilikuwa ikipata mapato yake kwa watu kila Alhamisi kwenda kukosha ng'ombe leo hawendi tena maskini serikali haipati lolote.

Mhe. Naibu Spiika, pana mashamba ya eka, kuna mashamba ya kilimo namueleza mtoto wangu Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi kama hajui lile eneo lote ni mali ya serikali, ni mali ya Wizara ya Kilimo lakini leo maskini wamepewa wapinzani majengo yale wanafanyia siasa. Ukienda jioni wanahesabu tarehe tu basi, tarehe 15, 25, 31 anaapishwa. Hiyo ndio hali iliyopo pale. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, namuomba Mhe. Waziri mtoto wangu, Waziri msikivu aende pale akafanye utafiti mashamba yale yote awanyang'anye wapinzani na zile nyumba ambazo wanakaa wapinzani awatoe, kama hana vya kuzifanya nyumba zile basi mimi ninao vijana niwape wakae ambao wanaiunga mkono Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inayoongozwa na Dkt. Ali Mohamed Shein. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa muda hautoshi na wachangiaji ni wengi nataka kidogo nitembee katika kituo cha kilimo kilichoko Chamanangwe.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda hamna una dakika mbili tu za kumalizia.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Naam! Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika: Una dakika mbili za kuamlizia.

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Mhe. Naibu Spika, mimi ni mzee wako niongeze tatu. *(Makofi/Kicheko)*

Maana wakati wa kupiga kura mimi nilipinga dakika kumi nilitaka kumi na tano. Kwa hivyo, nakuomba kama mzee wako niongeze tatu.(*Kicheko*).

Mhe. Naibu Spika: Endelea Mheshimiwa. *(Makofi).*

Mhe. Mussa Ali Mussa: Mhe. Naibu Spika, kuna kituo cha kilimo Chamanangwe cha Ufugaji wa ng'ombe, kituo kile tulipata mfadhili kutoka Kenya, kilikuwa na ng'ombe wakubwa kama hayo magari huko nje, kikitoa maziwa yakiweza kutumika kwa Pemba nzima. Leo kituo kile kipo tu hakuna ng'ombe hakuna majani pale yanayopandwa. Sasa hivi ni yale yale ninayokueleza mashamba yale yalikuwa ya babu yangu lakini yalipochukuliwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, mimi nilifurahi sana kwa sababu nilijua yataendelezwa na kweli yaliendelezwa na kweli yalielezwa.

Lakini baada ya miaka minne mitano iliyopita sasa hivi ule umekuwa uwanja wa mambo ya maajabu, ukienda pembezoni humu watu ni hayo hayo wamejenga vibanda wanahesabu tarehe. Kwa hivyo, namuomba Mhe. Waziri ambaye naye ni mtoto wangu akija Pemba anitafute anitafute tuingie Chamanangwe nimuoneshe maeneo yetu ya Serikali ya Mapinduzi, serikali tukufu nimkabidhi ayafanyie kazi na ayatengenezee nyaraka, yawe mikononi mwake ili serikali ipate mapato, kulikoni kuyawacha tu yakapotea. Pia na hayo maeneo niliyomzungumzia ya Dodeani, nayo yanahitaji kuwa na nyaraka na yale ya hodhi za ng'ombe pia yanahitaji kuwa na nyaraka. Kwa hivyo, namuomba akija afuatane na mimi ili nimpatie maelekezo mazuri, nimpatie na mipaka mizuri ili akabidhishe mali zile kwa serikali ili serikali yetu ipate mapato kupitia kwenye mashamba yetu. Tuwangojee watu wanaongojea tarehe 15 na 30 shauri yao.

Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hii ripoti. *(Makofi).*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji wetu anayefuatia ni Mhe. Ali Suleiman Ali na baadae atachangia Mhe. Hassan Hafidh Diaspora.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, kwa kunipatia nafasi hii na mimi kuwemo katika orodha ya wachangiaji katika wizara zetu hizi tatu. Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko pamoja na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi.

Pia Mhe. Naibu Spika, nawapongeza kwa dhati kabisa Waheshimiwa Mawaziri wote watatu na Makatibu Wakuu, na watendaji wao wote wa wizara hizi kwa kazi nzuri wanazofanya na tunaishi katika mazingira ambayo yako vizuri.

Mhe. Naibu Spika, nianze na Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango, nampongeza kwa dhati kabisa, na nampongeza kwa umahiri wake, kwa jitihada zake na kuwa msikivu katika kazi zake, lakini akishirikiana na Katibu Mkuu wetu, Naibu Katibu Mkuu, Makamishna, Wakurugenzi wote, na watendaji wote wa

wizara hii, kwa kuhakikisha kwamba wanadhibiti pato la nchi na wanakusanya ipasavyo, hili ndilo tunalolitaka na kila mmoja tunaona kwa macho na aliyekuwa hana macho kidogo anasikia. Kwa hivyo, nampongeza yeye na watendaji wake wote kwa kuhimili mambo haya ambayo tunategemea ndio uhai wa nchi yetu na maendeleo katika mambo yetu.

Mhe. Naibu Spika, nakuja katika Shirika la Bima, nawapongeza kwa dhati kabisa hapa nitakuwa nina maelezo machache lakini kwa ufupi kabisa. Mapato katika mwaka 2011 Bima walipata faida ya bilioni 9,600,000,000, mwaka 2012 walipata bilioni 10,500,000,000 mwaka 2013, walipata bilioni 13,000,000,000, mwaka 2014 walipata bilioni 18,308,000,000 na mwaka 2015 walipata bilioni 20,200,000,000 nawapongeza kwa dhati kabisa kwa hili.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu tumeshuhudia mwaka hadi mwaka pato linaongezeka. Kwa hivyo, najua kutoka mwaka 2016 au mwaka 2017 yatazidi zaidi. Lakini kwa bahati mbaya bado wana madeni wanadai, hivyo naiomba serikali kwa kupitia Shirika la Bima wajitahidi madeni yao yalipwe ili waongeze mtaji wao. Mwaka 2011 bilioni 4,000,000,000/-, mwaka 2012 bilioni 4,075,000,000/-, mwaka 2013 bilioni 4,000,000,000/-, mwaka 2014 bilioni 6,495,000,000/-, mwaka 2015 bilioni 7,515,000,000/-. Mhe. Naibu Spika, naomba sana hii jitihada wanayoifanya waongeze bidii, kwa sababu ni ushindani wa kibiashara na faida kwa nchi yetu.

Jengine Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Mfuko wa Hifadhi ya Jamii (*ZSSF)*, nawapongeza mengi wameyafanya na mengi wanayaendeleza na jitihada zao tunaziona. Narudia kuwaomba kauli moja tu, wakati umebadilika kuweka viwanja vya michezo ni faida kwa watoto na sisi wenyewe kwenda kustarehe kwenye siku kuu na mambo mengineyo. Lakini sasa wakati wa biashara kuongeza mfuko. Naomba sana viwanda ni jambo muhimu katika nchi yetu, Tanzania Bara wanalilia viwanda na tunashuhudia siku hadi siku watu wanaongezeka.

Kwa hivyo, mimi niombe tu *ZSSF* wanafanyakazi zao vizuri, lakini wawekeze kwenye biashara ya viwanda, watafute viwanda vyovyote vyenye tija, hasa tukizingatia sasa hivi ukenda sokoni hapo Shimoni doo zima la embe shilingi 3,000 wanazimwaga hata vya kuzifanya hawana. Kama tungekuwa na uwezo wa kupata viwanda vidogo vidogo au vya kati basi tungewasaidia wakulima wetu na wakaweza kujua kwamba wapi wanapeleka bidhaa zao.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa kuharakisha na kwa kuwa muda mdogo, nakuja katika Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, kila mmoja nimpe faida yake kwa

upande mwengine. Nampongeza tena Mhe. Waziri kama nilivyotangulia kutoa shukrani za mwanzo. Lakini nasema kwamba nampongeza Mhe. Waziri kwa jitihada zake za ufuatiliaji hasa kwenye zao la karafuu na membo mengineyo. Nimemshuhudia nasema tena Mawaziri tujaribu kutoka kufuatilia mambo yetu, tusikae maofisini kwa sababu biashara uifuate iliko ndio uweze kuipata na kuiuza, ukisema unakaa ofisini uletewe tu au utumishe tu basi unaweza kupotea.

Mhe. Naibu Spika, nampongeza Waziri alikwenda kukaa na maafisa wa Polisi, watu wa Mahakama, pamoja na *ZSTC,* akawaambia kwamba mpaka sasa hivi kuna kesi zinafika 80 au 50 kwa mfano, lakini kesi zote zimehukumiwa hakuna mfungwa hata mmoja aliyepatikana katika watu wanaokwenda kusafirisha magendo, kuna nini. Kwa hivyo, naviomba vyombo vinavyohusika tutoe nguvu kwa serikali yetu, wale wanaoibia serikali au wanaofanya magendo basi wachukuliwe hatua ili iwe ni fundisho kwa watu wengine, nampongeza Waziri kwa hilo.

Mhe. Naibu Spika, lakini na yeye nimwambie kwa kuwa Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko ina historia ya viwanda huko nyuma inakotoka, basi tufanye bidii aombe. Najua kujenga yeye sio rahisi wizara yake na serikali ilijitoa kwenye mambo ya kujiingiza kwenye biashara, isipokuwa itasimamia, basi tuingie ubia na mtu yeyote tutafute wawekezaji kutoka nje waweke viwanda kwa ajili ya mapato ya nchi yetu.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, najua muda unakwenda, ni kuhusu Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi. Nampongeza Mhe. Waziri kwa jitihada yake nzuri, tunamkuta mabondeni, na kila pahala. Kila sehemu ambayo inamgusa anakwenda, hasa katika sehemu ya uvuvi. Kwa hivyo, ningemuomba Mhe. Waziri tumezungumza mengi na mashirika ya nje hayo ya Korea, Wafilippine sijui na wengine China na wengineo wote, watakuja kuwekeza mambo ya samaki hapa kwetu au uvuvi wa bahari kuu, lakini bado mpaka leo tunasikia tu lakini vitendo hatujaviona. Kwa hivyo nimuombe sana Mhe. Waziri suala hili alifanyie kazi ili tuhakikishe kwamba vijana wetu wanapata ajira kutokana na sekta ya uvuvi.

Jengine Mhe. Naibu Spika, linaloniuma katika nafsi yangu ni kwamba Zanzibar tuna sehemu mbili, tuna Unguja na Pemba. Kwa Pemba tunajua asilimia kubwa ni mikarafuu na kwa Unguja asilimia kubwa na minazi. Lakini sasa hivi imekuwa ni kinyume nyume, imekuwa kama *vice versa* haipo, minazi inakatwa kwa makusudi na inakatwa bila ya mpango. Zamani minazi ilikuwa inakatwa ikifikia umri ambao haizai tena, lakini leo minazi michanga inakatwa na

serikali bado imekaa kimya. Mimi naiomba serikali kwa hili tusichukulie utani ili vizazi vyetu vije virithi raslimali hii ya minazi, basi serikali iweke juhudi za makusudi ili kuhakikisha kwamba inapiga marufuku na atakayekamatwa pia itungwe sheria apele jela asahaulike kiasi miaka 20 jela nafikiri wengine hawatofanya tena. Lakini tukiacha hapo Mhe. Naibu Spika, minazi itamalizika, zitakuwa nazi zinatoka kwa shemegi zetu Tanga huko, zinatoka sijui Morogoro, yaani jambo la ajabu kabisa.

Kwa hivyo, niiombe serikali Mhe. Naibu Spika, suala la minazi yetu lifanyiwe kazi ili tuhakikishe kwamba wananchi wetu wanapata kutumia nazi, kama alivyosema ndugu yangu, mdogo mdogo nani Mhe. Hidaya Ali Makame, alisema kwamba yeye wakati huo mduchu nashuhudia mafuta ya nazi. Mafuta ya nazi tuliyashuhudia kweli yanatoka Zanzibar yanasafirishwa Bara, mapipa kwa mapipa Mhe. Amina Salum wakati huo Waziri au sijui alikuwa Katibu Mkuu anajua yeye wakati huo. Lakini...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe umebakiza dakika mbili.

Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata): Eeeh! haya, ahsante. Lakini Mhe. Naibu Spika, tulishuhudia na wengine kati yao waliokuwa wanafanyabiashara walikuwa wanatulea sisi humu ndani wamefaidika. Kwa hivyo niombe tu nazi ni raslimali tosha kwa uhai wa nchi yetu.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, namuomba sana Mhe. Waziri katika kitabu hiki kimeelezea kwamba kuna jambo kubwa ambalo limejitokeza katika umwagiliaji wa mabonde yetu. Ukenda Mwera, ukenda Mtwango, sijui wapi huko mambo yote yameharibika, hadi Mwanakombo huko, kwamba hivi sasa vianzio vya maji vinavamiwa. Kwa hivyo, nimuombe sana Mhe. Waziri bado tuwe wakali katika kuhakikisha kwamba raslimali ya maji ndio uhai wa nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo nampongeza Mhe. Mwenyekiti wetu wa kamati, yeye na Wajumbe wake wote kwa taarifa nzuri waliotuletea hapa. Nasema kwamba taarifa hii imetosha kuwa ni kioo katika maelezo ya maendeleo katika wizara zetu tatu hizi, tuzifanyie kazi ili tuweze kupata tija kwa maendeleo ya nchi yetu.

Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti hii kwa asilimia mia moja. Ahsante Mhe. Naibu Spika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mjumbe. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hassan Khamis Hafidh Diaspora. Baada ya hapo atachangia Mhe. Hussein Ibrahim Makungu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi Hassan Khamis Hafidh Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Welezo, kwa kunipa nafasi jioni hii ya kuchangia taarifa hii muhimu kwa maendeleo ya nchi yetu, kwa maendeleo ya wana mapinduzi wa nchi hii na kwa maendeleo ya wakwezi na wakulima.

Mhe. Naibu Spika, kutokana na muda nitaomba nianze katika ripoti hii kwenye masuala ya mapato *ZRB*. Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa taasisi muhimu Zanzibar ni taasisi ya kukusanya mapato kwa sababu bila ya pesa hakuna linaloweza kufanyika. Mhe. Naibu Spika, taasisi hii ni taasisi muhimu ingawaje inakabiliwa na changamoto nyingi za kiutendaji. Miongoni mwa majukumu ya taasisi hii ni kukusanya mapato, kuwatafuta wasiolipa kodi, kuwatafuta wasiolipa kodi kwa wakati na kuwashtaki. Mhe. Naibu Spika, taasisi hii ina kazi nyingi, nilisema tangu kwenye hotuba yangu ya bajeti, ina kazi nyingi na inashindwa kufanyakazi zake kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, ukitembelea katika mahoteli utakuta kuna mambo mengi ambayo yote yanasababisha mapato yetu kwa maendeleo ya wakwezi na wakulima kupotea. Mhe. Naibu Spika, unaweza kumkuta mtu katoka nje nchi kama India ni mfanyakazi kaletwa Zanzibar kuja kupika, lakini ati unaambiwa analipwa mshahara shilingi dola 300 ili pasilipwe mapato. Mhe. Naibu Spika, naomba kusema kwamba mapato mengi *ZRB* yanavuja, ukiacha na mambo mengine kutokana na kuwa na kazi nyingi. Naiomba serikali iyapunguzie mambo haya na kuyaundia taasisi nyengine.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye *TRA*. *TRA* pia ni taasisi moja muhimu sana kwa sababu nayo inatutafutia pesa kwa maslahi na maendeleo ya wakwezi na wakulima wa nchi hii. Lakini makontena mengi yanayokuja nchini ukiyazingatia pale bandarini wanachokisema kilichokuwemo ndani ya kontena sio kile kilichokuwemo, kama utafanya utafiti wa kuyafungua makontena yale, na inawezekana wazi vikawa vinaingia vitu katika makontena yale ambavyo havipaswi kuingia nchini kwa mujibu wa kanuni na taratibu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nitakwenda *PBZ*. *PBZ* ni taasisi ya fedha ni benki ya Watu wa Zanzibar ya wakwezi na wakulima, inashangaza na inasikitisha kumuona *cashier* anatumia simu wakati akiwa anamuhudumia mtu. Mhe. Naibu Spika, naomba kusema tena jambo hili, haipendezi inatutoa katika

mstari wa kuwa nchi ya busara na hekma, kwa sababu haipendezi mhudumu kutumia simu wakati anamuhudumia mtu.

Mhe. Naibu Spika, kuna Mfuko wa Barabara. Mfuko huu unashindwa kufanyakazi zake kwa sababu ya kugaiwa shilingi moja. Nauombea ili barabara za Welezi na Magharibi ziweze kutengenezwa ugaiwe shilingi mia mbili.

Mhe. Naibu Spika, kadhalika kuna Mfuko wa Bima, yaani Shirika la Bima. Naomba sana shirika hili libadilishe mwelekeo hawa watu wenye daladala watatumaliza wanatuuwa sana, wanatugonga kizembe kwa shilingi mia tatu, halafu hakuna kinacholipwa dereva wa daladala akishakugonga anakuja hospitali anakupa soda ya *fanta* na mambo mengine, baada ya siku tatu anakukimbia anakuacha na familia yako, familia zenyewe za kinyonge haziwezi kumuhudumia mgonjwa akiwa hospitali na wengine wanatakiwa kwenda India hakuna uwezo hufikia hadi kufa.

Mhe. Naibu Spika, naliomba sana Shirika la Bima lifanye kama Ulaya, anapogongwa mtu na gari basi mwenye dhamana ya kumtibu mpaka apone ni mwenye gari, kutokana na ile *full comprehensive insurance* aliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo Zanzibar ni nchi ya wakulima, ni nchi ya Mapinduzi na ni nchi ya wakulima na wakwezi. Haiwezekani hata siku moja nchi hii, Mzee Abeid Aman Karume alitujengea nyumba za Michenzani, Bambi, Dunga, Pemba na mwahali mwengine kwa sababu ya wanyonge, kwa sababu ya wakwezi na wakulima. Lakini leo tunawapa matajiri ma-*bourgeoisie*, mabwanyenye wanajenga nyumba kwa sababu ya matajiri na sio kwa sababu wakwezi na wakulima.

Mhe. Naibu Spika, Fumba na hapa Mbweni zinajengwa nyumba thamani yake kuzinunua ni dola laki mbili na nusu au dola laki tatu. Mimi mkwezi na mkulima, Mwakilishi wa wakwezi na wakulima, nitamaliza Uwakilishi kwa miaka mitano kuinunua nyumba ile sithubutu na wala sijaribu. Mhe. Naibu Spika, hii sio sahihi, tunachokifanya nchi hii ni lazima tuwaangalie wenye kipato cha chini, lazima kiwaangalie wakwezi na wakulima kwani wao ndio wenye nchi hii na wao ndio wanatakiwa wafaidike na sio mtu mwengine mgeni, kwa sababu ya kitu kinatakiwa kiwango kikubwa cha pesa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko. Mhe. Naibu Spika, nilisema siku zote katika hotuba ya bajeti, mfanyabiashara hana Dini, Dini ya mfanyabiashara ni faida na kitabu chake ni ghilba. Leo hii nitatoa mfano. Tulipochangia bajeti mwaka mmoja uliopita, mchele wa jasmini

ulikuwa ukiuzwa shilingi 34,000/- kwa kipolo cha kilo 25. Leo nimekwenda kuuliza unauzwa shilingi 43,000/- na hakuna kilichopanda kwa miezi 9, hii ni kwa sababu hakuna kitu kinachoitwa Tume ya Bei.

Mhe. Naibu Spika, hapo zamani nimeuliza na nimefanya utafiti nasikia ilikuwepo Tume ya Bei huwezi kupandisha wala kupunguza bei mpaka uruhusiwe na Tume ya Bei, vitu vyote vilikuwa vinakuwa-*regulated* na nilisema, hata tulipotoka katika mfumo wa Kisoshalisti na tukaingia kwenye mfumo wa Ki-capitalist nchi kama Marekani, Canada na nchi nyengine bado zina-*regulate* bei zao, lakini Zanzibar bei tunamuachia tajiri na tajiri hana Dini, Dini yake ghilba, faida na kitabu anachokifuata yeye anakijua mwenyewe.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo nakwenda Shirika la Viwango (*ZBS*). Kumekuwa na utaratibu wa wafanyabiashara wa magari kuleta Zanzibar wanaleta magari mengi. Lakini kumejitokeza wajanja wachache wako nchi za Dubai na nchi nyengine wameingia *contract* na serikali, kufanya kitu kinaitwa *PVOC*. Mhe. Naibu Spika, *PVOC* ni kweli inakubalika lakini utashangaa mfanyabiashara yule yeye anapata asilimia 70, serikali inapata asilimia 30 katika kitu kile, halafu hana hata kimoja anachokifanya. Mhe. Naibu Spika, naomba, na nchi yetu ni masikini, kazi ile ifanywe Zanzibar isifanywe nje ya nchi, ili faida ile yote tuipate Zanzibar na inawezekana. Tayari *ZBS* wameanza kuifanya kazi ile kwa zile gari zote ambazo zinaingia nchini hazijakaguliwa.

Mhe. Naibu Spika, hapo zamani mimi nakumbuka nimezaliwa Amani kulikuwa kuna viwanda vidogo vidogo, kulikuwa kuna Kiwanda cha Usumba, Kiwanda cha Sukari, Kiwanda cha Sabuni, kulikuwa kuna Kiwanda pale Maruhubi cha Samli. Mhe. Naibu Spika, viwanda vingi Zanzibar na ilikuwa watu wanapata ajira, viwanda sio chini ya 20, Kiwanda cha Viatu cha Bora, Kiwanda cha Sabuni, mule viwanda vidogo vidogo Kiwanda cha Samli, Kiwanda cha Madishi. Viwanda vingi vilikuwepo na vijana wakipata ajira, ilikuwa ikifika saa nane ya usiku kuna mabasi yanawasubiri watu na kuwachukua kuwapeleka majumbani, wote wameajiriwa na viwanda vile. Kwa hivyo, naomba serikali ifikirie tena angalau kuturudishia vile viwanda vyetu vya miaka thamanini ili tuweze kupata ajira nchini, viwanda vimepotea vilikuwepo, mpaka sigara tulikuwa tukizalisha wenyewe Zanzibar.

Baada ya hapo Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye wajasiriamali. Tumejitahidi tumefanya ...

Mhe. Naibu Spika: Umebakiza dakika tatu.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Tumefanya tulivyoweza wajasiriamali wako wengi, lakini bado tunashindwa kuwatafutia masoko.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea nakwenda katika Sekta ya Uvuvi. Nchi yetu imezungukwa na bahari lakini bado madiko yapo chungu nzima, wavuvi wako chungu nzima. Lakini leo Zanzibar samaki anauzwa ghali, mnyonge hali pweza, mnyonge hamli ngisi wala hamli chaza, kwa sababu vitu vyote hivyo vinauzwa ghali, vitu vyote hivyo anakula mtalii tu. Mhe. Naibu Spika, ni aibu kwa nchi ya Zanzibar iliyozungukwa na bahari. Kwa hivyo, naiomba serikali ifanye iwezekanavyo. Zamani samaki wakiuzwa kwa ratili, wakiuzwa na *Fisheries*, lilikuwepo Shirika la *Fisheries* linauza samaki kwa ratili. Kilimo Mhe. Naibu Spika, kulikuwa kuna maziwa yanauzwa wote tunakumbuka yalikuwa yanaendeshwa na serikali.

Mhe. Naibu Spika, mwisho namalizia kwa uchimbaji wa mchanga. Ni kweli nchi yetu imekuwa na mashimo mengi, mchanga unachimbwa. Lakini naiomba sana Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ifanye utafiti katika suala hili, kwa sababu ni lazima ije na *alternative*, wananchi wafanye nini, sio kuwazuwia tu wananchi wasichimbe mchanga. Mhe. Naibu Spika, wananchi wameanza kusema kwa sababu wao wameshajenga sisi wanataka kutuuwa. Naomba sana, sikatai wizara isifanye inavyotaka lakini wizara ifanye utafiti halafu ije na *alternative*.

Mhe. Naibu Spika, baada ya hayo, Mhe. Waziri wa Kilimo alituahidi kwamba baada ya miaka mitatu ataweza kuilisha Zanzibar mchele utakaolimwa Zanzibar. Zanzibar tunatumia tani 80,000 kwa mwaka.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe muda wako umekwisha.

Mhe. Hassan Khamis Hafidh: Namuomba Mhe. Waziri anijibu mpaka leo amefanya nini, amejitayarisha vipi na lini tutaweza kulima angalau tani 40,000 tu, nusu ya tunachokitumia kwa mwaka.

Baada ya hayo machache Mhe. Naibu Spika, na mimi naunga mkono hoja ya taarifa hii kwa asilimia 85 na asilimia 15 nina-*reserve* mpaka Waziri hawa wote watakaponijibu.

Mhe. Naibu Spika, la mwisho naomba kuwasilisha kwako. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mchangiaji anayefuata ni Mhe. Hussein Ibrahim Makungu baadae atakuja Mhe. Suleiman Makame Ali na Mhe. Maryam Thani dakika tano ameniomba.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Nabu Spika, nashukuru awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutujaalia jioni hii kufika hapa salama kujadili ripoti ya kamati, lakini pia niwashukuru Mawaziri wote watatu kwa kazi yao nzuri wanayoifanya na Serikali kwa ujumla, lakini pia niwashukuru wananchi wangu wa Jimbo la Mtoni kwa kuweza kuniwakilisha hapa leo hii kujadili ripoti hii ya Serikali yetu ya hapa Zanzibar. Lakini pia nimshukuru sana Mwenyekiti wa Kamati kwa kuwasilisha ripoti yao nzuri sana na Wajumbe wote niwashukuru sana na niwapongeze sana.

Mhe. Naibu Spika, mimi nianzie kwenye ukurasa wa 14 kwenye Wizara ya Fedha na Mipango nianze kwenye Benki ya Watu wa Zanzibar (*PBZ*) kwanza niwapongeze sana benki hii kwa juhudi zao kubwa na kuongeza wateja siku baada ya siku, kwa kweli mimi nafarajika sana kuona Benki ya Watu Zanzibar inafanya kazi vizuri, kwa hivyo nawapongeza sana nawashukuru, mpaka sasa wana matawi karibu 11 ndani ya Tanzania pamoja na Zanzibar jambo la kupigiwa mfano kabisa. Mimi binafsi natumia benki hii na nina akaunti hapa na pia nikiwa Tanzania Bara natumia sana benki hii ya *PBZ* pale Kariakoo.

Mhe. Naibu Spika, ninawashukuru sana taasisi hii ilivyojipanga ukenda pale tawi la Benki ya Tanzania Bara hasa Dar es Salaam Kariakoo, kwa kweli ukifika wanakutambua na ukitizama wafanyakazi wa pale asilimia kubwa ni Wazanzibari kutoka Zanzibar, kwa kweli tunafarijika tunasikia kama tupo nyumbani kwa kutupokea na kutuhudumikia hata kama unakosa kitambulisho basi wao wanakutambua na unapata pesa zako unalipwa bila ya matatizo yoyote. Kwa hivyo mimi nawapongeza sana kwa kututambua kwa sababu sisi tunapokwenda Tanzania Bara tunakuwa wageni na kidogo tunakuwa woga lakini tunapokwenda benki yetu pale kwa kweli wanatushughulikia vizuri na mimi niwapongeze.

Mhe. Naibu Spika, lakini changamoto kubwa naiona hapa katika benki yetu hii wakopaji wengi wanaokopa benki baadae wanashindwa kulipa deni. Mimi naomba sana iangalie hawa wanaokopa kama wafanya biashara wawe na vigezo vizuri bila ya hivyo benki hii itakuja kufilisika. Benki hii ni yetu kwa mujibu wa Serikali inasaidia mpaka Serikali kutoa faida yake inaiachia benki iongeze mtaji. Kwa hivyo mimi naomba sana waangalie vigezo wanapokopesha wafanya biashara ili benki hii iweze kupiga hatua kuweza kufanikiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye ukurasa Na. 3 Wizara ya Fedha Mipango Utekelezaji wa Maagizo ya Kamati iliyopita mwaka 2014/15.

Mhe. Naibu Spika, Mamlaka ya *TRA* Zanzibar mimi niipongeze sana sana kwa juhudi zao kubwa kwa makusanyo yao ya fedha nyingi ya walipa kodi hapa Zanzibar, wameweza kukusanya kwa miezi sita bilioni karibu mia moja na moja, sio jambo dogo kwa asilimia mia moja na kumi kupita mpaka malengo, Julai/Disemba 2016 mimi nawapongeza sana kwa juhudi zao kubwa hizi kwa kuongeza mapato ya Serikali yetu ya Zanzibar.

Lakini pia niipongeze sana Kamati iliyopita kwa juhudi zao kubwa wamefanya kazi kwa kutaka fedha hizi za *TRA* Zanzibar, makusanyo yabakie hapa hapa tuweze kuzitumia hapa hapa Zanzibar. Mimi nimshukuru sana na nimpongeze na nimkumbuke Mwenyekiti alikuwa Salmin Awadh Marehemu Mwenyezi Mungu amlaze mahali pema peponi inshaalla, kafanya kazi kubwa kwenye kazi hii kwenye kamati hii alikuwa Mwenyekiti, kuweza kufanya mpaka hizi fedha zimebaki Zanzibar kutumika hapa. Kwa hivyo wananchi wana hofu kubwa kweli kuona hizi pesa zinakwenda Tanzania Bara lakini kwa sasa fedha hizi zinatumika hapa wala wananchi wasiwe na hofu kwa kuona fedha zinaondoka zinakwenda Tanzania Bara, kwa hivyo hiyo kazi kubwa mimi nishukuru sana kero hii imemalizika.

Mhe. Naibu Spika, lakini jambo jengine nije kwenye *TRA* mbali ya kero hii imekwisha lakini kuna kero ndogo ndogo na hizo naomba zimalizwe hasa ukitizama Wajumbe wamechangia pia *TRA*, Naibu wetu Kamishna Mcha huyu ni mtu mwenye cheo kikubwa lakini leo akienda kwenye ngazi za Bara anakuwa mtu wa nne, hili jambo sio zuri. Mimi naomba sana aangaliwe kama yeye Naibu Kamishna basi awe chini ya Kamishna, hii ni Jamhuri ya Muungano ni chombo chetu pamoja. Kwa hivyo naomba Kamishna wetu awe na heshima kubwa akienda kwenye vikao awe mtu wa pili sio mtu wa nne. Kwa hivyo mimi naomba changamoto hii pia iangaliwe naamini pia kwa mujibu wa Muungano wetu inawezekana Kamishna wetu akawa mtu wa pili.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kwa upande mwengine kero hii kwa upande wa ajira *TRA* muda mrefu makubaliano haya yamefanyika kwa asilimia 21kwa 79. Mimi niseme ukienda Tanzania Bara pale utakuta *custom* zote ukenda upande wa Tanzania Bara hasa hapa Dar es Salaam, humkuti Mzanzibari anatoka Zanzibar yupo pale, unakuta wote wageni wanakuwa hata hawakujui kama wewe Mwakilishi au wewe nani au wewe kiongozi, wao wanaona watu wote hawafahamu. Kwa hivyo mimi naomba sana *TRA* iangalie upande wa Tanzania Bara pia Wazanzibari wakuwepo pale bandarini, wajue kuna watu wanakuja sio

wafanya biashara wanakwenda na mizigo yao midogo midogo, matokeo yake wanaambiwa walipe kodi.

Kwa hivyo ile mizigo mtu akiwa pale Mzanzibari atasaidia kusema huyu si mfanya biashara, huyu mtu wa kawaida anapita tu na matembezi yake au mambo yake binafsi. Hivyo naomba hii asilimia 21 kwa 79ifanyiwe kazi tupate ajira kule na *TRA* iunganishwe Wazanzibari waende kule kufanya kazi mbali na wao wako hapa kutoka Tanzania Bara, mimi sikatai tunashirikiana vizuri. Lakini na sisi tuende kule tukae na sisi tufanye kazi vizuri kushirikiana na watu wanaowatambua huyu fulani na huyu fulani kwa sababu mtu anatoka hapa Zanzibar itasaidia kuondosha hizi kero ndogo ndogo na mambo yanayokwenda sasa hivi, kuwa hayafahamiki mambo ya mizigo.

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi pia niseme kitu kimoja mimi nitoe mfano wangu mmoja, kuna siku moja nilikamatwa mimi na gari yangu mimi niko Zanzibar gari yangu ilikamatwa kule, juzi juzi sio muda mrefu inafika miezi minne imekamatwa ile gari imekamatwa na hawa jamaa wanaitwa *First team* wa *TRA* wanawafahamu wenyewe, yule dereva wangu akawaambia mimi nakwenda kumchukua Mheshimiwa baadae *Airport*, akasema haiwezekani hii gari inatoka Zanzibar kwa hivyo lazima hii gari niifungie, yule dereva akanipigia simu nikazungumza na mtu wa *TRA First Team* anaitwa Arnest, namwambia mimi naitwa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu hiyo gari ni yangu, ananambia jina la Makungu kwanza Zanzibar hamna wala hakai mtu Makungu Zanzibar.

Nikamwambia nikaja hapo utakuja kunifahamu tutaelezana, akanambia mimi sikufahamu. Akaniuliza jina lako kamili unaitwa nani, nikamwambia kwenye gari jina lipo limeandikwa Hussein Ibrahim Kibwana Makungu ndio jina langu halali, ndio hichi hapa kitambulisho changu, anasema siamini ananiambia wewe nani, nikamwambia mimi Mzaramu, ananiambia Mzaramu atakaa Zanzibar, unaona tatizo letu hilo.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilipokwenda Dar es Salaam nikaenda mpaka Ofisini nikawaambia mimi naitwa fulani fulani fulani nikamuonesha kitambulisho changu. Sasa historia ya Zanzibar kwa kweli wenzetu hawaijui mimi naomba sana wafahamishwe historia. Zanzibar imepatikana vipi wafahamishwe hii nchi ya Mapinduzi wafahamishwe imekuwaje mpaka tumezaliwa sisi wafahamishwe, wasijibu maneno waliyokuwa hawayafahamu. Mhe. Naibu Spika, wakiambiwa mtu fulani wachunguzwe, naomba historia waambiwe Zanzibar ni nchi ya Kimapinduzi, kuna mambo moja, mbili wayafahamu yote nchi moja tumeungana kwa nia njema. Kwa hivyo mimi naomba watu wa *TRA*

kidogo wapewe elimu kwa ajili ya watu wa Zanzibar na wafahamu hichi chombo ni kikubwa na Zanzibar ni nchi ina mamlaka yake vile vile. Kwa hivyo mimi naomba hiyo ifahamike kidogo.(*Makofi*).

Lakini Mhe. Naibu Spika, nitoe mfano mwengine, mimi nilikuwa Mjumbe wa Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi miaka minne iliyopita ya Baraza hili la Wawakilishi, ilikuwa tatizo kubwa changamoto moja ya Muungano hapa *Qatar Air Line* ilikuwa haiwezi kutua. Sisi Wajumbe wa Kamati tulikuwa tunapigania mamlaka tukienda pale tunaambiwa *Qatar* inataka kutua, *Turkish Air line* inataka kutua, tunashindwa kutua pale, ilikuwa changamoto kubwa Tanzania Bara hawatoi kibali cha kutua ndege ile wanasema ikitoka Arusha iende *Qatar* wakati wale wanataka kupita hapa. Lakini namshukuru sana sana Naibu Waziri Mhe. Issa Haji Ussi Gavu ile kazi akaichukua akenda Dar es Salaam yeye akenda kwa Marehemu Mungu amlaze mahala pema Samuel Sitta akenda kumueleza ile hali, kuna moja mbili tatu, ukitizama Mhe.Issa Haji Ussi Gavu kafanya kazi nzuri alipokuwa Naibu Waziri wa Mawasiliano.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kwa sababu ukitizama ndege inapotua hapa kuna kodi sisi tunapata, kuna *Airport* tumejenga kwa mkopo kutoka *Exim Bank* karibu bilioni ilikuwa 78, ikenda 124, sasa hivi iko 146 Dola za Kimarekani. Sasa kama hizi ndege hazitui hapa tutapata wapi hizo fedha za kulipa hayo madeni. *Airport* yetu inatengenezwa tuishukuru Serikali mwanzo ilikuwa na matatizo lakini walikuja washauri wakandarasi wazuri kutoka Ufaransa, wakai-*design* ile *Airport* na hatimae sasa hivi karibu itakwisha na *Airport* ile itakuwa nzuri itafanya kazi itasaidia mapato. Mimi naomba sana hii changamoto ya kuwa ndege hazitui hapa kama *Qatar Air* inatua *Turkish Air* inatua, na ndege ya Ethiopia na *Kenya Airways*, *Oman Air* na *Fly Dubai* na nyengine Emirate zitue tupate fedha, ili kila ndege zikutua ndio ile *Airport* itaingiza fedha kwa ajili ya kulipa huu mkopo tunaodaiwa hapa Zanzibar kwa ajili ya kupata mapato ….

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa umebakiza dakika mbili.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Naibu Spika, wacha nimalize. Mhe. Naibu Spika, nije kwenye utekelezaji wa malengo ya ukusanyaji wa Mapato wa Bodi ya Mapato. Mimi kwanza niipongeze sana hii Bodi ya Mapato yetu Zanzibar *ZRB* kwa kazi yao kubwa hasa malengo waliyoweza kukusanya kwa miezi sita bilioni 134 kwa kweli kazi sio ndogo. Lakini mimi niseme Mhe. Naibu Spika, matatizo ya kodi katika ripoti imesema hawa watalii wanaokuja *package tourism* hawa waangaliwe toka wanaingia *Airport* wanakwenda wapi hoteli gani ili mapato yao yadaiwe, kwa sababu hawa ndio wenye fedha nyingi hawa wageni kutoka nje na watalii wa kuja kutumia na hawa mapato yao

yanapotea, wanakuja kukamatwa watu wanyonge walipishwe makodi kufidia. Kwa hivyo mimi naomba sana *ZRB* muangalie tangu *Airport* hii *package* inakwenda wapi ya *tourism*, hoteli gani imefanya *booking* wanakwenda mfuatilie kule kule.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine mimi niseme Mhe. Naibu Spika, *ZRB* kweli inafanya kazi kubwa lakini iangalie wanapokwenda mahoteli saa nyengine wanasema lazima chumba kifunguliwe. Kwa hivyo mimi nawaomba sana wakae washirikiane na wakuu wa hoteli ili wawe pamoja kuliko kufungua vyumba wale wageni wanakuwa na wasi wasi wanaona kama kuna tatizo baina ya …….

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa muda wako umekwisha.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, mimi naunga mkono ripoti asilimia mia kwa mia ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante ninakushukuru. Mchangiaji wetu mwengine ni Mhe. Suleiman Makame Ali na baada ya hapo kuna wachangiaji watu watachangia kwa dakika tano tano, ataanza na Mhe. Maryam Thani, atakuja Mhe. Jaku Hashim Ayoub ikisha atakuja Mhe. Said Soud Said. Mhe. Suleiman karibu.

Mhe. Suleiman Makame Ali: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi nashukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kuchangia ripoti hii ya kamati ya fedha, biashara na Kilimo.Mhe. Naibu Spika, kwanza niwashukuru Wajumbe wa Kamati hii ya Fedha, Biashara na Kilimo chini ya Mwenyekiti wao Mwenyekiti hajiri, mbunifu, shupavu Mhe. Yussuf Hassan Iddi kwa kazi nzuri waliyoifanya na leo kutuwasilishia ripoti hii tunayoijadili.

Mhe. Naibu Spika, pia niwapongeze Mawaziri hawa watatu kwa wanavyofanya kazi nzuri ya kuhakikisha kuwa wanazisimamia Wizara zao na kutekeleza kuhakikisha kwamba ilani ya Chama cha Mapinduzi inatekelezeka.

Mhe. Naibu Spika, mimi niende kwenye masuala ya ufugaji wa samaki, wafugaji wa samaki wana changamoto nyingi sana Serikali imewataka wananchi kwamba wajihusishe na masuala ya ufugaji samaki, lakini wafugaji hawa wanapata adha ambayo kwamba inawakabili ikiwemo mitaji na nguvu kubwa wanayoitoa. Kwa hivyo hapa niiombe Wizara inayohusika kuwapatia mafunzo wafugaji wa samaki hawa hawana taaluma ya kutosha jinsi wanavyofugwa samaki. Mhe. Naibu Spika, nithubutu kusema kwamba

wafugaji wa samaki wamehamasika sana zaidi hususani kule Pemba. Jimboni kwangu Ndagoni kuna kama mabwawa matatu wanafuga samaki lakini wote ukiangalia taaluma hawana pia uwezo mdogo. Kwa hivyo hapa niiombe Wizara na Serikali kwa ujumla kwamba ihakikishe wafugaji hawa wanawezeshwa kwa hali yoyote ile ili kuhakikisha kwamba wanafuga samaki kama inavyokusudiwa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye masuala ya misitu. Mhe. Naibu Spika, misitu Zanzibar inatoweka na sasa hivi kuna ukataji wa miti wakati wa usiku kwa kutumia misumeno ya moto. Kwa hivyo hapa pia vile vile niiombe Wizara husika ishirikiane waunde kamati kwenye zile Shehia zenyewe ili kuwadhibiti hawa wahalifu, kwa sababu mpaka usiku saa sita au saba unasikia misumeno ya moto inanguruma, kwa vile waunde kamati hizi washirikiane na Masheha ili kuwadhibiti hawa tukomeshe suala hili la ukataji wa misitu.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la uvuvi. Uvuvi ni kazi moja kubwa ambayo kwamba Wazanzibari wengi wanaishi kwenye mwambao ya bahari wanaitegemea kazi ile, lakini kuna sheria nyingi ambazo kwamba zinawabana baadhi ya wakati mwengine na leo hapa tumemsikia Mhe. Hidaya Ali Makame alisema kwamba pweza hawapatikani, lakini sasa pweza watapatikanaje wakati pweza anakaa kwenye maji si chini ya pima kumi naa, pweza yule hapatikani bila ya kwamba mvuvi kuna zana maalum za kwenda kuvulia. Sasa Mhe. Naibu Spika, pia vile vile niungane na Mhe. Hidaya hapa alisema kuhusu masuala ya uvuvi harama ni kweli sikatai uvuvi haramu upo, lakini hii Wizara ihakikishe kwamba uvuvi haramu wanaukomesha ni kutafuta vyombo vya kuwadhibiti hawa wanaofanya uvuvi haramu, lakini tukisema kwamba uvuvi haramu wavuvi wasivue mfano itakuwa leo pweza hapatikani, samaki hapatikani kwa sababu wote wavuvi wanakwenda kule baharini kutafuta hivi vitu kutuletea sisi na sisi tukapata kunufaika.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye suala la maghala. Kuna maghala mengi ya Serikali lakini sasa hivi ukiangalia maghala yale hayafanyi kazi mengine ni mabovu haiba yake imepotea kabisa, yamekaa tu maghala yale hayaulizwi chochote mengine yamekodishwa. Kwa hivyo hapa nimuombe Mhe. Waziri kwamba kuhakikisha kwamba kwenye masuala haya ya maghala turudi kule kule kama zamani kuhakikisha kama maghala haya yanafanya kazi ipasavyo na waliokuwa tayari wameshakodishwa lakini hawashughulikii waweze kunyang'anywa wapewe watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, niende kwenye Shirika la Biashara (*ZSTC).* Umuhimu wa zao la karafuu ni zao la taifa kwa nchi yetu hii ya Zanzibar lakini niiombe

Wizara husika hapa kupitia shirika hili kwamba wahakikishe kule kwenye sehemu nyengine za karafuu ambako hakufikiki kuna barabara mbovu waweze angalau kutengeneza barabara zile kwa kiwango cha fusi, ili wakulima wetu wanufaike na waweze kuvuna mavuno yao ili wapate kwenda kuuza kwa uhakika.

Mhe. Naibu Spika, pia vile vile niende kwenye suala la *ZSTC* kuhakikisha kwamba vile vituo vyote vya karafuu ambavyo ni vya zamani vyengine ni vibovu basi wahakikishe wanawaboreshea wakulima wetu, na kuwaondoshea usumbufu wajenge vituo vipya vya kisasa ili wakulima wetu waondokane na ule usumbufu wa kwenda kuuza karafuu ikawa siku nyengine banda linavuja karafuu zake zikavujiwa.

Baada ya hayo Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti hii asilimia kwa mia. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Suleiman Makame Ali. Sasa Mhe. Maryam Thani Juma.
dakika tano.

Mhe. Maryam Thani Juma: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, na mimi kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia kwa dakika tano machache ambayo nimeyaandaa katika ripoti hii. Mimi kwanza kabisa niende kwenye ujenzi wa chumba cha baharini.

Mhe. Naibu Spika, niungane na kamati kuwapongeza wawekezaji kushirikiana na *ZIPA* kwa kututengenezea chumba hichi kilichoko chini ya bahari katika Mkoa ule wa Kaskazini Pemba, kwa kweli hata mimi nilipotembelea katika chumba kile niliona chumba hichi kina thamani na kinaweza kutuingizia mapato mengi katika nchi yetu kutokana na watalii wanaokuja kukitembelea, au kuja kukodi katika chumba kile. Serikali ishirikiane na wawekezaji wajitahidi kuwaomba *ZIPA* ili watuongezee vyumba vyengine katika kisiwa chetu cha Pemba ili kuweza kuingiza mapato zaidi katika Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niende katika kipengele cha uimarishaji wa viwanda. Kwa kweli suala hili ni muhimu sana katika nchi yetu kwa sababu asilimia kubwa ya Wazanzibari ni maskini na ukizingatia kwamba ajira ni ngumu katika nchi yetu na kwa kweli hazipatikani, tutakapotengenezewa viwanda hivi vidogo vidogo tutaepukana na mrundikano wa ajira zinapotangazwa Serikalini, ajira mbili wanakwenda watu elfu mbili au elfu moja, watakapotutengenezea viwanda hivi

Serikali kupitia wawekezaji basi tatizo la ajira litapungua katika nchi yetu na vijana watapata kujiajiri wenyewe katika viwanda hivi vilivyopo nchini kwetu.

Mhe. Naibu Spika, naendelea katika ubora wa mezani zinazotumiwa na wafanya biashara hapa nchini, kwa kweli tutumiaji wa mezani katika nchi yetu wafanyabiashara wanaitumia vibaya mezani na hata Dini yetu ya Kiislamu imesisitiza sana suala la utumiaji vibaya wa mizani. Mhe. Naibu Spika, wafanya biashara wetu hawazichunguzi mezani zao au huwa wanazifanyia kusudi mimi nasema kusudi kwa ajili ya kuwadhulumu wananchi wetu, lakini serikali iangalie kwa kina suala hili. Mhe. Naibu Spika, hata suala hili katika Shirika letu la Biashara la *ZSTC* wanaopima karafuu kwa kweli mezani hii huwa wanaitumia vibaya na kupelekea wananchi kulalamika kwa wale ambao wanazalisha zao hili la karafuu na waliokuwa hawana mikarafuu wanakwenda kuokota zile moja moja basi wakifika pale wanadhulumiwa, hili kweli lipo. Serikali ijitahidi kuzungumza na watu hawa au kurekebisha hili ili wananchi waweze kupata haki yao kama inavyotakiwa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika sekta ya kilimo. Kwa kweli tunajua Wazanzibari wengi ni wakulima na ukulima huu wa mpunga ndio ambao tunahitaji upatiwe pembejeo za kutosha ili tuweze kuzalisha mpunga kwa wingi, pamoja na wale ambao wanalima regesheni na wale waliyokuwa na mashamba yao binafsi wapate mafunzo na utaalamu wa kuzalisha mpunga zaidi ili tuepukane na kuagizia mpunga kutoka Tanzania Bara ama sehemu nyengine. Ukulima huu wa mpunga uwekwe kipaumbele kutokana kutokana na mahitaji, naiomba serikali ijitahidi kwa hilo...

Mhe. Naibu Spika: Malizia Mheshimiwa dakika tano zako umezimaliza.

Mhe. Maryam Thani Juma: Kwa hayo machache Mhe. Naibu Spika, naunga mkono ripoti hii asilimia mia kwa mia.(*Makofi*).

Mhe. Nabu Spika: Ahsante sana Mheshimiwa. Mhe. Jaku Hashim dakika tano.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Ahsante sana Naibu Spika namimi itabidi nicharaze haraka haraka bila ya kuchelewa wala sitojiremba sana kumshukuru Waziri wala Naibu Waziri.

Mhe. Naibu Spika, Mhe. Waziri wa Fedha nakupa ushauri mbao uusikilize kwa makini, unataka uchumi ukuwe wala sitaki uje kunilipa mimi ni ushauri wa

haraka haraka, naomba unisikilize kwa makini Mhe. Waziri faida yetu sisi na Wazanzibari.

Bismillahi Mhe. Naibu Spika, "vita vya panzi neema ya kunguru". Mhe. Waziri wa Fedha unataka uchumi ukuwe hapa ni pakujipanga sasa hivi, nisikilize vizuri. Kama umesikia wenzetu hivi sasa mji unahamia Dodoma ndugu zetu wa Dar es Salaam au Tanzania Bara, hiyo ndiyo nafasi ya kuitumia, Mabalozi wanataka kuja kuhamia hapa Zanzibar, watafutie eneo ili waje wawekeze. Mtu hawezi kutoka Dar-es-Salaam kwenda Dodoma kwa masaa 10 kwa kutafuta viza tu wakati akipanda boti nusu saa keshafika, hapa ndio pakutengeneza sasa hivi.

Mhe. Naibu Spika, Mabalozi wengine nasikia harufu wanataka kuja kufungua Ubalozi wao mdogo, nafasi ndio hiyo. Nafikiri umeniskia Mhe. Waziri na kuna mengine hayawezi kuzungumzika hapa nitafute baadae nikushauri. Hii ndiyo njia pekee, huu ni ushauri kwa maslahi yetu sote, ingawa "*baniani mbaya kiatu chake dawa"* nitafute baadaye hiyo ni *hit point* kama *indicate*. Nafasi ni hii, mtu hawezi kuumiza mgongo wake kwenye basi saa 12 akenda kule Dodoma, maji yenyewe hayatoki, skuli hapana, hoteli ya kulala pale hapana. Mabalozi wengine wanataka kukwepa wanasema bora mtupeleke Zanzibar kufungua Balozi, wakija waruhusuni wala msitafute njia za kuwakwepa. Mengine nitafute siwezi kuzungumza hapa ni mambo muhimu hayo Mhe. Waziri.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, baada ya ushauri huo nije kunako kitengo cha *ZIPA*. Mhe. Naibu Spika, hawa vijana wa *ZIPA* wanafanya kazi kwa umakini wa hali ya juu tuwashukuru kwenye kitengo cha *ZIPA* hawa vijana wanafanya kazi kwa umakini wa hali ya juu tuwashukuru. Lakini kuna watendaji wa Kamisheni ya Ardhi au Wizara ya Ardhi, Maji inawarejesha nyuma na mifano ipo, mara ya kwanza, mara ya pili na mara ya tatu nimeshazungumza. Kuna mtu mmoja kwa *interest* zake mbili tatu miradi inakwama na hilo mliangalie mtafute njia wenyewe mimi kazi yangu kueleza tu.

Nije upande wa *ZSSF* kidogo tuwe makini ndugu zangu hapa ndio pa kusema, pesa mnazowekeza ni pesa za wananchi, pesa hizi mlizoziwekeza kipindi cha muda huu tungefungua benki kama tatu au nne na hizi pesa nafikiri hazikaguliwi na *auditor*. Tumepitisha sheria juzi tumewabana wananchi huku *ZSSF* inatanua pesa hazipo, miradi ya Tibirinzi, Kariakoo, mnara ule ni pesa nyingi tulizowekeza jamaa tuliangalie nalo.

Baada ya hapo nije kwenye suala la *TRA* Mhe. Waziri hapa naomba uunde Kamati itakayosaidia na waingie Wawakilishi. Juzi nilisema hapa mpaka mbatata na vitunguu vimezuiwa, sizungumzi kwa kubahatisha hayo. Hapa tunahitaji mbatata sisi, ndugu zetu walitaka kuzizuia zikapimwe. Tunapozungumza pale sijui mnatufahamu vipi, mbatata nazo pia, zuia *TV*, zuia kompyuta, zuia mambo mengine lakini mbatata nazo pia unataka kuzuia nazo nobe. Tutakwenda wapi? Tukikwambieni kweli hamfuatilii. Mnajua sisi uwezo wetu ni wakubwa wanaoumia ni wananchi, sisi tuna gari zina viyoyozi ndani hata habari ya nchi hatuwezi kuijua. Kwa hivyo Mhe. Waziri hapa uwe makini mtu ana TV yake moja anazuiwa, wafanyabiashara watoto wadogo wanapata mateso.

Mhe. Naibu Spika, nije kwenye Wizara ya Fedha, hapa kuna Mahakama ya Rufaa ya Kodi sijui kama Mwenyekiti keshateuliwa Kanuni hazipo hapo Mhe. Waziri, na hapa kuna kesi nane mpaka sasa hivi hazijui zianzie wapi. Sijui kama tumeshapitisha hiyo sheria hapa, tunafanya mambo ya ajabu ajabu. Pengine Serikali inahitaji kodi hapa, pengine kesi hizi tushindwe. Mhe. Naibu Spika, hapa nitahitaji maelezo.

Mhe. Naibu Spika, wafanyabiashara mimi nimeshaonewa nataka kwenda kwenye wapi kwenye kodi ya biashara lakini mambo ya ajabu hayo. Niiombe Wizara ya Biashara kwa maslahi ya Wazanzibari nyinyi ndio mlioshika mambo haya. Huko nje ma- *pharmacy* sasa hivi kama pahala dawa zote zinakuwa bei moja, mje na sheria au kanuni au mlete Mswada humu ndani tuuchangie, wanaoumia wananchi. Wizara ya Afya sasa hivi dawa hamna *pharmacy* zote ziwe bei moja na ndiyo ilivyo huko duniani, Oman tu hapo karibu ukinunua *panadol* duka hili na kwengine bei yake hiyo hiyo, tujaribu kuyadhibiti inawezekana kwa maslahi ya wananchi tusije tukawaumiza wananchi. Wizara ya Bishara naomba ikae na Manispaa, hii serikali isingekuwepo madarakani bila ya kuwepo wananchi, wananchi ndio waliyoitaka serikali hii, tulikubali hilo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sisi tumshukuru Alhamdulillahi Mwenyezi Mungu maslahi yetu sio mabaya, lakini anayeumia ni mdogo wa nchi hii. Wauza mikate ya boflo wanakwenda kunyanyaswa kwa kosa gani, hawachafui mazingira wale, ana susu lake na baiskeli akimaliza anaondoka, wanakwenda wakateswa utafikiri wafungwa gani yakhe. Waziri wa Biashara ulifuatilie ukae na Mhe. Waziri anayeshughulikia Wizara hii anayeongoza Manispaa wale na wao ni binadamu nao. Mkate wenyewe shilingi tu faida, wanakwenda kunyanyaswa, wanachukuliwa mikate yao haijulikani inakwenda wapi. Huu ndio ukweli ulivyo na sizungumzi kwa kubahatisha. Lakini waoneeni huruma, mkate

unachafua mazingira gani kwenye susu, wale wafanyabiashara wanaouza hebu tuangalie duniani kote hayapo haya. Thailand pale zinafungwa barabara Sokomviti ile saa 10 jioni mpaka saa 4 asubuhi watu wanafanya biashara usiku mchana. Tujifunze jamani, tusifanye kutaka kuwaonea wananchi. Hapo hapo pana kodi mbili hapa Wizara ya Biashara *ZBS* wanatoza kodi na Bandarini pale na tumepitisha juzi Bodi ya Chakula unatozwa kodi...

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim umebakisha dakika moja.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Eeeh! Mheshimiwa hii hatari, "haya aangukavyo ndivyo achinjwavyo."

Mhe. Naibu Spika, nije katika Wizara ya Kilimo kuhusu mchanga. Tunataka kufuta viwanja ndio hayo niliyouliza kuku na yai lipi lililokuja mwanzo duniani. Utajengaje kiwanja bila ya kuwa na mchanga, tunawaumiza wananchi jamani kawatafutieni viwanja vikubwa kule kwenye makuta. Wananchi ndio waliyoiweka serikali hii madarakani jamani, tusioni hapa sisi tunachezea *air condition* wananchi wanaumia, maisha magumu huko nje. Sisi wengine tumeshachukua posho kwa Dau (mshika fedha) sasa hivi hata shilingi hatuna hapa muda huu huu, tuwaangalie wananchi maslahi yao.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jengine la mwisho kwa kumalizia mimi sikubaliani na haya maoni ya Kamati, Mamlaka ya Maji (*ZAWA*) iharakishe kufikisha maji katika maeneo yanayohusika. Leo Michamvi tokea dunia ilipoanza kuna mahoteli manane au sita, anathaminiwa mtu mmoja huyo wananchi wanaumia, uhalali iko wapi, watu wanaumia kwa mtu mmoja tena ana uwezo wake *I don't know* yakhe, *what are we are doing?*

Mjumbe: Aah**!**

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Leo wananchi wa Michamvi ilani ya Chama cha Mapinduzi itafikaje kwa vitendo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Jaku Hashim Ayoub, muda wako umekwisha.

Mhe. Jaku Hashim Ayoub: Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa heshima na taadhima ahsante. *(Makofi)*

Mhe. Said Soud Said (Mhe. Waziri Asiyekuwa na Wizara Maalum): Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi.

Kwanza nachukua nafasi hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi kwa kuweza kuwateuwa wazalendo kuongoza Wizara hizi ambazo sasa hivi zinajadiliwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Kilimo awali ya awamu iliyopita ilikuwa kama yatima ambayo ilikuwa haina mtu maalum wa kuitetea wala wa kuisimamia. Wizara hii iliyumba sana na ilionekana wazi kabisa kwamba nyenendo na taratibu za Wizara hii zilikwamisha maendeleo ya Wazanzibari kwa muda mrefu. Wizara hii kule Pemba ina wataalamu wengi tena sana, lakini wataalamu wote walikuwa wamekaa kwa imani zao zilizokuwa potofu, walikuwa wanasubiri serikali itakayokuja na hatimaye wakaikosa serikali hiyo imebakia ile ile Serikali ya Mapinduzi. Lakini kwa jitihada ya Waziri ambaye yupo kwenye wizara hii, nawapongeza sana wataalamu wale kwa kurudisha ari yao ya kufanya kazi na hatimae leo wizara hii naamini wazi kabisa kwamba itaweza kufanya maajabu kwa muda mfupi sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Biashara nampongeza sana Mhe. Waziri kwa jitihada yake kubwa ambayo ameionesha kwa muda mfupi sana kiasi cha kwamba leo hii biashara imekua kwa kiasi kikubwa na hasa zao la karafuu limeongeza tija na kuonekana kwamba ni zao ambalo sasa hivi linaendewa mbio na Wazanzibari wote kila mmoja anaharakisha namna ya kupanda mikarafuu ili aweze kupata namna ya kujikwamua kiuchumi.

Mhe. Naibu Spika, wizara hii kwa uhakika kabisa sasa hivi ni kitu ambacho kinapigiwa mfano kwa Zanzibar ukilinisha na huko nyuma wizara hii ilikuwa ikiongozwa na mtu ambaye hakuwa na nia ya kuleta maendeleo ya Wazanzibari. Lakini bahati nzuri sasa hivi wizara hii inaongozwa na mtu ambaye nina imani kabisa kwa uzalendo wake mabadiliko mengi yataweza kuonekana kwa muda mfupi sana.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Fedha ambayo kwa kweli inaongozwa na mzalendo mwenye ari ya Mapinduzi ya Zanzibar na nina imani kabisa kwamba ari yake imetuwezesha sisi kuona mabadiliko mbali mbali ambayo yanafanywa na serikali ikiwemo hata wazazi wetu kuweza kupata 20,000 (elfu ishirini) kila mwezi bila ya wasi wasi ikiwemo ari ya kuonekana kwamba mpaka mshahara unategemewa kupandishwa mwezi Aprili, kwa maana ya kwamba mapato yanaongezeka siku hadi siku kutokana na jitihada kubwa ya Waziri huyu pamoja na watendaji wake.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, inaonekana wazi kabisa kwamba wizara hii baada ya muda mfupi itaweza kuigeuza Zanzibar katika mazingira mazuri ya kifedha.

Ninachoomba sasa watendaji wote wa Wizara hizi ambao wanaozungumzwa hapa ni vizuri sasa wakawa na ari ya kuleta ile ari ya Mapinduzi ya Zanzibar ili kuwafanya Wazanzibari wawe na serikali ambayo inakuza uchumi, inakuza biashara na inakuza kilimo katika kujiletea maendeleo Wazanzibari.

Nawaomba Wawakilishi kuwa tayari kuwafichua wale wote wabadhirifu ambao kwa nia moja au nyengine wana nia ya kukwamisha maendeleo ya Serikali ya Zanzibar ili serikali iweze kuchukua hatua juu ya watu hao na kuweza kuwaondosha katika dhamana zao mara moja. Tunaamini kabisa kwamba harakati ambazo zinachukuliwa na Wizara hizi zitaweza kuleta maendeleo kwa muda mfupi sana katika visiwa vya Unguja na Pemba.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, ahsante sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Said Soud Said ahsante sana.

Waheshimiwa Wajumbe bado tumebakiza muda kama dakika kumi kwa ajili ya Waheshimiwa Mawaziri na wao kuweza kutoa ufafanuzi wa baadhi ya mambo ambayo hapa yameelezwa. Lakini vile vile na mwenyekiti kuweza kufanya majumuisho. Kwa maana hiyo basi ningemuomba Mwanasheria Mkuu aweze kututengulia Kanuni ya muda ili tuweze kuendelea na shughuli yetu na kumaliza shughuli hii leo.

KUONGEZA MUDA WA BARAZA

Mhe. Mwanasheria Mkuu: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na naomba nitoe hoja mbele ya Baraza hili ya kutenga kando Kanuni ya 23 ambayo ndiyo Kanuni ya Muda ili tuweze kuendelea na shughuli hii iliyokuwepo mezani mpaka pale tutakapoimaliza.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa hoja imetolewa wanaokubaliana na hoja hiyo wanyooshe mikono, wanaokataa, wanaokubali wameshinda.(*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)
(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Sasa Waheshimiwa Wajumbe nitamkaribisha Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed na baadae atafuatiwa na

Mhe. Balozi Amina Salum Ali na mwisho atakuja Mhe. Hamad Rashid Mohamed.

Karibu Mhe. Dkt. Khalid Salum Mohamed.

Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango: Mhe. Naibu Spika, kwanza naomba nianze kwa kumpongeza sana Mhe. Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi kubwa waliyoifanya, lakini vile vile kuandaa ripoti nzuri ambayo ina maelezo ya kina na wametupa na ushauri wao, wameonesha maeneo ambayo yana changamoto lakini na wametupatia ushauri wao, nawapongeza na nawashukuru sana kwa kazi hiyo nzuri waliyoifanya.(*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika, pia nichukue fursa hii kuwapongeza Waheshimiwa Wajumbe wote waliopata fursa ya kuchangia taarifa hii, wametoa maelezo yao, wametoa maoni yao na niseme kwamba maoni yao na ushauri wao tunauchukua. Kwa hivyo wale wote waliotoa maoni na ushauri basi ushauri huo na maoni hayo tunayachukua na tutayafanyia kazi ipasavyo.

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kuvipongeza sana vyombo vyetu viwili *TRA* na *ZRB*. Katika maelezo yangu sikusudii kujibu hoja za Waheshimiwa Wajumbe, nakusudia kutoa ufafanuzi lakini vile vile na mimi kutoa mchango wangu. Majibu ya yote yaliyoonekana na Kamati hii nitakuja kuyatoa mwezi wa Septemba. Kwa hivyo kwa wale ambao sitoyagusa maeneo yao katika ufafanuzi wangu naomba wastahamili mpaka mwezi huo.(*Makofi*).

Moja ya jambo nililotaka kulizungumza ambalo limezungumzwa na Waheshimiwa Wajumbe wengi ni suala la kuvuja kwa mapato. Takriban Wajumbe wote walizungumza hili kwa hisia na ni wajibu wao kufanya hivyo, kwa sababu mapato ya serikali ndiyo roho ya kuendesha nchi yetu. Lazima tukusanye mapato ili kuweza kutekeleza mipango ya maendeleo katika nchi. Kwa hiyo mandeleo katika nchi yetu yanategemea mapato. Kwa hivyo nawapongeza sana kwa *concerning* yao hiyo.

Mhe. Naibu Spika, niseme kwamba katika kuimarisha ukusanyaji wa mapato kwanza tujipongeze tumefanya kazi nzuri sana chini ya uongozi wa Rais wetu Dkt. Ali Mohamed Shein na miongozo yake ambayo anatupatia tumepata mafanikio makubwa sana katika kipindi cha miezi sita. Nathubutu kusema kwamba serikali hii katika kipindi hichi cha miezi sita imekuwa ikiendeshwa kwa fedha zinazopatikana kutokana na vyanzo vya ndani. Mishahara yote tunalipa kwa wakati lakini tumeweza kulipa mafao ya wastaafu wetu mpaka

mwezi wa Agosti 2016. Hayo ni mafanikio makubwa, Mawizara ya Tasisi zote zinapata mgao wao kwa mujibu wa *cash flow* zao. (*Makofi*)

Miezi kumi iliyopita tulikuwa tukikusanya mapato ya wastan wa shilingi bilioni 23 na bilioni 24. Lakini sasa tuko karibu bilioni 50 hayo yanaashiria kwamba bado tunayo fursa ya kuongeza mapato tukiongeza juhudi. Nitoe shukurani zangu za dhati kabisa kwa vyombo vyetu na watendaji wote, lakini niwapongeze pia walipa kodi wetu kwa kukubali kulipa kodi. Sasa kwa wale wachache ambao pengine kwa namna moja au nyengine hawajafahamu umuhimu wa kulipa kodi zao hao tutaendelea kuwafuatilia.

Kulikuwa na wasiwasi wa kwamba makusanyo haya ni asilimia 30 ambayo ni kiwango kidogo kuna Mjumbe mmoja alizungumza hilo. Nitoe wasi wasi kwamba milioni 30 hizi ukichukua makusanyo ya miezi 6 ambayo ni shilingi bilioni 249.47, lakini malengo kwa mwaka yalikuwa shilingi bilioni 824.36, lakini hizi shilingi bilioni 824.36 yanajumuisha fedha za kutoka nje. Sasa ukizichukua hizo utakuta kweli asilimia ya makusanyo yetu ni asilimia 30 na hizo fedha zinazotoka nje kwa nini hazikupatikana ni kwa sababu miradi ambayo tuliipanga itekelezwe bado iko katika hatua za maandalizi. Kwa hivyo fedha zake hazijaweza kuingia.

Mfano mradi wa *Terminal II* bado tuko katika matayarisho ya mradi huo kuanza na tunatarajia Mwenyezi Mungu akitujaalia utaanza ndani ya mwaka huu wa fedha. Lakini kuna bandari ya Mpigaduri bado fedha zake hazijaingia, kuna mradi wa *E-Government* bado pesa zake hazijaingia. Sasa hizo ndio zilizofanya asilimia hii iwe asilimia 30 lakini kwa mapato ya ndani *ZRB* kwa mujibu wa taarifa hii na takwimu zetu tumekusanya bilioni 138.75 wakati malengo yalikuwa shilingi bilioni 133.24 sawa na asilimia 104. *TRA* lengo lilikuwa kukusanya shilingi bilioni 91.92 lakini tumeweza kukusanya shilingi bilioni 101.3 sawa na asilimia 110. Ndio maana Mhe. Naibu Spika, nikasema kwamba Serikali hii tunaiendesha hivi sasa kwa fedha za vyanzo vyetu vya ndani. Tujipongeze sana tumpongeze Rais Dkt. Ali Mohamed Shein na tujipongeze wote kwa kazi nzuri lakini bado tuna *challenge* ya kuongeza juhudi ili mapato yaongezeke na fursa hiyo ipo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la manunuzi na uuzaji. Hili nalo lilizungumzwa kama ni sehemu ambayo inapoteza mapato ya Serikali au fedha za Serikali. Niseme tu Mhe. Naibu Spika, kwamba hivi juzi sote tumeshuhudia tumepitisha Sheria mpya ya Ununuzi na Uondoshaji wa Mali za Serikali. Kupitisha sheria ni jambo moja, sasa ni suala la utekelezaji wa sheria ile na katika hilo sisi tumejipanga na kubwa kwanza kutoa taaluma kwa vyombo vyetu ambavyo

vinaundwa ndani ya sheria ile ikiwemo Bodi ya Tenda, Wajumbe wake lazima katika kila Taasisi wapatiwe taaluma lakini hivi Vitengo vya manunuzi (*Procurement Management Unit)* watendaji wake wapatiwe na taaluma na maofisa wote wanaohusika. Lakini vile vile tutoe taaluma kwa *oversight organs* zetu. Kwa mfano Kamati yetu ya *PAC* lazima nayo inahitaji kupatiwa taaluma kuhusiana na sheria ile lakini ofisi ya *CAG* lazima tuipatie taaluma na kazi hiyo tunajipanga kuifanya, ili kuhakikisha kwamba manunuzi yetu na uondoshaji wa mali za Serikali unafanyika kwa mujibu wa sheria ambayo tayari tumeshaipitisha. (*Makofi*).

Kuna suala la mashamba ya mipira nalo hili nilitaka nilizungumzie kidogo na nisema tu Mhe. Naibu Spika, kwamba ni kweli Kampuni ya *AGROTEX* imeshindwa kuyaendeleza mashamba haya. Lakini niseme pia kwamba Kampuni hii imeondoka na madeni, madeni ya Serikali, kuna madeni ya wafanyakazi lakini pia kuna madeni ya *PBZ*, walikopa *PBZ* na bado hawajarudisha madeni hayo. Baya zaidi ambalo linatukwamisha katika juhudi zetu ni kwamba wenzetu hawa hawana mali zisizohamishika. Kwa maana ya *immovable assets* ambazo sisi tungeweza kuzishika ikawa ndio sehemu ya kuhangaikia kuzipata fedha zetu. Lakini pamoja na hayo tunaendelea kujadiliana na mwekezaji huyu na tuko katika hatua za mwisho hivi sasa kukatisha mkataba na Kampuni ile.

Vile vile niseme Serikali imeunda Kamati Maalum ya Wataalam na Kamati hii imeundwa na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais, na hivi juzi tulikutana na Kamati hiyo na tulikutana na Mhe. Makamu wa Pili wa Rais lakini imepewa kazi ya kuangalia suala zima la mashamba ya mipira, madeni yaliyoachwa lakini vile vile kuanza kufikiria mpango mbadala wa matumizi ya mashamba haya. Tayari ripoti ya mwanzo imeshatolewa inaendelea kujadiliwa na baadae mapendekezo yatatolewa Serikalini ili kuona hatua gani zichukuliwe katika kuyahami mashamba haya ya mipira yaliyopo katika maeneo mbali mbali ya visiwa vyetu vya Unguja na Pemba.

Mhe. Naibu Spika, kuna suala la jengo la abiria la uwanja wa ndege wa Abeid Amani Karume *Terminal II*. Kwanza niseme Serikali inaendeleza jitihada za kuhakikisha kwamba ujenzi wa jengo lile unaendelea. Kuna maelezo yalizungumzwa nataka niseme kwamba si sahihi kwamba kuna ndege zitakazoshindwa kuegeshwa katika uwanja ule kwa sababu zitazidi katika eneo la kurukia si sahihi, kwa sababu tayari kumefanyika mabadiliko ya michoro na ndege za aina zote ikiwemo *type 'E'* zitaweza kufunga kwenye madaraja yale ya kufungia ndege kwa upande wa Kusini ya uwanja ule. Kwa hivyo hiyo si sahihi. Lakini pia niseme kwamba si sahihi taarifa iliyotolewa ya kwamba

uwanja ule utagharimu jumla ya dola za Kimarekani milioni 218, sio sahihi. Ninamuomba sana Mheshimiwa aliyetoa taarifa hii au *figure* hii afuatilie atapata uhakika wa kiasi gani ambacho kimetumika au kitatumika katika ujenzi wa jengo lile. Lakini kama nilivyosema mwanzo jitihada kubwa inafanywa na tuna matumaini makubwa kwamba ndani ya mwaka huu wa fedha ujenzi ule utaendelea kama ulivyokuwa ukifanyika hapo awali.(*Makofi*).

Kuhusiana na suala la *ZSSF* kwamba wanatekeleza miradi na hawaikatii bima, taarifa hii nayo vile vile si sahihi. Niseme tu kwamba miradi yote ya *ZSSF* inakatiwa Bima, inawezekana Kamati yetu wakati inatembelea ilikuwa ama Bima hawaja-*renew* katika baadhi ya miradi au ilikuwa bado wako katika *process* ya kukatia bima miradi yao. Lakini jambo la mwanzo ambalo wanalifanya wenzetu wa *ZSSF* ni kuhakikisha kwamba miradi yao yote wanaikatia Bima ikiwemo viwanja vyetu vya Kufurahishia Watoto vya pale Kariakoo na kule Tibirinzi.

Kuna suala lilizungumzwa la *TCRA* na hapa niseme tu Mhe. Naibu Spika, kwamba ushauri uliotoka kwanza ni mzuri tunaupokea na nieleze kwamba tayari *ZRB* na Wizara yetu ya Fedha na Mipango inalifanyia kazi kujua matumizi ya simu kwa makampuni yote, ni kiasi gani cha matumizi ya simu yanatumika hapa Zanzibar na hicho tunakifanya kwa kutaka kujua wigo wa ukusanyaji mapato katika huduma hii ya simu inayotolewa na Makampuni ya simu yaliyopo hapa nchini. Kwani wazo zuri na sisi tunalifanyia kazi na inshaallah hivi karibuni tutapata taarifa ya timu yetu ya wataalam wanaoshughulika na suala hili.

Kuna suala la muda mrefu lilizungumzwa la upotevu wa fedha za Serikali na wale vijana wetu waliosimamishwa, nikiri kwamba ni kweli muda ulikuwa mrefu lakini ulikuwa mrefu kwa madhumuni maalum. Kamati iliundwa na Kamati hiyo tayari imeshakamilisha kazi yake na ripoti yao tayari wameshaiwasilisha lakini lazima niwaeleze Waheshimiwa Wajumbe wafahamu kwamba hawa vijana waliohusika ni vijana wataalamu na walitumia ule mtandao wa *effin* lazima kwanza uwe na taaluma ndio uweze kuingia katika ule mtandao na wanatumia taaluma katika kufanya hayo waliyoyafanya.

Kamati iliyoundwa iliomba kuongezewa muda karibu mara mbili na wakati mwengine walihitaji kupata wataalamu ambao wanaweza wakaingia kwenye mtandao ule na wakajua dosari zilizopo katika upotevu wa fedha zile, haikuwa kazi rahisi na ilibidi sisi tuwavumilie. Kwa sababu tulikuwa hatutaki kumuonea mtu tupate taarifa za uhakika na taarifa hizo ndizo tutakazozifanyia kazi baada ya kujiridhisha. Mhe. Naibu Spika, wamemaliza kazi yao na kinachofanyika

sasa hivi wametoa mapendekezo yao, sisi tunayaangalia mapendekezo yao na kujua hatua gani zinapaswa kuchukuliwa kwa kila mtu na kosa alilolifanya na yule ambaye hakuonekana na kosa basi hakutakuwa na haja ya kumchukulia hatua hiyo. Haya yote tunayafanya kwa umakini ili tusije tukamuonea mtu katika utaratibu mzima huu wa kuchukua hatua dhidi ya makosa yaliyofanywa.(*Makofi*).

Kodi ya miundombinu niiseme mbio mbio Mhe. Naibu Spika, ni kwamba vyanzo vyake viko vingi kuna *trade levy* ya asIlimia 5, na asilimia 5 hiyo asilimia 3 inakwenda kwenye Mfuko wa Miundombinu, asilimia 2 inakwenda kwenye Bajeti ya Serikali. Lakini kuna mauzo ya umeme ambayo tunachukua asilimia 2, lita moja ya petroli na *diesel* tunachukua shilingi 100 lakini wageni wetu wanaoingia kwenye mahoteli kwa kila mgeni analipa dola 1 kwa siku anayolala, na shilingi 2,000/- kwa abiria wanaoondoka kwenye bandari yetu ya Zanzibar kwenda katika bandari yoyote nje ya Zanzibar na shilingi 1000/- kwa abiria wanaondoka kwenye bandari yetu lakini wanaokwenda kwenye bandari nyengine ya Zanzibar kwa maana wanaosafiri kwenda Pemba, na shilingi 2000/- kwa abiria wa ndege wanaosafiri ndani ya Tanzania.

Fedha hizi zinaingia katika Mfuko wa Miundombinu (*Infrastructure Fund)*. Kwa mwaka 2016/2017 tukitizama ile hotuba ya Bajeti ya Serikali tutagundua kwamba moja ya miradi ambayo inatekelezwa kutokana na fedha zile ni upelekaji wa umeme vijijini na katika mwaka huu tulikusudia kupeleka umeme katika kisiwa cha Fundo. Kazi hiyo hivi sasa inafanyika, vifaa vishafika na kazi inaendelea.(*Makofi*).

Kuhusiana na maghala ya Serikali niombe tu kwamba hili tulichukuwe tulifanyie kazi na wakati wa mwezi wa Septemba inshaallah tutalitolea taarifa.

Suala la *TRA Deputy Commissioner* kuwa ni mtu wa nne katika *structure*, hili niliomba sana nimueleze ndugu yangu Abdalla Maulid Diwani, kwamba ile *structure* aliyotumia ameitafsiri sivyo ilivyo. Kwanza huyu Naibu Kamishna hayuko chini ya Kamishna wa *Customs and Excise*. Lakini pamoja na hilo *concern* yake tumeisikia, suala hili tunalizungumza katika vikao vyetu vya SMT na SMZ, na tumepewa jukumu maalum Mawaziri wawili wa SMT na SMZ kuangalia suala hilo. Lakini vizuri zaidi ni kwamba *TRA* ipo katika utaratibu wa kufanyiwa mabadiliko ya muundo wake. Kwa hivyo huo ni wakati muafaka ambao ninaamini nitakapozungumza na Waziri mwenzangu wa SMT na suala hilo nalo tutalijadili ili kuona jinsi gani tunaweza tukalirekebisha.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niliomba nichangie hayo na kama nilivyosema mwanzo maelezo kamili ya masuala na hoja mbali mbali za Wajumbe tutayatoa mwezi wa Septemba.

Ninakushukuru sana Mhe. Naibu Spika. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango. Sasa anayefuata ni Mhe. Balozi Amina Salum Ali ambaye ni Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko: Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa naomba nichukuwe nafasi hii kumshukuru Mwenyekiti wa Kamati yetu hii ya Fedha, Biashara na Kilimo na Wajumbe wote wa Kamati hii kwa kazi nzuri wanayoifanya na jitihada wanazozifanya kwa kutupa ushauri unaofaa kwa wakati na kushauriana kwa wakati kwa ajili ya kufanikisha majukumu yetu haya ambayo ni muhimu kwa ujenzi wa taifa letu. (*Makofi*).

Vile vile nichukuwe nafasi hii niwashukuru waliochangia wote katika taarifa hii ambao ni watu 20, wote wamechangia na wengine kwa maandishi taarifa ya Wizara yetu ya Biashara, Viwanda na Masoko.

Mhe. Naibu Spika, naomba nikiri kwamba michango iliyochangiwa na Wajumbe yote imetupa rai ya utekelezaji kwa ufanisi zaidi, imetukosoa kidogo pale ambapo pana haja ya kukosolewa lakini kubwa imeonesha nia ya kutaka kushirikiana na Wizara yangu kwa ajili ya kuendeleza hizi sekta ambazo tumekabidhiwa sisi katika Wizara yetu. Ninawashukuru na ninawahikishia kwamba Wizara yangu tutaendelea kuwa wawazi na kuwa tayari kurekebishana na kushauriana ili kwa sababu yale mambo ambayo tunataka tuyafanye katika kipindi cha mwaka huu na miaka inayokuja yafanikiwe.

Mhe. Naibu Spika, hoja nyingi zilizochangiwa zilikuwa zaidi katika mambo yanayohusu viwanda, biashara, *ZSTC* na mengine ambayo nitachangia kwa mujibu wa yalivyochangiwa.

Mhe. Naibu Spika, wachangiaji wengi walizungumzia suala zima la kuendeleza uchumi wa Zanzibar na kwa kweli uchumi wa Zanzibar tukiuangalia tumepiga hatua nzuri, ukiangalia mwaka wa jana na mwaka huu na ninaamini kwamba taarifa ya bajeti itakayosomwa mwaka huu itaonesha jinsi tulivyokuwa tumepiga hatua kubwa sana katika kuendeleza uchumi wa Zanzibar.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, uchumi wa Zanzibar sehemu kubwa unachangiwa kutokana na nguvu za maneneo yakiwemo ya kilimo, viwanda na sehemu nyengine muhimu. Ningeomba kwanza nizungumzie sekta hii ya viwanda ambayo watu wengi waliochangia Waheshimiwa Wajumbe wameizungumzia. Waheshimiwa wamezungumzia kwa uchungu sana na waliangalia tulikotoka huko nyuma na tulipo hivi sasa. Huko nyuma walizungumzia kwamba tulikuwa na viwanda vingi ambavyo Serikali ilikuwa ikiviendesha na vyengine wakiendesha watu binafsi, lakini viwanda vingi hivyo sasa hivi haviko kwa sababu vilipata matatizo na vikawa vyengine vikafungwa na vyengine vikauzwa maeneo yakabadilishwa kwa matumizi mengine. Kwa hivyo mimi naona michango yao ilikuwa ya uchungu baadhi yao, wana haki ya kuhisi vile lakini pia nakubali ushauri waliotoa kama viwanda tuangalie zaidi sio tu viwanda vikubwa lakini pia viwanda vyengine vidogo na vya wajasiriamali.

Mhe. Naibu Spika, ukiagalia takwimu za viwanda hapa Zanzibar asilimia 97 ya viwanda viliopo Zanzibar ni viwanda vidogo na hasa vya wajasiriamali. Hii inaonesha kwamba kuna kazi kubwa tunatakiwa tuifanye kuweza kwanza kuvijua viwanda hivi, kuvipanga vizuri na kuweza kuvielekeza ili viweze kukua vikawa vikubwa na viweze kutoa mchango mkubwa katika uchumi wa taifa letu. Viwanda vilioko hapa Zanzibar vingi vyao vinaajiri wafanyakazi kati ya wafanyakazi wawili mpaka wafanyakazi watano lakini vile vile kuna viwanda sasa hivi vya kati kati ambavyo serikali imejaribu kuvifufua. Hapo tulipo Mhe. Naibu Spika, tumeangalia mikakati ya kufufua viwanda hivi kwa mfano viwanda hivi viliopo kuna sheria ambazo zilipitishwa huko nyuma, kwa mfano Sheria ya Wajasiriamali ya mwaka 2006. Sheria hii imebidi ifanyiwe mapitio na Baraza lako Tukufu linakuwa na nafasi ya kuja kupitia sheria hii na kuona kwamba tumeweka sheria ambayo itakwenda na wakati na itakayoongeza ari kwa ajili ya wajasiriamali.

Sheria hii itajibu hoja zote ambazo zimezungumzwa sasa hivi. Hoja kwamba masoko, hoja ya kupatiwa fedha kwa ajili ya kuendesha shughuli zao, hoja ya mafunzo kwa ajili wapate kujua bidhaa gani watengeneze, sheria hii itajieleze yote patakuwa nafasi kuja kuipitia hapa na kutoa maamuzi ama kuiborosha zaidi na kuiwezesha ifanye kazi vizuri zaidi.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, kuna Sheria ya Viwanda ambayo imepitishwa 1989, sheria hii nayo imeshakaa muda mrefu kuna mambo hayajafanyiwa kazi, mambo mengine yako kwenye mabuku tu. Kwa hivyo sheria hii nayo kipindi cha mwaka unaokuja wa bajeti 2017/2018 nitapata nafasi vile vile kuipitia sheria hii na kupanga mkakati mzuri wa kuendelea viwanda kuweka vivutio

vya wawekezaji na vile vile kuwatazama wajasiriamali kwa upana zaidi na kuwapa fursa zaidi ili waweze kujiendeleza.(*Makofi*).

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, katika mkakati tunangalia kuanzishwa Mamlaka ya Kuendeleza Viwanda Vidogo Vidogo na sheria yake itakuja vile vile katika Baraza lako tukufu na tutakuja kuipitia na kuweka utaratibu mzuri kama ilivyo *SIDO* kule Bara na sisi tunatarajiwa kufikia huko ili viwanda hivi vya wajasiriamali na viwanda vidogo vidogo viwe na sehemu ambayo inashughulikia kwa ukamilifu.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kama sisi tunaangalia viwanda vyote viwanda vya kati, viwanda vikubwa na viwanda wajasiriamali, kwa nini tunafanya hivyo. Kuna Mheshimiwa moja alizungumzia kwamba tuangalie viwanda kwa sababu ya ajira, faida za viwanda nyingi sio tu ajira peke yake lakini pia mchango wa mapato katika taifa letu kuwapa vile vile mapato wana familia zetu na kadhalika. Ningeomba nitoe mifano tu hapa ili muelewe kwa nini sisi wizara yetu na Serikali inayoongozwa na Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein ina kipa kipa umbele suala zima la viwanda. Kwa mfano tunaangalia sekta ya chumvi, sekta imeajiri watu kama watu elfu kumi na tano na vikundi vya ushirika hamsini na sita, uzalishaji wa sekta hii ya chumvi mwaka 2015 ilikuwa tani 2,500 na mwaka 2016 tani 349.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, na Waheshimiwa Wajumbe hii sekta hii ni muhimu sana na itakuwa ni mkombozi wa wananchi wa Zanzibar. Vile vile sekta hii ya chumvi itakuwa ndio sekta mama ya kuanzisha viwanda (*chemical industries)* inasema viwanda kwa ajili ya madawa. Sasa hivi kuna *chloride* tunaagizia, kuna dawa nyengine sasa *carbonate* tunaagizia nje lakini sekta hii itakuwa ndio chimbuko la viwanda vya dawa ambavyo vitapanuka na kuwa vikubwa zaidi.

Mhe. Naibu Spika, twende katika sekta ya mwani. Sekta ya mwani hiki ni kilimo ambacho kinachukua ajira wananchi 23,000. Sekta hii imeweza kuzalisha mwani tani 16,000 kwa hesabu tuliyopewa na wenzetu wa Wizara ya Kilimo. Sasa hivi tunajitaarisha kuandaa utaratibu kama serikali itakubali mapendezo ambayo yametoka kwa wataalamu angalau tuwe na *pilot project* ya kuzalisha sabuni na dawa zinazotokana na mwani. Hiyo peke yake itaweza kuongeza ajira si tu kwajili ya wanayoshughulikia na kulima mwani lakini itaongeza ajira kwa wale ambao watasindika mwani na wale ambao watakuwa wanatoa sabuhi za mwani na ambao watakuwa wanauza sabuni hizi nchi za nje, tayari hapa mnyororo wa thamani tutakuwa tumeshaufanya.

Lakini jengine Mhe. Naibu Spika, tuangalie sekta ya uvuvi na hasa uvuvi wa dagaa kwa sababu sekta nyengine ya uvuvi kwa upana wake atakuja kueleza mwenzangu Waziri ya Kilimo. Lakini sekta ya dagaa sasa hivi imeajiri wananchi wanafika elfu kumi na imeshazalisha kwa mwaka jana tani 3,400 kwa thamani ya shilingi bilioni 396. Hii peke yake Mhe. Naibu Spika, niseme tu vile vile ni kiwanda ambacho kitawezesha kuongeza ajira lakini kitawezesha kuongeza mapato ya wananchi na mapato ya serikali.

Vile vile Mhe. Naibu Spika, viko viwanda kutokana na karafuu na viungo kuna utaratibu wa utalii na viwanda vya utalii na biashara ya utalii kwa sababu sio tu mahoteli, utalii maana yake kama viweko vitu vya kununua na ziwepo biashara za kununua vitu ambavyo wananchi watalii wakija waweze kuondokanavyo.

Lakini pia Mhe. Naibu Spika, huduma kwa mfano kama simu, huduma za fedha, usafirishaji haya yote ni mambo ambayo yanaongeza mapato katika uchumi wetu. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba kuna maeneo mengi tunayatizama kwa ukamilifu na kwamba sasa hivi katika bajeti inayokuja kipa umbele tulichotia ni kwamba kuanza kutekeleza baadhi ya miradi ya viwanda ili wananchi wapate na wao kujiajiri na wajasiriamali nao waweze kwenda mbele.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, hapa hapa nilizungumzia suala la wajasiriamali, wajasiriamali kama nilivyosema ni wengi hapa Zanzibar na kwa kweli wana matatizo kama walivyosema Wajumbe matatizo ya soko, mikopo, utaalamu, matatizo ya vifungushio, matatizo ya bidhaa zao wanazotoa hazikidhi ubora. Haya yote Mheshimiwa kama nilivyosema yanazingatia na nitakuja kuzungumza wakati tutakopokuja kuleta sheria hii ya Mswada wa SMEDA pamoja na sheria nyengine zinazohusu viwanda.

Niseme tu kwa upande wa masoko ningeomba tu kwamba Waheshimiwa wawe na subra kwasababu katika suala la masoko lazima tuwatoe kwanza wajasiriamali majumbani wanakozalisha bidhaa zao, halafu vile vile tuwaweze kuwapatia mahali maalum watakapoweza kuuza bidhaa zao. Kwa sababu sasa hivi bidhaa nyingi zipo na kila tukienda katika maonyesho tunakuta kila kipindi bidhaa ubora wake unabadilika na unakuwa mzuri zaidi. Lakini hatuwezi kuzipata kwa sababu mara nyingi hawana mahali pa kwenda kuziuza. Mhe. Naibu Spika, tumezungumza na Wizara ya Ardhi na tumewaomba katika *master plan* wanayoifanya watenge maeneo maalum kwa ajili ya wajasiriamali, kwa ajili ya viwanda na kwa ajili ya kuweka maeneo kwa ajili ya maghala.

Mhe. Naibu Spika, tukifanya hivyo tunaweza kila mtu atajua mahali gani aende akanunue kitu gani kwa sababu wale wazalishaji na wanaouza watakuwa wapo mahali ambapo tunaweza kuwagundua. Sasa hivi inabidi uwafuate majumbani inakuwa ni shida hatuwezi kuwajua kwa hiyo wanakosa masoko. Pia tumekubali ushauri wa kuwa na maonyesho mara kwa mara, ushauri wa kufanya *Sunday Market*, ushauri wa kuweza kuwasaidia na kuwaletea wageni mbali mbali wanaokuja katika ziara waone bidhaa zetu. Shauri kama hizi tumezipokea na tunazifanyia kazi na mtaona kipindi kinachokuja tutajaribu kuongeza jitihada katika maeneo hayo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, vile vile nilizungumza suala la *ZBS* yaani *Zanzibar Bureau of Standard* ni kweli chombo hiki kimeanzishwa lakini ukilinganisha hiki na cha Bara, wenzetu cha Tanzania Bara walianza muda mrefu, sisi tumeanza hivi karibuni. Lakini naomba nichukue nafasi hii niwapongeza sana watendaji wa *ZBS* kwa sababu wanafanya kazi kwa ari na kujituma na serikali chini ya uongozi wa Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein tumepatiwa fedha za kutosha kwa kuweza kununua vifaa vya maabara, ingawa fedha zile hazikutosha kumaliza matatizo yote lakini kwa kuanzia vifaa vyingi vya maabara tunatarajia kati ya mwezi wa Mei kabla ya bajeti vitakuwa vishafika na vitaanza kufungwa na tunajitahidi kutafuta vifaa vyengine.(*Makofi*).

Pia nilizungumzia suala la kuzuia vitu ambavyo ni *used* vinavyoingia ambavyo havina viwango ambavyo vikuukuu vilivyokuwa havitakiwi, tumeshazungumza na watendaji wetu *ZBS* na vyombo vinavyohusika kwa mfano kama chombo cha Mamlaka ya Vyakula na Madawa na kadhalika, kuona kwamba bidhaa zinazoingiza hapa Zanzibar zinakidhi haja na zinakidhi kwa ajili ya matumizi ya wananchi wetu. Kwa hivyo hilo nalo linafanyiwa kazi na pia kulikuwa na suala la bidhaa feki zinazoingia ama *counterfeit* nalo hilo tutalishughulikia kuona kwamba bidhaa zinazoingia Zanzibar zinakidhi haja lakini pia zinakwenda sambamba na bei ambayo vinauziwa.

Upande wa karafuu Mhe. Naibu Spika, Wajumbe wengi wamezungumzia suala zima la *ZSTC* na karafuu. Kwanza suala la magendo ambalo bado linatusumbua Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, lakini tunajitahidi na sasa hivi tunaingalia tena Sheria ya Karafuu na Sheria ya Magendo kuona labda pengine kuna kasoro kidogo au pengine sheria zile sio kali na kuzifanya ziwe kali kabisa. Kwa mfano Sheria za Magendo zinasema kama karafuu zikikamatwa nje kabla hujafika baharini hayo si magendo, tunataka kuangalia sheria kuona kwamba karafuu popote itakapokamatwa ikiwa sio wakati wa kuziuza karafuu na utaratibu haujafuatwa, hapo hapo iwe ni suala la magendo na mali ile itaifishwe. Maana sasa hivi hazitaifishwi, sasa hivi mali kama ile

inachukuliwa inaambiwa basi uza mrudishie mwenyewe fedha zake, tunataka sheria iwe kali mali zitaifishwe na anayehusika achukuliwe hatua ya kupewa kifungo kikali kirefu jela.(*Makofi*).

Vile vile Mhe. Naibu Spika, katika suala zima la *ZSTC* nilizungumza Kiwanda cha Makonyo. Kiwanda cha Makonyo katika dhana nzima ya mnyororo wa thamani, kile ndio kiwanda mama kitakachosaidia ukombozi wa maendeleo hasa katika biashara hii viwanda vinatokana na mazao ya kilimo. Kwa sababu sasa hivi tumeona kuna masoko na soko kubwa sana kwa upande wa marashi ya mimea, kwa upande vitu vyengine ambavyo vinatokana na mazao ya kilimo kama mafuta ya karafuu na kadhalika. Kwa hivyo kiwanda hiki ni kweli kina matatizo ya vifaa vyake vikongwe hata ukitaka kwenda kununua zile *spare parts* haziko duniani, kwa sababu kile kiwanda kimetengenezwa na kampuni ya Ufaransa na ni ya miaka mingi. Kwa hivyo sasa hivi mkakati uliopo ni kutizama kile kiwanda kwa ukamilifu na kuanza kuona kwa kiasi gani tutaweza kukibadilisha na kutia vifaa vya kisasa, vipya ili kiweze kiendane na wakati. *(Makofi)*

Jengine lilozingumzwa hapa Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu mezani ya karafuu zinatumia kwa ajili ya kupimia karafuu wakati wa mauzo. Ni kweli tumesikia kesi kama hizo lakini kesi kama hizo zimepungua sana, yaani watu kuwanyanganya wakulima ambao wanaendea kuuza karafuu zao. Mezani sasa hivi kwa mfano kama za Mkoani tumeshatia mezani mpya na tutanunua mezani nyengine za kuweza kuwasaidia wakulima ili wasidhulimiwe haki yao.

Jengine la karafuu Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba vyombo vya kuchekia karafuu kwa sababu karafuu inaponunuliwa inatakiwa ichungwe ile karafuu. Kwa hivyo tumeweza kupata mashine mbili tulizogawia na mfadhili mmoja, lakini mwaka huu tutatanunua mashine nyengine kwa ajili ya kusafisha karafuu ili karafuu ziweze kutolewa pale katika hali inayokubalika.(*Makofi*).

Jengine nilisema Mhe. Naibu Spika, katika utaratibu katika masuala haya haya yanayohusu karafuu na viungo. Mmoja wa Mheshimiwa alisema kwamba viungo tunavyoviuza nje viligunduliwa vina *DDT*. Ni kweli taarifa tulizozipokea kutoka Wizara ya Kilimo kwamba waligundua katika viungo (*spices) v*iliyouzwa nje vilikuwa na harufu harufu ya *DDT*. Hiyo sio nzuri kwa kweli haitujengei sifa ya bidhaa zetu. Lakini naomba nimuhakikishie Mhe. Mwakilishi kwa upande wa zao la karafuu hatujapokea kesi kama hizo, kwa nini kwa sababu kila mara tunawaambia wakulima wa karafuu wanaolima karafuu majamvi wanayotumia kwa ajili ya karafuu wasiyaweke pamoja na

majamvi mengine wakaanza ku-*spray* dawa za kuulia mbu. Kwa hivyo mpaka sasa hivi na Mwenyezi Mungu katuepushia mbali bado zao la karafuu tunaweza kudhibiti vizuri na hatujapata kesi ya kuingia *DDT* . Niombe tu kupitia hapa Mhe. Naibu Spika, kuwaambia wananchi wanaozalisha karafuu wanaopeleka karafuu na wanaokausha karafuu, kwa kweli wajitahidi kabisa kabisa waweke mbali majamvi na vifaa vyote vinavyotumia karafuu mbali na vitu ambavyo ni vya *chemical* au vitu ambavyo vinaweza kuleta madhara kwa wananchi, kwa sababu ukifanya hivyo sifa ya karafuu ya Zanzibar na mazao yote ya viungo vya Zanzibar vitakataliwa ulimwenguni, tutabakia na hasara kubwa hatutaweza kufanikisha maendeleo yetu.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu maghala ni kweli maghala tuliyokuwa nayo wakati ule kutoka tuko BIZANJE mengi yao yameuzwa kwa bei chee, nakubali niseme hivyo inanisikitisha sana mimi na wenzetu imewasitikisha, maghala mengine yamekodishwa kwa miaka mingi mengine mpaka 2029, 2027 mengine hayashughulikiwi Mhe. Naibu Spika, tumefanya ziara kutembelea maghala yote tumeambiwa maghala mengine muda ushakwisha kwa mshangao tumekuta maghala yale kumbe muda umeongezwa kwa sababu mengine hayako mikononi kwetu. Kwa hivyo nakubali maombi ambayo tumepewa na Kamati na tutakuja kujibu mwezi Septemba kwamba tuyapitie maghala yote na mengi ya maghala hayo hayatengenezwi, ukienda utakuta maghala yameachwa kama vihame watu wanatumia maghala na wamekodishwa kwa bei za chee vile vile. Kwa hivyo Mheshimiwa hapa kuna tatizo.(*Makofi*).

Lakini nakubali mapendekezo ya kamati ambayo wametwambia tuanze kuzungumza na wenzetu Wizara ya Fedha, kuona kwamba hii mikataba waliyokuwa wamepewa tuitizame mengine ikibidi ifutwe na wale ambao wamekodishwa sio ambao wanakaa sasa hivi basi wanyang'anywe yale maghala ili yapelekwe kwa wanaohusika. *(Makofi)*.

Mhe. Naibu Spika, suala la viungo yaani biashara hii na Mheshimiwa mmoja alinileta kwa maandishi suala zima la vanila. Naomba niwahakikishie Waheshimiwa Wajumbe kwamba katika mkakati wa sasa hivi kwa kushirikina na Wizara ya Kilimo tunataka tuanze kufufua mazao yetu ya zamani. Mazao haya Mhe. Naibu Spika, yamekufa kwa mfano vanila ilikuwepo watu sasa hivi walikuwa wakilima vanila zimeachwa. Mhe. Naibu Spika, kwa mfano mazao mengine, pilipili manga, pilipili hoho, sasa hivi tu kipindi hiki nimetakiwa mimi niuze makontena kumi ya pilipili hoho, pilipili manga lakini hakuna makontena kumi ya pilipili manga, nimekwenda mpaka Bara kwa sababu kilimo kipewa mgongo.

Kwa hivyo ninachoomba Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia Wizara ya Kilimo na sisi wote Wawakilishi tuanza kusimama imara kufufua mazao yetu haya kwa sababu soko lipo, soko sio tatizo lolote sasa hivi, masoko yapo lakini uzalishaji haupo wa kutosha wanakwenda watu Dubai wanapewa *order* tuleteeni kontena moja la pilipili hoho hakuna au wanaambiwa wapeleke kitu fulani wanakuwa hawana uwezo wa kupeleka. Kwa hivyo vita vyote sasa hivi kama Wazanzibari kama viongozi tushirikiane na Wizara ya Kilimo tuanze kulima kwa upande wetu sisi tunatafuta njia ya kuweza kupata mikopo kuwasaidia mfano masuala ya unyweshaji maji yale mashamba yawe mazuri, kutafuta vifungishio vya mazao yao kwa mfano yakiwa yamefanya kwenye viwanda, haya ndio tunataka tuyafanye. Lakini Mhe. Naibu Spika hiyo ndio hali.

Suala la nazi atakuja kujibu Mh. Waziri wa Kilimo, nazi hakuna. Sasa hivi bahati nzuri nazi sasa hivi *organic* wanaita nazi hai ina soko kubwa sana. Kuna kiwanda kimoja cha nazi mafuta ya nazi tumefungua pale cha Wachina, kipo viwanda vidogo vidogo pale. Lakini bahati mbaya hawezi kununua nazi za kuweza kufanya shughuli zake. Kwa hivyo inabidi nazi agizie Tanga au agizie Mtwara na Lindi waweze kufanya. Kwa hivyo ni kweli mimi ningeomba tu Waheshimiwa Wajumbe minazi imekatwa, kwa hiyo tuanze sasa hivi angalau basi kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo huo mradi utakaokuja wa nazi tuweze kudhidhibiti, misumeno hii imekata minazi na mikarafuu. Kwa hivyo misumeno hii ndio adui yetu namba moja katika suala zima la nazi.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala zima la *PVOC* ambalo lilizungumzwa kila mara ninapata masuala au napata hoja kuhusu suala zima la ukaguzi wa bidhaa niseme tu ukaguzi wa bidhaa siyo tu zuri kwa serikali lakini hata kwa wafanya biashara wenyewe.

Mhe. Naibu Spika, wafanya biashara wanapokuwa wanasafirisha bidhaa zao kupeleka Bara. Kule Bara kuna masharti marefu na moja sharti yao iliyoko Bara lazima bidhaa zikaguliwe nje na sio tu Bara hata ukenda Kenya, Uganda popote pale sasa hivi lazima biashara hizi bidhaa zikaguliwa nje. Sasa kama hatukufanya *PVOC* itakuwa tumekiuka masharti na bidhaa hizi mtakwenda kulipishwa faini mnakokwenda kule. Kwa hivyo mimi ningeomba tu nakubali kama kuna matatizo kwa sababu tulipokuwa tumeanzisha hii shughuli watendaji wetu wa Wizara ya Biashara wa *ZBS* walikuwa hawakwenda kukagua. Hivi leo wako wamekwenda kukagua sasa hivi kuona kwa kiasi gani hizi kampuni zinafanya kazi. Hivyo ningeomba tu Waheshimiwa Wajumbe wawe na subra na sisi tutaupitia tena utaratibu huu lakini kusema tuuondoshe moja kwa moja, hiyo niseme ili nisiwadanganye Waheshimiwa tutaitizama, lakini hatutoweza kuiondosha moja kwa moja, ila kila kukicha tujaribu

kuongeza uwezo wa *ZBS* lakini kusema tutaiondosha itakuwa ni sawa sawa nakujipiga wenyewe visu, wafanya biashara hamtoweza kuuza bidhaa zenu nje, lakini tutafuta utaratibu mzuri utakaotuwezesha na sisi kama serikali kupata mapato yanayotokana na biashara hii.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, suala la mizani nadhani mizani na bei. Kwanza suala la mizani Kitengo chetu kinachoshughulika mambo ya mizani wanapita kila wakati kwenda kutazama mizani na zinabadilishwa mizani zikionenaka kwamba zina mapungufu, mizani zile zinakuwa hazitumiki. Lakini kama bado kuna matatizo basi tutazidi kuongeza nguvu kwenda kuzitazama hizo mizani ambazo zinalalamikiwa.

La mwisho Mhe. Naibu Spika, ni kuhusu bei ya vyakula. Bei ya vyakula Mheshimiwa Mjumbe alitaka kwamba vyakula turudie utaratibu ule wa zamani wa kuwa na Tume ya Bei. Mhe. Naibu Spika, tukubali kwamba tumeshatoka huko hatuwezi kwenda huko tena, kwa sababu biashara sasa hivi imekuwa huria na hata vyombo vya kibiashara kama *WTO* na kadhalika hawataturuhusu kurudi tena katika utaratibu wa kuwa na mfumo wa Tume ya Bei. Kinachofanyika duniani kote sasa hivi hata nchi nilizozitaja za Magharibi ni kuona kwamba tunakuwa na bei elekezi, kama alivyosema yeye vyakula vimepanda bei kwa mfano kama mchele tukubali kwamba vyakula vinapanda bei kwa sababu kuna gharama nyengine hatuwezi kuzi *control* sisi SMZ. Kwa mfano angalieni jinsi dola ilivyopanda. Kwa hivyo dola ikipanda walivyokuwa wanaagiza vyakula kama hivi navyo vinaathirika bei inakuwa inapanda. Lakini kwa kiwango kikubwa sana tumejitahidi kuona kwamba tunawapa bei elekezi kwa kuangalia gharama zinazokuja zote kuanzia bei ya mchele, kodi na kadhalika na kuweza kuweka bei kama *ceiling* ambayo inaweza kuwakidhi wananchi wetu. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, niseme tu kwamba baada ya kujibu baadhi ya hizi hoja kama nyengine sijazijibu basi nitazijibu kwa maandishi wakati huo mwezi wa Septemba ndiyo tutaweza kutoa ufafanuzi ambao unatakiwa. Mimi naomba niseme kwamba sisi Wizara ya Biashara tunajitahidi na tuliomba tupewe bajeti kipindi kile na tukapewa bajeti ndogo kwa ajili ya kujiandaa na niseme kwamba tumejiandaa vizuri sana, bajeti yetu itakayokuja tutajibu hoja zenu zote ambazo mmezieleza hapa. Na ninaamini kabisa kabisa kwa nia njema na mapenzi aliyonayo Mhe. Rais wetu kwa Wazanzibari wetu tutaweza kufanya kazi vizuri na tutaweza kipindi cha miaka mitano hii kuweka hatua za msingi na za muhimu katika sekta hii ya biashara, viwanda na masoko. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, naomba niseme ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Mhe. Hamad Rashid Mohamed Waziri wa Kilimo, Maliasili na Uvuvi.

Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote naomba nimshukuru Mwenyezi Mungu, nikushukuru wewe mwenyewe lakini nataka nimshukuru Mwenyekiti na Kamati yake kwa kazi nzuri sana walioifanya na hayo ni matokeo ya kazi nzuri iliyofanywa na Ofisi ya Spika kwa kuzisaidia kamati zetu kufanya zetu kufanya kazi zake kwa ufanisi. Lakini vile vile na kuwasaidia hawa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi kufanya kazi yao kwa ufanisi mkubwa, tumeona michango iliyotoka hapa ni michango iliyofanyiwa kazi na inahitaji kuthamini na kufanyiwa kazi, na sisi tunaahidi kutekeleza kikamilifu.(*Makofi*).

Pili Mhe. Naibu Spika, naomba nimshukuru sana Mhe. Rais. Mhe. Rais ni kiongozi ambaye ana busara ya hali ya juu, uvumilivu na ndio maana kila wakati anapotoa maelekezo yake basi huwa anahakikisha kabisa amefanya utafiti yeye mwenyewe kwanza wa kutosha. Mimi nasema kiongozi wa aina yake kabisa. Kwa sababu hiyo ndio haya mafanikio unayoyaona pamoja na kelele zinazopigwa lakini unaona ukusanyaji wa kodi ulivyopanda vizuri, wananchi walivyoitikia katika sekta ya kilimo, viwanda na kadhalika. Yote haya ni kutokana na uongozi mzuri alionao Mhe. Rais na naomba tumpe *support* katika nia yake nzuri ya kuleta maendeleo.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jambo la tatu kamati imefanya kazi nzuri sana na mimi nataka niwapongeze kwa dhati kabisa, wakati wanapita Ofisini kwetu wanasema tuna maswali tatu tutakuuliza, lakini ukikaa nao wanakuuliza maswali zaidi ya kumi na tatu, na kila swali wanalouliza lina undani kabisa wamefanya *research* ya kutosha kabisa. Nasema kamati hizi zimesaidia sana serikali na ndio wajibu wa Baraza hili kuisaidia serikali, kuishauri serikali ili serikali iweze kufanya kazi yake. Naomba kuwapongeza sana.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sasa siku ya kujibu taarifa hii na tarehe yake bado ni mwezi wa Septemba, lakini kuna mambo ambayo yamesemwa katika michango waliyotoa Wawakilishi na wasingefurahi kama tungeondoka hapa bila ya kusema jambo lolote. Kwa hivyo mimi sitokwenda kwa ndani sana yale waliyosema isipokuwa kuna mambo matatu au manne nataka niyasemee.

La kwanza ni suala zima la uwekezaji. Mhe. Naibu Spika, hakuna nchi yoyote iliyoendelea duniani ambayo haikukaribisha wawekezaji wenye fedha, wenye teknolojia kuwekeza. Na kwa nchi ambazo nyingi hazijaendelea ni zile ambazo

hazikupata fursa ya kupata wawekezaji kama sisi ambavyo hatujapata fursa ya uwekezaji mapema. Lakini tuna bahati ya pekee, nasema ni bahati ya pekee kumpata mwekezaji ambaye ni mzalendo ni raia wenu wenyewe.

Leo Tanzania wawekezaji kutoka Kenya ni makampuni 360, makampuni ya Tanzania yaliyoko Kenya hayazidi 13, hiyo sio fahari. Kwa hivyo mukiwa na mwekezaji wenu mmoja mtunzeni, mleeni anachukua *risk* kubwa sana. Ndugu Bakhresa mimi nimeshangaa sana amewekeza kwenye Kiwanda cha Maziwa pale ni dola milioni sio chini ya 20,000,000 *very high risk* kwenye soko dogo, soko ambalo halina malighafi ya maziwa unakwenda kuziweka dola milioni 20,000,000. Kama si uzalendo asingefanya hakuna mfanyabiashara anayefanya hivyo. Hakuna mfanyabiashara yeyote anayewekeza pahala fedha ambapo haoni matunda yake kuzalisha kesho, amechukua *very high risk*, anahitaji lita 40,000 za maziwa kwa siku, hakuna hata lita 10,000 za maziwa anazopata kutoka pale, *very high risk*. Ndio sasa tunaanza *process* ya kumsaidia namna gani atapata maziwa yaweze kwenda kiwandani, matokeo yake anaagizia maziwa ya unga kidogo, ana-*process* na mengine kidogo ndio anapeleka.

Soko la pili la kuingia vile vile nalo ni tatizo amechukua *very high risk*, sio kila mfanyabiashara anaweza kufanya hivyo. Hiyo tunahitaji hawa wawekezaji kuwaenzi, kuwasaidia na kadhalika, na sio kile *investor* atakayekuja atakuja ku-*deal* na watu wa chini kwa sababu biashara yoyote duniani inajengwa na watu wa kati kati. Nalisema hili kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ili kilimo kibadilike, ili uvuvi ubadilike unahitaji wawekezaji kuja kukupa teknolojia mpya, yenye raslimali ili wawekeze ili nacho kilimo na ufugaji, uvuvi ubadilike. Sasa tusipowaheshimu hawa wawekezaji wetu tulionao na wengine wa nje wataogopa kuja. Mimi nawaomba sana Waheshimiwa Wawakilishi tulielewe kwamba hakuna nchi duniani iliyoendelea kama hakuna wawekezaji na wawekezaji ni watu wenye mambo mawili, fedha na teknolojia. Teknolojia hatuna, fedha hatuna basi upate mwekezaji akusaidie akuondoe pale ulipo ili na watu wako na wao waweze kufanya hiyo kazi.(*Makofi*).

Kwa hivyo hilo Waheshimiwa Wawakilishi naomba tulizingatie sana na tusiwaseme vibaya kama kuna kasoro tukae turekebishe kasoro. Ni kweli wanatafuta fedha lakini na *risk* wanaichukua vile vile ni kubwa, sio kwamba wakifika kesho wakiwekeza wanapata fedha, hapana kuna *high risk* anaichukua mtu mpaka aweze kupata pesa zake nyingi. Kwa hivyo nimesema hayo niyasema kama utangulizi kwa sababu katika sekta hizi tunazokuja nazo mbele ya safari tutawategemea *private sectors* hawa hawa watu wetu sisi, hawa hawa mmoja mmoja wafanyabiashara mmoja mmoja na nyinyi tunawategemea vile vile na kuna mwengine anaposema vile vile kwamba tufanye vizuri wakati

wewe ni mwekezaji wa humu humu ndani. Kwa hivyo nasema ni vizuri wawekezaji hawa tuwape kila heshima, tuwape kila msaada ili waweze kufanya vizuri.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo nataka nilielezee ni suala zima la uvuvi. Nataka nimshukuru sana Mhe. Rais katika vikao tulivyokaa naye, moja alichosema tunataka kuhakikisha raslimali hizi za baharini sasa zinawafaidia watu wetu na tunawasaidia watu wetu. Kwa hivyo alichokifanya ni nini? Kwanza akasema tuwe na kampuni yetu wenyewe ya uvuvi. Nataka kuwahakikishia Waheshimiwa kampuni ya uvuvi tayari ipo tumeshakwenda kwa Msajili ku-*register* tunategemea mwezi wa Machi wakati wowote itatangazwa rasmi. Nataka niwashukuru sana niyashukuru mashirika yetu ya *PBZ, ZSTC, ZSSF* na Bandari, mashirika manne haya yamekubali kutoa mtaji kwa ajili ya kuanzisha kampuni hii na wao ndio watakuwa *shareholder* wa kwanza. Kampuni hii itakapoanza inafanya mambo matatu makubwa.

La kwanza watahakikisha kabisa wana meli zao mbili za uvuvi, meli mbili rahisi sana kwani pesa zipo wataanza wao kuvua.

Pili, kuwa ni sehemu ya kuangalia raslimali tulizonazo ni kwa kiasi gani tunaweza kuwasaidia watu wetu na Mhe. Rais ameagiza anataka kuwaona wavuvi wetu wadogo wadogo wote angalau wanaondokana na boti wanazotumia sasa hivi wapate angalau bodi 500 za kuanzia, kama walivyofanya ndugu zetu wa Comoro na sisi tufanye. Nataka nichukue nafasi hii vile vile niwashukuru baadhi ya Wawakilishi wametuletea majina ya makampuni ambayo yako tayari kuwekeza hapa kwa ajili ya kuweka viwanda vya kuweza kuzalisha boti zetu hapa hapa na nawaomba waendelee kufanya kazi hiyo na sisi tunawapokea.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jambo la tatu ambalo tunalifanya sheria yetu ya uvuvi wa bahari kuu, kanuni ya zamani tuliyokuwa nayo ilikuwa hailazimishi meli kuteremsha samaki na kuweza kusafirisha nje. Sasa kanuni imebadilika tayari na inafanya kazi meli zote ambazo tunazipa leseni kuvua lazima zije Zanzibar au Dar es Salaam au Tanga ziteremshe samaki, wale wanaotaka kusafirisha nje wapitie kwenye bandari zetu na wale ambao hatukuwapa leseni kuvua waingie kwenye masoko yetu ya ndani. Sheria na kanuni iko tayari inafanya kazi na sasa hivi katika meli 37 ambazo zimepewa leseni mwezi huu wa Januari wanatakiwa tena ku-*renew* leseni yao, sharti la kwanza ni kuwaambia kwamba jee, mtakuja kuteremsha samaki na kusafirisha samaki kwetu, hamfanyi hivyo hatutowapa leseni bora samaki wakae pwani. Hilo ni jambo moja ambalo tumelifanya. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, lakini la tatu kubwa sana na hili nasema nawashukuru sana Wawakilishi, tunazo maeneo ya kufuga samaki 152, tatizo lao kubwa walikuwa ni suala zima la kupata vifanga vya samaki. Nataka niishukuru sana serikali yetu, niwashukuru sana ndugu zetu wa *JAICA* na Japan kwa kutupa msaada wa dola milioni 10 kwa kujenga *hatchery* ambayo inamalizika kuanzia mwezi wa Agosti mwaka huu tutazalisha vifaranga milioni 10 vya samaki.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, Pemba tunahitaji vifaranga milioni 2 hivi sasa, Unguja tunahitaji vifaranga 700,000. Nataka niwaambie wananchi kama kuna pahala pa kuweza kutengeneza pesa kwa haraka sasa ni kuingia katika ufugaji wa samaki. Vifaranga vipo, ukitaka vifaranga vya kaa vitakuwepo, vifaranga vya kasa ukitaka utapata, vifaranga vya samaki ukitaka utapata, vifaranga vya dagaa ukitaka utapata. Vyote vitakuwa vinazalishwa na leo ukitaka kupata nafasi hiyo baada ya wiki mbili tatu mkatembelee pale Beit-el-Ras kwenye kiwanda hicho kontena tayari zimeingia za mashine zenyewe na nakwambieni Agosti tayari *production* inaanza na watu wataanza kupata vifaranga. Tunaamini vifaranga hivi vyengine itabidi tusafirishe nje kwa sababu milioni 10,000,000 ni vingi sana, lakini nasema hiyo tayari ipo iko kwenye *program* nataka niishukuru sana serikali kwa kazi hiyo. (*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo tumelifanya namshukuru sana Mhe. Waziri wa Biashara na Viwanda amesema idadi ya watu wanaoshughulika na dagaa. Moja ambalo tunalolifanya ni kuwa na masoko ya uhakika. Soko la Malindi ambalo Mhe. Rais amekwenda kulikagua linaanza ujenzi wake mwezi wa Aprili, tunategemea katika kipindi cha miezi saba au nane inayokuja soko hili litakuwa kwa kiwango kikubwa sana limemalizika. Kwa upande wetu sisi serikali tulitakiwa tuweke miundombinu ya maji na umeme na kazi hiyo tumemaliza tunangoja sasa m-*consultant* afike pale na kazi iweze kujengwa. Fedha zake tayari zipo wala hakuna shida ya fedha.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, tulikuwa na upungufu wa dola milioni 1,000,000 naishukuru serikali Rais mwenyewe amesema dola milioni 1,000,000 itatoka kwenye mfuko wetu sisi wenyewe wa bajeti. Tumekamilisha hiyo kazi Mhe. Naibu Spika. Kwa hivyo, kubwa kwa wavuvi ninachoomba ni mambo matatu na nawaomba Waheshimiwa watusaidie na ilizungumzwa sana taarifa hii, suala la uvuvi haramu. Suala la uvuvi haramu ni tatizo la msingi na hili linahusu sote sisi wenyewe Wawakilishi tuzungumze na watu wetu suala zima la kupambana na uvuvi haramu na taarifa hii inasema jambo hilo hilo. Hilo litatusaidia sana kuweza kupata samaki.

Mhe. Naibu Spika, tumefuga samaki, pweza Kisiwapaza. Pweza ukienda ukimvua leo utapata kilo moja na nusu mpaka mbili, ukiweza kufunga ule wigo wa kufunga pweza katika miezi mitatu unapata kilo sita. Bahati mbaya ndugu zetu wa Kisiwapaza wakaingiza siasa kidogo wakenda wakavuruga ule mtego pale pweza wakaondoka, sasa tunataka kuanzisha maeneo mengine ambayo hatuna matatizo ya aina hiyo ili watu waweze kufaidika na ufugaji huu. Kwa hivyo suala la kufuga samaki, pweza na bidhaa za baharini ndio peke yake *solution* ya kuondoa matatizo ambayo tuliyonayo.

Mhe. Naibu Spika, jambo jengine ambalo limezungumzwa sana ni suala zima la ukataji wa miti ambalo nasema linatuchangia tatizo kubwa sana katika nchi yetu na taarifa ya kamati imesema. Mhe. Naibu Spika, kama hatukuhifadhi mazingira yetu, kazi kubwa tunayoifanya ya suala la umwagiliaji maji itakuwa limepotea. Mabonde kama ya Cheju tunategemea sana mito inayotoka Kianga na kadhalika. Leo watu wanajenga nyumba chini ya chanzo cha maji. Ni dhahiri kabisa mabonde haya yatakosa maji karibuni sana. Kwa hivyo ombi langu kubwa tujitahidi sana kutunza mazingira, minazi inakatwa tunalalamika mafuta ya nazi hapana, tulikuwa na minazi milioni 5,000,000 leo tuna minazi milioni 3,000,000 inakatwa kwa nguvu sana na *speed* ya kukatwa kubwa, watu hawapandi. Kwa hivyo hilo ni jambo moja ambalo lazima tulizingatie kama raslimali hizi hatukuzitunza vizuri hali yetu itakuwa mbaya sana. Kwa hivyo ningeomba Mhe. Naibu Spika, Waheshimiwa Wawakilishi tuzungumze na wananchi tuhakikishe kabisa tunatunza mazingira yetu.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, limezungumzwa sana suala la mchanga. Nataka nirudi tena kumshukuru sana Mhe. Rais, mwaka 2013, 2014 na 2015 serikali ilifanya utafiti juu ya raslimali hizi zinazohamishika, na utafiti huo ukaonesha kwamba matumizi yetu ya mchanga ni makubwa kuliko uhalisia wa mchanga uliopo. Lakini kubwa zaidi maeneo ambayo yanachimbwa mchanga ni yale maeneo ambayo yalikuwa katika *plan* yetu ni ya kilimo. Watu wako tayari wanakata minazi yao wanaipiga rangi, wanaiweka inakaa unafikiri pahala pale hapaoti kitu, anakaa miaka miwili au mitatu anakuja kuomba kibali akachimbe mchanga ni sehemu ya kilimo na kilimo hatuna. Serikali ikafanya utafiti wa kutosha sana. Mhe. Rais baada ya kuona kwamba kuna tatizo hilo akaunda kamati ya wataalamu wakapita wakaangalia wakafanya utafiti wa kutosha wakaja wakatoa taarifa serikalini.

Taarifa ikaja serikalini kwamba kuna upungufu mkubwa wa mchanga tumebakiwa na tani 400,000, mahitaji ya *private sectors* peke yake ni tani milioni 1,600,000. Kwa hivyo, serikali ikasema upo upungufu wa mchanga na ndio tangazo tulilotoa, upo upungufu wa mchanga raslimali hii imepungua.

Sasa wengine wanasema hii imepigwa marufuku, tulichosema upungufu upo na ni *really* upo. Mhe. Naibu Spika, alichokifanya Mhe. Rais baada ya kuona yote hayo kwa kupitia Baraza lake la Mapinduzi, akasema hebu tuunde Kamati ya Mawaziri na wataalamu wakaangalie zaidi. Kwa hivyo ikaundwa kamati mimi nikiwa Mjumbe, Mwenyekiti ni Waziri wa Uchukuzi na Waziri wa Ardhi na Makatibu wetu Wakuu na wataalamu wengine ndio wakasaidie kufanya utafiti wa ziada. Tumefanya utafiti huo tukenda tukatoa taarifa serikalini. Nasema Rais ni mtafiti sana akasema bado hebu jipangeni vizuri, akasema Makamu wa Rais nataka tena uongoze jopo la Mawaziri mwende mkakague maeneo hayo tutosheleze kwamba kweli tunaweza tukasema mchanga uko na uko wapi kama upo, kama haupo haupo kiasi gani ili baadae serikali itoe kauli.

Mhe. Naibu Spika, leo Makamu wa Pili wa Rais tumeongozana naye, tumekwenda kwenye maeneo tumeyakagua. Bahati mbaya mimi nilikuwa nakimbilia kikao nikawaacha wenzangu waendelee, wameendelea huko na hapa ameniita sasa hivi akaniambia tumemaliza kazi tukutane Jumamosi saa kumi na kamati yetu yote tuliyokwenda ili sasa twende serikalini, yaani kwa maana *cabinet* yote tuiambie jamani hali ni hii ili sasa serikali itoe kauli rasmi. Kwa hivyo katika kikao hiki Mhe. Naibu Spika, hatuna kauli rasmi ya serikali mpaka Baraza la Mapinduzi litakapokaa na baada ya taarifa hii kupelekwa ndio twende tupate kauli rasmi. Na huo ndio utaratibu wa serikali kabisa, serikali ikija ikitoa kauli inatoa kauli ambayo imepitishwa kwenye Baraza la Mapinduzi na ndio kauli ya serikali. (*Makofi*).

Kauli ya kwanza niliyoitoa ilikuwa ni taarifa tu kwa wananchi kwamba hali yetu ya mchanga sio nzuri, hiyo ndio kauli ya kwanza iliyotoka hatujasema tumezuia mchanga. Tusubiri serikali itapokaa na taarifa hii baadae tutakaa kikao cha Baraza la Mapinduzi na taarifa rasmi itatolewa kila mwananchi atajua nini cha kufanya au mchanga upo, haupo au ni jambo gani serikali itatoa kauli rasmi. Hilo ndio jambo ambalo tunaweza kulisema katika Baraza hili na hatuna *mandate* sasa hivi yakusema mpaka vikao hivi viweze kumalizika.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, jengine nimshukuru sana Mhe. Mussa amesema nikatembelee sana maeneo ya vituo vya Dodeani na kadhalika. Naomba niungane naye tutakwenda kuangalia hivyo vituo vyote na maeneo yote yale ambayo yalikuwa ya serikali yamechukuliwa tutayarudisha serikalini tuna mpango huo. Kulikuwa na mashamba 8,500 serikali ika-*commission* wataalamu kufanya utafiti tumeyagundua mashamba kama 5,500, sasa hivi tunaendelea na utafiti mwengine kukamilisha idadi yenyewe ili tujue mashamba hayo yako kwa nani na nani ameyachukua kama amechukua kiutaratibu au si utaratibu ili

serikali baadae iweze kuyarudisha na kuwakabidhi wananchi. Hiyo kazi inafanyika lakini nasema taarifa uliyotupa ni nzuri tutaifanyia kazi nakwenda kushirikiana na wewe kuweza kufanya hiyo kazi.

Mhe. Naibu Spika, eneo jengine ni suala zima la umwangiliaji maji. Tumejitahidi sana katika kipindi hiki katika hekta 8,500 za umwagiliaji maji, hekta mia nane na kiasi fulani hivi tunajitahidi sasa hivi kumwagilia maji. Lakini kulikuwa na mradi wa *Exim Bank* na huo nafikiri mnaufahamu kwa muda mrefu sana, wa hekta 1,600. Kwa bahati mbaya sana katika kipindi kilichotokea ule mradi kidogo ulichelewa lakini nataka nimshukuru sana Waziri wa Fedha na Katibu Mkuu wake tumeweza kufuatilia na sasa hivi nataka niwahakikishie Waheshimiwa tenda itatoka karibuni ya kuweza kuzilima hekta 1600 kwa kumwagilia maji. Tumepata dola 46 milioni ambazo naamini hizo tukijumuisha na zile ambazo tunazo tutakuwa na hekta kama 2300 za umwagiliaji maji na hizo zitatupa wastani wa tani zisizopungua 20,000 za mchele ambazo naamini kabisa tutakuwa tumepunguza kiwango kikubwa cha uagiziaji wa mchele.(*Makofi*).

Vile vile kuna kilimo cha juu ambapo tuna eka kama 33,000. Ni kweli kabisa tuna upungufu mkubwa sana wa matrekta, matrekta tuliokuwanayo msimu huu yalikuwa 20 lakini yalioweza kufanya kazi hasa ni matrekta kama 16. Serikali ilikuwa imezungumza na Kampuni ya Mahendra kupitia na Rais wetu katika ziara yake, wamekubali kutuuzia matrekta 100 lakini tuanze na matrekta 20. Tunaendelea na mazungumzo nao tunategemea wakati wowote *LC* itafunguliwa matrekta 20 yatapatikana. Lakini kubwa kilichofanya serikali baada ya kuona kwamba *department* yetu ya matrekta ilikuwa kama idara ndogo serikalini, sasa hivi imeanzishwa *agency* ya matrekta, yenyewe sasa itaweza angalau kushughulikia sekta nzima hii ya zana za kilimo yakiwemo pamoja na matrekta. Naamini kabisa hatua hiyo itatusaidia sana kutuondoa na utegemezi wa matrekta machache tuliyonayo, lakini vile vile tutakuwa na zana nyengine za kilimo.

Kwa mfano, kuna *power tillers* wale ambao wanalima kilimo cha juu matrekta sehemu nyengine hayafiki milima mikubwa, lakini *power tillers* zinaweza kutusaidia kutupunguzia tatizo hilo. Kwa hiyo, tuko kwenye programu hiyo na naamini kabisa *agency* yetu ya matrekta itafanya hiyo kazi na tutapungukiwa na tatizo hili ambalo tunalo hivi sasa.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema sikukusudia kusema maneno yote lakini kuna eneo moja tu la muhimu la mifugo. Ni kweli kabisa mashama yetu ya mifugo mengi au yote yako katika hali mbaya sana, nimekwenda kama mara

tatu barabara ni mbaya, miundombinu imekufa na kadhalika. Sasa hivi katika programu tulizonazo na hata juzi tumewasiliana na Tume yetu ya Mipango pamoja na Serikali ya New Zealand wanaisaidia Serikali ya Jamhuri ya Muungano Dola milioni sita. Tumewaoma Dola milioni tatu ili kufungua mashamba yetu haya, tunategemea vile vile programu hiyo itafanikiwa na hatimaye mashamba haya tutaweza kufanikiwa. Vile vile kwa fedha ndogo ambayo tunayo katika bajeti yetu tutahakikisha kabisa tunaanza kufufua pole pole mashamba haya.

Jambo ambalo la faraja kabisa ni ule mradi wetu 'kopa ng'ombe lipa ng'ombe', wananchi wameitikia vizuri sana na wanazalisha maziwa kwa vizuri sasa hivi, tunategemea mradi ule tuukuze ili sasa kila pahala tuwe na 'lipa ng'ombe, kopa ng'ombe' au 'kopa mbuzi lipa mbuzi'. Naamini kabisa na hiyo nayo inaweza itatuondolea matatizo haya ambayo tunayo hivi sasa.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, mwisho kama ulivyosema hatutakiwi kujibu hoja zote hizi hapa ni suala zima la pembejeo. Nimesikitika sana kusikia kama kuna pembejeo ya mpunga imetolewa hivi sasa kwa bahati mbaya imechanganyika sio nzuri, lakini kwa kweli kabla mbegu haijatumika tunaifanyia utafiti tunaangalia kabisa kama ni mbegu nzuri au mbaya. Kwa hivyo nasema tutaungana na Mhe. Mwakilishi tuone wale ambao wamepata mbegu mbaya tuipitie tuiangalie tujue tatizo ni nini, ili tuweze kusahihisha kasoro ambayo ipo. Nahakikisha kabisa kama wakulima walipata mbegu mbaya na mbegu hiyo imetoka kwetu tutawahakikishia kabisa tutawapa *replacement* ya mbegu ambayo ni sahihi na hata hayo makosa tutayachukulia hatua. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, naomba kuunga mkono hoja ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Mhe. Waziri. Sasa nimpe nafasi Mwenyekiti wa Kamati aweze kufanya majumuisho. Mwenyekiti karibu sana.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kufanya majumuisho ya kamati yetu, lakini la pili tuwashukuru Wajumbe wote waliochangia kwa maandishi na wale waliochangia moja kwa moja, lakini na wale ambao hawakupata nafasi ya kuchangia ripoti hii kutokana na sababu ya muda lakini wanaiunga mkono ripoti yetu ya kamati. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ripoti yetu imechangiwa na Wajumbe 40, Wajumbe 27 wamechangia moja kwa moja (Mubashara) na Wajumbe 13 wamechangia kwa maandishi.

Mheshimiwa kwa ruhusa yako naomba niwatambue Waheshimiwa waliochangia kwa majina kama ifuatavyo:

1. Mhe. Suleiman Sarahan Said
2. Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohammedali
3. Mhe. Rashid Makame Shamsi
4. Mhe. Shehe Hamad Mattar
5. Mhe. Panya Ali Abdalla
6. Mhe. Nadir Abdul-latif Yussuf Al-Wardy
7. Mhe. Asha Abdalla Mussa
8. Mhe. Miraji Khamis Mussa
9. Mhe. Abdalla Maulid Diwani
10. Mhe. Masoud Abrahman Masoud
11. Mhe. Bahati Khamis Kombo
12. Mhe. Omar Seif Abeid
13. Mhe. Dkt. Makame Ali Ussi
14. Mhe. Tatu Mohammed Ussi
15. Mhe. Hamad Abdalla Rashid
16. Mhe. Hidaya Ali Makame
17. Mhe. Mussa Ali Mussa
18. Mhe. Ali Suleiman Ali (Shihata)
19. Mhe. Hassan Khamis Hafidh
20. Mhe. Hussein Ibrahim Makungu
21. Mhe. Suleiman Makame Ali
22. Mhe. Maryam Thani Juma
23. Mhe. Jaku Hashim Ayoub
24. Mhe. Said Soud Said (Waziri Asiye na Wizara Maalum)
25. Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango
26. Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko
27. Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi

Waliochangia kwa maandishi kama nilivyosema awali ni 13 naomba nao niwataje kama ifuatavyo:-

1. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais
2. Mhe. Mtumwa Suleiman Makame
3. Mhe. Abdalla Ali Kombo
4. Mhe. Hamida Abdalla Issa
5. Mhe. Naibu Waziri wa Afya
6. Mhe. Waziri wa Habari, Utalii na Michezo

7. Mhe. Naibu Waziri wa Nchi (OR) Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ
8. Mhe. Shaibu Said Ali
9. Mhe. Naibu Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi
10. Mhe. Mgeni Hassan Juma
11. Mhe. Mwantatu Mbaraka Khamis
12. Mhe. Zulfa Mmaka Omar
13 Mhe. Salha Mohamed Mwinjuma . *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli Waheshimiwa Wajumbe wameifanyia haki sana Kamati yetu ya Fedha, Biashara na Kilimo. Michango yao Waheshimiwa Wajumbe ni mizuri sana kwa sababu ni michango inayojenga na kuongeza kasi ya utekelezaji wa watendaji wetu wa serikali. Sisi Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo tunathamini sana michango yenu na michango yote kwa kweli tunaichukua na itatusaidia sana katika kutekeleza shuguli zetu za kamati.(*Makofi*).

Mhe. Naibu Spika, sikusudii kujibu hoja kwa sababu utekelezaji wa maoni yetu pamoja na michango ya Waheshimiwa Wajumbe itawasilishwa kwenye Kikao cha Septemba kama Kanuni yetu kifungu cha 108(15) inavyoeleza. Kwa hivyo, Waheshimiwa Wajumbe tuwape muda serikali ifanyie kazi ya mapendekezo na maoni haya kwa kina kabisa ili ikifika katika kikao chetu cha Septemba iweze kutoa utekelezaji wa mapendekezo hayo kwa ufasaha kabisa. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nichukue fursa hii kuwapongeza Mawaziri wote wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, kwa umahiri na uchapaji kazi wao. Lakini shukurani za pekee zimwendee Mhe. Waziri wa Fedha na Mipango Dkt. Khalid Salum Mohamed, pili zimwendee Mhe. Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko, Balozi Amina Salum Ali na tatu zimwendee Mhe. Waziri wa Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi Mhe. Hamad Rashid Mohamed. Waheshimiwa hawa wamefanya kazi kubwa sana na wametoa uchambuzi na ufafanuzi wa baadhi ya hoja ili kukidhi kiu ya Waheshimiwa Wajumbe. Lakini pia wametupa mashirikiano makubwa sisi Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo wakati inatekeleza shughuli zake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, ni ukweli usiopingika kwamba Mawaziri wa awamu hii wana nia ya dhati kabisa ya kuleta mabadiliko ya wizara zao, katika kipindi hiki kifupi tumeshuhudia mabadiliko makubwa sana. Waheshimiwa Mawaziri tunawaomba sana *speed* muliyoanza nayo ni nzuri msipunguze kasi na sisi Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi tuzidi kuwaunga mkono Mawaziri hawa

na tuwape mashirikiano makubwa sana ili wapate nguvu mpya, ari mpya na kasi mpya ya kutekeleza majukumu yao. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, wizara hizi tatu, Wizara ya Fedha na Mipango, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko na Wizara ya Kilimo, Maliasili, Mifugo na Uvuvi ni wizara muhimu sana katika ustawi wa wananchi wetu. Kuimarika kwa wizara hizi kupelekea mafanikio makubwa kama ukuaji wa uchumi wetu, lakini ukuaji wa biashara za ndani na nje pamoja na sekta wa viwanda, lakini pia ongezeko la uzalishaji wa bidhaa za chakula na biashara. Hivyo basi tuwaombe sana Waheshimiwa Mawaziri wa Fedha, Waziri wa Kilimo na Waziri wa Biashara wahakikishe wanaongeza bidii na juhudi za kuhakikisha mafanikio haya yanafanikiwa ipasavyo, kwani Zanzibar yenye mafanikio makubwa na yenye kujitegemea inawezekana ikiwa kila mmoja wetu atatimiza wajibu wake. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, baada ya maelezo hayo nashukuru sana, ahsante sana naomba kuwasilisha. (*Makofi*)

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Yussuf Hassan Iddi, Mwenyekiti wa Kamati unatakiwa kutoa hoja.

Mhe. Yussuf Hassan Iddi (Mwenyekiti wa Kamati ya Fedha, Biashara na Kilimo): Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe mwenyekiti ametoa hoja wanaokubaliana na ripoti hiyo wanyanyue mikono. Wanaokataa, waliokubali wameshinda. (*Makofi*)

(Hoja ilitolewa iamuliwe)

(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii kwanza kabisa ...

(Hapa Wajumbe walikuwa wakipiga makofi sana)

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe na mimi naomba kusikilizwa sasa. Waheshimiwa Wajumbe na mimi nichukue fursa hii adhimu kwanza kuwashukuru na kuwapongeza sana Waheshimiwa Wajumbe wote ambao wameweza kuchangia waliochangia kwa maneno, lakini waliochangia kwa

maandishi. Michango yao imekuwa ni chachu kubwa sana ya maendeleo ya taifa letu.

Waheshimiwa Wajumbe shukurani za pekee na pongezi za pekee ziwafikie Mawaziri wa Wizara hizi tatu na hususan kwanza kwa kufikia au kwa kuzidi malengo ambayo tuliyategemea hasa katika kukusanya mapato. Lakini jengine vile vile kwa kutupa mwelekeo ambao kwa kweli unaonesha serikali hii imejidhatiti kuleta maendeleo katika taifa letu.(*Makofi*).

Kwa maana hiyo, nampongeza sana Mhe. Dkt. Ali Mohamed Shein kwa kweli kwa uongozi wake bora ulio makini hasa kwa kuweza kushirikiana na Mawaziri wake. Waheshimiwa sote tushirikiane sisi tulioko nyuma tushirikiane na walioko mbele kuhakikisha azma inafikiwa, ni muhimu sana mashirikiano yetu ili kuhakikisha azma ya serikali imefikiwa.(*Makofi*).

Niseme sasa baada ya kusema hayo najua mmechoka Waheshimiwa na nimeanza kupata vikaratasi vingi hapa lakini nilisema leo zege halilali tutafanya kazi tu. Kwa hiyo, nawashukuru kwa uvumilivu wenu na kwa maneno hayo naakhirisha kikao hadi kesho saa 3:00 asubuhi.

(Saa 3:00 usiku Baraza liliakhirishwa hadi
tarehe 24/02/2017 saa 3:00 asubuhi)